**23 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 23 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Kapinga.

Na. 388

### Sekondari ya Wasichana Mbinga Itapandishwa Hadhi Kuwa ya Kidato cha Tano na Sita

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, ni lini Shule ya Sekondari ya Wasichana Mbinga itapandishwa hadhi kuwa na kidato cha tano na sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari ya Wasichana Mbinga ina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi kidato cha nne. Shule hii ina miundombinu ya ziada ikijumuisha bweni moja na madarasa manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza maandalizi ya kuipandisha hadhi shule hiyo ambapo mwaka 2025/2026, shilingi milioni 228 imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bwalo na bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Wasichana Mbinga itapandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na sita baada ya kukamilisha miundombinu yote inayohitajika na kupata kibali kutokana na kukidhi vigezo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri ya kuona sasa Wilaya nzima ya Mbinga ambayo ilikuwa haina shule ya wasichana ya kidato cha tano na sita, tunakwenda kupata sasa kidato cha tano na cha sita. Pia, tayari kila kitu kiko tayari na mchakato huu umeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ilikuwa na upungufu sana wa kidato cha tano na cha sita na Shule hii ya *Mbinga Girls* itakuwa ni ya tatu. Je, Serikali iko tayari kuongeza jitihada za wananchi katika Kata ya Ngima pamoja na Kata ya Mhongozi ambazo hazina kabisa Shule za Sekondari? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benaya Kapinga, amekuwa akifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kuhakikisha kwamba Sekta ya Elimu Msingi katika Jimbo lake la Mbinga Vijijini inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba, hoja yake ni ya msingi sana. Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana kuendelea kujenga shule za kata, lakini pia kujenga shule za kidato cha tano na kidato cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kuwa, kama vile fedha tayari zimeshatengwa kwa ajili ya kuhakikisha shule hii ya *Mbinga Girls* inapandishwa hadhi kuwa ya kidato cha tano na cha sita, kwa hiyo, hata katika kata nyingine alizozitaja, Serikali itafika kuhakikisha inaongeza miundombinu inayohitajika ili shule hizo ziweze kupandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na sita na ziweze kuwanufaisha wanafunzi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SHICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Shule ya Sekondari Msangano, Shule ya Sekondari Uwanda iliyopo Kamsamba, Shule ya Sekondari Momba iliyopo Myunga na Shule ya Sekondari Mkulwe ni shule kongwe sana. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuzipandisha shule hizi hadhi ili ziweze kutoa huduma ya kidato cha tano na sita kwa Wanamomba na Watanzania wengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Momba, kwa sababu amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma za msingi kabisa ikiwemo kwenye Sekta hii ya Elimu msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne imekuwa ikifanya uwekezaji mkubwa sana kwenye upande huu wa elimu msingi. Zaidi ya shilingi trilioni 5.1 zimetumika kuwekeza katika upande huu na ndiyo maana utaona kuna shule mpya za kata zinajengwa, na pia kuna shule za kata ambazo zinapandishwa hadhi na kuongezewa miundombinu inayohitajika ya kuweza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita. Vilevile, hata katika wilaya anayotokea Mheshimiwa Mbunge, hilo limekuwa likifanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba, Serikali itaendelea na jitihada hizi, na katika kata hizi alizozitaja

ambazo zina shule za muda mrefu za kidato cha kwanza hadi cha nne, basi Serikali itafanya tathmini na kuona uhitaji. Kama vigezo vinakidhi, itaongeza fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu inayohitajika ili shule hizo ziweze kupatiwa hadhi ya kuwa kidato cha tano na cha sita ili iweze kuwanufaisha wanafunzi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kata ya Tumbakose ndiyo kata peke yake ambayo haina shule ya sekondari kwa Wilaya ya Chemba. Naomba kujua ni upi mkakati wa Serikali kutoa fedha ili tuweze kujenga shule ya sekondari katika kata hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Monni Mohamed amekuwa akifanya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya kimaendeleo kwenye jimbo lake. Vilevile, amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana kwa upande wa elimu msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa kwenye upande huu ili kuimarisha elimu msingi. Pia, imekuwa ikifanya maboresho na mwendelezo wa shule zetu za kata kwa sababu shule zetu hizi za sekondari za kata ni shule za kutwa. Vilevile, shule za kidato cha tano na kidato cha sita ni shule ambazo ni za Kitaifa na ni shule ambazo zinahitaji mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu yote inayohitajika ikiwemo mabweni, mabwalo, na madarasa kwa ajili ya kuhakikisha shule hizo zinapata hadhi ya kuwa kidato cha tano na cha sita na kuweza kupokea wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba hata katika Jimbo lake kwenye kata alizozitaja, Serikali itaendelea na mpango huo, itafika na itakuja kujenga miundombinu inayohitajika ili shule hizo zipandishwe kuwa kidato cha tano na cha sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Kimali ni kongwe sana na ina eneo kubwa tu kama ekari 15. Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi shule hiyo kupata kidato cha tano na cha sita? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Minza amekuwa akifanya ufuatiliaji na amekuwa akisemea uhitaji wa kuendelea kuboresha Sekta ya Elimu Msingi katika mkoa anaotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayo dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha Sekta hii muhimu ya Elimu Msingi na ndiyo maana tunaona shule mpya za kata zinajengwa, na miundombinu kadha wa kadha ya kuendelea kuimarisha shule zetu hizi katika upande wa shule za msingi na sekondari, inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika hii ya Kimali kwenye hii shule aliyoitaja, Serikali itaendelea kufanya tathmini na kuweka katika mipango yake upandishaji wa shule zetu hizi za sekondari za kata kuwa na miundombinu inayohitajika ili ziweze kuwa na sifa ya kupandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na cha sita.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Taska Mbogo.

Na. 389

**Ukarabati wa Shule Kongwe Nchini**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa Shule Kongwe nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya ukarabati wa shule kongwe nchini ambapo katika mwaka 2015/2016 hadi 2023/2024, shilingi bilioni 168.31 zilitumika kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za msingi 793 na sekondari 89.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024/2025, Serikali imetenga shilingi bilioni 26.13 kwa ajili ya ukarabati wa shule 259. Aidha, kutokana na baadhi ya shule kuwa chakavu, kiasi cha kutokarabatika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika baadhi ya shule kwa kujenga miundombinu mipya kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukarabati wa shule chakavu au kujenga miundombinu mipya katika shule zisizokarabatika kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa kwenye Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Mpanda, Shule za Kashaulili, Msakila, Mlala, Azimio, Shanwe, Misunkumilo, zote zilizoko kwenye Manispaa ya Wilaya ya Mpanda hazijakarabatiwa na ni shule kongwe ambazo zina takribani ya zaidi ya miaka 50. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzikarabati shule hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa kumekuwa na kutegeana kati ya Halmashauri na Wizara ya Elimu kuhusu ukarabati wa shule kongwe nchini, je, ni nani mwenye jukumu la kukarabati shule hizi? Ni Halmashauri au Wizara ya Elimu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Taska Mbogo, kwa swali lake linalolenga kuendelea kuimarisha Sekta ya Elimu Msingi. Pia, kuhusiana na swali lake la kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Taska Mbogo, kwamba, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti ili kuhakikisha inafikia shule kongwe ambazo ni chakavu na kuboresha miundombinu ya shule hizo ili ziweze kuwanufaisha wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Serikali imekuwa pia ikijenga shule mpya kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika upande wa elimu msingi. Naomba nimhakikishie kwamba, Serikali itaendelea na mipango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, utaona kwamba, tayari katika upande wa shule zetu za msingi (shule kongwe) zaidi ya shule kongwe 793 zimefikiwa na kukarabatiwa kwa gharama ya shilingi bilioni 70.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba katika mwaka wa fedha huu 2024/2025, shilingi bilioni 26.13 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati shule kongwe za msingi 259. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba, Serikali itafika katika Manispaa ya Mpanda kwa ajili ya kuendelea na kazi hiyo ya ukarabati wa shule zetu za msingi ambazo ni kongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Taska Mbogo, kwa kuzingatia msingi na dhana ya

ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu wa msingi kabisa wa kukusanya mapato na kupanga maendeleo. Kwa hiyo, jukumu na wajibu wa msingi wa kufanya maendeleo ikiwemo maendeleo katika Sekta ya upande wa Elimu (ukarabati, kujenga miundombinu yote inayohitajika kutoa elimu msingi), huo ni wajibu wa mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika ni Serikali Kuu kuja kuongeza nguvu katika wajibu wa msingi ambao unakuwa umetekelezwa na mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, naomba niendelee kuwakumbusha Wakurugenzi wote wa mamlaka zetu za Serikali za Mitaa waendelee kutimiza wajibu wao wa kukusanya mapato na kupanga maendeleo na kutenga fedha kwa ajili ya maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwemo katika Sekta hii muhimu ya Elimu Msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Shule ya Msingi Namanyere ni miongoni mwa shule kongwe zilizopo Wilaya ya Nkasi. Umezungumza hapa kwamba, kuna fedha ambayo mmetenga kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe. Je, Shule ya Msingi Namanyere ni miongoni mwao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Aida Khenani, amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana wa kuhakikisha kwamba anasemea changamoto katika upande wa Sekta ya Elimu Msingi katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie kwamba, katika fedha ambazo zitakwenda kukarabati shule za msingi 259, tutaweka kipaumbele kufika katika shule hii ya Msingi Namanyere ambayo na yenyewe ni chakavu ili na yenyewe iweze kuwa

katika hali nzuri na wanafunzi waweze kupata sehemu nzuri ya kusomea na walimu wapate sehemu nzuri ya kufundishia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

Na. 390

**Ukarabati wa Shule za Msingi Nchini**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati shule za msingi nchini kwa kuwa shule nyingi ni chakavu.?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa shule chakavu za msingi na sekondari ambazo zinahitaji ukarabati ambazo zimekuwa zikikarabatiwa au kujengewa miundombinu mipya kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022/2023 na 2023/2024, Serikali imetoa shilingi bilioni 70.39 kwa ajili ya ukarabati wa shule 793 za msingi. Aidha, mwaka 2024/2025 Serikali ilitenga shilingi bilioni 26.13 kwa ajili ya ukarabati wa shule 259.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukarabati wa shule chakavu au kujenga miundombinu mipya katika shule zisizokarabatika kadri ya upatikanaji wa fedha.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali na mipango mizuri ya Serikali ya kuendelea kukarabati shule kongwe. Hata hivyo, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kalenga, tunazo shule nyingi chakavu ambazo zimejengwa miaka ya 1960 na 1970. Kwa mfano, ipo Igumila, Mgama, Nyamihuu, Lupembelwasenga, Lyamgungwe, Malagosi, Kihanga, Mlanda, Mkombe, Magulilwa na shule nyingine zilizojengwa miaka ya 1950 (Kiponzelo na Ifunda). Je, ni nini mpango wa haraka wa Serikali kutupelekea fedha ili tuweze kukarabati hizi shule kongwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Jackson Kiswaga, kwani kwa hakika amekuwa akipaza sauti kuwasemea wananchi wake katika changamoto mbalimbali. Nia na madhumuni ni kuona kwamba, wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Jackson Kiswaga kwamba, mipango ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kuimarisha Sekta ya Elimu Msingi, na ndiyo maana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, zaidi ya shilingi trilioni 5.1 zimetumika kuendelea kuimarisha upande huu wa elimu msingi. Katika fedha hizo, shilingi trilioni 5.1 shule chakavu zimekuwa zikifikiwa kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinaboreshwa na zinakarabatiwa ili wanafunzi wetu wapate sehemu nzuri ya kusomea na walimu kupata sehemu nzuri ya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika naomba nimhakikishie Mheshimiwa Jackson Kiswaga kwamba, shule chakavu katika kata alizozitaja, Serikali itafika kwa awamu. Itatenga fedha kufikia shule hizo iweze kuzikarabati ili ziweze kuwa katika hadhi nzuri ziweze kuwanufaisha wanafunzi walimu wetu wapate sehemu nzuri ya kufundishia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikikarabati hizi shule kongwe, hasa za sekondari, lakini ukweli ni kwamba, shule hizi zamani zilivyojengwa miundombinu yake kwanza, ilikuwa na uchache ukilinganisha na udahili wa sasa hivi. Kwa mfano, Shule ya Sekondari ya Tarime sasa hivi ina michepuo mingi, mmeikarabati, imependeza, lakini ina upungufu wa mabweni. Je, lini Serikali itaenda kujenga mabweni walau mawili, kwenye Shule ya Sekondari ya Tarime? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther Matiko amekuwa akisemea sana masuala ya elimu, lengo lake likiwa ni kuendelea kusisitiza na kuishauri Serikali ifanye uwekezaji zaidi na kuboresha upande wa elimu ya msingi. Naomba nimhakikishie, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba, Serikali inatenga fedha kuboresha miundombinu na hasa kwenye shule zile chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa hoja yake ya msingi na Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne tayari imefanya uwekezaji mkubwa, imejenga mabweni 2,308. Kwa hiyo, unaona kabisa dhamira ya Serikali kuendelea kuboresha miundombinu katika shule zetu hizi. Kwa hiyo, hata katika Shule hii ya Tarime Serikali itafika, itafanya tathimini na italeta fedha, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, inajenga miundombinu ya bweni, kama ulivyoomba Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nauliza kwa msisitizo, ni lini Shule ya Uri iliyoko Kibosho Kati na Shule ya Okaseni iliyoko Uru Kusini katika Kata ya Uru Kusini zitafanyiwa marekebisho kwenye vyoo na mabwalo ya kulia kwa sababu watoto hao hawajielewielewi tu? Ni lini hasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nampongeza Mheshimiwa Shally Raymond kwa swali lake zuri kabisa ambalo lina lengo la kuboresha upande wa sekta ya elimu msingi katika mkoa anaotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri afanye tathmini ya miundombinu katika shule hizi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, aweke katika mipango ya kibajeti ili fedha ziweze kutengwa na zifike, na kupitia mapato ya ndani waanze kufanya ukarabati katika vyoo hivyo na kujenga bwalo, na Serikali Kuu itakuja kuongeza nguvu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi ya Nyanzwa na Shule ya Msingi ya Ibumu ni chakavu mno kiasi kwamba kuna baadhi ya madarasa yamefungwa, hayatumiki; pia, wanafunzi wanakaa chini na kusababisha ufaulu kuathirika kabisa. Je, nini mkakati wa kuhakikisha shule hizi zinakarabatiwa kwa haraka sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa swali lake hili zuri kabisa. Naomba nitumie nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri kwamba, kupitia mapato ya ndani wahakikishe madawati yanapatikana kwa ajili ya wanafunzi. Wanafunzi wetu hawatakiwi kukaa chini, kwa hiyo, kupitia mapato ya ndani waanze kutengeneza madawati ili wanafunzi waweze kupata madawati katika shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ukarabati wa shule hizi alizozitaja, Mkurugenzi aanze; afanye tathmini, aweke katika

mipango. Kupitia mapato ya ndani, waanze, lakini Serikali Kuu kupitia bajeti ambayo inatengwa kila mwaka tutafika kuja kuongeza nguvu kuhakikisha kwamba, miundombinu katika shule hizi chakavu inaimarika, na wanafunzi wetu wanapata sehemu nzuri ya kusomea, na walimu pia wanapata sehemu nzuri ya kufundishia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata.

Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge. Sasa aulize swali lake.

Na. 391

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Katika Kata za Jimbo la Nkenge**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Vituo vya Afya vitajengwa Kata za Kilimalile, Mabale, Minziro, Mutukula, Ruzinga, Ruyango, Kitobo na Bugandika - Nkenge? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Serikali imetenga shilingi bilioni 53.5, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata 214 za kimkakati, ambapo kila kituo kitapokea shilingi milioni 250. Katika Jimbo la Nkenge, fedha hizo zitapelekwa katika Kata ya Mutukula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati na zitakazokidhi vigezo kote nchini, zikiwemo Kata za Halmashauri ya Missenyi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitoe salamu za pongezi kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli, pamoja na kuomba maombi haya ya vituo hivi, lakini tayari fedha za kujenga Kituo cha Afya cha Mutukula tumeshazipokea, na ujenzi unaanza. Eneo hilo litajenga kituo hicho ambacho ni cha kimkakati, kitasaidia Kata ya Minziro pamoja na Mutukula yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mawili ya nyongeza. Ndani ya kata nilizotaja hapa, Kata ya Ruzinga, ambayo ina vijiji viwili na wananchi wenye mwamko mkubwa wa kuchangia maendeleo wameshaanza kujenga kituo cha afya kwa fedha zao na Mbunge nimeshawapelekea mifuko 100 ya simenti, ujenzi unaendelea. Je, sasa lini Serikali itawaunga mkono kwa kuwapelekea fedha, ili waweze kukamilisha kituo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kata hizi ambazo nimezitaja zote ni za kimkakati; Kilimilile, Mabare, Buyango, Kitobo, Bugandika ikijumlishwa na Bugolola, ni maeneo ambayo yanahitaji vituo vya afya. Je, ni nini neno la faraja la Serikali, ili wananchi hawa waweze kupata vituo vya afya na kuleta msawazo mzuri wa huduma za afya ndani ya Jimbo la Missenyi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Kyombo amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana wa kuhakikisha kwamba, sekta ya afya msingi katika jimbo lake inaendelea kuhudumiwa na kuimarika. Ni dhahiri Wanamisenyi na Wanankenge wanafahamu kwamba, tayari kilio chao ambacho Mheshimiwa Mbunge alikiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, cha kuomba fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati katika Jimbo la Misenyi, tayari amekisikia na ndiyo maana zimeteremka shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwanza nianze kwa kuwapongeza wananchi wake kwa maana wamehamasika, tayari wametafuta rasilimali fedha na nguvu zao na kuanza kujenga kituo cha afya kingine. Serikali tayari imeleta shilingi milioni 250 kwa ajili ya kituo hiki cha mkakati katika Kata ya Mutukula na kwenye kata hii nyingine ambayo wananchi tayari wameanza kuhamasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatafuta fedha na kuhakikisha inakuja kuunga mkono jitihada hizo. Fedha zitatafutwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, na pia Serikali Kuu itaunga mkono jitihada hizo ili zisipotee na hiki kituo cha afya kijengwe, kikamilike, kiweze kutoa huduma za afya bora kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwenye kata nyingine, Serikali itaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba inafikia kata mbalimbali za kimkakati na kujenga vituo hivi vya afya ili viweze kuwanufaisha wananchi wapate huduma bora zaidi za afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu na itafika kwenye kata hizi alizozitaja kwa ajili ya kujenga vituo vya afya ili wananchi waweze kupata huduma bora ya afya msingi katika jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali, baada ya kuomba kwamba, kuna uhitaji mkubwa wa kujengewa kituo cha afya katika Kata ya Ngombasi, Serikali imeniitikia na kutuletea shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mgombasi. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza ku-*comment*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa Waheshimiwa Wabunge walipaza sauti kuwasemea wananchi wao wakiiomba Serikali ya Awamu ya Sita iweze kuwaletea fedha, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio hicho cha Waheshimiwa Wabunge kimesikika, na ndiyo maana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha kwa ajili ya kuanza kufikia vituo vya afya hivi vya kimkakati na kuvipelekea shilingi milioni 250 kama tulivyowasikia hapa Waheshimiwa Wabunge wanakiri kwamba tayari fedha hizo wameanza kuzipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuwaagiza Wakurugenzi wote wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kuhakikisha pindi wanapopokea fedha hizi, waweze kwa uharaka kabisa, kusimamia ujenzi wa vituo hivyo vya afya vya kimkakati ili majengo yaanze kujengwa na mengine yakamilike kwa ukamilifu wake na kuanza kutoa huduma hizi za msingi kabisa za afya kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ni lini Serikali italeta fedha na kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha kimkakati katika Kata ya Misunkumilo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Sebastian Kapufi kwa swali lake lenye manufaa makubwa sana, kwa ajili ya wananchi wake kutoka kwenye jimbo lake. Dhamira ya Serikali ni kutoa hizi fedha, shilingi

milioni 250 kwa kuanza, kwa ajili ya kujenga miundombinu ya msingi kabisa katika vituo vya afya vya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hata kwenye jimbo lake naye shilingi milioni 250 hii itamfikia kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha kimkakati ambacho kwa kweli alipaza sauti kuomba Serikali iweze kumletea fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali sikivu ya Awamu ya Sita imesikia. Fedha zitafika, kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki ili wananchi wake wapate huduma bora za afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Makanya ina wananchi wengi, sekondari zaidi ya tatu na shule za msingi zaidi ya nane. Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kujenga kituo cha afya katika Kata hii ya Makanya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Shekilingi, amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wake wanapata maendeleo. Katika Kipindi cha Miaka Minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, zaidi ya shilingi trilioni 1.29 zimetumika kwa ajili ya kuendelea kuimarisha Sekta ya Afya Msingi, vituo vya afya zaidi ya 300 vimejengwa katika kipindi hiki cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 kila jimbo linapelekewa shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza kujenga majengo ya awali ya awamu ya kwanza katika vituo vya afya vya kimkakati. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Shabani Shekilindi kwamba, hata katika Kata hii ya Makanya, Serikali itafika kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kituo cha afya ili kuweza kuimarisha sekta hii muhimu kabisa ya afya msingi katika jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Jimbo la Newala Vijijini. tunavyo vituo viwili vya zamani vya afya, Chihangu pamoja na Mkwedu, ambavyo havina wodi za kulaza wagonjwa. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye vituo hivi ili vijengewe wodi, kwa ajili ya kulaza wagonjwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwa swali lake hili zuri kwa ajili ya wananchi wa Newala Vijijini. Serikali imekuwa ikijenga miundombinu ya vituo vya kutolea huduma ya afya msingi kwa awamu na imekuwa ikitenga na kupeleka fedha kwa awamu kuanza kujenga majengo na kuanza kutoa huduma. Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu yote ya msingi inayohitajika katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri wa Newala Vijijini aweze kufanya tathmini na kuweka katika mipango ya kibajeti, kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, ujenzi wa wodi hii, kwa ajili ya kulaza wagonjwa. Serikali Kuu itaendelea kuunga mkono jitihada hizi ambazo zinakuwa zimefanyika na halmashauri zetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Maandalizi ya Kituo cha Afya katika Jimbo la Mwibara yamekamilika. Je, ni lini sasa pesa hizo zitafika huko? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Charles Kajege kwa swali lake zuri. Ninaomba niendelee kutoa taarifa kwamba, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga shilingi bilioni 53.5, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo yote 214.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Charles Kajege kwamba, Jimbo lake la Mwibara ni wanufaika wa fedha hii. Fedha italetwa, shilingi milioni 250, kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati, ili kiweze kutoa huduma ya afya bora kwa wananchi wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 392

**Kuwekeza kwenye Eneo la *EPZA*, Bunda**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuwekeza kwenye eneo la EPZA katika Halmashauri ya Mji wa Bunda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza hatua za awali za upembuzi yakinifu sambamba na kuandaa mpango kabambe, ambapo kukamilika kwa hatua hizi kutalifanya eneo hili liwe tayari kwa uendelezaji miundombinu na hatimaye kulitangaza kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya Serikali ni kulifanya eneo hili liwe muhimu kwa uchakataji wa bidhaa za kilimo, uvuvi, madini na nguo kwa kutumia malighafi zote zinazopatikana Kanda ya Ziwa. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Robert Chacha Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja la nyongeza. Ni lini sasa Serikali itakamilisha huo upembuzi yakinifu ili eneo hili liweze kutumika kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali katika Halmashauri ya Mji wa Bunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Robert Chacha Maboto kwa ufuatiliaji kwa ajili ya maendelezo katika Jimbo lake la Bunda, mahsusi kwenye sekta ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tayari tumeshaanza kazi hiyo na tunategemea katika mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026 kazi hii itakamilika ili sasa tuweze kuweka ile Mpango Kabambe *(Master Plan)*, ambapo humo kutawekwa sasa mahitaji mengine muhimu ya uendelezaji eneo hili, ikiwemo miundombinu ya viwanda, huduma za biashara na vyumba vya ubaridi, *cold rooms,* kwenye maeneo mahsusi, hasa ya uvuvi na pia, sekta ya mifugo kwa sababu, kule kuna mifugo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunadhani Mkoa wa Mara uwe wa kimkakati kwenye sekta ya mifugo, uvuvi na pamba, ambayo inalimwa sana kwenye mkoa huu. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Serikali ya Awamu ya Nne iliainisha Eneo la *KIA,* kama eneo la uwekezaji maalum. Sasa je, Serikali ina mpango gani wa kuwekeza pale pamoja na kujenga bandari kavu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, na pia, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Pallangyo kwa kuuliza na kukumbushia uwekezaji katika eneo hilo la *KIA*, kule jimboni kwake. Kama nilivyosema *EPZA* au maeneo mengine ya uwekezaji, karibu katika mikoa yote tayari tuna mpango huo wa kuendeleza ikiwemo katika eneo hilo la *KIA*, Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nalo pia lipo kwenye mipango hii ambayo tunaamini sasa wakati tunaandaa mpango huu kabambe wa mwaka, Mpango wa Taifa 2025 – 2050 maana yake hayo mambo yote yatawekwa huko. Tunaamini kwamba katika mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji alishasoma hapa, itaingizwa kwenye utekelezaji katika mipango ya Wizara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Hili eneo Tairo la *EPZA* ni zaidi ya miaka 10; tangu nikiwa Mbunge wa Vijana, nimekuwa nikilizungumzia. Wananchi wamelipwa fidia muda mrefu sana, na Serikali imekuwa kila siku ikisema kwamba inalifanyia kazi. Je, Waziri haoni sasa kwamba kuna haja ya kuweka kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha ili utekelezaji wake wa kuwekeza uwanufaishe akina mama, vijana, na wakazi wa Bunda waweze kupata ajira kutokana na uwekezaji wa malighafi zinazopatikana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nampongeza pia Mheshimiwa Ester Bulaya ambaye ameongezea, lakini kama nilivyomjibu Mheshimiwa Maboto, kwamba tayari katika mwaka wa fedha 2025/2026 ambao unakuja ndipo utekelezaji utakapoanza na ndiyo hoja ya msingi ambayo Mheshimiwa Maboto aliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Bulaya, kwamba mipango ya Serikali itatekelezwa kutokana na upatikanaji wa fedha. Tunaamini kwa mipango mizuri chini ya Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Awamu hii ya Sita ni mashahidi, kwamba maeneo mengi ambayo yalikuwa yamekaa kwa muda mrefu, yameanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba na hili pia litakuwa ni eneo ambalo Mheshimiwa Rais anakwenda kuweka historia kwa kuhakikisha kwamba maeneo ya uwekezaji yote ambayo yamekaa muda mrefu sana, kwa sababu fedha imeshafidiwa, wananchi wataenda kufaidika na uwekezaji katika maeneo hayo. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalumu sasa aulize swali lake.

Na. 393

**Kuwezesha Wananchi wa Vijijini Kupata Nishati Safi ya Kupikia**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi wa kuhakikisha wananchi wa vijijini wanatumia nishati safi ya kupikia badala ya kuni na mkaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024 – 2034, ambapo kwa sasa imetoa ruzuku ya 20% hadi 50% ya bei ya mitungi ya gesi ya *LPG* takribani 452,445 kwa watumiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali kupitia *REA* itasambaza majiko banifu 200,000 yenye bei ya punguzo la hadi 75% pamoja na kuwezesha ufungaji wa mifumo ya nishati safi ya kupikia katika taasisi za umma zinazohudumia watu zaidi ya 100. Aidha, Serikali imekamilisha kusambaza umeme katika vijiji vyote na inaendelea kuhimiza matumizi ya majiko ya kupikia yanayotumia umeme ikiwa ni njia mojawapo ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi wa vijijini badala ya kutumia kuni na mkaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walio wengi, hasa wanaoishi maeneo ya vijijini, wamekuwa wakipata changamoto kubwa pale mitungi ya gesi inapokwisha ili waweze kuongeza ile gesi. Gharama hii ya mitungi ya gesi ambapo wanaongezea ni shilingi 55,000/= na shilingi 25,000/= kwa mitungi ile midogo. Kwa hiyo, wananchi wengi wanapata changamoto kubwa sana.

Je, kwa nini Serikali isiongeze ruzuku ili hawa wananchi waweze kununua ule mtungi wa kati ya shilingi 30,000 na ule mtungi mdogo uwe angalau shilingi 10,000, ili kuhakikisha wananchi wanaweza wakamudu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; pia wananchi bado wanatumia kuni na mkaa katika maeneo mengi. Pamoja na kutumia hizo kuni na mkaa, haya majiko banifu aliyoyasema Mheshimiwa Waziri yatakuwa ni mkombozi kwao kwa sababu yatakuwa yanatumia kuni kidogo na mkaa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kuwa wataanza na majiko 200,000. Haya majiko 200,000 ni chini ya asilimia tano ya wananchi wanaoishi katika kaya zile vijijini. Je, ni kwa nini, Serikali isiweke ruzuku angalau mkafikia 50% ya majiko banifu ili wananchi hawa waweze kuyatumia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na umuhimu wa kuendeleza ruzuku ili wananchi wa vijijini waendelee kupata majiko haya kwa bei rahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mkakati huu ni mkakati wa miaka 10 na ndiyo tumeanza. Kadiri ambavyo tunaendelea, tayari, kwa mfano sasa hivi tuna Mkakati wa Matumizi Bora wa Nishati, ambao pia tunahusisha sekta binafsi kwa maana ya kuongeza mitaji, kuweka *model* mpya za biashara kwa ajili ya kusaidia upande huu wa nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie, kwa mikakati ambayo tunayo kwa miaka 10 hii, tunaweza kufikia pale ambapo tumejipanga. Kwa kuwa mikakati iko mingi, hapa ni mwanzoni tu tumeanza na majiko 200,000, lakini huu ni mradi mmoja wa *REA*. Tuna wadau wengine, kwa mfano *UNCDF* ambao wamewekeza kwa teknolojia zaidi ya saba na wenyewe tunaendelea, walianza na mikoa minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna-*involve* wawekezaji wengine vilevile waendelee kuja na teknolojia hizi na waende katika mikoa, zisadie siyo tu kwa upande wa *LPG,* bali ni pamoja na upande wa matumizi ya teknolojia nyinginezo kwa ajili ya kupunguza gharama na kumrahisishia mwananchi wa kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mikakati ipo, hii tuliyoisema hapa ni michache ya *REA*. Pia tunahusisha wadau wa sekta binafsi kupanua wigo na kuhakikisha pale ambapo tumepanga kufikia

2030 kwa Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati na 2034 kwa Mpango wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, tunafikia malengo ambayo tumejipangia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Tunaishukuru Serikali kwa mpango wake mkubwa wa kusambaza umeme vijijini. Katika mwaka huu wa bajeti tumebakiza mwezi mmoja. Je, Serikali imefikia hatua gani katika kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini vilivyokusudiwa kwenye mwaka huu wa bajeti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati na miradi mbalimbali ya kuendelea kupeleka umeme katika vitongoji. Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, sasa hivi tuna mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 15 kwa kila jimbo, miradi hii inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumza, Serikali imekuja na mkakati wa kupeleka umeme katika vitongoji 20,000; na tumeshaanza awamu ya kwanza ya kupeleka umeme katika vitongoji 9,000, na kwa sasa hivi tuko katika hatua ya kuwatafuta Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba miradi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji inaendelea kwa kadiri ya namna ya miradi yenyewe mahususi ilivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Miaka yote tangu tunaanza kutumia mitungi ya gesi, midogo na mikubwa bei imekuwa kati ya shilingi 22,000/= na shilingi 25,000/=; shilingi 50,000/= na shilingi 60,000/= ile mitungi ya kilo 15. Ni lini hiyo unayoiita ruzuku ya Serikali imeanza kutumika kama hatujawahi kuona upunguzaji wa bei ya hii mitungi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali hilo hilo, je, kwa nini kusiwe na bei elekezi kwamba baada sasa ya ruzuku iuzwe kwa kiwango hiki tofauti na ilivyo sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mitungi ambayo amesema bei yake ni bei ya kujazia, mtungi wenyewe ule mdogo unajazwa kati ya shilingi 22,000 mpaka shilingi 25,000, lakini bei yenyewe halisi ya kununua pamoja na mtungi ni zaidi ya shilingi 45,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ambacho imekifanya sasa hivi ni kupunguza gharama ya matumizi kwa mtumiaji wa kwanza. Kwa hiyo, mitungi hii ambayo inaenda 452,000 mwananchi badala ya kununua, kwa maeneo ya mjini tumepeleka ruzuku takribani mpaka 25%, lakini maeneo ya vijijini ni kati ya 55% mpaka 75%. Kama mtungi ulikuwa unauzwa shilingi 45,000 ule *complete,* basi unauzwa kati ya shilingi 17,000 mpaka shilingi 21,000, ina maana ni zaidi ya nusu ya bei yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sasa hivi ruzuku ambayo tumeiweka ni kuhakikisha tunaongeza matumizi kwa mtumiaji wa kwanza, ambapo badala ya kununua mtungi kwa gharama ya 100%, basi tumepunguza mpaka gharama ya 50%. Ndiyo maana katika kila wilaya kuna mitungi takribani 3,255, kwa sababu ndiyo mkakati tunaanza na tutaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Katika maeneo ya vijijini hasa maeneo ya wafugaji, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wale wananchi kuwapelekea teknolojia ya *Biogas* au kuwajengea majiko yanayotumia samadi ya gesi ambayo ni rahisi na bei yake ni ndogo, kwa sababu haihitaji ku-*refill* mitungi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi kupitia wenzetu wa Umoja wa Ulaya, kupitia Mfuko wa *UNCDF* ambao una teknolojia hizi nyingine, kwa mfano kama *Bioethanol*; pamoja na *Biogas*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaangalia kwa umahususi eneo hili la wafugaji kuona na wenyewe wananufaika na mradi huu ambao unafanyika katika maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Nyang'hwale ina shule za sekondari zaidi ya 19, na sekondari 12 ni za *boarding* na wanatumia kuni nyingi sana kwa siku, na kuharibu misitu yetu. Je, Serikali iko tayari kwenda kuwafungia mitungi ile mikubwa ya kilo zaidi ya 1,000 kila sekondari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunao mpango wa kufunga nishati safi ya kupikia katika taasisi za umma kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI. Kwa hiyo, kadiri ambavyo tutaendelea, kwa sababu taasisi hizi tunapata miongozo ya wenzetu TAMISEMI, basi tutaendelea kuangalia namna ambavyo kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tunaweza kufikia taasisi hizo ambazo zipo katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwashauri wenzetu hususan katika halmashauri ambazo zina mapato ambazo zinaweza kufunga mifumo hii. Tunaendelea kuwashauri watumie mapato ya ndani kwa ajili ya kufanya hivyo, kwa sababu kiuhalisia inapunguza sana matumizi hata kwa shule yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anaweza akaangalia katika halmashauri yake, kama watakuwa

wana mapato kidogo, basi anaweza akamshauri Mkurugenzi wakaanza kwa baadhi ya sekondari vilevile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema Migilla.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina swali dogo la nyongeza. Wakati zoezi la ugawaji wa hii mitungi ya majiko madogo ya gesi ukiendelea, kulikuwa kuna kigezo cha kila anayetaka lazima awe na namba ya *NIDA* ndipo atauziwa kwa bei ya ruzuku. Sasa Je, hiki kigezo cha kuwa na *NIDA* ambapo wananchi wengi hawana, Serikali imejipangaje ili hawa wananchi wetu waweze kupata kwa urahisi zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi ambalo linaendelea, kwa kweli kwa kiasi kikubwa changamoto hii siyo kwa ukubwa huo, kwa sababu, katika kila wilaya tuna idadi mahsusi ya mitungi, na katika kila wilaya kwa kweli zoezi limeenda kwa haraka na baadhi ya wilaya mitungi imeisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoendeleza mkakati huko mbeleni nina uhakika wenzetu wenye mamlaka ya suala hilo watahakikisha kuwa zoezi hilo linakuwa endelevu na linafanyika kwa kasi ili wananchi waendelee kunufaika na fursa hizi ambazo zinahitaji vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwa sisi kufanya hivyo kwa sababu, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakitushauri hapa mara nyingi, kuhakikisha kwamba fursa hizi zinamfikia mwananchi mmoja, mmoja. Kwa maana ya udhibiti, hiyo ni moja ya njia nzuri kabisa ya hata sisi kuweza kutufanyia ufuatiliaji, kwa sababu tunakuwa tuna *database* ya mwananchi ambaye tumempa mtungi. Vilevile inaturahisishia ufuatiliaji, kuweza kujua mtungi ule umemfikia mtumiaji wa mwisho na kama ameujaza ama hajaujaza kwa maana ya zoezi la tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunaendelea kuboresha na wenzetu wa mamlaka husika wataendelea kuboresha kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwafikia wananchi wengi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, lini Serikali itaendeleaa na uuzaji wa mitungi hii ya ruzuku kwa baadhi ya wananchi; kwani sasa hivi baadhi ya wananchi wamekuwa wakifuatilia lakini hawapati mitungi hiyo kwa sababu imekuwa ni haba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeshasema katika swali la msingi, Awamu hii ya Kwanza ilihusisha mitungi takribani 452,445. Mkakati huu ni endelevu, Serikali inaendelea kujipanga kwa namna bora ya kuendeleza ruzuku ili kuweza kuwafikishia wananchi wengi zaidi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mitungi hii na miradi hii inaendelea, ni endelevu, na huko mbeleni wananchi wengi wataweza kunufaika zaidi.

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, ahsante sana, tunakushukuru sana kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali sasa aulize swali lake.

Na. 394

**Kujenga Maeneo ya Uvuvi Mbarali**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga maeneo rasmi ya Uvuvi kwa ajili ya Wavuvi Wilayani Mbarali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya uvuvi katika Wilaya ya Mbarali yapo kwenye Mto Ruaha ambao upo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha inayosimamiwa na Sheria za Uhifadhi. Kwa muktadha huo, kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi haina mpango wa kujenga miundombinu ya uvuvi kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuzingatia kuwa wakazi wengi wa Wilaya ya Mbarali wanajihusisha na shughuli za ufugaji samaki, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga kujenga shamba darasa la ufugaji samaki katika Kijiji cha Mwakaganga kilichopo Kata ya Ubaruku Wilayani Mbarali, ambapo lengo la shamba darasa hilo ni kutoa mafunzo kwa vitendo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki kwa wananchi wa Wilaya ya Mbarali. Hatua hii inatarajiwa kuwezesha ufugaji wa samaki wenye tija na manufaa kwa kuongeza upatikanaji ajira, kipato, lishe bora na kukuza uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Mbarali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi, pia ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Tunafahamu kuwa nchi nyingi ambazo zinalima mpunga wamekuwa wakitumia majaluba ya mpunga kuweza kufuga Samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanatoa elimu kama ambavyo nchi nyingine zinafanya na kutoa mbegu za muda mfupi ambazo zitaendana kwa msimu huu wa kilimo ili wakulima wa Mbarali wanavyolima waweze kuvua na Samaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunafahamu kuwa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inakwenda kutuchimbia

mabwawa saba Mbarali. Je, Wizara ya Mifugo na uvuvi, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, ina mkakati gani ili mabwawa haya yanavyokamilika, pamoja na kwamba yanakwenda kumwagilia mpunga, lakini vilevile yaweze kutumika kwa ajili ya uvuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kutimia majaluba kama sehemu ya ufugaji wa samaki ni kweli linatumika duniani kote. Ukienda Thailand, China, na Singapore wanatumia utaratibu huo, kwamba, mfugaji anaweza akatumia jaluba lake ambalo analima mpunga, akapandikiza vifaranga vya samaki na baadaye akapata matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, na ndiyo maana katika jimbo la Mheshimiwa Bahati tumetenga fedha kwa ajili ya kwenda kutenga shamba darasa ambalo litasaidia kutoa hiyo elimu ya namna gani tunaweza tukatumia majaluba hayo kwa ajili ya uvunaji wa Samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimkakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tayari tumeshalifanyia kazi, na tuko tayari kama Wizara kwenda hapo kufanya hiyo kazi ya kutoa elimu kwa wafugaji wetu na baadaye wafugaji wa samaki katika eneo hilo watapata faida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hili la pili la kutumia mabwawa ambayo yanajengwa na Wizara ya Kilimo, ni kweli, Wizara ya Kilimo ina mkakati wa kujenga mabwawa makubwa kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji, na sisi katika mabwawa hayo, kila bwawa ambalo linajengwa na Wizara ya Kilimo, tunapandikiza mbegu kwa ajili ya uvunaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mabwawa hayo ambayo yatajengwa katika Wilaya ya Mbarali tutakwenda kupandikiza samaki na mabwawa hayo yatakuwa na kazi ya kumwagilia, pia kuzalisha samaki katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi.

**MHE. *PROF.* PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wa Bwawa la Nyumba ya Mungu wana uhitaji mkubwa sana wa vizimba na mbegu bora za samaki. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kusaidia wavuvi hawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali hili amekuwa akilifuatilia sana hata Wizarani na namna ambavyo amekuwa akifuatilia uwekezaji mkubwa wa vizimba katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara bado inafanya utafiti katika Bwawa la Nyumba ya Mungu kuona, je, vizimba zinaweza kukaa maeneo hayo ama haviwezi? Kwa sababu, vizimba navyo pia havikai kila mahali, uko utaalamu wa kisayansi ambao ni lazima tujiridhishe kwamba vizimba hivi tukivipeleka vitakuwa na tija kwa wananchi wetu au lah.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mara tu utafiti utakapokamilika tupo tayari kupeleka vizimba katika maeneo hayo pamoja na kuwapa elimu wananchi wote wanaozunguka maeneo hayo ili Bwawa la Nyumba ya Mungu liwe na tija katika mazingira yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Mathayo.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba umeonekana kuwa na manufaa makubwa sana kwa wananchi wetu, lakini sasa katika kipindi kisichopungua

miaka mitatu, mfano pale Musoma ni vizimba 33 pekee ndivyo vimetolewa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inaleta vizimba vya kutosha ili watu wetu waendelee kupata ajira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vizimba vilivyokwenda katika Mkoa wa Mara hususan Wilaya ya Musoma Mjini, ni vichache. Kwa awamu ya kwanza tumeshapeleka vizimba hivyo ambavyo tumepeleka kwa wananchi wetu na wanaendelea vizuri na wengine wameshaanza kuvuna. Tayari sasa tunaingia kwenye awamu ya pili ambayo tumeanza wiki iliyopita kugawa vizimba vingine tena kwa awamu nyingine ili kuwanufaisha wavuvi wetu wanaozunguka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafika Musoma. Kwa hiyo, yale maombi ya wananchi wake ambayo wameomba vizimba, tayari tunavyo na tumeshafanyia *assessment* na tayari Benki ya *TADB* wameshakaanao, wameshakubaliana nao na wengine wameshasaini na mikataba, tutaleta vizimba vingine kwa awamu hii ya pili. Pia, tutaendelea kufanya *assessment* juu ya wale ambao wana uhitaji, tutaenda kuwaongezea pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya mwezi huu tutagawa vizimba vingine tena Musoma, Mwanza na kama ambavyo tumefanya Geita, maeneo ya Chato tumeshapeleka vizimba vingine kwa awamu hii ya pili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali hili liliulizwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo. Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ufugaji wa samaki kwenye vizimba umekuwa na tija sana kwa vijana hasa ambao wamechukua mikopo kwa ajili ya kufuga samaki. Wilaya ya Ilemela ilibahatika kupata vizimba 56, lakini

kuna changamoto ambayo imejitokeza sasa, kuna wawekezaji wanakuja kuwekeza, wanagombea mipaka katika maji na wale wenyeji waliopo. Je, Serikali ina mpango gani kuwapa maeneo ambayo yanakuwa yamepimwa ili kila mmoja aweze kupata eneo lake na wasiingiliane katika ufugaji huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii ndiyo kwanza tunaisikia sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tunaomba baada ya Bunge hili Tukufu, basi tutafanya mawasiliano na Mheshimiwa Mbunge tuone namna ya kwenda kusuluhisha ugomvi wa mipaka katika ziwa ndani ya wafugaji wetu wa vizimba ili kuwe na tija katika wafugaji hawa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia imefanya kazi nzuri sana ya kuchimba lambo la Kihumbu na Mheshimiwa Naibu Waziri alifika pale akaangalia lambo kwa ajili ya mifugo na Samaki. Lambo limefika 85%, ni lini sasa mtakamilisha lambo hili watu wapate huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari tumeshatenga fedha kwa ajili ya kwenda kukamilisha lambo hilo na mara tu baada ya Bunge hili tutakwenda kufanya mawasiliano na Mheshimiwa Mbunge, tuone namna nzuri ya kwenda kukamilisha jambo hili kwa sababu amelifuatilia kwa muda mrefu na sisi Wizara tumeshatenga fedha, basi ni suala tu la kumpa taarifa tumefikia wapi, na tunakwenda kufanya nini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana, ninakushukuru.

Wizara ya Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 395

**Kudhibiti Tembo Kata ya Engikaret – Longido**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuthibiti tembo waliovamia Kata ya Engikaret - Longido ili kunusuru maisha ya wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori na waharibifu, mwaka 2021 Serikali ilijenga Kituo cha Askari katika Wilaya Longido kwa lengo la kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo. Kituo hicho kina kikosi maalumu chenye Askari 18 wakiwemo Wahifadhi nane, Askari Wanyamapori wa Vijiji 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kituo kina gari moja na pikipiki nne zinazotumika kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo katika Vijiji vya Engikaret na Kiserian katika Kata ya Engikaret, Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo kufanya doria za mwitikio wa haraka ambapo kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, doria za kudhibiti matukio 34 zimefanyika katika Kata ya Engikaret.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, elimu ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu imeendelea kutolewa kwa wananchi 1,640 wa Vijiji vya Engikaret na Kiserian kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali kwa kuwa changamoto hii ya tembo kwenye Kata ya Engikaret inafanana kabisa na changamoto iliyopo kwenye Kata ya Matale 'C' Longido na miezi miwili iliyopita mwananchi mmoja aliuawa na tembo akiwa anafuata maji kwenye makazi ya binadamu. Je, Serikali haioni haja sasa kuwajengea wanyamapori hawa mabwawa ya maji mbali na makazi ya binadamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Meru maeneo yanayopakana na hifadhi ya wanyapori maeneo yote yana changamoto ya tembo kuharibu mazao yao. Je, Serikali itafanya mpango gani sasa kuwasaidia wananchi hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba changamoto katika eneo hili ni kubwa kwa sababu tunakabiliana na tembo wanaotoka kwenye hifadhi kule Kenya ya Amboseli, lakini vilevile tunakabiliana na tembo wanaotoka kwenye Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na hawa wote wanapita kuelekea kwenye hifadhi zetu maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kubaliana na changamoto hii tumefanya kikao na Mheshimiwa Mbunge wa eneo husika, na yeye ametusaidia kuainisha maeneo nane kwenye kata nane ambazo tunaweza kujenga mabwawa mbali na makazi ya wananchi. Timu yetu inafanya tathmini kuona uhalisia wa maeneo hayo ili kwa kutumia Mfuko ule wa *CSR* tuweze kujenga mabwawa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa maeneo haya akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa jimbo, wawe na subira wakati tunalifanyia kazi eneo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus Chinguile.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kudhibiti tembo katika Jimbo langu la Nachingwea, kwa sasa katika kata nane ikiwemo Mkoka, Mtua, Mbondo, Kilimarondo, Matekwe na Namapwia, Kiparamnero na Kiegei hawa wanyama tembo wamerudi kwa kasi kubwa. Je, Serikali ipo tayari sasa kuongeza nguvu ili kudhibiti tembo wasiweze kuleta athari kwenye maisha ya watu pamoja na mashamba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba miongoni mwa wilaya ambazo changamoto ya tembo ni kubwa ni pamoja na Nachingwea, na ni kwa sababu hiyo tumepeleka pale ndegenyuki mahususi katika wilaya ile ili itusaidie kufanya kazi ya kufukuza na kudhibiti tembo katika maeneo yale. Nitoe maelekezo kwa kikosi chetu kilichopo kule Kusini, kiende kikafanye kazi hii haraka sana kwenye hizi kata nane ili tuweze kuwanusuru wananchi na kadhia hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Je, kuna utafiti wowote unaofanyika kutokana labda na mabadiliko ya tabia za tembo au wanyama hawa ili kuona kama tunaweza kuishi nao kama wanavyoishi nao wengine wenzetu wa India kuliko kuendelea kuwa na mikakati ya kuwadhibiti tu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii ya mwingiliano wa

wanyama wakali na waharibifu na binadamu, Taasisi yetu ya *TAWA* imejielekeza kuhakikisha inafanya tafiti za mara kwa mara kuona jinsi ambavyo tunaweza kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyojifunza ni kwamba tembo ni mnyama ambaye anabadilika tabia zake mara kwa mara kulingana na mabadiliko mbalimbali. Kwa hiyo, wenzetu wanakuja na tafiti hizo ili kuona ni jinsi gani ambavyo tunaweza kuendelea kuishi nao, lakini vilevile kuondokana na changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo limeonekana ni kwamba pale ambapo binadamu wameacha uadui na tembo, kwa maana ya wameondokana na changamoto ya ujangili, basi ukorofi wa wanyama hawa unapungua, lakini pale wanapoona kwamba binadamu amekuwa anawawinda, na hivyo basi, na wenyewe wanakuwa *aggressive*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Jimbo la Kisesa Wilaya ya Meatu na maeneo mengine tembo wamezidi kuongezeka licha ya hii mikakati ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri analieleza Bunge, tembo wamezidi kuongezeka na kuleta athari kubwa kwa wananchi ikiwemo kubomoa nyumba zao, kumaliza mazao yao lakini kujeruhiwa na kuuawa. Je, leo Serikali inatoa tamko gani kwa Watanzania hawa ambao wanaishi maisha ya dhiki sana ya muda wote kutaka kuuawa, na nyumba zao kubomolewa na mazao yao kushambuliwa? Serikali inatoa tamko gani la suluhisho la mwisho la kumaliza tatizo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tembo wamekuwa ni changamoto kubwa, lakini kwa sababu tumebadilisha mfumo wa tulivyokuwa tukiishi nao zamani, tumekaribia sana maeneo yao, tumeingiza mifugo kwa kiasi kikubwa kwenye hifadhi zetu, hivyo kuwafanya

tembo wakatoka kwenye maeneo yao wakaja kwenye maeneo ambayo tunaishi sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebadilisha mfumo na kwa sababu hiyo, tumebadilisha aina ya vyakula walivyokuwa wakipata hifadhini, sasa wameanza kutumia vyakula ambavyo zamani walikuwa hawala, wanakula vyakula vyetu. Kwa hiyo, changamoto hii ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini tunachofanya? Kwenye maeneo haya yenye changamoto hizi, tunajaribu kutoa elimu kwa wananchi waelewe tabia za tembo ili tuache kuwavuruga kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunajenga mabwawa ndani ya hifadhi ili kuwazuia tembo wasije kutafuta maji kwenye maeneo ya wananchi; tatu, yapo maeneo ambayo changamoto kama imekuwa kubwa, tunajenga uzio wa umeme ili walau kujaribu kuzuia wasije kwenye maeneo ya wananchi; na nne, ni kutoa elimu kwa wananchi kuacha kujenga au kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya mapito ya tembo kwa sababu kwa kufanya hivyo tunawakaribisha waendelee kuishi na sisi. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuchukua jitihada mbalimbali kuhakikisha tunakabiliana na changamoto hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuku kwa kuweza kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Karatu imepakana na hifadhi kubwa mbili, Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kuna jitihada upande wa Ngorongoro inaendelea kufanyika na nyingine ipo kibajeti, lakini kuna huu upande ambao unapakana na Ziwa Manyara, kuna vijiji vya Endallah na Getamock, kuna changamoto kubwa sana ya tembo kuvamia makazi ya watu na kuharibu mazao, lakini hakuna kituo hata kimoja cha maaskari. Je, Serikali kwa

hatua za haraka, ipo tayari sasa kuweka vituo pale ili wananchi hawa waweze kuishi kwa amani katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali siku zote ipo makini kuhakikisha kwamba inalinda uhai wa wananchi. Kufuatia ushauri huu ambao umetolewa na Mheshimiwa Mbunge, tunaupokea, tutaufanyia kazi tuone jinsi ambavyo tunaweza kushughulikia jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunajua tembo wana faida sana, lakini tembo wanatuletea madhara makubwa katika maeneo yetu ambayo wananchi wanaishi kwa sababu tembo wanauwa watu, tembo wanakula mazao ya wananchi na hatimaye kusababisha hata umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba tembo wamebadilisha mienendo, wameacha kula vyakula vyao vya asili na sasa hivi wanakula vyakula hivi ambavyo wanadamu wanakula. Je, nini mkakati wa Serikali kwenda kuelimisha wananchi aidha wasilime yale mazao ambayo yanawavutia hawa wanyama tembo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunaona mabadiliko ya jinsi ambavyo tembo sasa wanakula aina ya mazao ambayo kiasili siyo mazao waliyokuwa wanakula, na hili ni kwa sababu tumevamia maeneo yao ndani ya hifadhi wakatoka nje kuja kwenye maeneo yetu, wakaonja vyakula tunavyotumia sisi. Kwa lugha ya mtaani, wamenogewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jitihada tunayofanya kwanza ni kuwaelimisha wananchi tuache kuingiza mifugo

hifadhini, tuache kwenda kufanya shughuli za kibinadamu karibu na hifadhi; shughuli ambazo zitawavutia tembo hawa kuja kwenye maeneo yetu na kuanza kula vyakula ambavyo kiasili siyo vya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tunajenga mabwawa ndani ya hifadhi ili kuhakikisha tembo hawa wanapata maji ndani ya hifadhi, wasitoke kwenye maeneo. Sasa wakati tunafanya jitihada hizi, vilevile, jitihada za kutoa elimu kwa wananchi ili kujua changamoto hii tunayokabiliana nayo na jinsi ambavyo tunaweza kuiepuka itakuwa inaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, aulize swali lake.

Na. 396

**Uandikishaji wa Vitambulisho vya *NIDA***

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, zoezi la uandikishaji wa Vitambulisho vya *NIDA* ni endelevu ukizingatia kila mwaka kuna vijana wanaopata sifa ya kuandikishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Sillo, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la usajili na utambuzi wa wananchi kwa ajili ya Kitambulisho cha Taifa ni endelevu na linafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Usajili na Utambuzi ya Mwaka 1986 na marejeo ya mwaka 2014. Aidha, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imepewa jukumu hilo la kisheria la kusajili,

kuwatambua na kuwapatia Vitambulisho vya Taifa wananchi wote waliokidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Busanda lenye kata 22, *NIDA* imefanikiwa kusajili na kuwatambua wananchi 197,758 sawa na 86.1% ya watu 229,621 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea; kutoa Namba za Utambulisho 175,762 sawa na 88.8% ya watu waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi la usajili mwaka 2016 pamoja na kuzalisha Vitambulisho vya Taifa 168,361 sawa na 95.78% ya *NIN (National Identification Number)* zilizozalishwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwamba zoezi hili ni endelevu, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa zoezi hili ni endelevu, je, Serikali haioni ni muda mwafaka sasa kuliboresha zoezi hili ambalo litakuwa linaandikisha vijana wengi wanaofikisha miaka 18 wanaotimiza masharti sasa liratibiwe kutoka vile vile kwenye shule na vyuo mbalimbali ambapo watakuwa wanahitimu kila mwaka wakitimiza masharti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa kuna vitambulisho ambavyo vimeshapelekwa huko kwa sababu vilichelewa kwenda, na sasa kuna mahali wananchi wamehama, na kuna wengine wamepoteza maisha, je, kuna mkakati gani kwenye vitambulisho ambavyo sasa vimejaa kule na havina mtu ambaye anavipokea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *NIDA* imekuwa ikiwasajili na kuwatambua watu wenye vigezo kwanza miaka 18 na kuendelea, lakini wenye vigezo na sifa katika mitaa, shehia pamoja na vijiji hapa nchini. Zoezi hili limehusisha pia shule ambazo zipo kwenye maeneo hayo na wanafunzi waliotimiza miaka 18 na kuendelea pia wamekuwa wakisajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa tunaenda kwenye mpango wa kutoa kwa jamii namba ambayo ni kuanzia mtu anapozaliwa, hili jambo likishaanza, basi litagusa wanafunzi wote ambao wapo shuleni wa kuanzia miaka 17 na kurudi chini ili kuhakikisha kwamba sasa wanafunzi wote ambao wana vigezo wanapata usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kwa vitambulisho ambavyo tayari vimeshazalishwa na wenyewe hawajulikani, *NIDA* imekuwa ikiwashirikisha viongozi wa mitaa, wa vijiji na shehia hapa nchini kuhakikisha kwamba inawajulisha wale wote ambao vitambulisho vimefika ili iwapatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pia Serikali imekuwa ikituma *message* fupi kwa njia ya simu kwa wale wote ambao vitambulisho tayari vimeshazalishwa ili waende kuvichukua tayari kwa matumizi mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 397

**Kutokomeza Magonjwa ya Michungwa Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kutokomeza magonjwa ya michungwa Wilayani Kilwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao ikiwemo zao la michungwa na maembe. Katika kufanikisha hilo, Serikali imegawa viuatilifu mbalimbali ikiwemo kivutia wadudu cha *Methyl Eugenol* kwa Wilaya ya Kilwa kwa ajili ya kudhibiti inzi wa matunda *(fruit fly)* wanaoshambulia matunda ya machungwa, maembe na matunda mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania inaendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora ya viuatilifu katika kilimo cha matunda ili kuongeza tija na uzalishaji. Aidha, niwatake wananchi kupitia halmashauri zao, kutoa taarifa za milipuko ya visumbufu ili Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania *(TPHPA)* kufanyia kazi kwa haraka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE.FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza nitoe pongezi kwa Serikali yetu kwa kuanzisha hii Taasisi ya Afya ya Mimea na Viuatilifu ambayo hivi karibuni ilikuja kutusaidia Kilwa kwa ajili ya kukabiliana na baa la senene waharibifu kwa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza la nyongeza: kwa kuwa magonjwa ya mimea yamekuwa yakitokea mara kwa mara hasa kwa zao la michungwa, minazi pamoja na ufuta, je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuweza kufungua kituo cha kuhudumia ukanda wote wa kusini ili kuweza kupambana kwa urahisi na kadhia hizi za magonjwa ya mimea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwamba Serikali imejipanga vipi au ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inaleta mbegu bora za mimea ya machungwa na minazi

ambayo ina tija kibiashara na kwenye upande wa lishe ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaibuka kiuchumi kupitia mazao haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye swali la kwanza la nyongeza la kuwa na kituo kwenye ukanda wa kusini, hili tunalichukua tukafanye tafiti mbalimbali zitakazowezesha mazingira ambayo tunaweza kuwekeza kwenye tafiti hizi na vituo vya kutolea elimu kwa ajili ya watu wanaohusika na masuala ya kilimo cha mazao ya matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu bora, hili tunalichukua, na tuna taasisi ambazo zinafanya kazi za utafiti wa mbegu bora za matunda, na hizi tutazielekeza kwenda huko kwa Mheshimiwa Ndulane kuona uwezekano wa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mbegu bora, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate Mbunge wa Kyerwa.

Na. 398

**Soko la Uhakika la Vanila**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia soko la uhakika Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa wanaolima zao la Vanila?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kutafuta soko la vanila kwa wakulima, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha taratibu za afya ya mimea ili kufungua soko la vanila China; na kukamilisha Mwongozo wa Usimamizi wa Tasnia ya Vanila nchini utakaosaidia wakulima kuzalisha vanila yenye ubora utakaokidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara imeandaa taarifa fupi yenye takwimu za vanila nchini *(Tanzania Vanilla Fact Sheet)* na kuwasilisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kusambaza katika Ofisi za Balozi mbalimbali ikiwa ni jitihaha za kuendelea kutafuta masoko ya nje ya zao hilo. Aidha, imeendelea kuhamasisha wakulima wa vanila kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili kufanya maamuzi ya pamoja, kuongeza ushirikiano na kupata masoko ya uhakika kwa mazao yao na kuboresha hali zao za maisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na juhudi za Serikali za kuwatafutia soko la uhakika wakulima wa vanila Wilayani Kyerwa bado wakulima wengi hawana ujuzi katika kilimo cha vanila. Je, Serikali iko tayari kwenda Kyerwa kuwapatia elimu wakulima wa vanila?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Serikali iko tayari kuwapeleka wataalamu Wilayani Kyerwa ili kukabiliana na ugonjwa wa mnyauko ambao unashambulia zao la vanila?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kweli kwa kufuatilia uimarishwaji wa uzalishaji wa zao la vanilla. Kuhusu ujuzi Wizara inaandaa wataalam watakaokwenda huko Kyerwa kwa ajili ya kuendelea kuwapa wananchi elimu kuhusu namna ya

maboresho ya kilimo hiki cha vanilla ambacho kwa kweli kwa ubora wake ni zao muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ikumbukwe kwamba zao hili lilikuwa linakwenda mpaka kwa kilo moja linauzwa laki moja katika soko la Dunia, na sasa kutokana na jinsi ambavyo maboresho yake yamepungua, sasa limerudi mpaka shilingi 3,000 kwa kilo kitu ambacho lazima Serikali ichukue hatua za haraka kuwasaidia wakulima hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ugonjwa wa mnyauko, Mheshimiwa Mbunge taasisi inayoshughulika na tafiti za magonjwa itachukua hatua za haraka ili kuja huko kwako ili kuona namna ya maboresho ya kuwasaidia wakulima kutambua namna ya kukabiliana na magonjwa haya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama ilivyo shida kwenye zao la vanila kupata soko, ni lini Serikali itawekeza nguvu kwenye zao la kahawa katika Wilaya ya Rungwe kwa maana wananchi wanaendelea kulima, lakini bei hiyo imekuwa chini sana. Ni lini mtatusaidia kuweza kupata bei ya juu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tulikuwa tunazungumzia suala la vanila, sasa limekuja swali la kahawa, una hiari ya kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani jana ulikuwa msikilizaji mzuri sana wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho. Alieleza kwa kina kuhusu namna mikakati ya Wizara ilivyo kwa sasa wanavyojipanga katika kupandisha thamani ya mazao yetu ambayo kimsingi ni ukombozi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bei ya kahawa kule Rungwe, Wizara kama ilivyojieleza kwenye hotuba yake ya bajeti jana, ina mikakati ya kwenda kuhakikisha kwamba zao hili linapata thamani, na Mheshimiwa Mwakagenda naomba uvute subira kidogo, wananchi watakwenda kunufaika na hiki ambacho Serikali imejipangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake.

Na. 399

**Upungufu wa Vitabu vya Kufundishia katika Shule za Sekondari – Mwibara**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaondoa tatizo la upungufu wa vitabu vya kufundishia katika shule za Sekondari Mwibara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ikiwemo vitabu vya kiada. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imechapisha jumla ya nakala 9,902,102 za vitabu vya kiada pamoja na Kiongozi cha Mwalimu. Vitabu hivyo vinahusisha shule zinazotekeleza mkondo wa amali ambazo zimesambaziwa vitabu kwa uwiano wa moja kwa moja, na shule zinazotekeleza mkondo wa jumla, ambazo zilisambaziwa vitabu kwa uwiano wa moja kwa moja na moja kwa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Bunda ina jumla ya wanafunzi 44,484 na usambazaji wa vitabu kwa Kidato cha

Kwanza mwaka 2025 imesambaziwa jumla ya vitabu 23,019 kwa masomo ya sayansi  na vitabu hivyo vimegawanywa kwa uwiano wa moja kwa moja na kwa masomo mengine yasiyo ya sayansi vitabu hivyo vimesambazwa kwa uwiano wa moja kwa mbili, moja kwa tatu, na moja kwa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nimeridhika na majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo aulize swali lake, kwa niaba Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Na. 400

**Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama za Mwanzo – Kalambo**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kasanga utaanza pamoja na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo Mwazye na Mwimbi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Aidha, majengo hayo yamejengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia mpango huo kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2024/2025 ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo 72 na Mahakama za Wilaya 15 unaendelea katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Kalambo na Jengo la Mahakama ya Mwanzo Kasanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo unatarajia kukamilika mwaka fedha 2025/2026 na sasa hatua za kuuhuisha zinaendelea. Majengo ya Mahakama ya Mwanzo Mwazye na Mwimbi yatajumuishwa katika mpango huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Serikali. Pia nashukuru kwa ujenzi huo wa mahakama uliyoanza. Pamoja na shukrani hizo, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mahakama za Mwanzo za Wilaya ya Kalambo zimechakaa, nini mkakati wa Serikali wa kukarabati Mahakama hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba Mahakama hapa nchini imeendelea na utaratibu wake wa kukarabati Mahakama ambazo ni chakavu, na hivyo nikuahidi kwamba Mahakama zilizoko Kalambo zilizochakaa zinakwenda kurabatiwa katika kipindi cha fedha ambacho ni cha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba sasa aulize swali lake.

Na. 401

**Utoaji Holela wa Vyeti vya Vifo**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU K.n.y. MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti utoaji holela wa Vyeti vya Vifo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa vifo vinavyotokea kwenye vituo vya tiba, husajiliwa katika vituo husika na Kibali cha Mazishi hutolewa ambacho humwezesha mwananchi kupata cheti kwenye ofisi ya Wilaya husika. Vilevile, vifo vinavyotokea nje ya vituo vya kutolea huduma za tiba, huthibitishwa na Afisa Mtendaji wa Kata ambapo mhusika atatakiwa kuwasilisha maombi yake na cheti hutolewa wilayani au Ofisi ya *RITA* Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu wa utoaji wa vyeti vya vifo kupitia kifungu cha 17 (2) cha Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 kinachobainisha kuwa cheti hicho kitatolewa kwa mwenza aliye hai na kama hayupo, cheti hicho kitatolewa kwa mtoto au ndugu wa marehemu baada ya kuthibitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa wananchi kutoa taarifa mara wanapogundua kuwa utoaji holela wa vyeti vya vifo ili hatua stahiki zichukuliwe kwa haraka kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU K.n.y. MHE. ISSA J. MTEVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mwuliza swali la msingi, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ushahidi wa taasisi ya *RITA* kutoa vyeti viwili kwa marehemu mmoja ambavyo vimeleta sintofahamu katika uendeshaji wa kesi. Je, Serikali iko tayari kufuatilia na kuondoa tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kuna watumishi wanaofanya hujuma hizi kwa makusudi, je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi wa kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaofanya hujuma hizi kwa makusudi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wale ambao watabainika kwenda kinyume na utaratibu wa utoaji wa hizi hati hatutasita kuchukua hatua, lakini suala la ufuatiliaji wa tukio la vyeti viwili kutolewa kwa kifo kimoja, nalo hili tunalichukua na tunakwenda kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naleta kwenu matangazo ya wageni waliopo Bungeni.

Kwanza tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndugu Issa Mwazembe, Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa na Katibu wa Seneti Mkoa wa Mbeya na Ndugu Nsollo Mlozi, Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Kilimo Benki ya *NMB,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni Profesa Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Dkt. Edwin Mhede, Naibu Katibu Mkuu Uvuvi; Ndugu Abdul Mhinte, Naibu Katibu Mkuu Mifugo; Balozi Dkt. Azizi Mlima, Mwenyekiti wa Bodi ya Ranchi ya Taifa *(NARCO);* Ndugu Mark J. Tsoxo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Mafunzo ya Mifugo Tanzania *(LITA);* na Profesa Sebastian Chenyambuga – Mwenyekiti wa Bodi Taasisi ya Utafiti wa Mifugo *(TALIRI)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Profesa Esron Karimuribo – Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari wa Wanyama Tanzania *(TVA);* Dkt. Florens Turuka, Katibu Mtendaji, Ofisi ya Rais Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Chakula na Kilimo; Bwana Geofrey Kirenga, Mjumbe wa Baraza la Kumshauri Rais Masuala ya Chakula na Kilimo; Dkt. Stella Bitanyi, Mtendaji Mkuu Wakala ya Maabari ya *Veterinary* Tanzania; Dkt. Pius Lazaro Mwambene, Wakala wa Mafunzo ya Mifugo *(LITA);* na Ndugu Mohamed Zuberi, na Meneja Mkuu Kampuni za Rachi za Taifa *(NARCO)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu John Chasama, Msajili Bodi ya Nyama Tanzania; Profesa George Msallya, Msajili Bodi ya Maziwa Tanzania; Profesa Erick Komba, Mtendaji Mkuu Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania; Dkt. Ismael Kimirei, Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Uvuvi *(TAFIRI);* Dkt. Semvue Mzighani, Mkurugenzi Mkuu Wakala wa Elimu ya Mafunzo ya Uvuvi *(FETA); CPA* Shaibu Matessa, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO),* na Ndugu Davis Mpotwa, Meneja Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Emanuel Sweke, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu; Dkt. Dafay Bura Buay, Mkuu wa Kituo cha Uhimirishaji Arusha; Mheshimiwa Meck Sadick, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya *SAMEKI Limited,* na Mkuu wa Mkoa Mstaafu; Mheshimiwa Fatma Nyangasa, Mkuu wa Wilaya ya Kondoa; na Ndugu Shaban Milao, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Kondoa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Kijaji ni familia yake kutoka Dodoma ni Dkt. Muhajir Kachwamba, mume wa Mheshimiwa Dkt. Kijaji. Karibu sana shemeji yetu, karibu Bungeni. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Samirah Muhajir Kachwamba, mtoto wa Mheshimiwa Dkt. Kijaji, karibu sana. *(Makofi)*

Aidha, tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Kijaji, Mbunge na Waziri ambao ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi

na Maafisa kutoka Wizara na Taasisi zake. Wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 16 wa Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Viongozi wa Chama na Serikali kutoka Kata ya Mtera, Jimbo la Kibakwe, Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma. Karibuni sana viongozi wetu, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake na Makundi Maalumu kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ambaye ni Ndugu Jacob Kateri, mjasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Esther Nicholus Matiko ambaye ni dada yeke, Ndugu Emmy Lema kutoka Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro ambaye ni *MC* maarufu sana pale Kilimanjaro. Popote alipo, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo ambaye ni Ndugu George Grace Msemo, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Katoliki Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani ambaye ni Ndugu Mohamed Manzi, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ambaye ni Ndugu Joel Kilowoko, mtoto wake kutoka nchini Uingereza. Karibu sana kijana wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni wapigakura wake kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro, wale

wageni wa Kilimanjaro. Simameni kama mpo, ahaa, yuko mmoja ahsante, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambao ni Viongozi wa Chama cha Wafugaji Tanzania kutoka Bunda, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaye Sheikh Ahmed Mohamed Kandauma kutoka Jijini Dar es Salaam; tunaye Ndugu Francis Mafuru na mama yake mzazi Ndugu Graceana Mauna kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Mkoa wa Mara, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wanne kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; tunao wanachama saba wa Kikundi cha *Shine Sisters* kutoka Wilaya ya Chamwino, Mkoani Dodoma; tunao wanafunzi 71 na walimu 11 wa Shule ya Msingi *Buyegi Archbishop* Malya kutoka Mkoani Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 40 wa Shahada ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; tunao wanafunzi 25 na walimu wanne wa Kituo cha Huduma ya Mtoto na Kijana kinachosimamiwa na Kanisa la *Tanzania Assembly of God* kutoka Dakawa, Mkoani Morogoro; na pia tunao wanafunzi 100 na walimu sita wa Shule ya Msingi *Maria De-Mathias* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sehemu inayofuata itaongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpishe.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**23 MEI, 2025**

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyochambua na kushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2024/2025, sasa naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Ukarimu, kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Mbili, ikiwa ni Mkutano mahsusi wa Bunge wa kuamua mambo yenye mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutimiza kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, na kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pongezi zangu za dhati kwa viongozi Wakuu wa Serikali, akiwemo Mheshimiwa Dkt. Philip

Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati na Mbunge wa Jimbo la Bukombe, kwa utendaji wao wa kizalendo na uliotukuka ambao unamwezesha Mheshimiwa Rais na kipenzi cha Watanzania kuendelea kutoa mchango wake muhimu kwa maendeleo na ujenzi wa Taifa letu na hivyo kumfanya ang'are kiuongozi katika duru za Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar, Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na kwa niaba ya wavuvi na wafugaji wote nchini napenda kuwaahidi kuwa tutaendelea kuwaunga mkono katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Profesa Mohamed Janabi kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika. Ninamtakia kila la heri katika majukumu yake mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo ni moja ya sababu zilizofanya aaminiwe na kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, ikiwa yeye ni mwanamke wa kwanza kutoka katika Bara la Afrika na mwanamke wa tatu duniani kushika nafasi hiyo yenye majukumu makubwa na madaraka mazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninakupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ilala, kwa kuendelea kumsaidia kwa umahiri na weledi mkubwa Mheshimiwa Spika katika kuendesha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuongoza Kamati zao katika kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kwa kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati na Sekretariati ya Kamati hii kwa kufanya uchambuzi makini wa Bajeti yetu. Ushauri wao umewezesha Wizara kufanya maboresho stahiki na ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika, unayo Kamati ambayo ni msaada mkubwa kwetu na kwa Taifa letu. Kwa upande wetu, tunaahidi kuendelea kuipatia Kamati yetu ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi na ushauri ili kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutumia fursa hii adhimu kumshukuru kwa dhati mdogo wangu, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mbunge wa Jimbo la Misungwi, kwa umahiri wake mkubwa wa kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake mzuri na wa kizalendo na ubunifu. Hakika ushauri wake una tija kubwa ambao umetusaidia sote kwa pamoja kufanya maboresho yenye tija ya usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Napenda kuwaambia wananchi na hasa Wajumbe wa Mkutano Mkuu kule Jimbo la Misungwi, walipata mwakilishi muhimu na makini sana. Waendelee kumshikilia, kazi yake ni njema sana *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza wataalam wetu wakiongozwa na Prof. Riziki Silas Shemdoe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ni Katibu Mkuu ambaye amevunja historia ya wengi, kwani ni Katibu Mkuu ambaye amehudumia Wizara akiwa na Mawaziri Nane, akiwa na Makatibu Wakuu Kumi, lakini yeye yuko pale pale. Ni Katibu Mkuu mchapakazi, anaifanya kazi yake nzuri sana ya ushauri na kiutalaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia Ndugu Abdul Rajab Mhinte, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulika na mifugo; na Dkt. Edwin Paul Mhede, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulika na Uvuvi. Hawa ndio nguzo ya Prof. Shemdoe, na wanamsaidia kazi vizuri sana kwa kuwa viongozi hodari na wabunifu na Watendaji wazuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara na kuwasimamia Watalaam wetu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru sana watumishi wote Wizarani kwa utendaji na ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yangu ambayo muda mwingi nipo nje ya nyumbani, isingekuwa rahisi bila maombi na dua njema kutoka kwa wapendwa wangu wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, namshukuru sana baba yangu Almaruhum Alhaji Abdallah Kijaji, alituaga wanae tarehe 10/5/2025 saa tisa na dakika tano mchana. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa maisha ya baba yangu na dua zake njema kwangu hadi akiwa kwenye kitanda chake cha umauti akiupambania uhai wake. Nashukuru sana kwa baraka zake alizoniachia na kunipa nafasi ya kumuuguza na hadi kumpumzisha kwenye bustani yake ya milele. Mwenyezi Mungu amrehemu na amjaalie kaburi lake kuwa moja ya mabustani ya Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mama yangu mpendwa *Hajat* Aziza Selemani, nasema ahsante kwa malezi yake na dua zake njema kwangu. Namwombea sana kwa Mwenyezi Mungu amjaze subra na aupokee huu msiba mzito, mume wake kipenzi kwa shukurani kuu kwa Mwenyezi Mungu. Unajua vile ambavyo bado mie mwanao nakuhitaji sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana mume wangu kipenzi, Dkt. Muhajir Kachwamba na watoto wangu wapendwa, Samirah na Aboubakar. Nimpongeze binti yangu Samira, hongera kwa umri wako mdogo umemaliza *degree* yako ya pili ya uchumi na sasa ndani ya nyumba yetu tunazo degree kumi za Uchumi. Hongera sana binti yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze pia mwanangu Aboubakar, leo ameingia kwenye mtihani wake wa Kidato cha Sita, mtihani wake wa mwisho namwombea kwa Mwenyezi Mungu afanye vyema na afuate nyayo za baba yake. Nasema ahsanteni sana kwa upendo, uvumilivu na utayari wao unaonipatia ari ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo, uzalendo na weledi wangu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninawashukuru sana viongozi wangu wa dini, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kuendelea kuniombea kwa Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema iliyoniwezesha kuendelea kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwaahidi Watanzania wote kwa ujumla, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uzalendo mkubwa na kutanguliza mbele maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia mchango wa sekta binafsi unaojumuisha wawekezaji wakubwa na wadogo wakiwemo wafugaji, wavuvi, wakuzaji viumbe maji, wachakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi, wahifadhi wa mazingira na ikolojia na wadau wengine wote waliopo katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo, taasisi za kifedha, na asasi zisizo za kiserikali kwa kuendelea kutuunga mkono katika harakati za kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Tunawashukuru sana na tunaahidi kuendelea kuwahudumia na kushirikiana nanyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukiendelea na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya viongozi na wanasiasa wakongwe ambao ni Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani, Ukanda wa Afrika; Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema, aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji wa Mahakama Kuu; Mheshimiwa Balozi Juma Volter Mwapachu, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Tabitha Siwale, aliyewahi kuhudumu katika nafasi ya Mbunge na Waziri wa kwanza mwanamke Tanzania. Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, aliyewahi kutumikia Taifa letu kwa nafasi ya Mbunge, Mkuu wa Mkoa na Waziri katika Wizara mbalimbali; na Mheshimiwa Cleopa David Msuya, aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika na Wabunge, familia, ndugu, jamaa na marafiki na Watanzania wote walioguswa na misiba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 23 Januari, 2025 kulitokea upepo mkali ndani ya Ziwa Rukwa, ambapo wavuvi wetu 540 walifikwa na maafa. Kati ya hao, wavuvi 531 waliokolewa, kutibiwa na kupona; na wavuvi tisa walifikwa na umauti. Tunashukuru juhudi za pamoja baina ya vyombo vya Serikali na wananchi wenyewe wakiwemo wavuvi, zilizowezesha kufanikisha zoezi la uokozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapa pole jamii ya wavuvi na Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, na marafiki kutokana na maafa hayo. Tutaendelea kuyaenzi mema yote waliyotenda wakiwa hai ikiwa ni sehemu ya mchango wao wa Ujenzi wa Taifa letu na tunawaombea Marehemu wote kwa Mwenyezi Mungu ili aziweke roho zao mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/2025, na Mpango na Bajeti ya Fungu 99 la Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2025/2026 kama ilivyo kwenye kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie hali halisi ya ujumla katika sekta zetu za mifugo na uvuvi. Sekta ya Mifugo imeendelea kuwa ni sekta muhimu katika maendeleo ya wananchi na uchumi wa Taifa letu. Katika mwaka 2023, Sekta ya Mifugo ilichangia 6.2% ya pato la Taifa na kukua kwa asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Sekta hii inatoa ajira kwa kaya milioni 4.6 katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo. Sekta hii imekuwa na mchango mkubwa katika uzalishaji wa malighafi za viwanda na kuchangia ongezeko la upatikanaji wa fedha za kigeni kupitia mauzo ya mazao ya nyama na ngozi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali imeendelea kuhamasisha na kusimamia uzalishaji wa mifugo ya aina mbalimbali nchini. Hatua hii imechangia kuongezeka kwa thamani ya mifugo kutoka shilingi 30,489,866,668,000 kwa mwaka 2023/2024 hadi shilingi 33,216,845,677,000 kwa mwaka 2024/2025 kwa makundi yote ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa idadi ya mifugo katika kipindi cha marejeo. Mathalani idadi ya ng'ombe imeongezeka kwa 3.4%, idadi ya mbuzi imeongezeka kwa 3.6% na idadi ya kondoo imeongezeka kwa 9.66%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa 9.4% kutoka tani 963,856.55 zenye thamani ya shilingi trilioni 9.48 mwaka 2023/2024 hadi tani milioni 1.05 zenye thamani ya shilingi trilioni 10.38 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, kiasi cha nyama ya ng'ombe kilichozalishwa ni tani 666,227.02, nyama ya mbuzi ni tani 150,014.29, nyama ya kondoo tani 31,647.60, nyama ya kuku ni tani 147,449.98. Aidha, ongezeko hilo limechangiwa na wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao, kuimarika kwa udhibiti wa magonjwa, uboreshaji wa mbari za mifugo na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni matokeo chanya ya utayari na jitihada za dhati za mfugaji namba moja nchini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyeamua kuzipa kipaumbele sekta za uzalishaji tangu alipoingia madarakani miaka minne iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania, imeendelea kuhamasisha ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa, hali iliyosababisha ongezeko la uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 3.7 zenye thamani ya shilingi trilioni 3.8 mwaka 2023/2024 hadi kufikia lita bilioni 4.01 mwaka 2024/2025 zenye thamani ya shilingi trilioni 3.21 sawa na ongezeko la 1%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la uzalishaji wa maziwa limechangiwa na utoaji elimu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kibiashara pamoja na kuongezeka kwa ng'ombe wa maziwa kutoka milioni 1.32 kwa mwaka uliopita hadi ng'ombe 1.41 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa malisho kwa ajili ya mifugo. Katika mwaka 2024/2025, Serikali imetenga hekta 23,589.7 za malisho na kufanya ardhi iliyotengwa kwa ajili ya malisho kufikia hekta 3,489,701.13 kutoka hekta 3,466,111.43 kwa mwaka uliopita. Hali ya upatikanaji wa malisho katika ardhi ya malisho nchini imeongezeka kutoka tani 110,659,032 mwaka uliopita hadi tani 110,983,390.54 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea na jitihada za upatikanaji wa malisho kwa ajili ya mifugo kwa kuongeza uwekezaji na kuhamasisha Sekta Binafsi na wafugaji wenyewe kutenga na kuendeleza ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa chanjo za magonjwa mbalimbali ya mifugo ambapo katika mwaka 2024/2025 jumla ya dozi milioni 728.15 zimesambazwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi imeendelea kuwa Sekta muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi ilichangia 1.7% kwenye pato la Taifa letu na kukua kwa 1.4%. Aidha, Sekta ya Uvuvi inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni sita katika mnyororo wa thamani wa sekta hii zikiwemo ajira za moja kwa moja kwa wavuvi wapatao 201,661 na wakuzaji viumbe maji 49,084.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Watanzania 4,631 wameajiriwa katika viwanda 64 vya kuchakata mazao ya uvuvi hapa nchini, ambapo kati ya hivyo, viwanda 56 vinasafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia uzalishaji katika Sekta ya Uvuvi ambapo hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya tani 599,200 za mazao ya uvuvi zilizalishwa zenye thamani ya shilingi trilioni 3.44 ikijumuisha tani 466,956.88 za samaki kutoka uvuvi wa asili na tani 132,243.45 kutoka ukuzaji viumbe maji. Uzalishaji huu umeongezeka ikilinganishwa na tani 472,579.34 zilizozalishwa katika kipindi kama hiki mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2024/2025 kiasi cha tani 510,547.33 za samaki, zenye thamani ya shilingi 3,429,209,793,380 zilivunwa ikilinganishwa na tani 463,996 za samaki zenye thamani ya shilingi 3,174,094,804,000 zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Mavuno hayo sasa yameongezeka kwa 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, biashara ya mazao ya uvuvi imeendelea kuimarika katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025, jumla ya tani 39,841.98 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 148,041 wenye thamani ya shilingi bilioni 480.55 waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 34,308 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 124,732 wenye thamani ya shilingi bilioni 389.81 waliouzwa nje ya nchi katika kipindi kama hiki mwaka uliopita, hili likiwa ni ongezeko la 16.3% la mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio hayo yametokana na juhudi za dhati zinazofanywa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kuiwezesha Sekta hii hususan kuwapatia wavuvi wetu boti na vifaa vyake vya kisasa. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2024/2025. Katika mwaka 2024/2025, Fungu 99 lilitengewa jumla ya shilingi 460,333,602,000. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 97,215,432,000 kilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi 363,118,170,000 kilitengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2025,

jumla ya shilingi 131,956,236,286.44 zimetolewa sawa na 28.67% ya bajeti yote iliyotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliidhinishiwa kutumia shilingi 97,215,432,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 44,847,492,000 ni matumizi ya mishahara na shilingi 52,367,940,000 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hadi kufikia Aprili, 2025, shilingi 53,268,629,752.59 zimepokelewa, sawa na 54% ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 31,981,441,661.2 sawa na 71.31% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 21,287,188,091.39, sawa na 40.65% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliidhinishiwa shilingi 363,118,170,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 242,078,803,000 ni fedha za ndani na shilingi 121,031,367,000 ni fedha za nje. Hadi Aprili, 2025 jumla ya shilingi 86,562,975,004.59 sawa na 23.84% ya Bajeti ya Maendeleo zimepokelewa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 85,005,495,004.59 ni fedha za ndani, sawa na 35.11% ya bajeti ya fedha za maendeleo za ndani, na shilingi 1,557,480,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 69,105,000,000 ambapo Sekta ya Uvuvi ilipaswa kukusanya shilingi 33,000,000,000 na Sekta ya Mifugo shilingi 36,105,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2025, Wizara imekusanya maduhuli ya shilingi 56,068,897,105.84 sawa na 97.94% ya lengo lililokusudiwa. Aidha, katika makusanyo hayo, Sekta ya Mifugo imekusanya shilingi 29,467,520,317.28 kati ya shilingi 30,087,000,000 zilizokusudiwa kukusanywa ikiwa ni sawa na 96.56% ya lengo hilo. Sekta ya Uvuvi yenyewe imekusanya maduhuli ya

shilingi 26,601,376,788.56 kati ya shilingi 27,500,000,000 iliyokusudiwa, sawa na 96.73%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imetekeleza maeneo manne ya kipaumbele ambayo ni: -

(i) Kuongeza uzalishaji, masoko, na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(ii) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi;

(iii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; na

(iv) Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kupata mifugo bora na ufugaji wenye tija. Maeneo yaliyopewa umuhimu mkubwa ni pamoja na kuimarisha huduma za uhimilishaji, uzalishaji na usambazaji wa mitamba, uzalishaji wa kuku wa nyama na mayai pamoja na kuboresha biashara ya mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za uhimilishaji, Wizara kupitia Kituo chetu cha Uhimilishaji cha Taifa kwa mwaka 2024/2025 kimezalisha jumla ya dozi za mbegu 110,434 sawa na 73.62% ya lengo la kuzalisha dozi 150,000. Aidha, kati ya dozi hizo zilizozalishwa, dozi 92,587 zimesambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya kuhimilisha mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kituo chetu cha Uhimilishaji kimepokea dozi za mbegu 5,200 kutoka kwa wadau wa nje ikiwemo dozi 4,200 za mbegu ya ng'ombe wa maziwa na dozi 1,000 za ng'ombe wa nyama ambazo zimesambazwa tayari kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kituo kimeendelea kuwajengea uwezo wahimilishaji ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya wahimilishaji 232 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa wamepatiwa mafunzo na wamewezesha uhimilishaji wa ng'ombe 72,731 katika mikoa yote 26. Uhimilishaji huo wa mifugo kwa mwaka 2025 umeendelea kukua ikilinganishwa na ng'ombe 67,355 waliohimilishwa katika kipindi kama hiki mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji na usambazaji wa mitamba, katika jitihada za kuendelea kuboresha mbari za mifugo nchini, Serikali imeendelea kuyaimarisha mashamba matano ya kuzalisha mifugo yenye jumla ya ng'ombe 6,542. Aidha, katika mwaka 2024/2025, mashamba hayo yamezalisha jumla ya mitamba bora 416 sawa na 41.6% ya lengo la kuzalisha mitamba 1,000 na mitamba 147 tayari imesambazwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mashamba ya watu binafsi nane yamezalisha mitamba bora 3,066 na tayari mitamba 2,893 imeshasambazwa. Ni wazi Serikali itaendelea kuboresha mashamba yake kwa kuwekeza zaidi kutokana na ongezeko la mahitaji ya mitamba ili kutosheleza mahitaji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uzalishaji wa kuku wa nyama na mayai, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kuweza kuwekeza kwenye sekta ya kuku, ili kutoa ajira kwa wananchi walio wengi, hasa vijana na wanawake. Hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya mashamba 25 ya kuku wazazi na vitotoleshi 28 yenye mtaji wa shilingi 543,999,040,000 yameanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uwekezaji huo umewezesha kuzalisha jumla ya vifaranga vya kuku 71,526,458 ambavyo vyote vimesambazwa nchi nzima. Kati ya vifaranga hivyo, 59,112,160 ni vya kuku wa nyama; 3,726,804 vya kuku wa mayai; na 8,687,494 ni vya kuku chotara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwekezaji uliofanyika kwenye mashamba ya kuzalishia vifaranga nchini, umesababisha kupungua kwa uingizaji wa vifaranga vya kuku wazazi kutoka

milioni 1.37 mwaka 2023/2024 hadi vifaranga milioni 1.16 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mauzo ya vifaranga kwenda nje ya nchi yamepungua kutoka vifaranga 2,701,429 mwaka 2023/2024 hadi vifaranga 1,909,078 mwaka 2024/2025. Upungufu wa mauzo ya vifaranga nje ya nchi umetokana na kuimarika kwa soko la ndani, hususani uanzishwaji wa mashamba makubwa yanayofuga kuku kibiashara. Nawapongeza sana wawekezaji wetu kwa mashamba haya ambayo yameendelea kuwekeza na kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara ya mifugo na mazao yake, hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya ng’ombe 3,411,000, mbuzi na kondoo 3,330,000 wenye thamani ya shilingi trilioni 3.7 waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini, ikilinganishwa na ng’ombe milioni 2.96 na mbuzi na kondoo milioni 2.83 waliokuwa na thamani ya shilingi trilioni 3.4 waliouzwa kwa mwaka wa fedha uliopita 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la mifugo iliyouzwa katika minada linatokana na kuhamasika kwa wafugaji kuvuna mifugo yao na kuanza kufuga kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mkakati wa kukuza mauzo nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza fedha za kigeni, Wizara kupitia Bodi ya Nyama, imeendelea kuratibu mauzo ya nyama kwenda nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya tani 9,863.41 za nyama, sawa na asilimia 89.9 ya lengo la kuuza tani 10,971 zenye thamani ya shilingi trilioni 3.7, zimeuzwa katika masoko ya nje ya nchi ikilinganishwa na tani 9323 zenye thamani ya shilingi trilioni 3.4 zilizouzwa nje kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha uliopita 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo kwa mwaka 2024/2025 yameongezeka kwa asilimia 5.75. Nyama hiyo imeuzwa katika nchi za Bahrain, Comoro, Hong Kong, Jordan, Kenya, Kuwait, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*) na Vietnam. Kipekee kabisa, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan kwa kuendelea kufungua milango ya Taifa letu na sisi kuweza kuyafikia masoko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa maji, malisho na vyakula vya mifugo; katika mwaka 2024/2025 Wizara imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo, ambapo imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa mabwawa manne ya Bukabwa – Butiama, Kihumbu - Bunda, Isulamilomo – Nsimbo, na Kwenikwembe - Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabwawa haya yana uwezo wa kuhifadhi wastani wa lita milioni 120 za maji kila moja zinazotosheleza kunywesha uniti za mifugo takribani 100,000 kwa mwaka. Utekelezaji wa kazi ya ujenzi wa mabwawa haya umeongeza upatikanaji wa maji kwa mifugo, hivyo kuchangia katika ustawi wa mifugo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha uzalishaji na utendaji kazi katika mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na mbegu, katika mwaka 2024/2025, Wizara imekamilisha ujenzi wa ghala katika shamba la malisho lililopo katika Kituo cha TALIRI, Mpwapwa, kwa ajili ya kuhifadhia malisho na mbegu za malisho. Vilevile, ujenzi wa ghala katika Shamba la Mbegu za Malisho la Vikuge, Kibaha, unaendelea na umefikia 60% huku katika Shamba la Mbegu za Malisho la Langwira, Mbarali, ujenzi ukiwa umefikia 45%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utatuzi wa Migogoro Baina ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi: Mahusiano mazuri baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ni nyenzo muhimu katika uzalishaji, ustawi na maendeleo ya Sekta ya Mifugo. Ili kuimarisha mahusiano hayo, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwajengea uwezo wafugaji kuhusu umuhimu wa kumiliki na kuendeleza ardhi ya malisho na ufugaji wenye tija. Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa mashamba darasa ya malisho na kushiriki katika utekelezaji wa Kampeni ya Tutunzane, kule Mvomero, Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampeni ya Tutunzane, Mvomero, ilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tarehe 3 Agosti, 2024 kwa lengo la kuhamasisha wafugaji kumiliki ardhi kwa ajili ya malisho, kuendeleza ardhi ya malisho kwa kuotesha malisho na kuzingatia hifadhi ya mazingira. Wizara imewezesha kampeni hiyo kwa kutoa jumla ya kilo 15,000 za mbegu za malisho aina ya *Juncao* na kilo 527 za mbegu za malisho aina ya *Rhodes* kwa wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji wa Rasilimali za Vyakula vya Mifugo. Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya biashara ya vyakula vya mifugo pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika usindikaji wa vyakula vya mifugo. Katika mwaka 2024/2025 jumla ya tani 720,000 za vyakula vya mifugo zenye thamani ya shilingi trilioni 1.15 zilizalishwa, ikilinganishwa na tani 380,000 kwa mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la 89.47%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maono makubwa na upendo wa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara inaendelea kutekeleza Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora kwa vijana, ili kuwawezesha kujiajiri kupitia uwekezaji katika shughuli za ufugaji nchini. Kupitia Programu hiyo, jumla ya vikundi 20 vyenye vijana 106 vimepatiwa ekari 1,761 katika Ranchi ya Kagoma na kupewa mkopo usio na riba wa jumla ya shilingi 934,231,000 kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* kwa ajili ya kuendesha shughuli za unenepeshaji ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2025 jumla ya ng'ombe 627 wenye thamani ya shilingi 451,440,000 walinunuliwa kwa wastani wa shilingi 720,000 kwa kila ng'ombe na kunenepeshwa. Kati ya ng'ombe hao 452, wenye thamani ya shilingi 402,280,000/=, waliuzwa kwa wastani wa shilingi 890,000/= kwa kila ng'ombe na kupatikana kwa faida ya shilingi 76,840,000/= ikiwa ni wastani wa faida ya shilingi 170,000/= kwa kila ng'ombe, kwa kijana, kwa muda wa miezi mitatu tu. Hakika tumeanza na kazi inaendelea. Vijana wetu kaeni mkao wa kazi, kwani utajiri upo kwenye mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kudhibiti magonjwa yanayovuka mipaka kwa kusimamia na kuratibu shughuli za uchanjaji wa mifugo. Hadi Aprili, 2025 jumla ya dozi 398,752,227 za chanjo mbalimbali za mifugo zimetumika kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa 13 ya kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengine kwa kuratibu uogeshaji wa mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Aprili, 2025 jumla ya michovyo 1,337,306,118 ya mifugo imefanyika. Michovyo hii ni sawa na 66.9% ya lengo la mwaka la michovyo 2,000,000,000. Aidha, uogeshaji wa mifugo umesaidia kupunguza matukio ya vifo vya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kampeni ya chanjo na kujenga uelewa kwa wadau juu ya Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, Wizara imefanya uzinduzi wa hamasa ya kampeni ya chanjo Kitaifa kwa kuwakutanisha wadau wa mifugo 762 wakiwemo Makatibu Tawala wa Mikoa 26, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Sehemu ya Mifugo na Maafisa TEHAMA kutoka Halmashauri zetu zote184.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, Serikali imenunua jumla ya hereni za kidijitali 36,323,300, kwa ajili ya utambuzi wa mifugo. Aidha, jumla ya ng'ombe 19,099,100, mbuzi na kondoo 17,224,200 wanatarajiwa kupatiwa chanjo na kutambuliwa kwa kuwekewa hereni za kidigitali na taarifa zao kuingizwa kwenye Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la utambuzi wa mifugo ni kukidhi matakwa ya soko la kikanda na Kimataifa linalohitaji kila mnyama na mazao yake kuwa na alama ya utambuzi, kuwezesha wafugaji kupata mikopo na bima, kudhibiti wizi wa mifugo, kurahisisha ufuatiliaji, udhibiti wa magonjwa na kuwezesha Serikali na wadau kuweka mipango ya kuhudumia mifugo na wafugaji, kwa kuwa idadi yao itajulikana sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upumzishaji wa Shughuli za Uvuvi kwa Muda. Serikali imetekeleza Mkataba wa Kikanda wa Uhifadhi wa Ziwa Tanganyika wa Upumzishaji wa Ziwa Tanganyika kuanzia Tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti kila mwaka, ili kuongeza uzalishaji wa samaki. Katika mwaka 2024, mavuno ya samaki kutokana na upumzishwaji huo yaliongezeka kwa 55.3% kufikia tani 38,999 zenye thamani ya shilingi 324,845,566,002 katika kipindi cha miezi minne tu, baada ya kufungua ziwa Septemba, ikilinganishwa na tani 25,113.42, zenye thamani ya shilingi 166,476,911,002 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la uzalishaji samaki, kiasi cha mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ya nchi kutoka Ziwa Tanganyika kwa Mwaka 2024 kiliongezeka hadi kufikia tani 1,227.21 zenye thamani ya shilingi 180,684,608,011. Hii ikiwa ni ongezeko la 84% ukilinganisha na mwaka uliopita wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uzoefu na mafanikio yaliyopatikana kwa kupumzisha Ziwa Tanganyika Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Bukoba Vijijini, pia imepumzisha Ziwa Ikimba, Kagera, kwa muda wa miezi sita kuanzia Tarehe 12 Aprili, mpaka 12 Septemba, 2025. Sambamba na kupumzisha ziwa hilo, Serikali imepandikiza vifaranga 2,000,000, ili kuongeza uzalishaji wa samaki wa asili kwa lengo la kuongeza kipato na lishe kwa maeneo yanayozunguka ziwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea na utafiti wa uwezekano wa ufugaji wa kutumia teknolojia ya vizimba kwa maziwa makuu, mabwawa pamoja na maji madogo nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2024 Wizara imetambua maeneo 99 yenye jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba 220.22 yanayofaa kwa ufugaji wa vizimba katika Ziwa Victoria na kuyafanyia tathmini ya kimkakati ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo fursa, na tumeamua kugeuza fursa hizo kuwa matunda mema kwa Watanzania na

Taifa letu. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, ameamua kutekeleza kwa vitendo Kauli ya Baba wa Taifa aliyowahi kusema kwamba, kitakachotutofautisha sisi na wao siyo uwezo wa kufikiri, bali uwezo wa kuamua lililo sahihi baada ya kufikiri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele ya kwanza imegongwa. Naomba kwa ridhaa yako taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, umebakiwa na dakika nane.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Naomba sasa niende kwenye Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/2026. Mpango na Bajeti ya Fungu 99 kwa Mwaka 2025/2026 umeandaliwa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali, kama ambavyo tumekuwa tukifanya miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi utatekelezwa kupitia vipaumbele vifuatavyo:-

i) Kuongeza uzalishaji, masoko, thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

ii) Kuimarisha ulinzi, usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi;

iii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; na

iv) Kuimarisha utafiti, mafunzo, huduma kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Fungu 99, tumepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 74,105,001,000. Kati ya kiasi hiki, shilingi

38,300,000,000 zinatarajiwa kukusanywa kupitia Sekta ya Mifugo na shilingi 35,805,001,000 kupitia Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nihitimishe hotuba yangu, na kwa unyenyekevu mkubwa kutumia fursa hii kuwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yetu kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kabisa kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na maarifa pamoja na maelekezo anayotupatia kama Wizara, kuhakikisha rasilimali za mifugo na uvuvi zinachangia katika uchumi wa Taifa letu kwa maendeleo endelevu. Nampongeza sana kwa ujasiri na uzalendo wake wa kuzipa kipaumbele sekta za mageuzi ambapo, mifugo na uvuvi tukiwa tuna mchango mkubwa kwenye maisha ya wananchi na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu ninamshukuru sana kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri kwenye Wizara mbalimbali na sasa kama Waziri mwanamke wa kwanza kuongoza Wizara ya Mifugo na Uvuvi tangu Taifa letu lipate uhuru. Imani hii ni kubwa sana kwangu, kwani ameona ninaweza kusimamia utekelezaji wa maono yake kwenye sekta hii muhimu kwa uchumi wa wananchi na Taifa letu. Vitabu vyetu vya Dini vinasema, hisani hulipwa kwa hisani. Ahadi yangu kwake ni kwamba, mimi pamoja na wenzangu Wizarani tutamlipa kwa vitendo kwa kuhakikisha maono yake yanatimia na matarajio ya wafugaji na wavuvi yanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wafugaji wote nchini. Nawashukuru sana wafugaji wote wa nchi hii. Ni wazi kwamba nilipoteuliwa kuja kwenye Wizara hii, wapo waliosema atawaweza wafugaji wa nchi hii? Majibu wanayo wafugaji wenyewe wakiongozwa na ndugu yangu Mrida Mshota, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania. Tumetulia, tunafuga mifugo yetu kwa amani kabisa na

sasa tunakwenda kuhakikisha kuwa tunayafikia masoko yote kwa ajili ya mifugo yetu na mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mfugaji namba moja nchi hii alishakamilisha kazi yake ya Diplomasia ya Uchumi, masoko yapo tayari dunia nzima. Kubwa zaidi ametuwezesha kupata chanjo kwa ajili ya mifugo yetu nchi nzima. Zoezi lililofanyika kipindi cha awamu ya kwanza na sasa ameweza tena si mwingine ni Mama Mlezi wa Taifa na mfugaji namba moja ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wafugaji tunasema, Mheshimiwa Rais tupo tayari kwa mambo mawili makubwa. Moja, ni kumpa kura zote ifikapo mwezi Oktoba, 2025 ili tuendelee kunufaika na utumishi wake; na pili, ni kupeleka mifugo yetu na mazao yake duniani. Hakika tunakwenda kumlipa mama yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wavuvi wenzangu, kuanzia Ikimba hadi Bahari ya Hindi, ahsante sana kwa ushirikiano wao na kujitoa kwao kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Wamekuwa mashuhuda wa kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na tumeona kwa pamoja jinsi alivyobadilisha maisha ya wavuvi hapa nchini kwa kutuwezesha kupata boti mpya za kisasa za uvuvi pamoja na vizimba vya kufugia samaki ambavyo matunda yake tunayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wavuvi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia vitendea kazi hivyo na tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza kipato pamoja na kuboresha maisha yetu. Hivyo, sisi wavuvi tunatambua kwamba tuna deni kwake na tunamwahidi kwamba tunaenda kulilipa mwezi Oktoba, 2025 kupitia boski la kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Kondoa ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na ya Taifa letu. Naomba niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na

maarifa makubwa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wana-CCM wenzangu ndani ya Jimbo la Kondoa kuanzia ngazi ya shina hadi wilaya; na leo tukiwa tumewakilishwa hapa Bungeni na viongozi wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania kata zote 21; Jumuiya ya Wazazi Kata zote 21 pamoja na sekretarieti yetu ya Wilaya, nina uhakika kazi ya Kamsese ndani ya Jimbo la Kondoa siyo za kumulika kwa tochi, zinaonekana wazi kwa sekta zote za kiuchumi na kijamii. Naye mnamwona bado yupo imara kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana kwa tamko lao Wanakondoa kwamba hawahitaji mabadiliko ya uongozi kwenye Jimbo la Kondoa. Nami ninawaambia kuwa nipo tayari kwa mchakamchaka mwingine kwa miaka mitano ijayo, na ndipo tulipoelekezwa tuseme kwamba Kazi na Utu, Tunasonga Mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba fedha kwa heshima na taadhima. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaomba kutumia jumla ya shilingi 476,655,072,000. Kati ya fedha hizi, shilingi 101,516,670,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 375,138,402,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHE. DKT. ASHATU KACHWAMBA KIJAJI (MB.), WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyochambua na kushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Mwaka 2024/2025, sasa naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2024/2025. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2025/2026.

### Shukrani, Pongezi na Pole

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma na Ukarimu, kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Mbili, ikiwa ni Mkutano mahsusi wa Bunge wa kuamua mambo yenye mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutimiza kipindi cha miaka minne (4) ya uongozi wake na kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na mafanikio makubwa. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kutumika katika Wizara mbalimbali ambapo, kwa sasa, umeniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Vilevile, nimpongeze ***Ndg*. Abdul Rajab Mhinte** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu (Mifugo), ambapo pamoja na viongozi na watendaji wenzetu tuliowakuta ndani ya Wizara tunaamini ushirikiano wetu utaleta mageuzi chanya ya kisekta, ambayo ni mojawapo ya falsafa ya 4R za Mheshimiwa Rais.

3. ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali; akiwemo **Mheshimiwa *Dkt*. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; **Mheshimiwa *Dkt*. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa; na **Mheshimiwa *Dkt*. Dotto Mashaka Biteko (Mb.)**, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, na Mbunge wa Jimbo la Bukombe, kwa utendaji wao wa kizalendo na uliotukuka ambao unamuwezesha Mheshimiwa Rais na kipenzi cha Watanzania kuendelea kutoa mchango wake muhimu kwa maendeleo na Ujenzi wa Taifa letu na hivyo kumfanya ang'are kiuongozi katika duru za Kitaifa na Kimataifa.

4. ***Mheshimiwa Spika**,* napenda kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuendelea kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo ni moja ya sababu zilizofanya uaminiwe na kuchaguliwa kuwa Rais wa **31** wa Umoja wa Mabunge Duniani, ukiwa ni mwanamke wa kwanza kutoka katika Bara la Afrika na wa tatu (3) Duniani kushika nafasi hiyo yenye majukumu makubwa na madaraka mazito. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu** (**Mb**.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mbunge wa Jimbo la Ilala, kwa kukusaidia kwa umahiri na weledi mkubwa wa kuendesha shughuli za Bunge. Pia, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuongoza Kamati zao katika kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

5. ***Mheshimiwa Spika**,* nachukua fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika** (**Mb**.), Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kwa kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hii muhimu kwa mustakabali mpana wa maendeleo ya Taifa letu. Vilevile, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ninawashukuru viongozi, wajumbe wote, pamoja na Sekretarieti ya Kamati hii kwa kufanya uchambuzi makini wa Bajeti yetu. Ushauri wenu

umewezesha Wizara kufanya maboresho stahiki na ya kimkakati. Hakika, Mheshimiwa Spika unayo Kamati ambayo ni msaada mkubwa kwetu na kwa Taifa letu. Kwa upande wetu, tunaahidi kuendelea kuipatia Kamati hii ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi na ushauri ili kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa.

6. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutumia fursa hii adhimu kumshukuru kwa dhati ndugu yangu, **Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti** (**Mb**.), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mbunge wa Jimbo la Misungwi, kwa umahiri wake mkubwa wa kuchapa kazi, ushauri wake mzuri, na ubunifu wenye tija uliotusaidia sote kwa pamoja kufanya maboresho yenye tija ya usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

7. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwapongeza ***Prof.*** **Riziki Silas Shemdoe** (**Katibu Mkuu-Wizara ya Mifugo na Uvuvi**), ***Ndg.*** **Abdul Rajab Mhinte** (**Naibu Katibu Mkuu-Mifugo**), na ***Dkt.*** **Edwin Paul Mhede** (**Naibu Katibu Mkuu-Uvuvi**), kwa kuwa viongozi hodari na wabunifu wa kuziendeleza Sekta na Watendaji wazuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara na kuwasimamia Watalaam wa Wizara kwa ufanisi. Pia, ninawashukuru sana Watumishi wote Wizarani kwa utendaji na ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu kikamilifu.

8. ***Mheshimiwa Spika**,* katika utekelezaji wa majukumu yangu ambayo muda mwingi nipo nje ya nyumbani usingekuwa rahisi bila maombi na dua njema kutoka kwa watu wangu wa karibu. Namshukuru sana mama yangu mpendwa, ***Hajat*** **Aziza Selemani**, namshukuru mume wangu kipenzi, ***Dkt.*** **Muhajir Kachwamba**, na watoto wangu, **Samirah** na **Aboubakar**. Ahsanteni sana kwa upendo, uvumilivu, na utayari wenu unaonipatia ari ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo, uzalendo na weledi wangu wote. Vilevile niwashukuru sana viongozi wangu wa dini, ndugu, jamaa, na marafiki wote kwa kuendelea kuniombea kwa Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema iliyoniwezesha kuendelea kulitumikia Taifa letu. Nichukue fursa hii kuwaahidi Watanzania

wote kwa ujumla nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa kutanguliza mbele maslahi ya Taifa letu.

9. ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati na kwa namna ya kipekee ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Kondoa kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wanaendelea kunipatia katika kuwatumikia wana-Kondoa wenzangu na kuwawakilisha vyema katika Bunge hili Tukufu na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo letu. Naomba nichukue fursa hii kuwaahidi kuwa nitaendelea kuwa mtumishi wenu na muda wote nitadumu katika kuwatumikia kwa umahiri na moyo wa dhati.

10. ***Mheshimiwa Spika***, natambua mchango wa Sekta Binafsi, unaojumuisha wawekezaji wakubwa na wadogo wakiwemo wafugaji, wavuvi, wakuzaji viumbe maji, wachakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi, wahifadhi wa mazingira na ikolojia (ambayo ni muhimu kwa uendelevu wa Sekta za Mifugo na Uvuvi) na wadau wengine wote waliopo katika mnyororo wa thamani wa mazao ya Mifugo na Uvuvi. Pia, ninapenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Taasisi za kifedha, na Asasi zisizo za Kiserikali kwa kuendelea kutuunga mkono katika harakati za kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Tunawashukuru sana na tunaahidi kuendelea kuwahudumia na kushirikiana nanyi.

11. ***Mheshimiwa Spika***, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa ***Dkt. Samia Suluhu Hassan,*** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Aidha, nampongeza Mheshimiwa ***Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi*** kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nichukue fursa hii kumpongeza ***Dkt.* Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Urais wa Zanzibar. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na kwa niaba ya wafugaji na wavuvi napenda kuwaahidi kuwa tutaendelea kuwaunga mkono katika Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2025

**Salamu za Pole**

12. ***Mheshimiwa Spika***, wakati tukiendelea na utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya viongozi na wanasiasa wakongwe ambao ni:- **Mheshimiwa *Dkt.* Faustine Engelbert Ndugulile (Mb.)** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Ukanda wa Afrika; **Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema,** aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji wa Mahakama Kuu; **Mheshimiwa *Balozi* Juma Volter Mwapachu**, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); **Mheshimiwa Tabitha Siwale**, aliyewahi kuhudumu katika nafasi ya Mbunge na Waziri wa kwanza mwanamke Tanzania**; Mheshimiwa *Profesa* Philemon Sarungi**, aliyewahi kutumikia Taifa letu kwa nafasi ya Mbunge, Mkuu wa Mkoa, na Waziri katika Wizara mbalimbali; **Mheshimiwa Cleopa David Msuya** aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninatoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Wabunge, familia, ndugu, jamaa na marafiki na Watanzania wote walioguswa na misiba hiyo.

13. ***Mheshimiwa Spika***, itakumbukwa kuwa tarehe **23 Januari 2025** kulitokea upepo mkali ndani ya Ziwa Rukwa, ambapo wavuvi **540** walifikwa na maafa. Kati ya hao, wavuvi **531** waliokolewa, kutibiwa na kupona na wavuvi tisa (**9**) walifikwa na umauti. Tunashukuru juhudi za pamoja baina ya vyombo vya Serikali na wananchi wenyewe wakiwemo wavuvi zilizowezesha kufanikisha zoezi la uokozi. Nitumie fursa hii kuwapa pole jamii ya wavuvi na Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, na marafiki kutokana na maafa hayo.

***Tutaendelea kuyaenzi mema yote waliyotenda wakiwa hai ikiwa ni sehemu ya mchango wao wa Ujenzi wa Taifa letu na tunawaombea marehemu wote kwa Mwenyezi Mungu ili aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina.***

14. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/2025, na Mpango na Bajeti ya Fungu **99 -** Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2025/2026.

## B. HALI HALISI YA UJUMLA KATIKA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

### *SEKTA YA MIFUGO*

15. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mifugo imeendelea kuwa Sekta muhimu katika maendeleo ya wananchi na uchumi wa Taifa. Katika Mwaka 2023, Sekta ya Mifugo ilichangia asilimia **6.2** ya Pato la Taifa (GDP) na kukua kwa asilimia **5.** Aidha, Sekta hii inatoa ajira kwa Kaya milioni 4.**6** katika mnyororo wa thamani wa Sekta ya Mifugo, Sekta hii imekua na mchango mkubwa katika uzalishaji wa malighafi za viwanda na kuchangia ongezeko la upatikanaji wa fedha za kigeni kupitia mauzo ya mazao ya nyama na ngozi nje ya nchi.

16. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Serikali imeendelea kuhamasisha na kusimamia uzalishaji wa mifugo ya aina mbalimbali nchini. Hatua hii imechangia kuongezeka kwa thamani ya mifugo kutoka shilingi **30,489,866,668,000** kwa mwaka 2023/2024 hadi shilingi **33,216,845,677,000** kwa mwaka 2024/2025 kwa makundi yote ya Mifugo. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya Mifugo katika kipindi cha marejeo mathalani idadi ya ng'ombe imeongezeka kwa asilimia **3.4** kutoka ng'ombe **37,913,129** hadi **39,241,375**, mbuzi kwa asilimia 3.6 kutoka mbuzi **27,586,547** hadi **28,595,597**, na kondoo kwa asilimia 3.2 kutoka kondoo **9,373,407** hadi **9,658,880**. Pia, kuku wameongezeka kwa asilimia 5.0 kutoka kuku **103,080,708** hadi **108,221,085**, ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka **47,391,131** hadi **49,754,408** na kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **55,689,577** hadi **58,466,677**. Vile vile, nguruwe wameongezeka kwa asilimia 5.1 kutoka nguruwe **3,901,096** hadi **4,131,962**. (**Kiambatisho Na.1A, 1B, na 1C**).

17. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo uzalishaji wa nyama

umeongezeka kwa asilimia **9.4** kutoka tani **963,856.55** zenye thamani ya shilingi **9,476,474,305,000** Mwaka 2023/2024 hadi tani **1,054,114.03** zenye thamani ya shilingi **10,378,706,595,000** mwaka 2024/2025**.** Katika Mwaka 2024/2025**,** kiasi cha nyama ya ng'ombe kilichozalishwa ni tani **666,227.02**, nyama ya mbuzi tani **150,014.29**, nyama ya kondoo tani **31,647.60,** nyama ya kuku tani **147,449.98**, na nyama ya nguruwe tani **58,775.14** ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani **612,808.50**; mbuzi tani **134,403.35**; kondoo tani **28,290.00**; kuku tani **132,442.28**, na nguruwe tani **55,912.42** kwa Mwaka 2023/2024. (**Kiambatisho Na.2**). Aidha, ongezeko hilo limechangiwa na wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao, kuimarika kwa udhibiti wa magonjwa, uboreshaji wa mbari za mifugo na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi

18. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania, imeendelea kuhamasisha ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa, hali iliyopelekea ongezeko la uzalishaji wa maziwa kutoka lita **3,969,887,235.74** zenye thamani ya shilingi **3,175,909,788,592** Mwaka 2023/2024 hadi kufikia lita **4,009,985,321.20** Mwaka 2024/2025 zenye thamani ya shilingi **3,207,988,256,976** sawa na ongezeko la asilimia **1.** Kati ya hizo, lita **2,587,651,655.20** zimetokana na ng'ombe wa asili na lita **1,387,620,068** zimetokana na ng'ombe wa maziwa.

Kiasi kidogo cha maziwa, lita **34,713,597** zimetokana na wanyama wengine ikiwemo mbuzi wa maziwa. Ongezeko la uzalishaji wa maziwa limechangiwa na utoaji elimu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kibiashara ambapo wafugaji **1,040** walipewa mafunzo Mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na wafugaji **1,109** waliopata mafunzo Mwaka 2024/2025; na kuongezeka kwa ng'ombe wa maziwa kutoka **1,321,677** Mwaka 2023/2024 hadi ng'ombe **1,410,891** Mwaka 2024/2025. Aidha, maziwa yanayokusanywa yameongezeka kutoka lita **93,427,734.54** Mwaka 2023/2024 hadi lita **95,614,978.76** Mwaka 2024/2025 (sawa na ongezeko la **2.3%**). Ongezeko la maziwa yanayokusanywa limetokana na kuongezeka kwa vituo vya kukusanyia maziwa kutoka **258** Mwaka 2023/2024 hadi **269** Mwaka 2024/2025 ikiwa ni ongezelo la 4.3%. Vilevile, usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **81,800,654.8** Mwaka 2023/2024 hadi lita **90,416,788.5**

Mwaka 2024/2025 ikiwa ni ongezeko la **11.7%**. Ongezeko la usindikaji limetokana na ongezeko la maziwa yanayokusanywa katika vituo vya kukusanyia maziwa.

19. ***Mheshimiwa*** *Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa malisho kwa ajili ya mifugo. Katika Mwaka 2024/2025, Serikali imetenga hekta **23,589.7** za malisho na kufanya ardhi iliyotengwa kwa ajili ya malisho kufikia hekta **3,489,701.13** kutoka hekta **3,466,111.43** Mwaka 2023/2024. Hali ya upatikanaji wa malisho katika ardhi ya malisho nchini imeongezeka kutoka tani **110,659,032.16** Mwaka 2023/2024 hadi tani **110,983,390.54** Mwaka 2024/2025. Kiwango hicho hakitoshelezi mahitaji ya tani **158,000,000** kwa mifugo iliyopo. Hata hivyo, Serikali inaendelea na jitihada za upatikanaji wa malisho kwa ajili ya mifugo kwa kuongeza uwekezaji na kuhamasisha Sekta Binafsi na wafugaji kutenga na kuendeleza ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo.

20. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendeleza jitihada za kuongeza upatikanaji wa vyakula vya mifugo, malisho na mbegu za malisho kwa kuwekeza katika mashamba yake na kuhamasisha wafugaji kuzalisha malisho. Katika Mwaka 2024/2025, mashamba ya Serikali na Binafsi yamezalisha jumla ya tani **222.54** za mbegu za malisho (***nyasi, mikundekunde na vipando***) zenye thamani ya shilingi bilioni **1.7** ikilinganishwana tani **127.8** zilizozalishwa Mwaka 2023/2024 zenye thamani ya shilingi bilioni **1.08**. Pia, jumla ya tani 1**4,185** za malisho (***hei na saileji***) zenye thamani ya shilingi bilioni **3.8** zimezalishwa ikilinganishwa na tani **4,744** zilizozalishwa Mwaka 2023/2024 zenye thamani ya shilingi bilioni **1.4.** Kwa upande wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa uzalishaji umefikia tani **720,000** zenye thamani ya shilingi trilioni **1.15.** Uzalishaji huu ni sawa na asilimia **45** ya lengo la kuzalisha tani **1,600,000. (Kiambatisho Na. 3A na 3B).**

21. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo na kuimarisha afya ya wanyama kwa kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa chanjo nchini. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya dozi **728,153,645** za chanjo za magonjwa mbalimbali ya mifugo zimesambazwa. Kati ya hizo, dozi **153,952,375** zimezalishwa nchini ambapo dozi **58,822,475**

zimezalishwa na Taasisi ya Chanjo Tanzania (*Tanzania Vaccine Institute* - TVI) na dozi **95,129,900** zimezalishwa na viwanda vingine vya Sekta Binafsi; na dozi **574,201,270** zimeingizwa kutoka nje ya nchi. Pia, uchanjaji wa mifugo unaofanywa na Serikali pamoja na wadau umechangia kudhibiti magonjwa na hivyo kuimarisha afya ya mifugo. Aidha, udhibiti wa magonjwa yaenezwayo na kupe na wadudu wengine kwa kuogesha mifugo umechangia kupunguza kiwango cha vifo vitokanavyo na magonjwa yaenezwayo na kupe kutoka asilimia **48** hadi asilimia **45** ya vifo vyote.

***SEKTA YA UVUVI***

22. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Uvuvi imeendelea kuwa Sekta muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Katika Mwaka 2023, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia **1.7** kwenye Pato la Taifa (GDP) na kukua kwa asilimia **1.4**. Aidha, Sekta ya Uvuvi inatoa ajira kwa Watanzania takriban **milioni 6,** zikiwamo ajira za moja kwa moja kwa wavuvi wapatao **201,661** na wakuzaji viumbe maji **49,084** katika mnyororo wa thamani wa Sekta ya Uvuvi. Kwa upande mwingine, Watanzania **4,631** wameajiriwa katika viwanda **64** vya kuchakata mazao ya uvuvi hapa nchini ambapo kati ya hivyo, viwanda **56** vinasafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi **(Kiambatisho Na.4).** Pia, Sekta ya Uvuvi huongeza usalama wa chakula na lishe kwa kuchangia asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama.

23. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia uzalishaji katika Sekta ya Uvuvi ambapo hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya tani **599,200.33** za mazao ya Uvuvi zilizalishwa zenye thamani ya shilingi **3,439,345,531,380** ikijumuisha tani **466,956.88** za samaki kutoka uvuvi wa asili na tani **132,243.45** kutoka ukuzaji viumbe maji ikilinganishwa na tani **472,579.34** zilizozalishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/2024. Aidha, katika mwaka 2024/2025 kiasi cha tani **510,547.33** za samaki, zenye thamani ya shilingi **3,429,209,793,380** zilivunwa ikilinganishwa na tani **463,996.89** za samaki zenye thamani ya shilingi **3,174,094,804,000** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/2024. Mavuno hayo ni sawa na ongezeko la asilimia **10.03** la uzalishaji wa samaki kutoka katika maji ya asili na ukuzaji viumbe maji nchini. Pia, ulaji wa samaki,

kwa mtu kwa mwaka hapa nchini umefikia kiasi cha kilo **7.9** ikilinganishwa na wastani wa dunia wa kilo **20.3** kwa mtu kwa mwaka kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO).

24. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji huu wa samaki ni mdogo ukilinganisha na mahitaji ya samaki ya wastani wa tani **1,253,344.7** kwa mwaka. Ili kuondoa nakisi hii, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kuhakikisha inakidhi mahitaji ya samaki nchini zikiwemo kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Uvuvi, kuhamasisha uwekezaji na uendelezaji wa ukuzaji wa viumbe maji na Uvuvi wa bahari kuu.

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, biashara ya mazao ya uvuvi imeendelea kuimarika katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025, jumla ya tani **39,841.98** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **148,041** wenye thamani ya shilingi bilioni **480.55** waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani **34,308.94** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **124,732** wenye thamani ya shilingi bilioni **389.81** waliouzwa nje ya nchi katika kipindi kama hiki mwaka 2023/2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia **16.13** la mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi **(Kiambatisho Na.5).**

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI MWAKA 2024/25

### Bajeti iliyoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

26. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, **Fungu 99** lilitengewa jumla ya shilingi **460,333,602,000**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **97,215,432,000** kilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kiasi cha shilingi **363,118,170,000** kilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hadi Aprili 2025, jumla ya shilingi **131,956,236,286.44** zimetolewa sawa na asilimia **28.67** ya bajeti yote iliyotengwa.

**Matumizi ya Kawaida**

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliidhinishiwa kutumia shilingi **97,215,432,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi **44,847,492,000** ni Matumizi ya Mishahara **(PE**) na shilingi **52,367,940,000** ni Matumizi Mengineyo (***OC***). Aidha, hadi kufikia Aprili, 2025, shilingi **53,268,629,752.59** zimepokelewa, sawa na asilimia **54.79** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi **31,981,441,661.2** sawa na asilimia **71.31** ni kwa ajili ya Mishahara (**PE)** na shilingi **21,287,188,091.39**, sawa na asilimia **40.65** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**


28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya Mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliidhinishiwa shilingi **363,118,170,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **242,078,803,000** ni fedha za ndani na shilingi **121,039,367,000** ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya shilingi **86,562,975,004.59** sawa na asilimia **23.84** ya Bajeti ya Maendeleo zimepokelewa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi **85,005,495,004.59** ni fedha za ndani, sawa na asilimia **35.11** ya bajeti ya fedha za maendeleo za ndani, na shilingi **1,557,480,000** ni fedha za nje.

**Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi **69,105,000,000** ambapo Sekta ya Uvuvi inapaswa kukusanya shilingi **33,000,000,000** na Sekta ya Mifugo Shilingi **36,105,000,000**. Wastani wa makusanyo ambayo Wizara inapaswa kukusanya kwa mwezi ni shilingi **5,758,750,000**, ambapo Sekta ya Uvuvi inatakiwa kukusanya wastani wa shilingi **2,750,000,000**, na Sekta ya Mifugo kiasi cha shilingi **3,008,750,000** kwa kila mwezi.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2025, Wizara imekusanya maduhuli ya shilingi **56,068,897,105.84** sawa na asilimia **97.94** ya lengo la kukusanya shilingi **57,587,500,000**. Aidha, katika makusanyo hayo, Sekta ya Mifugo imekusanya shilingi **29,467,520,317.28** kati ya shilingi **30,087,500,000** sawa na asilimia

**96.56** ya lengo la makusanyo la miezi kumi ilihali Sekta ya Uvuvi imekusanya maduhuli ya shilingi **26,601,376,788.56** kati ya shilingi **27,500,000,000** sawa na **asilimia 96.73** ya lengo la makusanyo kwa miezi kumi. (**kielelezo Na. 1**).




**Kielelezo Na 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025 hadi Aprili, 2025 Sekta ya Mifugo**

**Maeneo ya Vipaumbele katika Mwaka 2024/2025**

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara imetekeleza maeneo manne (**4**) ya kipaumbele ambapo utekelezaji wake umezingatia matakwa ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (**2025**); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (***FYDP*** III) kwa kipindi cha 2021/2022 – 2025/2026; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025; Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025; na Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030 (***Sustainable Development Goals–SDGs*, 2030**). Aidha, utekelezaji huo umezingatia Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006; Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015; Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024; Mpango Mkuu wa Sekta ya Kilimo 2050 (***Agriculture Master Plan*** - ***AMP***, 2050), Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (***ASDP*** II); Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi wa Mwaka 2021/22–2036/37. Utekelezaji wa vipaumbele hivi umewezesha Wizara kupata mafanikio na matokeo ambayo yameelezwa katika Hotuba yangu. Aidha, vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kuongeza uzalishaji, masoko, na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;
(ii) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi;

(iii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; na
(iv) Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**Sera, Sheria na Kanuni**
32. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuweka mazingira wezeshi ya uzalishaji na biashara katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 kupitia Sheria na Kanuni za Mifugo na Uvuvi zinazosimamiwa na Wizara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya Marekebisho ya Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura **388** na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Sura 280. Vilevile, Wizara imefanya marekebisho ya kanuni zifuatazo: *The Fisheries (**Amendment**) Regulations, GN. Na. **539V/2024** Fisheries Laboratory Fees GN.Na.**539W/2024**;* na *The Meat Industry (**Location, Design, Construction and Operation of Livestock Market**) (**Amendment**) Regulations, GN.Na.**539Q/2024;*** na *The Fisheries (**Amendment**) Regulations GN. Na. **251/2025**.*

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuendeleza shughuli za ukuzaji viumbe maji, Wizara imeandaa Kanuni za Ukuzaji Viumbe Maji **(*The Fisheries Aquaculture Regulation*)** GN. Na. ***885/2024***. Kanuni hii inalenga kuhakikisha shughuli za ukuzaji viumbe maji zinatekelezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Aidha, Kanuni zilizofanyiwa marekebisho ni: *The Fisheries (**Amendment**) Regulations, GN. Na. **539V/2024;** Fisheries Laboratory Fees GN.Na.**539W/2024***; na *The Meat Industry (**Location, Design, Construction and Operation of Livestock Market**) (**Amendment**) Regulations, GN.Na.**539Q/2024;*** na *Fisheries (**amendiments**) Regulation GN. Na **251/2025.***

34. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Kanuni ya Uvuvi ya Mwaka 2009 na kuandaa kanuni mpya ili iendane na mabadiliko ya kisera, kiuchumi na kiteknolojia. Kanuni mpya inalenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kulinda maeneo muhimu ya mazalia na makuzi ya samaki,

kudhibiti mbinu, njia, zana na teknolojia za uvuvi; na kuboresha mazingira ya biashara kwa kulinda usalama na ubora wa mazao ya uvuvi. Kadhalika, kuimarisha usimamizi na udhibiti wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na kuzalisha nyavu, maduka ya samaki na kusambaza zana za uvuvi, uzalishaji na usambazaji wa barafu. Pia, Kanuni zinalenga kukidhi matakwa, masharti na viwango vya masoko ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuandaa na kuhuisha miongozo mbalimbali ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi ili kuwa na uvuvi endelevu. Aidha, Mwongozo wa Usimamizi wa Uvuvi katika Maji Madogo na Maeneo Oevu; Waraka wa Wavu wa Dagaa katika Ziwa Victoria; na Waraka wa Wavu wa Dagaa na Migebuka katika Ziwa Tanganyika zimeandaliwa.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) ikishirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi; na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (***SMT/SMZ***) ilifanya mapitio ya Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya **388** ya Mwaka 2020 ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 3 Septemba, 2024. Maboresho hayo yanalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi wa uvuvi na kuimarisha masuala ya kiutendaji ya DSFA.

37. ***Mheshimiwa*** Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara ilipewa maelekezo ya kuunganisha Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) na Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) ili kuunda taasisi moja na kuongeza ufanisi katika kuendeleza mazao hayo. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara imekamilisha kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutunga Sheria ya Bodi ya Mazao na Miundombinu ya Mifugo Tanzania ya Mwaka 2025, ambapo Waraka huu upo kwenye ngazi ya maamuzi. Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Uvuvi, Sura 279. Mapendekezo ya marekebisho yanajumuisha kipengele cha kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji Tanzania ambayo itakuwa na jukumu la

kuendeleza, kusimamia, kudhibiti, na kuhifadhi rasilimali za uvuvi na ukuzaji Viumbe Maji.

## D. UZALISHAJI, MASOKO NA UBORESHAJI WA MBARI ZA MIFUGO

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kupata mifugo bora na ufugaji wenye tija. Maeneo yaliyopewa umuhimu mkubwa ni pamoja na kuimarisha huduma za Uhimilishaji; Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba; Uzalishaji wa Kuku wa Nyama na Mayai pamoja na kuboresha Biashara ya Mifugo na Mazao yake.

### Huduma ya Uhimilishaji

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa (National Artificial Insemination Center- NAIC) ni kituo pekee cha Serikali kinachotoa huduma ya uhimilishaji nchini Tanzania. Kituo hiki ni muhimu kwa mikakati ya Serikali ya kuboresha mifugo nchini ili kuongeza tija ya uzalishaji wa nyama na maziwa. Kituo kina jumla ya madume bora ya ng'ombe wa nyama na maziwa **35** ambayo huzalisha mbegu kwa ajili ya uhimilishaji. Katika Mwaka 2024/2025, madume hao 35 wamezalisha jumla ya dozi za mbegu **110,434** sawa na asilimia **73.62** ya lengo la kuzalisha dozi **150,000**. Aidha, kati ya dozi hizo zilizozalishwa, dozi **92,587** zimesambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya kuhimilisha mifugo yao. Pia Kituo cha Uhimilishaji kimepokea dozi za mbegu **5,200** kutoka kwa wadau wa nje ikiwemo dozi **4,200** za mbegu ya ng'ombe wa maziwa na dozi **1,000** za ng'ombe wa nyama ambazo zimesambazwa kwa wafugaji. Vilevile, Kituo kimeendelea kuwajengea uwezo wahimilishaji ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya wahimilishaji **232** kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) wamepatiwa mafunzo na wamewezesha uhimilishaji wa ng'ombe **72,731** katika mikoa **26.** Uhimilishaji huo wa mifugo kwa mwaka 2025 umeendelea kukua ikilinganishwa na ng'ombe **67,355** waliohimilishwa katika kipindi kama hicho Mwaka 2023/2024.

### Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuendelea kuboresha mbari za mifugo nchini, Serikali inaendelea kuyaimarisha mashamba matano (**5**) ya kuzalisha mifugo yenye jumla ya ng'ombe **6,542**. Aidha, katika Mwaka 2024/2025, mashamba hayo

yamezalisha jumla ya mitamba bora **416** sawa na asilimia **41.6** ya lengo la kuzalisha mitamba **1,000** na mitamba **147** imesambazwa kwa wafugaji. Pia, mashamba ya watu binafsi (**8**) yamezalisha mitamba bora **3,066** na kusambaza mitamba **2,893**. Vilevile, Serikali itaendelea kuboresha mashamba yake kwa kuwekeza zaidi kutokana na ongezeko la mahitaji ya mitamba ili kutosheleza mahitaji hayo.

41. ***Mheshimiwa spika***, ili kuongeza tija na uzalishaji wa mifugo nchini, Serikali imeboresha mbari za mifugo ambapo katika kipindi cha Mwaka 2024/2025, imeingiza jumla ya ng'ombe **4,345** na mbuzi/kondoo **45,292** wa mbegu. Mifugo hiyo, imeingizwa kutoka nchi za Kenya, Afrika kusini, Malawi, Zambia, Burundi, Namibia, Korea kusini na Uganda. Aidha, kwa madhumuni hayohayo, jumla ya dozi **32,211** za mbegu za ng'ombe ziliingizwa kutoka nchi za Indonesia, Denmark, Brazil, Canada, Uingereza na Marekani. Kati ya hizo, dozi **31,138** hazijatenganishwa kijinsi, dozi **1000** zimetenganishwa kijinsi na dozi **73** ni za viinitete kwa ajili ya shughuli za kiutafiti.

**Uzalishaji wa Kuku wa Nyama na Mayai**

42. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kuweza kuwekeza kwenye sekta ya kuku ili kutoa ajira kwa wananchi walio wengi hasa vijana na wanawake. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya mashamba 25 ya kuku wazazi na vitotoleshi 28 yenye mtaji wa shilingi **543,999,040,000** yameanzishwa. Aidha, uwekezaji huo umewezesha kuzalisha jumla ya vifaranga vya kuku **71,526,458** ambavyo vimesambazwa kote nchini. Kati ya vifaranga hivyo, **59,112,160** ni vya kuku wa nyama, **3,726,804** vya kuku wa mayai na **8,687,494** vya kuku chotara.

43. **Mheshimiwa *Spika*,** kutokana na uwekezaji uliofanyika kwenye mashamba ya kuzalishia vifaranga nchini umepelekea kupungua kwa uingizaji wa vifaranga vya kuku wazazi (Day Old Chicks Parent Stock – DOC) kutoka **1,371,746** mwaka 2023/2024 hadi vifaranga **1,157,974** mwaka 2024/2025. Aidha, mauzo ya vifaranga kwenda nje ya nchi yamepungua kutoka vifaranga **2,701,429** mwaka 2023/2024 hadi vifaranga **1,909,078** mwaka

2024/2025. Upungufu wa mauzo ya vifaranga nje ya nchi umetokana na kuimarika kwa soko la ndani hususani uanzishwaji wa mashamba makubwa yanayofuga kuku kibiashara (Broiler and layers commercial farms) kama vile Voncavy Morogoro, Hills Bagamoyo, Kerege Bagamoyo, Akaji- Bagamoyo na Interchick ambapo mahitaji ya mashamba hayo yamekuwa makubwa.

44. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wadau wa Maendeleo kwa kushirikiana na Serikali wameendelea kuimarisha Tasnia ya Kuku nchini kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha vyama vya wafugaji kwa kuanzisha *Tanzania Poultry Executive Compact Committee* (TPECC) yenye wajumbe toka Serikalini na Sekta Binafsi kwa lengo la kuhakikisha Tasnia ya Kuku nchini inaratibiwa na kupewa msukumo wa kipekee. Kwa muda wa mwaka mmoja Kamati hiyo imeonesha mafanikio katika Tasnia ya Kuku ikiwemo kuandaa Mpango Mkakati wa Tasnia ya Kuku na kufanya kongamano lililowaleta pamoja wadau **2,000** wa Tasnia ya Kuku toka nchi zote zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

**Biashara ya Mifugo na Mazao yake**

45. **Mheshimiwa *Spika*,** hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya ng'ombe **3,411,000,** mbuzi na kondoo **3,330,000** wenye thamani ya shilingi trilioni **3.7** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **2,957,724** na mbuzi na kondoo **2,828,243** waliokuwa na thamani ya shilingi trilioni **3.4** waliouzwa katika Mwaka 2023/2024. Ongezeko la mifugo iliyouzwa katika minada linatokana na kuhamasika kwa wafugaji kuvuna mifugo yao.

46. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza Mkakati wa kukuza mauzo nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza fedha za kigeni, Wizara kupitia Bodi ya Nyama imeendelea kuratibu mauzo ya nyama kwenda nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya tani **9,863.41** za nyama zimeuzwa sawa na asilimia **89.9** ya lengo la kuuza tani **10,971**. Kiasi hicho kinajumuisha tani **1,150.54** za nyama ya ngómbe, tani **6,380.63** za mbuzi, tani **2,104.85** za kondoo, tani **199.61** za nyama ya kuku na tani **27.83** za nguruwe zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni **44.07** zimeuzwa katika masoko ya nje ya nchi ikilinganishwa na tani **9,326.3** zenye thamani ya Dola

za Kimarekani milioni **39.3** zilizouzwa kipindi kama hicho katika Mwaka 2023/2024. Mauzo kwa Mwaka 2024/2025 yameongezeka kwa asilimia **5.75** ikilinganishwa na mauzo yaliyofanyika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita. Aidha, nyama ya mbuzi imeendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia **64.69** ya mauzo ya nyama nje. Hii ni kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya kuongeza ushirikiano na fursa za kibiashara nje ya nchi, masoko ya nyama yameendelea kuongezeka kufikia nchi **11** ambazo ni Bahrain, Comoro, Hong Kong, Jordan, Kenya, Kuwait, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*) na Vietnam.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa (*Tanzania Dairy Board-TDB*) imeendelea kusimamia biashara ya maziwa nchini ambapo jumla ya lita za maziwa **90,416,788.5** zenye thamani ya shilingi bilioni **226** zilisindikwa na kuuzwa katika masoko ya ndani ya nchi. Aidha, vibali vya kuingiza maziwa kutoka nje ya nchi vimepungua kutoka 782 vyenye jumla ya lita **11,747,150** zenye thamani ya shilingi **23,423,652,811.8** Mwaka 2023/2024 hadi vibali **630** vyenye jumla ya lita **10,089,767.50** zenye thamani ya shilingi **22,969,085,568.85**. Kupungua kwa kiasi cha maziwa yanayoingizwa nchini kutoka nje ya nchi kunatokana na juhudi za Serikali za kuweka mazingira mazuri kwa Sekta Binasi, hivyo kuwezesha ongezeko la usindikaji ndani ya nchi. Kwa sasa, Kiwanda cha Kusindika Maziwa cha *ASAS Dairies* kimeanza uzalishaji wa maziwa ya unga. Kiwanda hicho kina uwezo wa kusindika lita 100,000 za maziwa ya unga kwa siku.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa biashara ya mazao ya mifugo nchini kwa Mwaka 2024/2025, kumechangia kuongezeka kwa ulaji wa mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka. Mathalani, kiwango cha unywaji wa maziwa kimeongezeka kutoka wastani wa lita **67.5** Mwaka 2023/2024 hadi lita **68.1** Mwaka 2024/2025, ulaji wa nyama kutoka kilo **16** Mwaka 2023/2024 hadi kilo **17.6** Mwaka 2024/2025 na ulaji wa mayai kutoka **107** Mwaka 2023/2024 hadi **119** Mwaka 2024/2025 kwa mtu kwa mwaka. Pamoja na ongezeko hilo, ulaji wa mazao hayo bado haujafikia viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa

Mataifa (FAO) ambavyo ni lita **200** za maziwa, kilo **50** za nyama na mayai **300** kwa mtu kwa mwaka.

49. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa ngozi umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika Mwaka 2024/2025, jumla ya vipande vya ngozi **15,191,500** (***ng'ombe 4,735,000, mbuzi* 7,728,000 *na kondoo* 2,728,000**), vyenye thamani ya shilingi **34**,**125,750,000** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni **14.69** (***ng'ombe milioni* 4.6, *mbuzi milioni* 7.5 *na kondoo milioni* 2.6**), vyenye thamani ya shilingi bilioni **32.1**, vilivyozalishwa Mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limechangiwa na wadau kupatiwa mafunzo kuhusu ufugaji wa kisasa, uchunaji wa ngozi na uhifadhi wa ngozi.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** biashara ya ngozi imeendelea kuimarika na kuchangia katika Pato la Taifa, hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya vipande **1,651,088** vya ngozi vyenye uzito wa kilo **6,287,881** (*ng'ombe vipande* **1,232,833**, *mbuzi vipande* **298,978** *na kondoo vipande* **119,277**) vyenye thamani ya shilingi bilioni **7.95** viliuzwa katika nchi za Nigeria, Kenya, Djibout, Ethiopia, China na Pakistan ikilinganishwa na vipande vya ngozi **1,542,916** vyenye uzito wa kilo **5,777,669.5** (*ng'ombe vipande* **1,034,447**, *mbuzi* **355,928** *na kondoo vipande* **152,541**) vyenye thamani ya shilingi **bilioni 7** vilivyouzwa katika nchi za Nigeria, Kenya, Ghana, Togo, Ethiopia na Pakistan Mwaka 2023/2024. Aidha, mauzo ya ngozi kwenda nje ya nchi yameongezeka kutokana na mahitaji ya soko la ngozi isiyosindikwa kuongezeka katika nchi za Nigeria na Togo. Pia, Wizara imewawezesha wamiliki wa machinjio za kisasa zilizo chini ya *Export Processing Zone Authority* (EPZA) kwa kuwaondolea kodi ya kusafirisha ngozi nje ya nchi. Hatua hii imeleta mafaniko ya kupata soko la ngozi ya mbuzi na kondoo nje ya nchi.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Tasnia ya Ngozi imeendelea kusimamia biashara na ubora wa ngozi kwa kusajili na kutoa leseni kwa maghala **44** ya ngozi kwa kampuni zinazosafirisha ngozi kwenda nje ya nchi. Aidha, katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Sekta Binafsi kutoa mafunzo kuhusu uendelezaji wa zao la ngozi nchini. Wakaguzi wa

ngozi **20** wa mikoa ya Kilimanjaro na Tanga wamejengewa uwezo kuhusu utambuzi wa ngozi bora. Pia, wachunaji wa ngozi **280** kutoka machinjio ya Tanga na Dar es salaam wamejengewa uwezo kuhusu uchunaji bora wa ngozi unaozingatia mahitaji ya soko.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika ngozi ambapo hadi Aprili 2025, viwanda vitatu (**3**) vinavyofanya kazi ambavyo ni: Himo Tanners and Planters (***Kilimanjaro***); ACE Leather (T) Ltd. (***Morogoro***); na Phiss Tanners (***Pwan***i). Viwanda hivyo vinasindika ngozi hatua ya kati na mwisho. Viwanda hivyo vinasindika jumla ya vipande **212,100** vya ngozi ya ng'ombe na **814,000** vya ngozi ya mbuzi na kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni **21.5** (***Kiambatisho Na*.6).** Aidha, Wizara imefanikiwa kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa malighafi bora kwa kuwaunganisha wamiliki wa viwanda vya kusindika ngozi na wazalishaji wa ngozi. Pia jumla ya vipande **270,921** vya ngozi za kondoo na mbuzi vilivyosindikwa (wet blue) vimeuzwa katika nchi za Pakistan, China na Djibout kwa thamani ya shilingi **348,264,335.**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza thamani ya zao la ngozi, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi ambapo katika Mwaka 2024/2025, jumla ya jozi za viatu **3,391,200** zimezalishwa ikilinganishwa na jozi **3,028,700** zilizozalishwa Mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs) **151** wanaotengeneza bidhaa za ngozi pamoja na ongezeko la upatikanaji wa ngozi bora (***Kiambatisho Na***. 7).

**Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara, imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo ambapo imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa mabwawa manne (**4**) ya Bukabwa (***Butiama***), Kihumbu (***Bunda***), Isulamilomo (***Nsimbo***), na Kwenikwembe (***Kilindi***). Mabwawa haya yana uwezo wa kuhifadhi wastani wa lita milioni **120** za maji kila moja yanayotosheleza kunywesha uniti za mifugo (***livestock unit***) takribani **100,000** kwa mwaka. Utekelezaji wa kazi

ya ujenzi wa mabwawa haya umeongeza upatikanaji wa maji kwa mifugo hivyo kuchangia katika ustawi wa mifugo katika maeneo hayo.

55. ***Mheshimiwa Spika**,* katika jitihada za kuendelea kutenga maeneo ya malisho, katika Mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, imeandaa mipango ya matumizi ya ardhi iliyowezesha kutenga hekta **23,589.70** za maeneo ya malisho. Mipango hiyo imefanyika katika vijiji **58** vya Wilaya **10** za Bariadi (***Simiyu***), Chunya (***Mbeya***) Buhigwe (***Kigoma***), Shinyanga (***Shinyanga***), Sumbawanga (***Rukwa***), Mlele (***Katavi***), Kaliua, Nzega (***Tabora***), Mbongwe (***Geita***) na Morogoro DC (***Morogoro***) na kufanya ardhi iliyotengwa kwa ajili ya malisho kufikia hekta **3,489,701.13** kutoka hekta **3,466,111.43** Mwaka 2023/2024. Aidha, hadi kufikia 2024/2025 kati ya maeneo hayo, hekta **1,349,486.29** kwenye vijiji **365** zimepimwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

56. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa malisho na mbegu za malisho, Serikali imeendelea kuwekeza kwenye mashamba yake kwa kuongeza eneo la uzalishaji wa malisho na kutoa hamasa kwa wafugaji kupitia mashamba darasa, kulima na kuendeleza maeneo ya malisho. Katika Mwaka 2024/2025, jumla ya tani **222.54** za mbegu za malisho (***nyasi, mikundekunde na vipando***) zenye thamani ya shilingi bilioni **1.7** zimezalishwa**,** ikilinganishwa na tani **127.8** zilizozalishwa Mwaka 2023/2024. Pia, jumla ya tani 1**4,185** za malisho (***hei na saileji***) zenye thamani ya shilingi bilioni **3.8** zimevunwa na kusindikwa katika mashamba ya Serikali na Binafsi ikilinganishwa na tani **4,744** zilizovunwa Mwaka 2023/2024.

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uzalishaji na utendaji kazi katika mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na mbegu, katika Mwaka 2024/2025, Wizara imekamilisha ujenzi wa ghala katika shamba la malisho lililopo katika Kituo cha TALIRI Mpwapwa kwa ajili ya kuhifadhia malisho na mbegu za malisho. Vilevile, ujenzi wa ghala katika Shamba la Mbegu za Malisho la Vikuge (***Kibaha***) unaendelea na umefikia asilimia **60,** huku katika Shamba

la Mbegu za Malisho la Langwira (***Mbarali***) ujenzi ukiwa umefikia asilimia **45**.

**Utatuzi wa Migogoro Baina ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi**

58. ***Mheshimiwa Spika***, mahusiano mazuri baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ni nyenzo muhimu katika uzalishaji, ustawi na maendeleo ya Sekta ya Mifugo. Ili kuimarisha mahusiano hayo, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwajengea uwezo wafugaji kuhusu umuhimu wa kumiliki na kuendeleza ardhi ya malisho na ufugaji wenye tija. Mathalani, Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa mashamba darasa ya malisho na kushiriki katika utekelezaji wa Kampeni ya TUTUNZANE Mvomero, Morogoro. Kampeni ya TUTUNZANE Mvomero ilizinduliwa na Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 3 Agosti, 2024 kwa lengo la kuhamasisha wafugaji kumiliki ardhi kwa ajili ya malisho, kuendeleza ardhi ya malisho kwa kuotesha malisho na kuzingatia hifadhi ya mazingira.

Wizara imewezesha Kampeni hiyo kwa kutoa jumla ya kilo **15,000** za mbegu za malisho, aina ya *Juncao,* na kilo **527** za mbegu za malisho aina ya *Rhodes,* kwa wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini. Lengo la kugawa mbegu hizo kwa wafugaji ni kuongeza upatikanaji wa malisho na hivyo kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

**Ushirikishwaji wa Wadau katika Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (***World Wildlife Fund*** – **WWF**), kupitia Programu ya SOKNOT, imewezesha ujenzi wa mbauti tatu (**3**) za kunyweshea Mifugo katika Wilaya ya Mwanga, uanzishwaji wa mashamba darasa manne (**4**) ya malisho, yenye ukubwa wa ekari mbili (**2**) kila moja, katika Wilaya ya Longido (***Lerang'wa, Sinya, Tingatinga na Olmolog***) na mashamba darasa mawili (**2**) katika Wilaya ya Mwanga (***Karambandea***) yenye ukubwa wa ekari tano (**5**) kila moja, ambayo yataendelea kutumika katika kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji wa malisho.

60. ***Mheshimiwa Spika***, sanjari na kuanzisha mashamba darasa, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali la Watu na Wanyama Pori (***Tanzania People and Wildlife*** -**TPW**), imewezesha uendelezaji wa ekari **1,300** katika vijiji **24** kwa kuondoa vichaka, mimea vamizi na kudhibiti mmomonyoko wa udongo kwa kufukia makorongo, yenye urefu wa kilometa **75,** katika kongani za malisho za Lelek, Muriamunyi, Muriatata katika Wilaya ya Longido, pamoja na Mwada – Nkaiti katika Wilaya ya Babati. Ushirikiano wa Serikali na TPW pia umejenga uwezo wa jamii za wafugaji katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara kuhusu usimamizi na uendelezaji wa nyanda za malisho kwa njia endelevu, kuboresha miundombinu ya maji na malisho, kuimarisha mfumo wa kutatua na kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**Uendelezaji wa Rasilimali za Vyakula vya Mifugo**

61. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa maeneo ya kuzalisha, kuuza na kuhifadhi rasilimali za vyakula vya Mifugo, ambapo katika mwaka 2024/2025 jumla ya maeneo **803** (***279 ya kuzalisha, 437 ya kuuza na 87 ya kuhifadhi rasilimali za vyakula vya Mifugo***) yamekaguliwa na kupatiwa vibali kwenye mfumo wa utoaji vibali wa Mifugo Intergrated Management Information System – MIMIs. Aidha, jumla ya maeneo mapya **29** {***Arusha (4), Dar es Salaam (11), Morogoro (2), Pwani (6), Njombe (2), Tanga (1), Manyara (1), Rukwa (1) na Kigoma (1)***} ya kuzalisha vyakula vya Mifugo yamesajiliwa. Usajili huu umeongeza maeneo ya kuzalisha vyakula vya Mifugo kutoka **250** mwaka 2023/2024 hadi **279** mwaka 2024/2025.

62. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya biashara ya vyakula vya mifugo ndani na nje ya nchi na kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika usindikaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa. Katika Mwaka 2024/2025, jumla ya tani **720,000** za vyakula vya mifugo, zenye thamani ya shilingi trilioni 1.15, zilizalishwa ikilinganishwa na tani **380,000** kwa Mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia 89.47. Aidha, kati ya vyakula hivyo vilivyosindikwa; Tani **504,000** ni vyakula vya kuku wa nyama na mayai, sawa na asilimia **70;** Tani **144,000** ni vyakula vya

nguruwe, sawa na asilimia **20;** na Tani 72,000 ni vyakula vya ng'ombe wa maziwa, sawa na asilimia **10**.

**Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani wa Mifugo na Uvuvi**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuratibu, kuwezesha na kusimamia shughuli za utafiti wa mifugo na uvuvi nchini. Kazi hizo zimefanyika katika vituo nane (**8**) vya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (***TALIRI***) na vituo vitano (**5**) vya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (***TAFIRI***). Aidha, jumla ya Tafiti **67** zimeratibiwa kati ya **52** zilizopangwa.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI na TAFIRI imesambaza teknolojia **14** zilizozalishwa kutokana na tafiti zilizofanywa kwa lengo la kuwafikia wadau katika mnyororo wa thamani wa mifugo na uvuvi. Teknolojia mbalimbali zikiwemo mbari bora za ng'ombe, mbuzi na kuku; Udhibiti wa vimelea sugu vya magonjwa; Malisho bora ya mifugo; Vikusanyia samaki na uongezaji wa thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi. Vilevile, teknolojia bunifu ya "*Vua, Uza, Nunua Kidigitali*" imeanzishwa kwa ajili ya kuwapunguzia wavuvi gharama za uvuvi na kurahisisha biashara ya samaki nchini.

**Mafunzo**

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuratibu, kuwezesha na kusimamia shughuli za Mafunzo ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Mifugo na Uvuvi (***LITA na FETA***). Jumla ya wanafunzi **6,013** wamedahiliwa kati ya **6,430** waliopangwa kudahiliwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu (***Sustainable Agriculture Tanzania - SAT***) imehuisha mitaala mitatu (**3**) ambayo ni *Animal Health and Production*; *Bioscience Laboratory Technology*; na *Range Management and Animal Feed Production Technology*; na kuandaa mitaala miwili mipya ya *Meat Technology*; na *Dairy Technology*. Mitaala hiyo itawezesha vyuo vya mafunzo ya Mifugo kutoa elimu kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

**Huduma za Ugani**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kurahisisha Utoaji wa Huduma za Ugani, Wizara imeendelea kuhamasisha wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbe maji kuunda vikundi na vyama vya ushirika. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya vikundi 960 vya wafugaji na vyama vya ushirika **62** vyenye wafugaji **29,265** vimeanzishwa. Aidha, Wizara imeendelea kutoa huduma za ugani kwa wananchi kupitia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Siku ya Chakula Duniani ambapo jumla ya wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbe maji **192,370** wamepatiwa huduma hizo.

**Utekelezaji wa Programu ya BBT**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) kwa vijana ili kuwawezesha kujiajiri kupitia uwekezaji katika shughuli za ufugaji nchini. Kupitia Programu hiyo, jumla ya vikundi **20** vyenye vijana 106 wamepatiwa ekari **1,761** katika Ranchi ya Kagoma na kupewa mkopo usio na riba wa jumla ya shilingi **934,231,000** kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa ajili ya kuendesha shughuli za unenepeshaji ng'ombe.

68. ***Mheshimiwa Spika***, vijana hao walianza kazi ya unenepeshaji wa ngo'mbe Januari, 2025 ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya ng'ombe **627** wenye thamani ya shilingi **451,440,000** walinunuliwa na kunenepeshwa kwa wastani wa shilingi **720,000** kwa kila ng'ombe. Kati ya ng'ombe hao, **452** wenye thamani ya shilingi **402,280,000** waliuzwa kwa wastani wa shilingi **890,000** kwa kila ng'ombe na kupatikana kwa faida ya shilingi **76,840,000** ikiwa ni wastani wa faida ya shilingi **170,000** kwa kila ng'ombe.

**Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa chanjo za magonjwa mbalimbali ya mifugo ambapo katika Mwaka 2024/2025, jumla ya dozi **728,153,645** sawa na asilimia **65** ya lengo la mwaka la dozi **1,120,000,000** zimesambazwa nchini. Kati ya chanjo zilizosambazwa, jumla ya dozi **153,952,375** zimezalishwa na viwanda vya ndani ya nchi ambapo dozi **58,822,475** zimetoka Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) na dozi **95,129,900** zimezalishwa

na viwanda binafsi. Aidha, dozi **574,201,270** zimeingizwa kutoka nje ya nchi. Serikali inaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza zaidi ili kuongeza uzalishaji na aina za chanjo ili kupunguza utegemezi wa chanjo kutoka nje na kuongeza ajira nchini.

**Uchanjaji wa Mifugo Dhidi ya Magonjwa ya Kipaumbele**
69. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kudhibiti magonjwa yanayovuka mipaka kwa kusimamia na kuratibu shughuli za uchanjaji wa mifugo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya dozi **398,752,227** za chanjo mbalimbali za mifugo zimetumika kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele. Aidha, mifugo iliyochanjwa ni Ng'ombe **4,970,170** dhidi ya Homa ya Mapafu; Ng'ombe **1,811,295** dhidi ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo**;** Ng'ombe **27,790** dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba; Ng'ombe **719,694** dhidi ya Chambavu**;** Ng'ombe **79,117** dhidi ya Ndigana Kali na Ng'ombe **130,780** dhidi ya Mapele ya Ngozi**.** Pia chanjo zingine zilizotolewa ni pamoja na Kimeta kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo **2,420,160;** Kichaa cha Mbwa na Paka **290,519;** na Sotoka kwa Mbuzi na Kondoo **1,582,811.**

Vilevile, uchanjaji wa kuku umefanyika dhidi ya Mdondo kuku **199,592,105**, Gumboro kuku **61,256,411,** Mahepe kuku **115,977,094,** na Ndui kuku **10,105,719.** Uchanjaji wa mifugo unaiwezesha Tanzania kuendelea kukidhi masharti ya biashara ya mifugo na mazao yake kulingana na matakwa ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Biashara Duniani (WTO) na hivyo kuongeza fedha za kigeni na mchango katika Pato ghafi la Taifa (GDP).

**Uogeshaji wa Mifugo**
71. **Mheshimiwa *Spika,*** Serikali inaendelea kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengine kwa kuratibu uogeshaji wa mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya michovyo **1,337,306,118** ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng'ombe **619,731,619**, mbuzi **497,805,601**, kondoo **198,572,994** na punda **21,195,904**. Michovyo hii ni sawa na asilimia **66.9** ya lengo la mwaka la michovyo

**2,000,000,000**. Aidha, uogeshaji wa mifugo umesaidia kupunguza matukio ya vifo vya mifugo nchini kutoka asilimia **48** ya vifo vyote katika Mwaka 2023/2024 hadi asilimia **45** kufikia Aprili, 2025.

**Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kampeni ya chanjo na kujenga uelewa kwa wadau juu ya Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, Wizara imefanya uzinduzi wa hamasa ya kampeni ya chanjo kitaifa kwa kufanya kikao kazi kilichofanyika Mkoani Dodoma tarehe 18-19/12/2025. Kikao kazi hicho kiliwakutanisha jumla ya wadau **762** wakiwemo Makatibu Tawala wa Mikoa **26**, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Sehemu ya Mifugo na Maafisa TEHAMA kutoka Halmashauri **184**, wawakilishi wa vyama vya kitaaluma (TVA, TAVEPA na TSAP), viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya wafugaji na wafugaji kutoka Halmashauri **184** Tanzania Bara. Aidha, Wizara imefanya kikao cha hamasa juu ya Kampeni kwa jumla ya wafugaji na vyama vya wafugaji **189** kutoka halmashauri **184** Tanzania Bara. Katika kikao hicho mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo umuhimu wa chanjo na utambuzi wa mifugo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mwongozo wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa ambao umeainisha majukumu ya kila mdau katika Kampeni hii. Mwongozo huo umesambazwa kwa wadau wote kwa ajili ya utekelezaji.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za udhibiti wa magonjwa ya mifugo na kuendelea kukidhi vigezo vya biashara ya mifugo kikanda na kimataifa, Serikali inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa kwa kununua na kusambaza chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe **(Contagious Bovine Pleuropneumonia - CBPP)** dozi **19,099,100** kwa ajili ya kuchanja jumla ya ng'ombe **19,099,100** na chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo **(Peste des Petits Ruminants - PPR)** dozi **17,230,000** kwa ajili ya kuchanja mbuzi na kondoo **17,230,000** na chanjo ya Mdondo wa Kuku **(Newcastle Disease-ND)** dozi **40,000,000** kwa ajili ya kuchanja kuku wa asili **40,000,000.** Chanjo hizi zimezalishwa na viwanda vilivyopo ndani ya nchi. Aidha, ili kuwezesha Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya kuchanjia, pikipiki **700**

na vishikwambi **4,500.** Pia, Wizara imeandaa mgao wa chanjo, vifaa vya chanjo na kuwasilisha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

74. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za afya ya wanyama nchini zikiwemo tiba na chanjo kwa mifugo, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania limesajili madaktari wa wanyama **57** kati ya **80** waliotarajiwa kusajiliwa. Ongezeko hili la madaktari waliosajiliwa linafanya idadi yao kufikia **1,013,** kati yao wanaume ni **901** na wanawake ni **112**. Aidha, wataalamu wasaidizi **575** wa afya ya wanyama wameandikishwa na kuorodheshwa kati ya wataalamu wasaidizi **3,000** waliotarajiwa kuorodheshwa na kufanya idadi yao kufikia **6,315,** kati yao wanaume ni **4,014** na wanawake ni **2,301**. Pia, leseni 34 zimetolewa kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji **13** na wataalamu **14** wa maabara, Idadi hiyo inafanya wakaguzi wa nyama kufikia **967**, wahimilishaji **103** na wataalamu **96** wa maabara. Vituo **355** vya kutolea huduma za afya ya wanyama vimesajiliwa kati ya vituo **300** vilivyotarajiwa kusajiliwa na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia **2,834**. Usajili wa vituo vya kutolea huduma za afya ya wanyama umeongezeka kupita lengo lililowekwa kutokana na kuhamasika kwa wadau mbalimbali kuwekeza katika huduma.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi wa huduma za afya ya wanyama, Wizara kupitia Baraza la Veterianari Tanzania imefanya ukaguzi wa vituo **1,249** kati ya vituo **2,578** vya kutolea huduma za afya ya wanyama vilivyotarajiwa kukaguliwa. Aidha, vyuo **11** vya mafunzo ya afya na uzalishaji wa wanyama kati ya vyuo 21 vimekaguliwa ambavyo ni Chuo cha LITA Mpwapwa, Visele na TRACID (Dodoma), Kaole (Bagamayo), Borigaram (Kigamboni), CANRE (Bonyokwa), Kilacha (Kilimanjaro), Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji, NAIC (Arusha), DECOHAS (Dodoma), Hagafilo (Njombe) na Dabaga (Iringa). Ukaguzi huo umebainisha umuhimu wa kuimarisha mafunzo kwa vitendo ili wahitimu wawe na weledi wa kutosha.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa wataalamu wa afya ya wanyama wanakuwa na weledi na umahiri unaohitajika, Baraza la Veterinari Tanzania limeendelea kusimamia mafunzo ya uanagenzi kwa wahitimu wa Shahada ya Udaktari wa Wanyama. Aidha, wahitimu **76** wanaendelea na mafunzo hayo katika vituo **40** vilivyopo Tanzania Bara na Zanzibar, kati ya wahitimu **170** waliotarajiwa kujiunga na mafunzo hayo. Aidha, mitihani ya kuandikisha wataalamu wa stashahada ya afya na uzalishaji wa wanyama imefanyika kwa wahitimu **1,358** kati ya wahitimu **1,500** wa stashahada ya afya ya wanyama waliotarajiwa kufanya mtihani huo.

**Uzalishaji wa Samaki katika Maji ya Asili**

77. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji na upatikanaji wa samaki katika maji ya asili umeendelea kuimarika nchini. Hadi kufikia Aprili 2025, kiasi cha tani **466,956.88** za samaki zenye thamani yaq shilingi trilioni 3.12 zilivunwa sawa na asilimia **101.88** ya lengo la kuvuna tani **458,333.33**, ikilinganishwa na tani **429,168.39** zenye thamani ya shilingi trilioni **2.94** zilizovunwa katika kipindi kama hiki Mwaka 2023/2024. Uzalishaji wa samaki katika Mwaka 2024/2025 umeongezeka kwa asilimia **16.31** ikilinganishwa na Mwaka 2023/2024. Aidha, ongezeko hili limechangiwa na juhudi za Mheshimiwa. **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwawezesha wavuvi kupata vifaa vya kisasa na pembejeo zikiwemo boti za kisasa.

78. ***Mheshimiwa Spika***, mgawanyo wa uzalishaji wa tani **472,579.34** za samaki katika maji ya asili kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 umejumuisha: tani **279,333.01 (59.82%)** kutoka Ziwa Victoria; tani **98,755.26 (21.15%)** kutoka Ziwa Tanganyika; tani **56,038.41** (**12%)** kutoka Bahari ya Hindi; tani **11,305.24 (2.42%)** kutoka Bwawa la Mtera; tani **9,361.73 (2%)** kutoka Ziwa Nyasa; tani **7,019.1 (1.5%)** kutoka Ziwa Rukwa; tani **2,911.26, (0.62%)** kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu; na tani **2,232.87** (**0.48%)** kutoka maji madogo.

**Upumzishaji wa Shughuli za Uvuvi kwa Muda**

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imetekeleza Mkataba wa Kikanda wa Uhifadhi wa Ziwa Tanganyika (LTA) wa upumzishaji wa Ziwa Tanganyika kuanzia tarehe **15 Mei** hadi **15 Agosti** kila mwaka ili kuongeza uzalishaji wa samaki. Katika Mwaka 2024, mavuno ya samaki yaliongezeka kwa asilimia **55.3** kufikia tani **38,999.82,** zenye thamani ya shilingi **324,845,566,002.38** katika kipindi cha miezi minne **(4)** baada ya kufungua Ziwa (Septemba – Desemba, 2024) ikilinganishwa na tani **25,113.43,** zenye thamani ya shilingi **166,476,911,002.19** kwa kipindi kama hicho Mwaka 2023 kabla ya kupumzisha Ziwa.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ongezeko la uzalishaji samaki, kiasi cha mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ya nchi kutoka Ziwa Tanganyika kwa Mwaka 2024 kiliongezeka kufikia tani **1,227.21** zenye thamani ya shilingi **180,684,608,011.64** ikilinganishwa na tani **664.11** zenye thamani ya shilingi **97,036,183,747.23** Mwaka 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia **84.79**. Pia, samaki wa mapambo waliouzwa nje ya nchi waliongezeka kutoka samaki **166,024** Mwaka 2023 hadi samaki **234,331** Mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia **41.14**.

81. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na uzoefu uliopatikana kwa kupumzisha Ziwa Tanganyika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Bukoba Vijijini pia imepumzisha Ziwa Ikimba, Kagera kwa muda wa miezi 6 kuanzia tarehe 12 Aprili mpaka 12 Septemba, 2025. Sambamba na kupumzisha Ziwa, Serikali imepandikiza vifaranga vya samaki **2,000,000** ili kuongeza uzalishaji wa samaki wa asili kwa lengo la kuongeza kipato na lishe kwa maeneo yanayozunguka Ziwa hilo. Aidha, Serikali inaendelea na utafiti wa uwezekano wa ufugaji wa kutumia teknolojia ya vizimba kwa maziwa makuu, mabwawa na maji madogo nchi nzima.

**Biashara ya Mazao ya Uvuvi**

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia biashara ya mazao ya uvuvi. Biashara ya mazao hayo imeendelea kuimarika katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025, jumla ya tani **44,317.78** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **176,009**

wenye thamani ya shilingi **527,881,020,227.09** waliuzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrahaba wa shilingi **15,534,200,070.45.** Aidha, katika kipindi cha 2023/2024 tani **41,271.07** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **134,572** wenye thamani ya shilingi **515,781,009,645.78** waliouzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrahaba wa shilingi **14,446,071,447.27.** Ongezeko la mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi Mwaka 2024/2025 ni asilimia **7.38** ikilinganishwa na Mwaka 2023/2024.

83. ***Mheshimiwa Spika*** katika Mwaka 2024/2025, jumla ya tani **89.78** za samaki, zenye thamani ya shilingi **514,051,697.83** zimeingizwa nchini na kuliingizia Taifa mrahaba wa shilingi **164,379,257.57,** ikilinganishwa na tani **12.90** za samaki, zenye thamani ya shilingi **252,414,478.09** zilizoingizwa nchini na kuliingizia Taifa mrahaba wa shilingi **46,848,503.84,** katika kipindi kama hiki mwaka 2023/2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia **595.97**.

**Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi**

84. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuimarisha uhifadhi, ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Bahari ya Hindi, mabwawa ya Nyumba ya Mungu na Mtera kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali kufanya doria mbalimbali kwa siku kazi **3,168** ikilinganishwa na siku kazi **2,912** zilizofanyika Mwaka 2023/2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia **8.72** la siku kazi.

85. ***Mheshimiwa Spika***, matokeo ya doria hizo yaliwezesha kukamatwa kwa zana haramu za uvuvi, vyombo vya uvuvi na samaki wachanga zikiwemo; makokoro **334**, nyavu za makila zenye macho madogo **3,914**, nyavu za timba **10,717**, kamba za kuvutia kokoro mita **355,670**, nyavu za dagaa chini ya milimita nane **89**, vyandarua **42**, samaki wachanga kilo **50,270**, kaa hai wachanga kilo **9,766**, jongoo bahari kilo **550**, kamba koche wachanga **5,088**, nyavu za dagaa (gizagiza) chini ya **8** milimita **1,015**, mitumbwi **447**, injini za kupachika **52**, kasia **454** na watuhumiwa **942**.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanikiwa kuondoa uvuvi haramu wa kutumia vilipuzi (blast fishing) katika Ukanda wa Bahari ya Hindi ambapo kwa sasa hali hiyo imedhibitiwa kuanzia vyanzo, wasambazaji na watumiaji wa vilipuzi na kwa zaidi ya mwaka hakuna matukio ya uvuvi huo kwa ukanda wote wa Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara imeweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji ili uhalifu huo usiendelee siku zijazo. Kwa upande wa Maziwa Makuu, Wizara inaendelea na kazi ya kusafisha na kuondoa zana haramu za uvuvi. Kazi hiyo imefanikisha kugundua na kunasa mtandao mpana wa uingizaji wa nyavu haramu ambazo hutumika kwa uvuvi haramu. Mafanikio yote yanayopatikana yanatokana na ushirikishwaji thabiti wa wadau mbalimbali wa Sekta ya Uvuvi wakiwemo Viongozi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (*Beach Management Units* - BMUs) na Asasi Zisizo za Kiserikali (NGO).

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa maeneo ya mazalia na makulia ya samaki katika Ziwa Victoria kwa kuweka alama zinazobainisha mipaka ili kudhibiti shughuli za uvuvi na uharibifu wa mazingira. Hatua hiyo itawezesha samaki kukua na kuzaliana. Katika Mwaka 2024/2025 kwa kuanzia, Wizara imenunua na kusanikisha jumla ya maboya **32** ambayo yamewekwa kwenye maeneo ya mazalia ya samaki katika Halmashauri za Misungwi na Nyamagana.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

88. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuthibiti ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanya kaguzi **943** kwenye viwanda **47** vya kuchakata mazao ya uvuvi, viwanda **17** vya mabondo, maghala **135** ya kuhifadhia mazao yaliyokaushwa, maghala ya ubaridi **(*cold storage*)** **53,** vituo **37** vya kuhifadhia samaki hai wa mapambo, mialo **33** ya kupokelea samaki, mipaka, maeneo ya viwanja vya ndege na masoko ya samaki nchini.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuthibiti ubora wa mazao ya uvuvi, jumla ya vyombo **782** vya kusafirisha mazao ya uvuvi (***magari na maboti***) vilikaguliwa na kupewa cheti cha ubora (***Approval***

***Certificate***) baada ya kukidhi vigezo. Aidha, vibali vya kusafirisha mazao ya uvuvi ndani ya nchi (***Movement Permit***) **54,638** vilitolewa. Sanjari na hivyo jumla ya vyeti vya afya **12,293** (***Export Health Certificate***) vilitolewa kwa mazao ya uvuvi yanayosafirishwa nje ya nchi.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara imerasimisha maghala ya samaki wakavu na wabichi katika Mikoa ya Songwe Tunduma (**92**), Kigoma (**7**), Ukerewe (**15**), Sirari (**22**), Kagera (**5**), Mafia (**7**), Mwanza (**15**), Dar es Salaam (**28**). Lengo la kurasimisha ni kuhakikisha Wizara inaendelea kusimamia ubora na usalama wa mazao ya Uvuvi pamoja na Serikali kupata mapato na takwimu sahihi za mazao ya Uvuvi.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Serikali imeendelea kuhakikisha inapunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kwa kuongeza thamani na ubora kwa kuendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ambapo imefanikisha ujenzi wa chanja **90** za kukaushia Dagaa katika mikoa ya Tanga **20** (***Mkinga na Pangani***), Lindi **40** (***Kilwa***), Pwani **30** (***Bagamoyo na Mafia***). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya kikanda ya LVFO (*Lake Victoria Fisheries Organisation*) imetoa mafunzo kwa wadau **200** katika Mwalo wa Kijiweni, Sengerema kuhusu kuongeza thamani kwenye zao la Dagaa wa Ziwa Victoria.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mazao ya uvuvi yanauzwa katika soko la Ulaya, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) na *Trade Mark East Africa* (TMEA) iliwajengea uwezo Wakaguzi **26** kwa kuwapatia mafunzo ya ubora na viwango. Aidha, viwanda **15** (***Ukanda wa Ziwa Victoria 11 na Ukanda wa Pwani 4***) vya kuchakata mazao ya uvuvi vinavyopeleka mazao katika soko la Ulaya vilikaguliwa na kupewa vyeti vya kukidhi vigezo vya ubora na usalama. Pia, mialo **15** inayopokea samaki wanaosafirishwa kwenda soko la Ulaya ilikaguliwa.

**Maabara ya Uvuvi Tanzania**

93. ***Mheshimiwa Spika***, shughuli za uchunguzi wa samaki na mazao mengine ya uvuvi yanayoenda kwenye masoko ya ndani,

kikanda na kimataifa zimeendelea kuimarika nchini. Hadi kufikia Aprili 2025, kiasi cha sampuli **2,938** za samaki na mazao mengine ya uvuvi zilifanyiwa uchunguzi wa vimelea na kemikali sawa na asilimia **117.52** ya lengo la kufanyia uchunguzi sampuli **2,500** za samaki na mazao mengine ya uvuvi, ikilinganishwa na sampuli **2,721**, zilizofanyiwa uchunguzi katika kipindi kama hiki Mwaka 2023/2024. Uchunguzi wa sampuli katika Mwaka 2024/2025 umeongezeka kwa asilimia **8.68** ikilinganishwa na Mwaka 2023/2024. Aidha, Maabara imeendelea kuhuisha hadhi ya Ithibati kupitia kaguzi za kina za Taasisi ya Ithibati ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADCAS) na kukidhi kiwango cha kimataifa cha **ISO/IEC17025:2017**. Haya yote yamefanikiwa kutokana na juhudi za ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,*** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongeza bajeti katika Maabara hii.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

94. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika ukuzaji viumbe maji. Hadi kufikia Aprili, 2025, uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe maji umefikia tani **132,243.45** kutoka tani **43,415.95** za mwaka 2023/2024. Uzalishaji huu unajumuisha tani **43,590.45** za samaki, tani **88,615.20** za mwani mbichi, tani **2.57** za kaa, tani **35.23** za majongoo bahari na vipande **360** vya lulu. Mazao haya yana thamani ya shilingi **315,272,488,000** (**Kiambatisho Na. 8**). Ongezeko hili linatokana na juhudi za Wizara kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji katika Sekta Binafsi ili kukidhi mahitaji ya mazao ya ukuzaji viumbe maji hususani samaki. Ongezeko hili limeenda sambamba na kuongezeka kwa idadi ya miundombinu ya uzalishaji wa viumbe maji ambayo imeongezeka hadi kufikia mabwawa **34,642**, na vizimba **1,636** na vitotoleshi vya kuzalisha vifaranga **49** ikilinganishwa na mabwawa **34,417**, na vizimba **1,215** na vitotoleshi **41** mtawalia kwa mwaka 2023/2024. Ongezeko la vizimba limechangiwa na juhudi za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwawezesha wakuzaji viumbe maji kupata mikopo isiyo na riba na yenye masharti nafuu kwa vizimba vya kufugia samaki.

95. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuimarisha ukuzaji viumbe maji kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaranga vya samaki na vyakula vya samaki. Uzalishaji wa vifaranga umeongezeka hadi **123,877,354** (***Vituo vya Wizara vifaranga* 2,370,788*, Taasisi za Umma vifaranga* 9,567,623 *na vituo Binafsi vifaranga* 111,938,943**) ukilinganisha na vifaranga **66,684,806** vilivyozalishwa mwaka 2023/2024 (***Kiambatisho Na.9***). Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya vitotoleshi vya kuzalisha vifaranga kutoka **41** kwa mwaka 2023/2024 hadi **49** kwa mwaka 2024/2025. Aidha, matumizi ya chakula cha samaki nchini yameongezeka hadi tani **15,226,665** kutoka tani **7,911.4**, mwaka 2023/2024. Kiasi hicho kina jumuisha tani **5,879** zilizozalishwa nchini na tani **9,347.665** zilizoingizwa kutoka nje ya nchi (***Kiambatisho Na.10***), ikilinganishwa na tani **3,455.4** zilizozalishwa nchini na tani **4,456.0** zilizoagizwa kutoka nje ya nchi kwa mwaka 2023/2024. Pia, jumla ya wananchi **11,216** (***Wanawake* 6,000*; Wanaume* 5,216**) walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ukuzaji viumbe maji.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025**,** Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji kwa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa forodha katika uingizaji wa pembejeo na vifaa mbalimbali vya ukuzaji viumbe maji nchini. Aidha, kutokana na msamaha huo, Wizara imetoa vibali **110** vikiwemo **81** vya kuingiza chakula cha samaki kutoka nje ya nchi kwa Kampuni **19** (***Kiambatisho Na.11)***, vibali **3** vya ukuzaji viumbe maji bahari (***Kiambatisho Na.12)*** na **26** vya ufugaji samaki kwa vizimba (***Kiambatisho Na.13)***. Aidha, leseni **10** za kusafirisha mwani nje ya nchi zimetolewa kwa makampuni **10** ambapo jumla ya kilo **7,101,708** zenye thamani ya shilingi **7,456,793,400** zimesafirishwa kwenda nchi za China, Ufaransa, Afrika Kusini, Chile, Marekani, Hispania, Korea Kusini na Denmark. (***Kiambatisho Na.14***).

97. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa shughuli za ukuzaji viumbe maji zinatekelezwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni, Wizara imefanya kaguzi **40** za mazao ya ukuzaji viumbe maji katika uingizaji na usafirishaji nje ya nchi, bandarini na viwanja vya ndege, vitotoleshi **26,** vizimba **610**, mabwawa **225**, matanki **12**

na viwanda viwili (**2**) vya chakula cha samaki. Aidha, wasimamizi wa maeneo hayo wamepatiwa elimu na ushauri wa kitaalam kwenye mikoa ya Mwanza, Kagera, Morogoro, Simiyu, Pwani na Dar es Salaam.

98. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetoa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, uhifadhi na uongezaji thamani zao la Mwani kwa wakulima **2,563** kupitia mashamba ya mfano. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) pamoja na Shirika la Posta Tanzania imefanya tathmini ya uanzishwaji wa matumizi ya mifumo rasmi itakayorahisisha upatikanaji wa masoko kwenye mauzo ya zao la Mwani na bidhaa zake. Ambapo, jumla ya wakulima **202** wa zao la Mwani kutoka mikoa ya Tanga **(37)**, Lindi **(16)** na Mtwara **(149)** wamepata elimu juu ya mfumo huo.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuongeza upatikanaji wa samaki ili kuimarisha usalama wa chakula na lishe kwa wananchi kwa kupandikiza vifaranga katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya vifaranga 2,739,630 vya samaki, vyenye thamani ya shilingi 273,963,000 vimepandikizwa katika Ziwa Ikimba **(2,000,000)** lililopo Wilaya ya Bukoba na mabwawa yaliyopo Halmashauri za Mufindi – Bwawa la asili la Nzivi (300,000) na Bwawa la Kihanga (300,000); Igunga - Bwawa la Mwamapuli (13,830); Ngara (1,000), Lushoto - Bwawa la Gereza la Lushoto (60,000); Shule ya Irente (3,000); Sekondari ya Magamba (1,800); Bwawa la kikundi cha Ngulwi (20,000) na Halmashauri ya Tunduru vijiji vya Hulia na Misyaje (40,000).

## E. TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

### Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)

100. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia TALIRI imeendelea kufanya utafiti kwenye nyanja mbalimbali za mifugo na malisho ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili 2025, miradi **54** ya utafiti inatekelezwa, kati ya hiyo miradi minne (**4**) ni mipya.

Utekelezaji wa miradi ya utafiti unahusisha uboreshaji mbari za ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na malisho. Aidha, matokeo ya utekelezaji wa miradi ya utafiti yamechangia kuibua na kusambaza teknolojia bora za mifugo na malisho ambapo jumla ya teknolojia za ng'ombe chotara wa nyama **195** walizalishwa na kufanyiwa tathimini na **139** kati ya hao walisambazwa katika mikoa ya Dodoma (***Bahi, Mpwapwa, Kongwa***) na Morogoro (***Morogoro*** DC). Pia, teknolojia ya ng'ombe chotara wa maziwa **85** walizalishwa na kufanyiwa tathmini. Aidha, ng'ombe **68** kati ya hao walisambazwa kwenye mikoa ya Tanga (***Muheza na Tanga Jiji***); Mbeya (***Mbeya Jiji***); Pwani (***Mkuranga***); na Dodoma (***Mpwapwa na Bahi***).

101. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TALIRI inahifadhi na kutunza mbari za mifugo ya asili yenye sifa maalumu zikiwemo ukuaji, uhimilivu wa magonjwa na uzalishaji kwa ajili ya utafiti. Aidha, jumla ya mbuzi **375** walizalishwa na kufanyiwa tathimini na mbuzi **122** kati ya hao walisambazwa katika mikoa ya Kilimanjaro (***Siha***), Dodoma (***Dodoma Jiji, Mpwapwa na Bahi***); Pwani (***Kisarawe na Mkuranga***); Mbeya (***Mbeya Jiji***); Dar-esSalaam (***Ilala***) na Arusha (***Longido na Meru***). Vile vile, TALIRI imeendelea kuhifadhi mbari mbili (2) za kondoo (***Black Head Persian - BHP na Red Maasai***) ambapo jumla ya kondoo **72** walizalishwa na 0**5** walisambazwa katika Halmashauri ya Wilaya za Siha na Longido. Pia, utafiti wa kupata kuku wa asili aina ya Horasi unaendelea kufanyika kupitia mradi wa Tropical Poultry Genetic Solution (TPGS) ambapo jumla ya vifaranga 1,**532** vya Horasi na mayai **2**,**095** yako kwenye mashine za kuengulia. Aidha, jumla ya kuku bora **1**,**400** wenye thamani ya shilingi **17**,**477**,**000** waliotokana na utafiti huu wameuzwa kwa wafugaji kwa bei ya ruzuku. Pia vifaranga 21,**000** vya Sasso na Kuroiler vilitotoleshwa katika Kituo cha TALIRI Naliendele na kusambazwa kwa wafugaji katika mikoa ya Lindi (***Mtama na Ruangwa***) na Kilimanjaro (***Siha na Hai***). Aidha, katika kutekeleza mpango wa mafunzo kwa wafugaji na kuboresha lishe shuleni, TALIRI imefanikiwa kujenga jengo la kufugia kuku katika shule ya Nandagala iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na tayari kuku **1,400** wenye thamani ya shilingi **2**,**940**,**000** wamenunuliwa na wanakuzwa katika hatua za awali (***brooding***) katika Kituo cha Naliendele ili kupelekwa katika shule hiyo.

102. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TALIRI inafanya utafiti wa malisho ambapo jumla ya kilo **5,298** za mbegu za nyasi (***punje***) zimezalishwa na kilo ***2,451*** zimesambazwa; kilo ***500*** za mbegu za nyasi (***vipando***) zimezalishwa na kilo ***318*** zimesambazwa katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, Taasisi imezalisha jumla ya marobota **36,250** ya nyasi kavu (***hay***) na marobota **35,691** yameuzwa kwa wadau wa mifugo katika mikoa ya Mwanza, Tanga, Dodoma, Mbeya na Iringa. Pia, TALIRI imeanza mkakati wa kuzalisha kwa wingi mbegu aina tano (**5**) za malisho zilizopatiwa Ithibati kutoka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (*Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI*). Kazi hii ya uzalishaji mkubwa wa malisho na mbegu za malisho itafanyika katika vituo vya Mpwapwa, Uyole, Kongwa na Tanga ambapo katika Mwaka 2025/2026, Taasisi imetenga jumla ya shilingi **1,600,000,000** katika bajeti ya maendeleo.

103. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wadau wananufaika na matokeo ya utafiti nchini, Wizara kupitia TALIRI imeanzisha Kituo cha Utafiti Kanda ya Magharibi (Nsimbo - Katavi) ambapo taratibu mbalimbali za kuanza utekelezaji wa shughuli za utafiti zinaendelea. Aidha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo imewafikia wafugaji 41,390 na kuwapatia elimu mbalimbali juu ya matumizi ya teknolojia bora za mifugo ili kuongeza tija ya uzalishaji. Vile vile, TALIRI kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula Duniani (***FAO***) wanatekeleza mradi wa kuboresha mbari za mifugo nchini. Pia, Taasisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Enviro-Cow kwa kufikia na kufuatilia jumla ya wadau **1,523** wa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Vilevile, kupitia Mradi huo, sampuli **284** za manyoya ya ng'ombe wa maziwa na sampuli **468** za chakula kinacholishwa ng'ombe hao zimechukuliwa na kuchakatwa ikiwa ni pamoja na kuchukua taarifa za uzalishaji wa hewa joto (***Methane***). Lengo kuu la utafiti huo ni kubainisha ng'ombe ambaye ni mstahimilivu kwa mazingira yetu ya kitropiki, mfanisi katika ulaji chakula na anazalisha maziwa mengi. Kwa upande mwingine, utekelezaji wa mradi wa kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa barani Afrika umeendelea kutekelezwa na TALIRI kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Kimataifa (*International Livestock Research Institute* – ILRI) katika halmashauri **24** nchini. Mradi huo umewezesha upatikanakaji wa kanzidata,

kutathmini na kuorodhesha aina ya ng'ombe bora wa maziwa kwa uchambuzi wa vinasaba na kutoa elimu kwa wafugaji lengo ikiwa ni kumuwezesha mfugaji kunufaika na ufugaji. Mradi unawafikia na kuwatembelea wafugaji wa ng'ombe wa maziwa **5,153** na ng'ombe wa maziwa wapatao **7,600** kila mwezi na kuandaa na kutunza takwimu mbalimbali za uzalishaji.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI)**

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia TAFIRI imeimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu za uvuvi, ili kupanga mipango madhubuti na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi ambapo imetoa mafunzo kwa wakusanyaji takwimu za uvuvi **1,200** katika maeneo ya Bahari ya Hindi (**250**), Ziwa Tanganyika (**138**), Ziwa Victoria (**144**), Bwawa la Mtera (**24**), Ziwa Manyara (**10**), Mto Mara (**112**) pamoja na kufanya sensa za uvuvi katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Bwawa la Mtera, Ziwa Manyara, Mto Mara, Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa;  na maji madogo (Bwawa la Nyumba ya Mungu, Ziwa Babati, Ziwa Eyasi, Ziwa Natron na Ziwa Tlawi).

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TAFIRI imekamilisha na kuzindua usanifu wa programu tumizi inayoitwa ***Vua, Uza, Nunua Kidigitali*** wenye lengo la kuwezesha wavuvi kutambua maeneo ya mavuvi ili kupunguza gharama za uvuvi na kurahisisha biashara ya samaki. Jumla ya wadau **979** kutoka katika Wilaya **14** za ukanda wa Pwani na Zanzibar wameshiriki katika mafunzo ya mfumo, kati ya hao **332** wanatumia mfumo huo. Aidha, TAFIRI imeweka vikusanyia samaki **10** (***Fish Aggregating Devices*** - FADs) katika maeneo ya Bagamoyo na inaendelea kuweka katika maeneo ya mkoa wa Tanga (***Moa***), Lindi (***Kilwa***) na Pwani (***Mkuranga na Bagamoyo***) ili kuwawezesha wavuvi wadogo kufikia maeneo yenye samaki wengi na kukuza uchumi wao na wa nchi kwa ujumla.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TAFIRI imekamilisha Mkakati wa Uvunaji wa Pweza. Mkakati huo utawezesha kukamilika kwa mchakato wa upatikanaji wa nembo ya kiikolojia kwa zao la pweza ikiwa ni kigezo cha ubora na uvuvi endelevu wa zao la pweza nchini. Hatua hiyo itaendelea kuimarisha bei ya

zao la pweza kwenye soko la kimataifa. Aidha, TAFIRI imeanza kuandaa Mkakati wa Uvunaji wa Dagaa wa Baharini kwa lengo la kuimarisha uvuvi uendelevu wa dagaa, kuongeza kipato cha wavuvi na kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika uchumi wa nchi.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha zaidi ufugaji samaki kwa vizimba, Wizara imetambua maeneo **99** yenye jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba **220.22** yanayofaa kwa ufugaji huo katika Ziwa Victoria na kuyafanyia tathmini ya kimkakati ya mazingira. Aidha, zoezi hilo linalenga kuwapunguzia gharama wananchi wa kawaida wanaotaka kuwekeza katika ufugaji samaki kwa vizimba na kuhakikisha kuwa unafanyika kwa uendelevu bila kuathiri ikolojia. Pia, zoezi hilo ni endelevu ambapo kazi ya kubaini maeneo yanayofaa kufuga samaki kwa vizimba inaendelea katika maziwa makuu ya Tanganyika na Nyasa pamoja na maeneo mengine ya maziwa madogo na mabwawa makubwa nchini.

**Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (*LITA*) imeendelea kuimarisha mazingira ya utoaji mafunzo kwa kukamilisha ujenzi na uwekaji wa samani katika kumbi nne **(4)** za mihadhara, zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **528** kwa pamoja, katika Kampasi za Morogoro na Mpwapwa. Aidha, utekelezaji wa miradi mipya ya ujenzi wa kumbi tatu **(3)** za mihadhara, hosteli nne **(4)** na jengo moja la utawala unaendelea katika Kampasi za Kikulula, Buhuri, Madaba na Kampasi mpya ya Songwe. Pia, mradi wa ukarabati mkubwa wa kiwanda kidogo cha maziwa sanjari na ujenzi wa darasa jipya la mafunzo ya teknolojia ya maziwa pamoja na ukarabati mkubwa wa mfumo wa umwagiliaji malisho unaendelea kutekelezwa katika Kampasi ya Tengeru kwa ushirikiano baina ya Serikali na nchi ya Poland.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, LITA imeendelea kutekeleza jukumu lake la kutoa mafunzo kwa kudahili wanafunzi **4,928** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ikilinganishwa na wanafunzi **4,454** waliodahiliwa

katika mwaka wa masomo 2023/2024. Idadi hiyo ni ongezeko la wanafunzi **474,** sawa na asilimia **10.64.** Aidha, jumla ya vituo **126** vyenye sifa za kuwezesha mafunzo kwa vitendo ambavyo ni mashamba ya Serikali ya kuzalisha Mifugo (*LMUs*), Taasisi za Mafunzo na Utafiti wa Mifugo (*TALIRI na SUA*), NARCO, Maabara (*TVLA*), Vituo vya Ufuatiliaji Magonjwa ya Mifugo Kanda (*ZVC*) na Mashamba ya wawekezaji binafsi wa mifugo vinatumika kuhudumia wanafunzi **2,900** kutoka Kampasi nane **(8)** za LITA wakati wa mafunzo kwa vitendo uwandani.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, LITA imetoa mafunzo mbalimbali ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kwa wafugaji **50** kwa ufadhili wa TADB. Aidha, mafunzo rejea ya teknolojia ya maziwa yametolewa kwa wakufunzi **16** wanaofundisha moduli za mazao yatokanayo na mifugo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Warsaw Poland katika Kampasi ya Tengeru.

111. ***Mheshimiwa Spika***, LITA imeendelea kutoa mafunzo rejea ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kwa wafugaji na Maafisa Ugani wa Mifugo **708** kupitia Mradi wa Maziwa Faida kwa ushirikiano na Serikali ya Ireland katika Kampasi ya Buhuri, Tanga. Aidha, mabinti rika **160** wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali kupitia ufugaji bora wa kuku, nguruwe na mbuzi katika Kampasi za Mpwapwa na Mororogo kwa ushirikiano baina ya Serikali na Shirika la BRAC Maendeleo Tanzania. Kupitia mradi huu, kaya za wafugaji **3,014** zimefikiwa na kupewa huduma za ushauri na wanafunzi wa Kampasi zote za LITA kupitia moduli za *outreach, excursions* na mafunzo kwa vitendo uwandani.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia LITA imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Kampasi zake tisa (09). Aidha, ujenzi wa hosteli mbili (2) za wasichana zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **432** umekamilika na majengo yameanza kutumika katika Kampasi za Mpwapwa na Morogoro. Pia, ujenzi wa majengo mawili yenye kumbi nne (4) za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **528** kwa pamoja umekamilika na kumbi kuanza kutumika katika Kampasi za Mpwapwa na Morogoro. Ujenzi wa hosteli nne (4)

zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **600** kwa pamoja na kumbi za mihadhara sita (6) zenye uwezo kuchukua wanafunzi **600** kwa pamoja unaendelea katika Kampasi za Kikulula, Madaba, Buhuri na Kampasi mpya ya Songwe.

**Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA)**

113. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, FETA imeendelea kutekeleza jukumu lake la kutoa mafunzo ya uvuvi ngazi za Astashahada na Stashahada kwa wanafunzi **1,085**. Aidha, ili kuhakikisha FETA inazalisha wataalamu bora watakaoleta tija, imejikita katika kuandaa mitaala bora na ya kisasa inayozingatia mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ili kutoa mafunzo zaidi kwa vitendo, ubunifu wa teknolojia, ujasiriamali na kuwezesha wahitimu kujiajiri.

114. ***Mheshimiwa Spika***, FETA imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki **5,263** yaliyolenga kuimarisha uelewa wa jamii katika kufaidika na fursa za uvuvi zilizopo katika Uchumi wa Buluu. Mkazo zaidi ukiwekwa katika makundi mahusus ya vijana na wanawake, na wale wenye mahitaji maalum kama vile watu wenye ulemavu. Mafunzo ya muda mfupi yalikuwa katika maeneo mahususi na ya kipaumbele kwa Taifa ikiwemo: Ufugaji wa majongoo bahari (**534**); unenepeshaji wa Kaa (**327**); kilimo na uongezaji thamani wa Mwani (**625**); mbinu bora na ufugaji wa samaki kibiashara (**1,965**); uchakataji, ubora na uongezaji thamani ya mazao ya uvuvi (**756**); Kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kwenye mnyororo wa thamani (**573**); Usalama kwenye maji (**224**); Ufundi stadi wa matengenezo ya majokofu na vipoza hewa (**84**); na Usimamizi wa rasilimali za uvuvi (**175**).

115. **Mheshimiwa *Spika***, ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia FETA imeongeza miundombinu na vifaa ikiwemo eneo la ekari **50** katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza kwa ajili ya kujenga Kampasi mpya ya Kibirizi; Ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za mihadhara katika Kampasi ya Nyegezi Mwanza zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **100** kwa kila ukumbi; Ununuzi wa Kompyuta **30**; Boti ya mafunzo moja (**1**); Vifaa vya kuongozea boti

(*echosounder* **2** *na GPS* **2**); Vifaa vya ulinzi na mifumo yake **15**; na Projekta **10**.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania - TVLA**

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kupitia Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) imezalisha na kusambaza chanjo za mifugo za magonjwa ya kipaumbele. Aidha, jumla ya dozi **58,822,475,** zenye thamani ya shilingi **3,860,250,000,** sawa na asilimia **85.9** ya lengo la dozi **68,510,250** zimezalishwa hadi Aprili, 2025. Mchanganuo wa chanjo hizo ni; dozi **363,500** za chanjo dhidi ya Kimeta, Dozi **105,250** za chanjo dhidi ya Chambavu, dozi **7,625** za chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba, dozi **5,493,200** za chanjo dhidi ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, dozi **180,900** za chanjo dhidi ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi, dozi **236,050** ya mchanganyiko wa chanjo dhidi ya magonjwa ya Kimeta na Chambavu, na dozi **52,435,950** za chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo wa Kuku.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jukumu la usajili na udhibiti wa viuatilifu vya mifugo nchini, TVLA imetoa jumla ya vibali **61** kati ya lengo la kutoa vibali **130** hadi Aprili, 2025 ambayo ni asilimia **46.9** ya vibali vya kuingiza viuatilifu vya mifugo (***Acaricide import permit***) vyenye jumla ya lita **619,803.9**, kilo **9,000** na vidonge **1,410**. Aidha, Wakala ilifanya programu za kuelimisha wadau wa mifugo juu ya ubora na matumizi sahihi ya viuatilifu katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma na Kigoma ambapo jumla ya wadau **258** walifikiwa kati ya wadau **400** waliopangwa kufikiwa sawa na asilimia **65** ya lengo la Mwaka 2024/2025.

118. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza jukumu la kuhakiki ubora na usalama wa vyakula vya mifugo nchini, Wakala imefanya uhakiki kwenye jumla ya sampuli **2,220** kati ya lengo la sampuli **5,045** kwa mwaka sawa na asilimia **44.4**. Aidha, Wakala ilitembelea na kufanya ukaguzi na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wazalishaji na wauzaji **58** wa vyakula vya mifugo katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro.

119. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala imeendelea kuimarisha shughuli za utoaji wa huduma za afya ya mifugo nchini kwa kukarabati na kununua vifaa kwenye maabara zake za kanda. Vituo vya Mwanza na Maabara Kuu ya Veterinari Temeke zimefanyiwa ukarabati uliogharimu shilingi milioni **155**. Aidha, Wakala imeendelea na ujenzi wa jengo la maabara ya uzalishaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo yatokanayo na virusi. Jengo hilo litagharimu kiasi cha shilingi bilioni **2.6** ambapo utekelezaji wa ujenzi umefikia asilimia **25.** Kukamilika kwa ujenzi huu kutasaidia kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa chanjo za magonjwa ya kipaumbele kutoka chanjo aina saba (**7**) za sasa hadi kufikia chanjo aina **12**.

120. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala inaendelea kujenga jengo la ghorofa nne la maabara na Ofisi ya Kituo cha Wakala Mkoani Dodoma. Aidha, ujenzi huo utagharimu shilingi bilioni **6.6** ukiwa na lengo la kuimarisha shughuli za Wakala katika kanda ya Kati. Vilevile, Wakala imenunua magari matatu (**3**) yaliyogharimu kiasi cha shilingi milioni **401**. Pia, imejenga vichomea taka tisa (**9**) vyenye thamani ya shilingi **396,500,000** kwenye vituo vya Wakala nchini.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

121. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) imeendelea kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ambapo hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025, Mamlaka imetoa leseni 47 za Uvuvi wa bahari kuu, vibali nane **(8)** vya meli saidizi *(**supporting vessels**)*, vibali vinne **(4)** vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania ***(Areas Beyond National Jurisdiction - ABNJ)*** na vibali vitano **(5)** vya uwakala wa meli (***Agent Accreditation)*** na kuwezesha kukusanya kiasi cha shilingi bilioni **9.29** ikilinganishwa na leseni **72**, kibali kimoja **(1)** cha meli saidizi, vibali vinne **(4)** vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania na vibali vitatu **(3)** vya uwakala wa meli zilizotolewa Mwaka 2023/2024 na kukusanya jumla ya shilingi bilioni **10.12**. Pia, Mamlaka inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu ikiwa ni pamoja na kuingia makubaliano na makampuni ya uvuvi ya nje ya nchi na kuimarisha Makampuni ya Uvuvi ya Serikali ikiwemo TAFICO na ZAFICO.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia DSFA kwa kushirikiana na Kampuni ya ALBACORA Group ya Uhispania yenye Kampuni tanzu ya *Pemba Tuna Limited* imeendelea na taratibu za ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki katika Halmashauri ya Manispaa ya Tanga. Hadi sasa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) imefanyika, Cheti cha Motisha (***Certificate of Incentives***) kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimetolewa, kibali cha ujenzi kimetolewa na Mkandarasi ataanza ujenzi wa kiwanda kabla ya kumalizika kwa Mwaka 2024/2025. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani **2,400** kwa mkupuo na kuchakata samaki takribani tani **20** kwa siku na kutoa ajira kwa watu takribani **100** katika Awamu ya Kwanza.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala imeendelea kushirikiana na Kampuni ya ALBACORA Group katika kutoa mafunzo kwa mabaharia wa Kitanzani pamoja na kushusha samaki wasiolengwa katika Bandari ya Dar es salaam na kuuzwa katika soko la ndani. Aidha, hadi kufikia Aprili 2025, tani **80** za samaki wasiolengwa zilishushwa katika Bandari ya Dar es Salaam. Vilevile, mabaharia **14** wa Kitanzania (***Tanzania bara - 7 na Zanzibar - 7***) waliopewa mafunzo na ALBACORA Group waliendelea kufanya kazi katika meli za uvuvi za Kampuni hiyo. Pia, DSFA iliwezesha kupatikana kwa mtambo wa kutengeneza barafu wenye uwezo wa kutengeneza tani tano (**5**) kwa siku na kuhifadhi tani sita (**6**) kwa wakati mmoja na kukabidhiwa kwa TAFICO.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia DSFA imeendelea kukusanya takwimu za uvuvi wa samaki aina ya jodari kila mwezi katika mialo saba (**7**) kwenye maeneo ya Mtwara Mjini, Kilwa, Mafia, Nungwi, Wete, Kinondoni na Tanga jiji. Aidha, takwimu za mavuno ya samaki kwenye Bahari Kuu ya Tanzania na nje ya mipaka kwa meli za kitanzania na kwa mujibu wa taratibu za IOTC zimekusanywa ambapo tani **20,225** za samaki aina ya jodari na jamii yake ziliripotiwa kuvuliwa na meli za Tanzania na za nje.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi katika Bahari Kuu, DSFA imeendelea kutumia Mifumo ya Ufuatiliaji wa Mienendo ya Meli (***Vessel Monitoring System - VMS* na *Automatic Identification System – AIS***) na kuweka

Waangalizi wa Uvuvi (***Fishery Observers***) kwenye meli zilizopewa leseni. Aidha, DSFA imefanya ukaguzi wa meli za uvuvi zilizoomba leseni na vibali katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar na Victoria - Ushelisheli.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** DSFA kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (TNC) imekamilisha hatua za mwanzo za matumizi ya mfumo wa kielektroniki (***Electronic Monitoring System***) ambao utahusisha kufunga kamera kwenye meli zitakazovua Bahari Kuu. Mfumo huo utawezesha DSFA kuona shughuli za uvuvi wakati meli zikivua na kuwezesha Tanzania kutekeleza maazimio ya kikanda na kimataifa katika uhifadhi na usimamizi wa meli hizo na ukusanyaji wa taarifa na takwimu sahihi na kwa wakati.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

127. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeendelea kusimamia maeneo ya hifadhi za bahari **18** (***hifadhi za bahari tatu*** (**3)** ***na maeneo tengefu*** (**15)**). Aidha, MPRU imefanya doria **948,** ufuatiliaji wa kila wiki kwa maeneo yote, na kutoa mafunzo kwa wahifadhi **45**. Pia, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu imeshirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Shirika la SwAM, WCS, WWF na USAID Heshimu Bahari ili kuimarisha usimamizi wa hifadhi za bahari na maeneo tengefu.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu imeendelea kuboresha usimamizi wa rasilimali za bahari kwa kutumia teknolojia ya kisasa ikiwemo matumizi ya Ndege Nyuki (***Drone***) katika kufanya doria. MPRU kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Kanzidata kwa ajili ya usimamizi wa matumbawe nchini (***National Coral Reef Monitoring Data Base***). Aidha, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeandaa Mpango wa Kitaifa wa miaka mitano kwa ajili ya uhifadhi wa rasilimali za bahari na kuanzisha Kituo cha Kitaifa (***National Coral Reef Hub***) kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za bahari hususan matumbawe.

129. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia MPRU kwa kushirikiana na Shirika la ***Wildlife Conservation Society*** - WCS, imeendelea kuimarisha maeneo ya hifadhi kwa kuanzisha kituo cha kurejesha matumbawe yaliyoharibika, kufanya doria za nchi kavu na baharini. Aidha, imeanzisha maeneo vitovu sita (**6**) ya usimamizi wa matumbawe (***National Coral Reef Hubs***). Maeneo haya yanajumuisha usimamiaji jumuishi ukihusisha wanasiasa, wanajamii, wanasheria, wanasayansi, Wadau wa Maendeleo ambapo kwa pamoja hujadili na kutathmini hatma ya uhifadhi wa matumbawe katika maeneo yao ya kijiografia.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeendelea kuandaa mipango mbalimbali ya usimamizi, ikiwemo: Mpango wa Usimamizi na Uthibiti wa Umwagikaji Mafuta Baharini (***Oil Spill Contingency Plan***) katika maeneo ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu; Mpango Mkakati wa Kuhifadhi Matumbawe (***National Coral Reef Action Plan***); Upangaji wa Maeneo ya Baharini (MSP) na Kuandaa ramani ya mifumo ikolojia muhimu (***miamba ya matumbawe, nyasi bahari, mikoko na fukwe za mchanga***) kupitia dhana ya Upangaji Matumizi ya Maeneo ya Baharini (MSP).

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

131. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Serikali imeendelea kuliimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), ambapo kupitia ufadhili wa Programu ya Kuendeleza Uchumi na Jamii *(**Economic and Social Development Program-ESDP**)* ya Japan, ujenzi wa meli moja **(**1**)** ya Uvuvi wa Bahari Kuu unaendelea na unategemea kukamilika na kuwasili nchini ifikapo Mwezi Disemba, 2025. Kukamilika kwa meli hii kutaiwezesha TAFICO kuanza uvuvi wa Bahari Kuu na kufungua fursa zaidi katika Uchumi wa Buluu. Pia, kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi kutawezesha ununuzi wa meli mbili za uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, ukarabati wa gati kwa ajili ya kuegesha meli unaendelea. Pia, magari matatu (3) ya ubaridi yenye uwezo wa kubeba uzito wa tani kumi (10) kila moja na gari moja (1) lenye uwezo wa kubeba tani tano (5) kwa ajili ya kusafirisha mazao ya uvuvi yamenunuliwa.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) ni Kampuni ya kibiashara iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni ambayo inamilikiwa na Serikali kwa asilimia **100** na kwa kiasi kikubwa inajiendesha kwa mapato yake ya ndani. Katika Mwaka 2024/2025, Kampuni imekusanya jumla ya shilingi **5,975,044,928.56**. Aidha, NARCO inasimamia uendeshaji wa Machinjio ya Dodoma ambapo mapato yameongezeka kutoka shilingi **637,162,690** hadi kufikia **821,407,167** katika kipindi cha miezi tisa (**9**). Pia, NARCO imefanya ukarabati wa Machinjio hiyo ili kuboresha utoaji wa huduma za uchinjaji na uchakataji kwa wafanyabiashara binafsi wanaouza nyama nje ya nchi na kuongeza tija katika Machinjio hiyo.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NARCO imeendelea na jitihada za kuimarisha Sekta ya Mifugo ambapo NARCO imesaini mikataba na makampuni mawili ya *Tanzania Game and Livestock Breeders Ltd* na *Tan Choice Ltd* kwa lengo la kuzalisha kosaafu bora za mifugo katika Ranchi za West Kilimanjaro na Kongwa mtawalia. Aidha, NARCO inaendelea kukamilisha taratibu za kusaini mikataba na Makampuni mengine matatu (**3**) ya kimkakati ya Union Meat Co Ltd, Kahama Fresh na Liam Ranch Ltd kwa lengo la kuzalisha mifugo bora na mazao yake ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

134. ***Mheshimiwa Spika****,* katika Mwaka 2024/2025, NARCO imezalisha ndama **2,312**, sawa na asilimia **56.6** ya lengo la kuzalisha ndama **4,080**; Imesambaza kwa wafugaji mitamba **415**, sawa na asilimia **83** ya lengo la kusambaza mitamba **500** ili kuboresha kosaafu za mifugo; Imezalisha na kuuza tani **232.6** za nyama, sawa na asilimia **77.5** ya lengo la kuzalisha na kuuza tani **30**0 za nyama; Imenenepesha na kuchinja ng'ombe **2,326**, sawa na asilimia **93** ya lengo la kunenepesha na kuchinja ng'ombe **2,500**. Aidha, NARCO imefyeka na kuondoa vichaka katika hekta **600** kwenye Ranchi za Kongwa, Ruvu na West Kilimanjaro kuruhusu ukuaji wa malisho; Imezalisha marobota **50,000** ya hei, sawa na asilimia **76.9** ya lengo la kuzalisha marobota **65,000**; Imetoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji **225** kati ya wafugaji **400** waliolengwa, sawa na utekelezaji wa asilimia **56** ya lengo katika vijiji

vinavyozunguka Ranchi za NARCO; na Imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi **368** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini.

**Bodi ya Nyama Tanzania**

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania (*TMB*) imeendelea kusimamia, kuratibu na kuendeleza shughuli mbalimbali zinazofanyika katika Tasnia ya nyama nchini. Hadi kufikia Aprili, 2025 imefanya ukaguzi kwa wadau **10,082** wanaofanya shughuli za uzalishaji katika mnyororo wa thamani wa nyama, idadi hiyo ni sawa na asilimia **83.49** ya lengo la mwaka 2024/2025 la kukagua wadau **12,075**. Ukaguzi huo umekuwa ukifanyika kwa lengo la kuhakikisha nyama na bidhaa zake zinazoingia sokoni zinakuwa bora na salama ili kulinda afya za watumiaji wa bidhaa hizo. Aidha, ukaguzi na utambuzi huo umefanyika katika mikoa yote nchini.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kuhakikisha biashara ya nyama inaratibiwa na wahusika wanatambulika. Hadi kufikia Aprili, 2025 Bodi ya Nyama imesajili jumla ya wadau wapya **2,110** kati ya **5,097** waliopangwa kusajiliwa kwa mwaka sawa na asilimia **41.39**. Idadi hiyo inajumuisha wazalishaji wa Mifugo **68**, wafanyabiashara wa Mifugo **199**, miundombinu ya Machinjio **41**, magari maalumu ya kubeba nyama **97**, wasafirishaji wa nyama nje ya nchi **50**, wasindikaji wa nyama **25**, maduka na maeneo ya kufanyia biashara ya nyama **1,775**. Aidha Bodi imehuisha usajili wa wadau **6**,**486** kati ya **6**,**978** sawa na asilimia **92.83** ya lengo la mwaka.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Bodi ya Nyama imeendesha mafunzo kwa wasindikaji na wauzaji wa nyama **11,488** sawa na asilimia **95.02** ya lengo la kuwafikia wadau **12**,**090**. Mafunzo hayo yalitolewa ili kuboresha usalama wa nyama na bidhaa zake, kulinda afya za watumiaji na kuongeza thamani ya nyama. Mafunzo hayo yalitolewa kwenye Mikoa **18** ambayo ni: Dodoma, Morogoro, Iringa, Tabora, Shinyanga, Kigoma, Mwanza, Kagera, Mara, Dar-es-salaam, Pwani, Mtwara, Mbeya, Ruvuma, Songwe, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

**Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB)**
138. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania **(**TDB) imeendelea kuwahamisha wafugaji kufuga kibiashara ili kuwawezesha wafugaji kuzalisha maziwa mengi zaidi ambapo katika Mwaka 2024/2025, Bodi ya Maziwa Tanzania **(**TDB) kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imewezesha kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi **12,559,793,870** na ruzuku ya uchangiaji (***matching grant***) ya shilingi **631,150,000** kwa wanufaika **594** katika Tasnia ya Maziwa. Aidha, wafugaji wa ng'ombe wa maziwa **49,091** (***wanaume* 34,084 *na wanawake* 15,007**) wamepatiwa mafunzo yaliyojikita katika mbinu za ufugaji bora na yaliambatana na huduma za ugani ili kuongeza uzalishaji wa maziwa. Vilevile, vyama vya ushirika wa wazalishaji wa maziwa **33** vilihuisha uongozi wao huku vyama vipya **12** vimeanzishwa kwa lengo la kurasimisha biashara ya maziwa nchini.

139. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania **(**TDB) inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni (SMP) katika shule **140** nchini ambapo hadi Aprili, 2025 Mpango huo umewafikia jumla ya wanafunzi **102,446**. Aidha, nakala **3,600** za vitabu vya Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni zimesambazwa na Mpango huo unatarajiwa kuwafikia wanafunzi **1,609,687.**

140. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania **(**TDB) imesajili jumla ya wadau **436** wa Tasnia ya Maziwa kati ya **800** waliolengwa sawa na asilimia **54.5**. Wadau waliosajiliwa ni pamoja na wazalishaji **130**, wasindikaji **69**, wafanyabiashara **86**, waingizaji maziwa nchini **24**, wauzaji maziwa nje ya nchi **10**, wasambazaji wa maziwa saba (**7**) na wakusanyaji maziwa **41**. Aidha, maghala **33** ya kuhifadhia maziwa yamesajiliwa sambamba na wauzaji wa pembejeo watatu (**3**), wachuuzi wa maziwa tisa (**9**) na wasafirishaji maziwa **24.** Katika zoezi hilo, elimu kuhusu Sheria ya Tasnia ya Maziwa na Kanuni zake ilitolewa. Aidha, ili kuendelea kurasimisha biashara ya maziwa na kupunguza uuzaji holela wa maziwa, Bodi ya Maziwa Tanzania **(**TDB) imewezesha uanzishwaji wa sehemu maalumu za kuuzia maziwa (***milk selling points***) mbili katika maeneo ya Kisasa Sekondari na Uhindini Jijini Dodoma. Vilevile, mashine za kuuzia

maziwa (***milk ATM***) mbili zimewekwa katika eneo la Uhindini Jijini Dodoma na Njiro Jijini Arusha.

## F. MIRADI YA MAENDELEO

### Miradi ya Maendeleo chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)

141. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 ujenzi huo umefikia asilimia **81.9**. Ujenzi huo umehusisha gati lenye urefu wa mita za mraba **315** ujenzi wa gati umekamilika kwa asilimia **100**; Jengo la utawala asilimia **95**; Jengo la kuzalishia barafu, kuhifadhia, kuandalia samaki pamoja na soko la kuuzia samaki umefikia asilimia **89**; Kituo cha kusambazia maji safi asilimia **80**; kituo cha zimamoto asilimia **80**; Kituo cha kupozea umeme asilimia **82**; Kituo cha kuzalishia gesi ya naitrojeni asilimia **85**; pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuegesha magari; Tanki za kuhifadhia mafuta na Karakana ya kutengenezea meli ambao ujenzi upo zaidi ya asilimia **60**.

142. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza uzalishaji na tija katika uvuvi kwa Mwaka 2024/2025, Wizara imekamilisha kujenga jumla ya boti **59** na zana za uvuvi na kuzisambaza kwa wavuvi katika mikoa ya Tanga (**33**). Aidha, taratibu zinakamilishwa ili kusambaza katika mikoa ya Mtwara (**5**), Pwani (**8**), Lindi (**5**), Dar es Salaam (**5**) na Kigoma (**3**). Boti hizo zinagawiwa kwa mkopo wa masharti nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Pia, Wizara imeendelea kuimarisha Vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwa kununua boti tano (**5)** na injini zake na ndege nyuki mbili (**2**) kwa ajili ya doria (***surveillance drone***). Vilevile, katika kulinda mazalia na makulia ya samaki (***critical habitats***) maboya maalamu **32** yamewekwa katika maeneo mawili (**2**) ya mfano ya Ziwa Victoria ili kubainisha mipaka na kuzuia wavuvi kuingia kwenye maeneo hayo.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mialo miwili **(2)** ya Chato Beach **(95%)** na Ng'ombo **(30%),** masoko ya Kasanga **(90%)**, Manda **(40%)**, Zingibari **(40%)** na Tunduma (**34%**).

Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari Ruvula-Mtwara. Pia, Wizara imeendelea kuimarisha utendaji wa vituo vitano (**5**) vya Ukuzaji Viumbe Maji vya Machui, Ruhila, Nyengedi, Mwamapuli na Kingolwira kwa kuvipatia vitendea kazi ili kuboresha mazingira ya kazi na kutoa huduma stahiki za ugani na uzalishaji wa vifaranga.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kutoa mikopo isiyo na riba na yenye masharti nafuu wa kuwezesha wananchi vizimba vya kufugia samaki na pembejeo zake katika mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Kagera, Geita, Katavi, Rukwa na Kigoma. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya vizimba **480** vimekopeshwa kwa wanufaika **1,909**. Aidha, jumla ya tani **216.68** za samaki zenye thamani ya shilingi **1,576,132,969.36** zimevunwa kutoka katika vizimba **157** vya vikundi **32** na kufanya marejesho ya shilingi **1,528,734,615.66**.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za udhibiti wa magonjwa ya mifugo na kuendelea kukidhi vigezo vya biashara ya mifugo kikanda na kimataifa, Serikali inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa kwa kununua na kusambaza chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (***Contagious Bovine Pleuropneumonia*** - CBPP) dozi **19,099,100** kwa ajili ya kuchanja jumla ya ng'ombe **19,099,100** na chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (***Peste des Petits Ruminants*** - PPR) dozi **17,230,000** kwa ajili ya kuchanja mbuzi na kondoo **17,230,000** na chanjo ya Mdondo wa Kuku (***Newcastle Disease***-ND) dozi **40,000,000** kwa ajili ya kuchanja kuku wa asili **40,000,000**. Chanjo hizi zimezalishwa na viwanda vilivyopo ndani ya nchi. Aidha, ili kuwezesha Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya kuchanjia, pikipiki **700** na vishikwambi **4,500.** Pia, Wizara imeandaa mgao wa chanjo, vifaa vya chanjo na kuwasilisha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji. Vilevile, mgao wa pikipiki na Vishikwambi umeandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. **(Kiambatisho Na.15a na 15b).**

146. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, Serikali imenunua jumla ya hereni za kidijitali **36,323,300** kwa ajili ya utambuzi wa jumla ya ng'ombe **19,099,100,** Mbuzi na Kondoo **17,224,200** watakaopatiwa chanjo. Mifugo itakayochanjwa itatambuliwa kwa hereni za kidijitali na taarifa zao kuingizwa kwenye Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo. Aidha, lengo kuu la utambuzi wa Mifugo ni kukidhi matakwa ya soko la kikanda na kimataifa linalohitaji kila mnyama na mazao yake kuwa na alama ya utambuzi, kuwezesha wafugaji kupata mikopo na bima, kudhibiti wizi wa Mifugo, kurahisisha ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa na kuwezesha Serikali na wadau kuweka mipango ya kuhudumia Mifugo na wafugaji kwa kuwa idadi yao inajulikana.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imezindua Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (***Climate Smart Dairy Transformation Project*** - C-SDTP) wenye thamani ya shilingi **452,000,000,000** unaotekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 ambapo kazi za awali ikiwemo: kuajiri wataalaamu wa usimamizi wa Mradi, uzinduzi na kubainisha maeneo ya utekelezaji wa Mradi (***baseline survey***) zimefanyika. Mradi huo utatekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Njombe, Tanga, Morogoro, Pwani, Kaskazini Unguja, Mjini Magharibi, Kusini Unguja, Kaskazini Pemba, na Kusini Pemba. Mradi huo utahusisha jumla ya wadau wa Tasnia ya Maziwa wapatao **600,000** ambapo kati yao asilimia **40** ni wanawake na asilimia **30** ni vijana. Aidha, mradi huu utahusisha ununuaji wa ng'ombe **17,200** wa maziwa; Kujenga mabanda **5,000** ya ng'ombe; Kujenga mifumo **22,400** ya uvunaji wa maji ya mvua katika kaya zitakazochaguliwa; Kununua na kusakinisha mitambo **2,800** ya biogesi; Kujenga vituo **140** vya kukusanya maziwa na kukarabati vituo vya zamani **150**; Kununua dozi **929,000** za chanjo za mifugo; na Kujenga kilomita **140** za barabara katika maeneo ya Mradi.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, ili kuhakikisha maji ya mifugo, malisho na mbegu za malisho zinapatikana, Wizara imekamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhia malisho katika Kituo cha TALIRI Mpwapwa, ujenzi wa mabwawa manne (**4**) ya

kunyweshea mifugo ya Bukabwa (Butiama), Kihumbu (Bunda), Isulamilomo (Nsimbo) na Kwenikwembe (Kilindi).

149. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha upatikanaji wa malisho unakuwa wa uhakika, Wizara imeshiriki zoezi la upandaji wa malisho aina ya *Juncao* na *Rhodes* kwenye shamba la mfugaji lililokuwa limeandaliwa katika kijiji cha Mbwade (Kilosa) ikiwa kama sehemu ya uhamasishaji wafugaji kumiliki ardhi kisheria na kulima malisho. Aidha, Wizara ilikabidhi mbegu za malisho kwa wafugaji **15** ambapo jumla ya tani **5** za *Juncao* ziligawiwa kwa wafugaji **10** na kilo **50** za mbegu za *Rhodes* ziligawiwa kwa wafugaji watano (**5)**. Pia, Wizara inaendelea na kazi ya kusafisha eneo la malisho la Msomera kwa kuondoa vichaka katika eneo lenye ukubwa wa Hekta **1,000** ambapo mpaka sasa eneo lenye ukubwa wa Hekta **640** limeondolewa vichaka.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza ujenzi wa mashamba darasa ya ufugaji samaki ili kuongeza wigo wa huduma za ugani kwa kutoa mafunzo kwa vitendo ya ufugaji samaki katika Halmashauri mbalimbali nchini. Ujenzi wa mashamba darasa manne (**4**) katika Halmashauri za Wilaya za Moshi, Rombo, Mwanga na Mkuranga upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, mashamba darasa mawili (**2**) katika Halmashauri za Wilaya ya Songea na Ruangwa yamekamilika ambapo kwenye shamba darasa la Mpitimbi katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Kikundi cha Wafugaji Samaki Mpitimbi B chenye wanachama **15** (wanawake **6** na wanaume **6**) kimeanza kunufaika na mavuno ya awali ya kilo **63** za samaki zenye thamani ya shilingi **630,000**. Vilevile, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuanzisha mashamba darasa **16** katika Halmashauri za Masasi, Ngara, Geita, Chato, Kigamboni, Tunduma, Mbarali, Busokelo, Lushoto, Gairo, Dodoma, Iramba, Uyui, Maswa, Bariadi na Isimani.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Mradi wa Bahari Maisha katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari cha Machui - Tanga imejenga jengo la kutolea mafunzo lenye uwezo wa kuchukua watu **50**, kusanikisha mfumo wa

umeme wa jua wa kutosheleza mahitaji ya umeme ya kituo (***Paneli 64***, ***Betri* 3** na ***Inveta* 2**) na vifaa vya kutunza ubora wa maji (***UV light 2, Protein Skimmer 2**, water pump **1 & aerators 2***) na kufundishia (***LCD Projector)***. Vifaa vingine vilivyo nunuliwa ni pamoja na mashine ya kusaga mwani, pembejeo za kilimo cha mwani (***kamba* 688** *na* ***taitai bunda* 400**), ufugaji kaa (***mbegu* 8,000**) na ufugaji jongoo bahari (***wavu bunda* 15, *bomba* 45** na ***mbegu* 3,000**). Aidha, Mradi umewezesha kutoa mafunzo kwa wananchi **60** ikiwemo wakulima wa mwani, wafugaji wa jongoo bahari na kaa. Vilevile, Mradi umejenga hema la kukaushia Mwani kwa jua (***Solar Drying Tent***).

**Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Program* - AFDP)**

**152. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development program*-AFDP) imeendelea kuimarisha ubora na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa kwa kuendelea kujenga miundombinu ya uvuvi ikiwemo ujenzi wa vichanja** 40 **vya kukaushia Dagaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa; Ujenzi wa chumba cha ubaridi na mtambo wa kuzalisha barafu katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo; na Kukamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi Kilwa Masoko.**

153. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Pragramu hiyo imeendelea na ujenzi wa mabwawa **10** mapya ya ukuzaji viumbe maji ambapo ujenzi wake umefikia **asilimia 39**; Kuanza ukarabati wa mabwawa **10** yaliyopo Boma road; Ukarabati wa kitotoleshi; Ujenzi wa mifumo ya usambazaji maji; na Ujenzi wa darasa la kutolea mafunzo ya ukuzaji viumbe maji katika Kituo cha Kingolwira - Morogoro. Aidha, katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Rubambagwe-Geita ujenzi umefikia asilimia **70.** Vilevile, mtambo wa kutengeneza chakula cha samaki umenunuliwa.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Mradi wa Kuendeleza Lishe na Ufugaji Endelevu wa Viumbe Maji

kwa Wakulima Wadogo (ARNSA – *Advancing Resilient and Nutrition – Sensitive Smallholder Aquaculture*) imeendesha programu ya kutoa mafunzo kazini (***internship***) kwa vijana **18** ili kuwajengea uwezo kwa vitendo kuhusu ufugaji samaki katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Ruhila – Ruvuma. Aidha, watumishi wamejengewa uwezo wa kuzalisha Nzi Chuma (***Black soldier fly***) na kuwezesha miundombinu kwa ajili ya uzalishaji huo ambapo hadi sasa kilo **60** zimezalishwa na zinatumika kama chanzo cha protini katika chakula cha samaki. Pia, Kituo kimepatiwa mashine ndogo ya mkono ya kutengeneza chakula cha samaki yenye uwezo wa kuzalisha kilo **50** kwa siku kwa ajili ya kutolea mafunzo kwa wakulima na kutengeneza chakula kwa matumizi ya Kituo. Vilevile, Kituo kimetoa mafunzo kwa vikundi **12** vyenye jumla ya wananchi **122** katika Kata mbili **(2)** za Mkako na Matiri katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, na Kata mbili **(2)** za Mpitimbi na Mpandangindo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo ya ufugaji bora wa samaki kwa wananchi **125** wa vijiji vya Namahema, Nandagala, Chikoko, Chinokole na Shule ya Msingi Nanganga vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa. Baada ya mafunzo hayo, wananchi wamehamasika na kuanza kuchimba mabwawa ya kufugia samaki katika vijiji vya Namahema (**2**), Mchenganyumba **(2)**, Chikoko **(2),** Chinokole **(2)** na Shule ya Msingi Nanganga **(1).** Pia Kituo kilitoa mafunzo ya kilimo bora cha Mwani kwa wananchi **452** katika vijiji vya Shuka na Nachunyu ambavyo viko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtama.

## G. UTEKELEZAJI MIRADI YA KIKANDA

156. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Programu ya SADC ya Kuhamasisha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Kikanda na Ukuzaji viumbe maji endelevu (PROFISHBLUE) imekabidhi kwa Chama cha Ushirika wa Wavuvi cha BUKASIGA kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Mwanza gari lenye miundombiu ya ubaridi. Gari hilo aina ya Isuzu lenye namba za usajili T660 ELT ambalo lina uwezo wa kubeba tani tatu (3) litawezesha Ushirika huo kusafirisha samaki na mazao yake kupeleka katika masoko mbalimbali nchini kwa viwango vya ubora na usalama wa

chakula. Aidha, mradi huo pia umewezesha jumla ya watumishi **39** na wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs) **48** kujengewa uwezo kuhusu masuala mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi, ukuzaji endelevu wa viumbe maji na Uchumi wa Buluu.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Mradi wa Kikanda wa Ukuzaji Viumbe Maji (TRUEFISH) umewezesha mafunzo kwa wafugaji samaki **172** katika mikoa ya kanda ya ziwa kuhusu ufugaji samaki, ushonaji nyavu, kuongeza thamani ya mazao ya samaki, kuendesha boti na kuogelea. Mafunzo hayo yalilenga kuongeza tija katika mnyororo wa thamani kwenye Tasnia ya Ukuzaji Viumbe maji. Aidha, kupitia Mradi huo, Wizara inaandaa Mkakati wa Taifa wa Afya ya Viumbe Maji (***National Aquatic Health Strategy***) kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa afya na kudhibiti magonjwa ya viumbe maji nchini.

**MASUALA MTAMBUKA**

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na benki za TADB, CRDB na NMB imeendelea kuiwezesha sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mifugo na uvuvi. Hadi kufika Aprili 2025, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi **664,894,120,000** imetolewa. Kati ya fedha hizo, shilingi **397,800,000,000** zilitolewa kwa wanufaika **207** wa Sekta ya Uvuvi kwa ajili ya vizimba, Boti, ujenzi wa mabwawa ya samaki na wafanyabiashara wa samaki; na shilingi **267,094,120,000** zilitolewa kwa wanufaika **289** wa Sekta ya Mifugo kwa ajili ya ununuzi wa ng'ombe wa maziwa.

159. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeweza kuwaunganisha wanufaika 37 na vyama vya ushirika 68 wa Sekta za Mifugo na Uvuvi na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo. Wizara inaendelea na mazungumzo na vyama 3 vya ushirika na taasisi ya *Private Agricultural Sector Support* (*PASS*) ili taasisi hiyo iweze kudhamini mikopo kwa wadau hao yenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ufugaji na uvuvi. Aidha, Wizara tahakikisha wanufaika wote wanarejesha mikopo kwa wakati.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025, jumla ya watumishi **153** wamepandishwa vyeo; watumishi 14 wamebadilishwa kada; na **71** wameajiriwa. Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza Mwongozo wa Kudhibiti VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma ambapo elimu imetolewa kwa watumishi **933** kuhusu VVU/UKIMWI, Magonjwa yasiyoambukizwa na kuhamasisha upimaji wa afya. Pia, watumishi **933** wamehamasishwa na kushiriki bonanza la michezo na mashindano ya SHIMIWI, ili kupunguza Magonjwa Yasiyoambukiza.

161. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ambapo wadau **558** ikiwemo wadau **408** kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela na wadau **150** kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa. Aidha, vikundi 13 vya ufugaji kwa njia ya vizimba vimepatiwa elimu juu ya mabadiliko Tabianchi na mbinu za kuhimili athari ili kuwa na uvuvi endelevu.

162. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kuhamasisha ufugaji unaozingatia utunzaji wa mazingira na kukabiliana na Mabadiliko Tabianchi ambapo jumla ya wafugaji **189** ikiwemo 139 kutoka Halmashauri za Wilaya ya Magu na **50** kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa wamejengewa uelewa kuhusu ufugaji endelevu unaohimili Mabadiliko Tabianchi.

163. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha mifumo ya TEHAMA ya Wizara inatoa huduma bora kwa wananchi na inasomana na mifumo mingine ndani ya Serikali. Mifumo hiyo ni pamoja na *Mifugo Integrated Management Information System (**MIMIS**)* na *Fisheries Revenue Collection Information System* (FiRCIS) inayotumika kwenye usimamizi na utoaji wa vibali mbalimbali vya kusafirisha mazao ya mifugo na uvuvi na ambayo imeunganishwa na mfumo wa TAUSI wa OR-TAMISEMI. Vilevile, Wizara imesanifu na kutengeneza mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kuwezesha uratibu wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi Mifugo Kitaifa kwa lengo la

kusajili chanjo zinazotolewa kuanzia ngazi za msingi na kuhakikisha mifugo yote inayochanjwa inasajiliwa kwenye mfumo.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhana ya Diplomasia ya uchumi, katika Mwaka 2024/2025, Wizara ilikuwa mwenyeji wa mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa na kutumia fursa hiyo kutangaza mafanikio na fursa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Miongoni mwa mikutano ni pamoja na Mkutano wa Tatu (**3**) wa Ukuzaji Viumbe Maji wa Afrika Mashariki uliofanyika kuanzia tarehe 13 hadi 15 Agosti, 2024 jijini Mwanza; Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Bahari, Maji ya Ndani na Uvuvi kwa Nchi za Umoja wa Afrika, Karibiani na Pasifiki uliofanyika kuanzia tarehe 9 hadi 13 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam; Jukwaa la Buluu la Chakula la FAO uliofanyika tarehe 8-13 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam; na Kongamano la Tatu (**3**) la Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kwa Uchumi wa Buluu uliofanyika tarehe 2931 Oktoba 2024 jijini Arusha.

165. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2024/2025, Wizara imeendelea kushiriki Mikutano ya Kikanda ikiwemo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) ambayo pamoja na mambo mengine ilipitia utekelezaji wa Mpango wa kudhibiti Uvuvi haramu, usimamizi wa Uvuvi na ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba; Aidha, Wizara ilishiriki Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko Tabianchi (COP 29) uliofanyika Baku, Azerbaijan ambapo ilipata nafasi ya kutangaza fursa za uwekezaji kwenye sekta za mifugo na uvuvi.

166. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Wizara inaendelea kushirikiana na taasisi za Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kukuza ushirikiano na kushirikiana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya sekta za Mifugo na Uvuvi. Miongoni mwa taasisi hizo ni pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC), Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (***Lake Victoria Fisheries Organization*** - LVFO),Taasis ya Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), Taasisi ya Sayansi za Bahari Magharibi mwa Bahari ya Hindi (***Western Indian Ocean Marine Science Association*** - WIOMSA),

Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (***South West Indian Ocean Fisheries Commision*** - SWIOFC) na Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (***Lake Tanganyika Authority*** - LTA).

**MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026**

167. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti ya (Fungu 99) - Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2025/2026 umeandaliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (FYDP III) kwa kipindi cha 2021/2022 – 2025/2026; Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030 (Sustainable Development Goals – SDGs, 2030).

168. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango huu umezingatia Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006; Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015; Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024; Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo - Awamu ya Pili (ASDP II); Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi (2022/23-2036/37); Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo (*Livestock Sector Transformation Plan – LSTP*) kwa Kipindi cha Mwaka 2022/23 hadi 2026/27; na Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi ya Mwaka 2021/2022 – 2026/2027**.** Vilevile, Mpango na Bajeti ya Wizara umezingatia Hotuba ya Mheshimiwa, **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, aliyoitoa wakati akihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 (Dodoma) na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

**Vipaumbele vya Mpango**

169. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi utatekelezwa kupitia vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kuongeza uzalishaji, masoko, na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(ii) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi;
(iii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; na
(iv) Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026**

170. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, **Fungu 99,** limepangiwa kukusanya jumla ya shilingi **74,105,001,000.** Kati ya kiasi hicho, shilingi **38,300,000,000** zinatarajiwa kukusanywa kupitia Sekta ya Mifugo na shilingi **35,805,001,000** kupitia Sekta ya Uvuvi. Aidha, mchanganuo wa makisio ya makusanyo hayo kwa kila kifungu umeainishwa katika **Jedwali: 1**

Mchanganuo wa Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026

| GFS Code | GFS Code Description | Annual Budget Estimates |
|---|---|---|
| **Kifungu 7001: Veterinary Services** | | |
| 11510106 | Export Duty | 420,000,000 |
| 14210137 | Receipt from Veterinary Charges | 14,607,000,000 |
| 14220168 | Compounding Fee | 216,666,666 |
| 14220174 | Livestock Movement Permit | 14,000,000,000 |
| **Jumla Ndogo - 7001** | | **29,243,666,666** |
| **KifuFungu 8001: Livestock Production and Marketing** | | |
| 14220168 | Compounding Fees | 216,666,667 |
| 14220175 | Livestock Market Fees | 6,595,000,000 |
| 14220190 | Receipt from Sale of Semens and Liquid Nitrogen | 430,000,000 |
| 14220191 | Receipts from Sale of Heifers | 880,000,000 |
| **Jumla Ndogo - 8001** | | **8,121,666,667** |
| **Kifungu 8002: Grazing Land and Animal Feed Resources Development** | | |
| 14220168 | Compounding Fees | 216,666,667 |
| 14220193 | Receipts from sale of Seeds and Hay | 200,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 14220217 | Movement Permits fee other than Livestock Market | 323,000,000 |
| **Jumla Ndogo - 8002** | | **739,666,667** |
| **Kifungu 9001: Maendeleo ya Uvuvi** | | |
| 14210147 | Fishing Licences & Export | 2,049,000,000 |
| 14210148 | Export Royalty | 18,796,000,000 |
| 14210149 | EEZ Licenses | 3,824,001,000 |
| 14220161 | Miscellaneous Receipts | 237,000,000 |
| 14220168 | Compound fees | 943,000,000 |
| 14220213 | Prawn Fishing Licenses | 212,000,000 |
| 14220216 | Receipts from sale of Laboratory& Inspection Services | 1,900,000,000 |
| 14220217 | Movement permit | 7,679,000,000 |
| 14220222 | Import Royalty | 30,000,000 |
| **Jumla Ndogo - 9001** | | **35,670,001,000** |
| **Kifungu 9002: Ukuzaji Viumbe maji** | | |
| 14220194 | Receipts from Sale of Fish and Fingerlings | 330,000,000 |
| **Jumla Ndogo - 9002** | | **330,000,000** |
| **Jumla Kuu** | | **74,105,001,000** |

## H. MIRADI NA SHUGULI ZITAKAZOTEKELEZWA MWAKA 2025/2026

### Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo na Uvuvi

171. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo: Kukamilisha Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko; na Kufanya upembuzi yakinifu pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (***ESIA***) kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Bagamoyo.

172. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa masoko saba (7) ya Uvuvi ya Tunduma (Tunduma), Kyamkwikwi (Muleba), Masuche (Momba), Manda (Ludewa), Zingibari (Mkinga), Kasanga (Kalambo) na Mbamba bay (Nyasa). Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha ujenzi wa mialo sita (6) ya Chato beach (Chato), Kalungu (Nkasi), Ng'ombo (Nyasa), Kayenze (Ilemela) Chifunfu (Sengerema), igabiro (Bukoba). Pia, Wizara itakamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya ukuzaji viumbe maji vya

Nyengedi, Ruvula, na Rubambagwe. Vilevile, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa Vituo vitatu (3) vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi vya Sota (Rorya), Simiyu (Busega), na Nyakalilo (Sengerema).

173. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kukamilisha ujenzi wa minada **23** ikiwemo minada **17** ya awali, minne ya (**4**) upili na miwili (2) ya mipakani. Aidha, kukamilika kwa minada hiyo kutaboresha na kuimalisha mazingira ya biashara ya mifugo nchini. Pia, Wizara imepanga kujenga miundombinu ya Mnada wa Awali wa Mikongeni Awamu ya Pili; Kununua na kusambaza mashine **10** za kuchunia ngozi ili kuboresha biashara ya zao la ngozi; Kukamilisha ujenzi wa vituo **10** vya kukusanyia maziwa; na Kununua na kusambaza mitamba bora **400** kwenye mashamba ya Serikali.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa kwa kuzingatia Mabadiliko ya Tabianchi (***Climate Smart Dairy Transformation Project*** - C-SDTP) wenye lengo la kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa kwa kununua ng'ombe **1,500**; Kununua dozi **2,000** za mbegu zilizochambuliwa (***sexed semen***) kwa ajili ya uhimilishaji; Kuimarisha upatikanaji wa malisho kwa kununua kilo **1,000** za mbegu za malisho; Udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwa kununua dozi **30,000** za chanjo ya Ndigana Kali (ECF), dozi **100,000** za chanjo ya Homa ya Mapafu (CBPP), dozi **16,163** za chanjo ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD), na dozi **16,163** za chanjo ya ugonjwa wa Kutupa Mimba (***Brucellosis***).

175. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa C-SDTP utaboresha huduma za ugani kwa kutoa mafunzo kwa wahimilishaji 53; Kuimarisha miundombinu ya ng'ombe wa maziwa kwa kujenga mazizi **1,315;** Kukarabati vituo **15** vya kukusanyia maziwa na kuviwekea vifaa; Kukarabati Kituo cha Karantini ya Mifugo cha Kwala kwa ajili ya kuwezesha biashara za kimataifa; na Kufanya tathmini ya awali ya upunguzaji wa gesi joto zinazotokana na shughuli za ufugaji. Pia, mradi utanunua *computer* **44,** *printer* **2**, pikipiki **122**, vishikwambi **100**, vifurushi vya ugani (extension kits) **100** na magari **12**. Pia, wataalamu **50** wa maabara watajengewa uwezo wa mbinu bora

za utambuzi wa magonjwa ya mifugo; na Kufanya mapitio ya Mtaala wa Kufundisha Mafundi Sanifu wa Maziwa (dairy technologists). Vilevile, Wizara itajenga majosho **34** mapya.

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa mbegu za malisho kutoka tani **222.54** hadi kufikia tani **333.54** kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya Vikuge na Langwira; Kujenga ghala la kukaushia na kuhifadhia mbegu za malisho katika shamba la Vikuge; na Kununua vifaa shamba. Aidha, Wizara itaboresha na kuendeleza hekta 1**,000** za eneo la malisho la Kitwai Simanjiro; Kusambaza mbegu za malisho kwenye mashamba darasa **300** ya malisho katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kujenga visima **8** na mbauti **50** kwa ajili ya kunyweshea mifugo maji. Pia, kukamilisha miradi ya ujenzi wa mabwawa, visima virefu, maghala ya kuhifadhia malisho katika mashamba ya Vikuge na Langwira, ukarabati wa mfereji wa umwagiliaji katika shamba la Langwira; na Kuondoa vichaka katika eneo la malisho la Kijiji cha Msomera.

177. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kuendelea na Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa. kwa lengo la kudhibiti na kutokomeza magonjwa manne (**4**) ya kipaumbele kwa kununua dozi **30,000,000** za Chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Mapafu ya Ng'ombe (**CBPP)** kwa ajili ya kuchanja jumla ya ng'ombe **30,000,000;** dozi **30,000,000** za chanjo dhidi ya ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (**PPR)** pamoja na Ndui kwa ajili ya kuchanja mbuzi na kondoo **30,000,000.** Aidha, Wizara itanunua jumla ya dozi **500,000** za chanjo ya Kichaa cha Mbwa ili kuwezesha Kampeni ya Kutokomeza Kichaa cha Mbwa ifikapo 2030.

**Utafiti na Mafunzo**

178. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kuwezesha vijana kujiajiri kwa kuwekeza katika shughuli za ufugaji, uvuvi na ukuzaji viumbe maji kupitia Programu ya BBT. Kwa upande wa Sekta ya Mifugo, Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vijana **240** kwenye vituo nane (**8)** vilivyopo katika Taasisi za LITA na TALIRI na

kuanzisha vituo vipya viwili (**2**) katika mikoa miwili (**2**). Aidha, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Programu hiyo itaendelea kutoa mafunzo ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba kwa vijana **200** na kuwawezesha kupata mitaji.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kutekeleza programu ya BBT kupita mradi wa unenepeshaji wa mbuzi na kondoo, uzalishaji wa malisho na vyakula vya mifugo katika Kituo cha TALIRI - Kongwa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa lengo la kutoa mafunzo kwa vitendo ya unenepeshaji wa mbuzi na kondoo kwa vijana na wanawake ili waweze kujiajiri katika mnyororo wa thamani. Aidha, kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya machinjio ya kisasa ya mbuzi na kondoo, mabanda 10 yenye uwezo wa kufuga mbuzi 2,000 kwa wakati mmoja, mabucha 10, visima 2 vya maji, ofisi ya mradi, jengo kwa ajili ya majiko ya kuchoma nyama na vibanda vya kupumzikia wateja. Pia, tutajenga miundombinu ya ufugaji mbuzi na kondoo yenye uwezo wa kubeba mbuzi 15,000 kwa wakati mmoja katika vitalu vya Ranchi ya Taifa (NARCO). Vilevile, kupitia mradi huu tutajenga miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia teknolojia ya *Centre Pivot Irrigation* kwa ajili ya kilimo cha malisho na mbegu za malisho.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi **8** za LITA na **5** za FETA. Aidha, Wizara itaratibu na kuwezesha mafunzo kwa Wakufunzi (***Teaching Methodology***) kutoka Kampasi za LITA na FETA na Vyuo Binafsi vinavyotumia Mitaala ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Pia, Wizara itahuisha Agenda za Utafiti wa Mifugo na Uvuvi ili kuendana na mahitaji ya sasa.

**Huduma za Ugani**

181. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha uhawilishaji wa maarifa na teknolojia mpya kwa wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbe maji, Wizara itaendelea kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani **1,000** wa Mifugo na Uvuvi; Kutoa elimu kupitia maonesho ya kitaifa, kikanda na kimataifa; na Kununua na kusambaza Pikipiki

**200** kwa Maafisa Ugani. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbe maji. Pia, boti **110** zitanunuliwa na kukopeshwa kwa walengwa kwa masharti nafuu. Vilevile, Wizara itahuisha Mwongozo wa Utoaji Huduma za Ugani wa Mifugo na Uvuvi.

182. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kuijengea uwezo Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa maabara ya kuzalisha chanjo za virusi katika Taasisi ya Chanjo Tanzania ambapo ujenzi wake umefikia asilimia **25,** na kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya kujenga uwezo wa kuzalisha chanjo kwa wingi. Aidha, Serikali itaendelea kuijengea uwezo Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania ili iweze kufanya utambuzi wa magonjwa ya mifugo kwa kuzingatia ithibati ya kimataifa, na kuimarisha ubora na uwezo wa maabara za kanda, kuongeza upatikanaji wa vitendea kazi, ukarabati na ujenzi wa jengo jipya lenye ofisi na maabara katika Kituo cha Kanda ya Kati Dodoma.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuimarisha na kurasimisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu sahihi za uvuvi na kuwatambua rasmi wavuvi (***kwa kuwapatia kadi za kielektoroniki***) na shughuli zao nchini, kutoa mafunzo kwa wakusanyaji takwimu za uvuvi, kufanya sensa za uvuvi katika Ziwa Victoria, Nyasa na Rukwa; na maji madogo (***Bwawa la Nyumba ya Mungu, Maziwa ya Eyasi, Natron na Tlawi***) ili kupata takwimu na kuwezesha upangaji wa mipango madhubuti na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Aidha, Wizara itafanya tathmini kutambua na kuainisha mchango wa uvuvi katika maji madogo kwa lengo la kuchochea na kuimarisha usimamizi na uzalishaji kwenye maji madogo

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za Uvuvi kwa kununua ndege nyuki (**2**), kuweka maboya (**79**) ya kuonesha mipaka katika Maeneo Tengefu matatu (**3)** katika Ziwa Victoria (**1**), Ziwa Nyasa (**1**) na Ziwa Rukwa (**1**). Aidha, Wizara itaimarisha mashirikiano na taasisi mbalimbali katika kufanya doria zenye siku

kazi **8,400** ili kudhibiti Uvuvi na biashara haramu na kuchochea Uvuvi endelevu katika maeneo yote ya Uvuvi. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi (*BMUs*) **60** kwa kuvijengea uwezo na kufanya tathmini ya utendaji wa vikundi hivyo nchini. Pia, Wizara kupitia TAFIRI itafanya mapitio ya Mwongozo wa Usimamizi wa Matumizi ya Taa za sola katika shughuli za uvuvi; kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Uingizaji wa Zana za Uvuvi pamoja na Mkakati wa Uvunaji wa Sangara nchini.

185. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kusimamia uthibiti wa ubora na masoko ya mazao ya Uvuvi kwa kuwajengea uwezo wakaguzi **42** na wadau **500**; kuimarisha Vituo **20** vya Uthibiti wa Ubora na Masoko ya mazao ya Uvuvi kwa kuvipatia vitendea kazi; Kufanya kaguzi za kawaida **9,200;** Kaguzi **800** za kila robo mwaka, kuandaa mwongozo wa usimamizi wa biashara na mabucha ya samaki na kuboresha kanuni zinazosimia ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ili kuendana na matakwa ya masoko ya ndani, kikanda na kimataifa hususan masoko ya samaki na mazao yake kwa nchi za EU, China, Saudi Arabia na Marekani.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuimarisha udhibiti ubora wa mazao ya uvuvi na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira ili kuongeza thamani katika mnyororo wa mazao ya uvuvi ikiwemo matumizi ya nishati ya jua ***(solar drier)*** kwenye ukaushaji wa mazao ya uvuvi pamoja na kusanikisha mitambo ya kuzalisha barafu.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake na vijana kushiriki katika usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi pamoja na kuhamasisha wanajamii **2,000** katika Sekta ya Uvuvi kuhusu namna ya kujikinga na unyanyasaji wa kijinsia, kuweka mikakati ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, pamoja na kujikinga na maambukizi dhidi ya VVU.

**Maabara ya Uvuvi Tanzania**

188. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi itaendelea kutoa huduma za uchunguzi wa samaki na mazao ya uvuvi kwa ajili ya kulinda afya ya jamii na usalama wa vyakula nchini; Kuboresha mazingira ya kazi, kutoa mafunzo kwa watumishi na kuongeza vitendea kazi; Maabara imepanga kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi nchini kwenye sampuli **3,000** za samaki, vyakula vya samaki, maji, udongo, mazao mengine ya uvuvi na vifungashio. Aidha, Maabara itaendelea kukamilisha mchakato wa ithibati (Accreditation) na kuboresha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Kanda ya Pwani (Dar es Salaam); Kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli zinazofanywa na Maabara ya Taifa ya Uvuvi (FLSU) kupitia fursa za maonesho na warsha mbalimbali.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

189. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji wa vifaranga na utoaji wa huduma bora za ugani kwa kusimamia na kuendesha vituo nane (**8**) vya ukuzaji viumbe maji (Ruhila – Ruvuma, Kingolwira – Morogoro, wamapuli – Tabora, Machui – Tanga, Nyengedi – Lindi, Ruvula – Mtwara, Kunduchi - Dar es Salaam na Rubambagwe - Geita) ili viweze kuzalisha vifaranga milioni **15.** Aidha, Wizara inatarajia kutoa huduma za ugani kwa wakuzaji viumbe maji wapatao **15,000** ili waweze kuzalisha kwa tija na kufuata sheria, kanuni na taratibu. Pia, kukamilisha ujenzi wa mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji katika Halmashauri **20** nchini. Vilevile, Wizara itafanya kaguzi na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za uzalishaji na udhibiti wa magonjwa katika mashamba ya samaki, vitotoleshi na viwanda vya chakula cha samaki katika Mikoa **15.** Vilevile, Wizara itakamilisha kufanya mapitio na kuhuisha Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji (***National Aquaculture Development Strategy*** *2018 – 2025 -* ***NADS***) ili kupata mkakati mpya (***NADS*** *2025 – 2030*).

**Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP)**

190. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea na Ujenzi wa Soko la Samaki Kipumbwi – Pangani; Ukarabati na upanuzi wa miundombinu katika vituo vya ukuzaji

viumbe maji vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Ruvuma), Mwamapuli (Tabora) na kukamilisha ujenzi wa kituo kipya cha Rubambagwe (Geita). Pia, Wizara itaendelea na ujenzi wa vichanja **40** vya kukaushia Dagaa pamoja na kununua na kusimika mtambo wa kuzalisha barafu katika mwalo wa Kilwa Kivinje mkoani Lindi.

## I. TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

### Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)

191. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI, itaendelea kufanya tafiti katika maeneo ya kipaumbele ikiwemo uzalishaji wa mbegu mama za malisho, jiwelishe na utafiti wa kuku wa asili jamii ya Horasi na kusimamia utafiti wa Mifugo nchini. Katika mwaka 2025/2026, TALIRI imepanga kuzalisha tani saba (**7**) za mbegu mama, zilizopata ithibati na kuzalisha marobota **110,000** ya majani makavu na kulima ekari **50** zitakazotumika kuzalisha malisho katika kituo kipya cha Nsimbo. Aidha, TALIRI itanunua mitambo ya kuzalisha jiwelishe la mbuzi utakaozalisha mawelishe **112,000** kwa mwaka. Katika kuendeleza utafiti wa uzalishaji wa kuku wa asili jamii ya Horasi, TALIRI itazalisha na kukuza vifaranga **2,500** vya kizazi cha pili na kuchagua kuku **450** kwa ajili ya utafiti. Aidha, TALIRI itahuisha vibali **21** na kutoa vibali vipya **50** vya Maadili ya Utafiti.

### Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)

192. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TAFIRI itaendelea kufanya tafiti katika maeneo ya kipaumbele ambayo ni kuzalisha vifaranga bora vya samaki na chakula bora cha samaki ili kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi kwenye uchumi wa nchi; Kuweka vifaa **20** vivutia samaki (*Fish Agregating Devices* - FADs) katika maeneo ya Mkoa wa Tanga (***Mkinga***), Pwani (***Mkuranga***) na Lindi (***Kilwa***); na Kufanya utafiti wa pweza, kambamiti, samaki wanaoelea, na jodari. Aidha, TAFIRI itafanya tathmini ya kimazingira kwa ajili ya kuweka vizimba katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, Ziwa Nyasa na Tangayika. Pia, TAFIRI itafanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika na Ikimba.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

193. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) inatarajia kudahili wanafunzi **5,736**, kutoa mafunzo ya muda mfupi ya Mifugo kwa kaya **1,500** za wafugaji na kuendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi tisa (**9**) za LITA. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na wadau itatekeleza Programu ya Elimu na Ujuzi wa Kazi za Uzalishaji (***Education and Skills for Productive Jobs Program-for-Results - Phase*** II); na Kuendelea kujenga Kituo cha kubadilishana teknolojia (***African Modern Agriculture Technology Exchange Training Centre***) ambacho kitakuwa ni kampasi ya tisa (**9**) ya LITA katika Mkoa wa Songwe. Pia, LITA itatoa mafunzo kwa wakufunzi **35** na wanafunzi wa Stashahada **30** wa fani ya Afya ya Mifugo kupitia mradi wa EDUVET, chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (***EU***).

**Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

194. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wakala ya Mafunzo ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) inatarajia kudahili wanafunzi **1,681**, na kutoa mafunzo ya muda mfupi ya wavuvi na wakuzaji viumbe maji **6,095**. Aidha, Wakala itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Gabimori; Kuanza ujenzi wa Kampasi mpya ya Kibirizi; Kukarabati na kuongeza vifaa vya mafunzo katika Kampasi za Mbegani, Nyegezi na Mikindani. Pia, Wakala kwa kushirikiana na wadau itatekeleza Programu ya Elimu na Ujuzi wa Kazi za Uzalishaji (***Education and Skills for Productive Jobs Program-for-Results - Phase* II);**

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

195. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) itaendelea kutekeleza mradi wa uhifadhi na usimamizi wa pamoja maeneo ya hifadhi yaliyopo katika mpaka wa Tanzania katika Wilaya ya Mkinga na Diani-Chale - Kenya (***Transboundary Marine Conservation Area*** - TBCA) ili kuweza kusimamia kwa pamoja rasilimali hizo. Aidha, MPRU kupitia ufadhili wa Mfuko wa Mazingira Duniani (***Global Environmental Facility*** - GEF) itatekeleza mradi wa usimamizi na ulinzi wa rasilimali za matumbawe katika maeneo ya

Kilwa, Mafia na Tanga, pamoja na kuendeleza usimamizi wa maeneo ya hifadhi kupitia mipango ya uuzaji hewa ukaa (***Blue Carbon***) kwa kushirikiana na vijiji na mamlaka mbalimbali katika maeneo ya Hifadhi.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia MPRU itaendelea kutangaza maeneo yaliyohifadhiwa na vivutio vya utalii vilivyomo pamoja na kuboresha miundombinu ya utalii wa kiikolojia (*ecotourism*) ili kuongeza idadi ya watalii kutoka ndani na nje ya nchi na kuongeza mapato yatokanayo na utalii bahari na kwenye maji baridi. Aidha, MPRU itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa hoteli za kiikolojia za kitalii katika maeneo yaliyohifadhiwa ili kuongeza idadi ya watalii na mapato ya Serikali.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

197. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kuliimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania (***TAFICO***) kwa kuwezesha ununuzi na usimikaji wa mtambo wenye uwezo wa kuzalisha tani **10** za barafu kwa siku; Ujenzi wa ghala la ubaridi lenye uwezo wa kuhifadhia samaki tani 40 kwa siku; Kukamilisha ununuzi wa meli mbili (**2**) za Uvuvi wa Bahari Kuu kati ya nne (4) zilizopo kwenye mpango; Kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya Uvuvi; na Ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chakula cha samaki wafugwao (Fish Feed Mill) chenye uwezo wa kuzalisha tani 30 kwa siku kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi (***Agriculture and Fisheries Development Program***-AFDP). Hatua hizi zitaliwezesha Shirika hilo kuzifikia fursa za Uchumi wa Buluu na kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika Pato la Taifa Aidha, TAFICO itaimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi katika biashara ya mazao ya uvuvi na kubadilishana uzoefu wa uvuvi wa Bahari Kuu.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

198. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) inatarajia kutoa leseni na vibali kwa meli **89** zinazofanya shughuli za uvuvi katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu**.** Aidha, DSFA kwa kushirikiana na ALBACORA Group itaendelea

kutekeleza makubaliano ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, kushusha tani **100** za samaki wasiolengwa na kujenga uwezo wa mabaharia wa kitanzania katika Uvuvi wa Bahari Kuu.

199. **Mheshimiwa *Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Serikali, kupitia DSFA, itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari kwa kuweka Waangalizi wa Uvuvi, kufanya ukaguzi wa meli na kufanya doria majini na angani. Pia, DSFA itafanya ufuatiliaji wa meli **89** za Uvuvi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (***Electronic Monitoring System***) kwa kufunga kamera kwenye meli.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, **DSFA** itatoa elimu kwa wadau kuhusu vivutio na fursa zinazopatikana kwenye Uvuvi wa Bahari kuu, kufanya mazungumzo na wawekezaji ili kuhamasisha ukataji wa leseni na uwekezaji katika Uvuvi wa Bahari Kuu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ya bandari na viwanda vya samaki.

201. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa fedha 2025/2026, DSFA kwa kushirikiana na taasisi za utafiti nchini itaendelea kuwezesha tafiti katika Bahari Kuu ili kuimarisha uhifadhi, usimamizi, udhibiti na uendelezaji wa uvuvi kwa ajili ya kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika Pato la Taifa na kuboresha kipato kwa jamii ya wavuvi.

**Bodi ya Nyama Tanzania (TMB)**

202. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imepanga kufanya ukaguzi kwa wadau **15,784** wanao jishughulisha katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa nyama, kusajili wadau **4,883** na kuhuisha usajili wa wadau **10,901** ili kuhakikisha nyama na bidhaa za nyama zinazozalishwa hapa nchini zinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Aidha, Bodi itatoa mafunzo ya ufugaji kibiashara kwa wafugaji **300**, kutoa elimu ya uandaaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu za usafi kwa wadau **12,090**. Pia, Bodi imepanga kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi, kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa shughuli za Bodi.

**Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB)**

203. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Bodi ya Maziwa Tanzania **(**TDB) imepanga kutoa mafunzo ya ufugaji bora hususani matumizi ya teknolojia za kisasa za uzalishaji wa maziwa kwa wadau **1,200** wa Tasnia ya Maziwa; uzingatiaji wa Sheria ya Tasnia ya Maziwa Sura **262** kwa wadau **800**; kufanya ukaguzi wa wadau **1,200** katika maeneo ya uzalishaji wa maziwa, vituo vya kukusanyia maziwa, viwanda vya kusindika maziwa, biashara ya maziwa, bandari na vituo vya mipakani. Aidha, TDB imepanga kusajili wadau **800** na kuwawezesha kurasimisha biashara zao. Pia, TDB imepanga kutoa mafunzo kwa wakaguzi **184** wa maziwa kuhusu masuala ya kisheria na kitaalam ya kuzingatia katika ukaguzi wa maziwa, kuwezesha uanzishwaji wa vyama vitano (**5**) vya ushirika wa wadau wa Tasnia ya Maziwa, kuimarisha mifumo ya takwimu kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), na kukuza mawasiliano miongoni mwa wadau wa Tasnia ya Maziwa na kujenga uwezo wa watumishi wa TDB kupitia Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko Tabianchi (C-SDTP).

204. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kusogeza huduma karibu zaidi na wadau wa Tasnia ya Maziwa nchini, TDB itafungua vituo zaidi vya kanda na mipakani na kuimarisha ofisi za kanda zilizo funguliwa. Aidha, TDB itaendelea kutafuta masoko na kuratibu biashara ya maziwa na kuhimiza matumizi ya maziwa na bidhaa za maziwa kupitia maadhimisho ya kitaifa na kimataifa.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

205. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia NARCO imepanga kuzalisha ndama **4,870**; kati ya ng'ombe wazazi **6,088** sawa na asilimia **80** ya uzalishaji; kusambaza mitamba **824** kwa wafugaji ili kuboresha kosaafu za Mifugo; Kuzalisha na kuuza tani **675** za nyama; Kunenepesha na kuchinja ng'ombe **6,750**; Kufyeka na kuondoa vichaka hekta **1,000** katika Ranchi za Kongwa, Ruvu na West Kilimanjaro kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho; Kuzalisha marobota **60,000** ya malisho; Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji **450** katika vijiji vinavyozunguka Ranchi za NARCO; na Kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi **500** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini katika

Ranchi za NARCO. Aidha, NARCO itaanzisha kambi moja ya Mifugo katika Ranchi ya Mkata (Livestock Guest House) kwa ajili ya kutunzia Mifugo wakati wa ukame na uhaba wa chakula.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imetenga fedha Tzs **3,469,716,480** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Livestock Guest House katika Ranchi ya Mkata. Maandalizi ya Mradi huu yako katika hatua ya kusainiwa kwa Mkataba kati ya NARCO na Mkandarasi SUMA JKT ili kujenga miundombinu yote ya Mradi huo itakayowezeshwa huduma ya guest ya mifugo kutolewa katika Ranchi hiyo.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA)**

207. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania itaendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa na uzalishaji wa chanjo kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa ya Mifugo nchini. Wakala imepanga kuzalisha dozi **105,000,000** za chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo; Kufanya uchunguzi wa sampuli **40,000** za wanyama ili kubaini magonjwa ya mifugo; Kuhakiki ubora na usalama wa vyakula vya mifugo kwenye sampuli **5,200** za vyakula vya mifugo; Kutoa vibali **200** na kuhuisha leseni **300** za kuingiza na kuuza viuatilifu nchini; Kuendelea na utafiti wa utengenezaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya Kichaa cha Mbwa, Mapele Ngozi, na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo. Aidha, Wakala itaendelea na ujenzi wa jengo la kisasa la kituo cha Wakala jijini Dodoma na kukamilisha ujenzi wa jengo la maabara ya kisasa ya uzalishaji wa chanjo za magonjwa ya Mifugo yatokanayo na virusi katika kituo cha TVI Kibaha.

**J. MASUALA MTAMBUKA**

**Uwezeshaji wa Sekta Binafsi**

208. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kuwezesha mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **680** kwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi; Kuendelea na mazungumzo na wafugaji pamoja na wavuvi na taasisi inayotoa dhamana ya mikopo (*PASS*); Kuendelea kushughulikia kero za wafugaji na wavuvi hususan zinazohusu biashara zao; Kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi;

Kuendelea kusaidia katika kuboresha maandiko ya biashara ya wafugaji na wavuvi kwa ajili ya maombi ya mikopo yao; Kuendelea kufuatilia katika taasisi za fedha na kwenye vyama vya wafugaji na wavuvi ili kujua sababu za kukwama kwa mikopo yao; na Kuendelea kutoa elimu ya fedha na biashara na umuhimu wa kutunza kumbukumbu na kuwa na akaunti za benki hasa akaunti za biashara ili wafugaji na wavuvi waweze kukopesheka kwa urahisi, kuliko kutumia mitandao ya simu katika mizunguko ya fedha zao.

**Utawala Bora, Jinsia na VVU/UKIMWI**

209. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeomba kupatiwa Ikama yenye jumla ya nafasi **183** kwa ajili ya ajira mpya **89**, uteuzi **3** upandishwaji vyeo **80**, na ubadilishwaji wa kada **11**. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya kutekeleza Mwongozo wa Kudhibiti VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma kwa kutoa elimu kwa watumishi **1,020** kuhusu VVU/UKIMWI, Magonjwa yasiyoambukizwa na kuhamasisha upimaji wa afya. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa kwa kuelimisha watumishi kuhusu Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma.

**Mazingira na Mabadiliko Tabianchi**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (***Environmental and Social Impact Assesment*** – ESIA) katika miradi nane (**8**) ambayo ni Bandari ya Uvuvi Bagamoyo; Masoko ya Samaki ya Tunduma, Kyamkwiki, Momba, Manda na Zingibari; na Mialo miwili (**Masuche na Ng'ombo**). Aidha, Wizara imepanga kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi **2,000** juu ya kupunguza athari mbaya za mazingira zinazotokana na shughuli zisizo endelevu za mifugo, uvuvi na ufugaji wa samaki pamoja na mbinu za kustahimili Mabadiliko Tabianchi katika Ukanda wa Pwani, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania. Vilevile, Wizara itafanya ukaguzi wa mazingira katika machinjio (**7**), viwanda (**20**) vya kusindika samaki na ngozi pamoja na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira (***Environmetal and Social Monitoring Plan*** - ESMP) katika miradi saba (7)

inayoendelea ambayo ni minada ya mifugo na masoko ya samaki. Pia, Wizara inaendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia katika taasisi zake 12.

**Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kuanzisha kanzidata kwa ajili ya usajili na kutoa vitambulisho vya kidigitali kwa wadau wote wa Sekta ya Uvuvi ili waweze kunufaika na kupata fursa mbalimbali za masoko. Aidha, Wizara itaendelea kuhakikisha maboresho kwenye mifumo yake ya TEHAMA na kuiunganisha na mifumo mingine ya TEHAMA ndani ya Serikali. Vilevile, Wizara imepanga kuboresha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA ili kuongeza ufasini na kasi kwenye usimamizi wa rasilimali za Mifugo na Uvuvi kupitia TEHAMA.

**Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa**

212. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha mahusiano katika uwekezaji, masoko na tafiti zinazohusu Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**K. HITIMISHO**

213. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapo hitimisha Hotuba yangu, naomba kwa unyenyekevu mkubwa kutumia fursa hii kuwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake na kwa mafanikio yaliyopatikana katika Mwaka 2024/2025, ambayo yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, Asasi zisizo za Kiserikali, Sekta Binafsi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuzitambua na kuzishukuru nchi za Marekani, Japan, Korea Kusini, Uingereza, Uholanzi, Ireland, Saudi Arabia, United Arab Emirates (UAE), Oman, Norway, Jumuiya ya Ulaya, Jamhuri ya Watu wa China, Ethiopia,

Jordan, Bahrain, Kuwait, Vietnam, Qatar, Comoro na Misri; kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Naomba pia kutambua na kuzishukuru jumuiya za kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Shirika la Maendeleo la Kiserikali la Nchi za Afrika Mashariki (IGAD), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).

215. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue fursa hii kuzishukuru taasisi zinazoendelea kutuunga mkono kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:- Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (Lake Victoria Fisheries Organization - LVFO), Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika Authority - LTA), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Tuna Commission - IOTC), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Commision - SWIOFC), Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (Indian Ocean Rim Association - IORA), Western Indian Ocean Marine Science Association (WIOMSA), Kamisheni ya Kimataifa ya Usimamizi wa Nyangumi (International Whaling Commission - IWC), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Commission - IOC), na Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness -AWARFA).

216. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue fursa hii, kutambua pia mchango wa mashirika mengine tunayoshirikiana nayo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ambayo ni: Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Kiatomiki (International Atomic Energy), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Misaada la Poland (Polish Aid), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ireland (TEAGASC), Serikali ya Uholanzi, na Serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (Economic and Social Development

Programme – ESDP), na Overseas Fishery Cooperation Foundation (OFCF) of Japan.

217. ***Mheshimiwa Spika***, nazishukuru pia taasisi za kifedha na Wadau wa Maendeleo kwa ushirikiano wao hasa, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GIZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA); na mashirika ya IAEA, UNIDO, ILRI, CIAT, ASARECA, CCARDESA na GEF kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

218. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za Bill and Melinda Gates Foundation, World Wide Fund for Nature (WWF), The Nature Conservancy (TNC), Wildlife Conservation Society (WCS), International Union for Conservation of Nature (IUCN), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection 143 of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC), Gatsby Africa pamoja na Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

219. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru tena Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na maarifa pamoja na maelekezo anayotupatia kama Wizara kuhakikisha rasilimali za Mifugo na Uvuvi zinachangia katika Uchumi wa Buluu ili kukuza uchumi wa Taifa kwa maendeleo endelevu. Nina imani kubwa chini ya uongozi wake

Taifa letu litapiga hatua kubwa za kiuchumi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwaka 2020 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Tatu wa Mwaka 2021/2022 – 2025/2026 utaendelea kutekelezwa kikamilifu hususan katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii tena kuwashukuru na kuwapongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo; Kamati ya Uongozi; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa maoni na ushauri unaolenga kuboresha na kuimarisha Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, niwashukuru wadau mbalimbali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, wafugaji na wavuvi hususan wanaozingatia Sheria katika utendaji wa kazi zao kote nchini kwa kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Napenda kuwaahidi kwamba Wizara itaendelea kusimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuunga mkono juhudi za wafugaji, wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa bidhaa za Mifugo na Uvuvi.

221. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kurejea tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti (Mb), Mbunge wa Jimbo la Misungwi na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri na ushirikiano wake katika kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, natoa pia shukrani zangu kwa Prof. Riziki Silas Shemdoe, Katibu Mkuu, Abdul Rajab Mhinte Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) na Dkt. Edwin Paul Mhede Naibu Katibu Mkuu (Uvuvi), Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi nzuri wanazozifanya.

222. ***Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Wafugaji wote nchini. Nawashukuru sana wafugaji wote wa nchi hii, ni wazi nilipoteuliwa kuja kwenye Wizara hii wapo waliosema atawaweza wafugaji wa nchi hii? Majibu wanayo wafugaji wenyewe wakiongozwa na ndugu yangu Mrida Mshota, Mwenyekiti wa Chama Cha Wafugaji Tanzania. Tumetulia, tunafuga mifugo yetu kwa amani kabisa na sasa

tunakwenda kuhakikisha tunayafikia masoko yote kwa ajili ya mifugo yetu na mazao yao. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mfugaji namba moja nchi hii alishakamilisha kazi yake ya Diplomasia ya Uchumi, masoko yapo tayari Dunia nzima, na kubwa zaidi ametuwezesha kupata chanjo kwa ajili ya mifugo yetu nchi nzima! Zoezi lililofanyika kipindi cha Awamu ya kwanza na sasa ameweza yeye tena si mwingine ni Mama Mlezi wa Taifa na mfugaji namba moja ndani ya Taifa letu. Sisi Wafugaji tunasema Mheshimiwa Rais tupo tayari kwa mambo mawili makubwa; moja ni kukupa kura zote ifikapo mwezi Oktoba 2025 ili tuendelee kunufaika na utumishi wako, na pili ni kupeleka mifugo yetu na mazao yake Duniani. Hakika Ihsani hulipwa kwa Ihsani, nasi tupo tayari kwa kazi.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa uvuvi hatuna la kuelezea zaidi ya kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyofanya mageuzi makubwa kwenye sekta hii, kwani sote ni mashuhuda tunaona namna alivyobadirisha maisha ya wavuvi hapa nchini kwa kutuwezesha kupata boti mpya za kisasa za uvuvi pamoja na vizimba vya kufugia samaki ambvyo matunda yake tunayaona. Aidha, sisi wavuvi tunakushukuru sana kwa kutupatia vitendea kazi hivyo na tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza kipato pamoja na kuboresha maisha yetu. Hivyo, tukuahidi tena Mheshimiwa Rais kuwa sisi wavuvi tuna deni kwako ambalo tutalilipa mwezi Oktoba, 2025 kupitia kwenye boksi la kura.

224. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Kondoa ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo na ya Taifa letu, naomba niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Kwa Wana CCM wenzangu ndani ya Jimbo la Kondoa kuanzia ngazi ya Shina hadi Wilaya na leo tukiwa tumewakilishwa hapa Bungeni na Viongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania Kata zote 21 na Jumuiya ya Wazazi Kata zote 21 pamoja na Sekretarieti ya Wilaya, nina uhakika kazi ya Kamsese ndani ya Jimbo la Kondoa siyo ya kumulika kwa tochi, zinaonekana wazi kwa sekta zote za kiuchumi na kijamii. Naye mnamuona bado

yupo imara kabisa na niwashukuru sana kwa tamko lenu Wanakondoa kwamba hamuhitaji mabadiliko ya Uongozi ndani ya Jimbo la Kondoa, nami nawaambia nipo tayari kwa mchakamchaka mwingine kwa miaka mitano ijayo na ndipo tulipoelekezwa tuseme #KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE.

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwisho lakini sio kwa umuhimu, niombe kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa ***Dkt. Samia Suluhu Hassan,*** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuzipa kipaumbele Sekta za uzaishaji ikiwemo Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, nimpongeze Rais kwa dhati ya moyo wangu kwa kuendelea kuziongezea bajeti ya utekelezaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji ambapo itaongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujuma.

**L. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026**

226. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99) inaomba kutumia jumla ya shilingi **476,655,072,000.** Kati ya fedha hizo, shilingi **101,516,670,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **375,138,402,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.** Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida: shilingi **101,516,670,000**
- Matumizi ya Mishahara: (PE) shilingi **47,264,785,000**
- Matumizi Mengineyo: (OC) shilingi **54,251,885,000**

(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo: shilingi **375,138,402,000**
- Fedha za Ndani shilingi **227,994,375,000**
- Fedha za Nje shilingi **147,144,027,000**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, ninaomba taarifa yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kutoa shukurani kwa niaba ya Kamati kwa kunipa nafasi ili niweze kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kamati za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Msingi wa uchambuzi wa taarifa hii ya utekelezaji wa bajeti ya Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6(1)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti na makadirio ya ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inahusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taarifa ya utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi iliyochambuliwa inagusa maeneo yafuatayo:-

(i) Hali ya jumla ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(ii) Tathmini ya jumla ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iii) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;

(iv) Tathmini ya Ukusanyaji wa maduhuli; na

(v) Upatikanaji wa fedha kutoka hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) iliyotaka matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti yatumike kufanya ulinganisho na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ninaomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo uliiwezesha Kamati kupata masuala ya kuzingatia kuhusu hoja inayojadiliwa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 27 na 28 Machi, 2025 Kamati ilikutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika maelekezo ya Kamati, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa majukumu, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99) ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 69.1. Hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 42.7 sawa na 62% ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2024/2025. Kamati

ilichambua maduhuli hayo ili kujiridhisha na juhudi za ukusanyaji wa maduhuli. Matokeo ya uchambuzi yanaonekana katika Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(i) Jumla ya makusanyo ya maduhuli hadi kufikia Februari, 2025 yamefikia 62% ya lengo la kukusanya shilingi 69.1;

(ii) Sekta ya mifugo imekusanya shilingi 22.7 sawa na 63% ya lengo la makusanyo hayo na;

(iii) Sekta ya uvuvi imekusanya shilingi 19.9 sawa na 60.3% ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya ukusanyaji wa maduhuli inaonesha kuwa jitihada zaidi za ukusanyaji mapato zinahitajika ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo na mtiririko wa fedha, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 363.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi 442 na fedha za nje ni shilingi 121. Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025, Wizara ilipokea 18.07% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ni wazi kuwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa na Serikali kupitia Wizara hii hauwezi kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa miwili ya Geita na Dodoma na kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali kupitia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Matokeo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki - Mwalo wa *Chato Beach* ulioko Mkoani Geita (Mradi Na. 4486),

una thamani ya shilingi bilioni 1.8. Mradi huu unalenga kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kutoka 50% hadi 10%, kuongeza fursa za ajira, kuongeza kipato kwa wananchi wa Chato na Taifa kwa ujumla, pamoja na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi. Aidha, utekelezaji wa mradi huo umefikia 91% na unategemewa kukamilika tarehe 30 Julai, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie eneo hilo kwa msisitizo. Mradi huu unalenga kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kutoka 50% hadi 10%, kuongeza fursa za ajira, kuongeza kipato kwa wananchi wa Chato na Taifa kwa ujumla pamoja na kukuza biashara ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huu, Kamati inashauri kuwa, eneo lote la mradi lijengewe uzio ili kudhibiti wizi na uharibifu. Pia Serikali kwa kushirikiana na halmashauri wahakikishe mradi huu unalindwa na kutumika ipasavyo ili kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, Kamati inashauri fedha za ukamilishaji wa mradi huu itolewe utekelezaji ufikie 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ambao umekamilika kwa 100% ni Mradi wa Ghala la Kuhifadhi Malisho. Pamoja na kuwa utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa 100%. Mradi huu unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa mitambo ya kuvunia majani, trekta na mashine ya kukatia na kufunga majani, miundombinu ya umwagiliaji pamoja na hatimiliki ya ardhi. Hali hii inaweza kuibua migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo una gharama ya jumla ya shilingi bilioni 24.98 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 23.2 ni gharama ya mkandarasi na shilingi bilioni 1.7 ni gharama ya mshauri elekezi. Utekelezaji wa mradi huu umefikia 93%. Hadi sasa mkandarasi amelipwa shilingi bilioni 18.14 sawa na asilimia 78.1 ya gharama ya mradi mzima. Kamati imeridhishwa na inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huu, utakaoiwezesha Wizara kuwahudumia wadau wake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha na matumizi ya kawaida. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99) ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 97.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 363.11 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kama ilivyofafanuliwa kwenye jedwali namba tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilipokea 23.2% ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara hii haitarajiwi kukamilisha majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri, fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, wakati wa kupitia na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utekelezaji kwa ushauri huo uko katika hatua mbalimbali. Kamati inashauri Serikali kuendelea kutekeleza na kukamilisha ushauri unaotolewa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Fungu 99 imekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa fedha ya bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi wa ulinganisho wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa makadirio ya maduhuli yalipangwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99) ili kujenga msingi wa maoni na ushauri kuhusu maduhuli. Kamati ilichambua maduhuli hayo kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

(i) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara hii yameongezeka kwa 7.24% ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kufikia 54.5% huku muda halisi wa utekelezaji wa bajeti ukiwa umefikia 66%, ni vigumu kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuzingatia uzoefu wa nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida, makadirio ya jumla ya bajeti ya nchi, huzingatia makadirio ya makusanyo kwa sekta moja moja. Uwekaji wa lengo la makusanyo usiozingatia uhalisia unaweza kuathiri uhalisia wa bajeti ya matumizi. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni kuwa, ni vizuri kila sekta inapokadiria ukusanyaji wa maduhuli izingatie uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya matumizi ya kawaida, Kamati ilichambua makadirio ya matumizi ya Fungu – 99 Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Matokeo ya uchambuzi yanaonyesha kuwa makadirio yameongezeka kwa 3.26% ikilinganishwa na mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo na kubaini mambo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yameongezeka kwa 1.67% ikilinganishwa na mwaka 2024/2025;

(ii) Utegemezi wa vyanzo vya nje kwa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii umeongezeka kwa 15.5% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha unaoisha, 33% ya bajeti ya maendeleo ilikuwa ni fedha za nje ikilinganishwa na 38% kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Pamoja na bajeti ya fedha za miradi kutoka nje kuongezeka kwa asilimia 21.57 kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ongezeko hilo haliendani na uhalisia uliojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha wa 2024/2025. Sekta ya mifugo na uvuvi ilipokea 1.2% tu ya makadirio ya fedha za nje kwa mwaka huo;

(iv) Uzoefu wa jumla wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kuwa, katika kipindi cha utekelezaji, 66%, Wizara ilipata fedha za maendeleo kwa 18.48% tu ya makadirio. Hali hiyo inaashiria kuwa ongezeko la bajeti kwa 3.26% linaweza lisiwe na uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matokeo hayo, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yana sura ya kuongeza ufanisi katika sekta hizo. Hata hivyo, iwapo changamoto za upatikanaji wa fedha zilizojitokeza katika mwaka wa fedha ulioisha hazitapatiwa ufumbuzi, makadirio haya yanaweza yasiwe na tija. Kamati ina maoni kuwa, upo umuhimu wa Serikali kuongeza mkazo katika upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kubaini matokeo ya bajeti inayojadiliwa (Fungu – 99), Kamati ilifanya mapitio ya maeneo ya vipaumbele katika bajeti ya mifugo na uvuvi. Kutokana na mapitio hayo Kamati ilibaini kuwa: -

(i) Maeneo yote ya vipaumbele yaliyobainishwa na Wizara yanaendana na mwelekeo wa nchi na mahitaji ya jamii. Hata hivyo, iwapo upatikanaji wa fedha zitakazoidhinishwa

kutokana na makadirio hayo utakuwa wa kusuasua, vipaumbele hivyo vitabaki na mwonekano unaovutia lakini usiokuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vipaumbele hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inastahili pongezi kwa nia yake njema ya kuboresha sekta hizo. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, zinapatikana kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa jumla. Maoni na ushauri katika sehemu hii vinatokana na kuzingatia vipaumbele vilivyobainishwa na Wizara kwa kulinganisha hali halisi ya sekta. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kama ifuatavyo:-

(a) Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti kwa sekta hizi na fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge itolewe kwa wakati.

(b) Kamati ina ishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa kisasa wa samaki katika vizimba ili kupata malighafi za kutosha kulisha viwanda vya samaki ndani ya nchi.

(c) Changamoto ya utoroshwaji wa mifugo na mazao ya uvuvi kwenda nje ya mipaka ya Tanzania na uingizwaji wa zana haramu za uvuvi katika maziwa makuu na bahari unachangia nchi kutonufaika ipasavyo na rasilimali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Kuimarisha doria za mara kwa mara katika vituo vyote vya mipaka, ili kudhibiti utoroshaji wa samaki; na

(ii) Kupunguza ushuru unaotozwa minadani na katika shughuli za uvuvi ambao ndiyo chanzo kikuu cha utoroshaji wa rasilimali hizo.

(d) Wingi wa tozo katika sekta za mifugo na uvuvi unakwamisha ukuaji wa maendeleo ya sekta hizo nchini na kusababisha maisha ya wafugaji na wavuvi kuendelea kuwa duni. Kamati inaishauri Serikali ifanye mapitio ya tozo hizo ili

kuziboresha na kupunguza kero kwa wafugaji na wavuvi. *(Makofi)*

(e) Kukosekana kwa Taasisi mahsusi za Usimamizi wa Utekelezaji wa Miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kamati inaishauri Serikali iharakishe kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Mamlaka ya Mifugo na Mamlaka ya Uvuvi.

(f) Kuhusiana na uhaba wa Maafisa Ugani katika sekta za mifugo na uvuvi;

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali:

(i) Kuendelea kuajiri Maafisa Ugani wa kutosha na kuwapa mafunzo ya mara kwa mara; na

(ii) Wataalamu waliopo wasambazwe katika maeneo husika ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya mifugo Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Tatizo la utoroshwaji wa mifugo kwa njia za panya limekuwa likiongezeka na kusababisha Serikali kukosa mapato, viwanda vya ndani kukosa malighafi na kupunguza ajira. Kamati inaishauri Serikali, kuweka mikakati ya kumaliza tatizo hili kwa kuweka ulinzi madhubuti katika maeneo yote ya mipaka.

(b) Uhaba wa malisho hasa kipindi cha ukame unaathiri mifugo na kusababisha wafugaji walazimike kutafuta malisho kwa kuhamahama ili kukabiliana na changamoto hiyo. Kamati inaishauri Serikali: -

(i) Ihakikishe vituo vyote vya *TALIRI* vinakuwa na mashamba ya kuzalisha chakula cha Mifugo; *(Makofi)*

(ii) Miundombinu ya mashamba ya mbegu na malisho iboreshwe ili kuongeza tija katika uzalishaji. Aidha, barabara

zinazofika kwenye mashamba ya mbegu na malisho ziboreshwe, ili ziweze kupitika wakati wote;

(iii) Serikali ijenge miundombinu ya umwagiliaji; na

(iv) Serikali ianzishe na kuimarisha mashamba ya malisho katika maeneo ya wafugaji na mashamba yaliyotelekezwa yafufuliwe. *(Makofi)*

(c) Changamoto ya magonjwa ya mifugo yanayotokana na kukosekana kwa mfumo rasmi wa chanjo, imeathiri biashara ya mifugo ya mazao yake. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya chanjo, ili kuongeza ubora wa mifugo na mazao yake.

(d) Utitiri wa tozo, kodi na ushuru unaweza kuleta changamoto za kibiashara na hivyo kuathiri biashara za mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya uvuvi; katika sekta ya uvuvi Kamati inashauri mambo yafuatavyo:-

(a) Wingi wa magugu maji ndani ya maziwa mengi nchini likiwemo Ziwa Victoria licha ya kukwamisha shughuli za usafirishaji wa abiria, pia huzuia shughuli za uvuvi, na hupunguza upatikanaji wa samaki. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati wa haraka wa kumaliza tatizo hili ambalo linachangia uhaba wa samaki. *(Makofi)*

(b) Sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu yanapotea kutokana na ukosefu wa nyenzo za uvuvi katika eneo hilo. Aidha, uwepo wa meli za kigeni zinazovua kunapelekea nchi kukosa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inashauri kwamba: -

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kununua meli nne za uvuvi na mbili za doria ili zisaidie kufanya uvuvi na doria kwenye eneo hilo;

(ii) Ufanyike ukaguzi wa mara kwa mara kwa meli za kigeni zinazovua katika eneo la Bahari Kuu;

(iii) Uhaba wa samaki katika bahari, maziwa, mabwawa na mito unasababishwa kwa kiasi kikubwa na uvuvi haramu ambao unaathiri mazalia na biashara ya samaki nchini. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali iwahamasishe wadau wa sekta binafsi ili waweze kushiriki katika udhibiti wa uvuvi haramu, na kwa maana hiyo kusaidia katika kuokoa tatizo hilo.

(iv) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa *(post-harvest losses),* unaokadiriwa kufikia 30% hadi 40% hususan katika maeneo ya vijijini, umesababisha sekta hii kutochangia ipasavyo katika pato la Taifa tofauti na ukubwa wake. Kamati inaishauri Serikali kujenga masoko katika mialo yote nchini ili kutoa fursa kwa wafugaji samaki kuhifadhi na kuuza mazao yao kwa viwango vya ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa vifaranga bora na vyakula vya samaki vyenye ubora, vinachangia udumavu wa samaki wanaofugwa. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha vituo vya kuzalisha, kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye uzalishaji wa vifaranga. Aidha, ubora wa vifaranga unatakiwa kuhifadhiwa katika maeneo ambayo yamezingatiwa na Serikali.

(v) Nyavu aina ya makila *(Gillnets)* maarufu kama Filimayaa zinazotumiwa katika Ziwa Tanganyika, husababisha samaki na dagaa kuoza katika muda mfupi. Kamati inaishauri Serikali ifanye ukaguzi wa mara kwa mara katika viwanda vya ndani pamoja na kuhakikisha inafanya ukaguzi wa kina kuhusu nyavu zinazoingizwa kutoka nje ya nchi; na mwisho itoe elimu kwa wavuvi wote katika maeneo ya Ziwa Victoria na maeneo mengine, pamoja na Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa niaba ya Kamati ninapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona umuhimu wa sekta ya mifugo na uvuvi. Kwa kipindi kifupi cha uongozi wake tumeshuhudia kiasi

kikubwa cha ongezeko la Bajeti ya Wizara hii kwa lengo la kuongeza tija katika sekta hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru na kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Kutokana na umuhimu wao, ninatamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao, lakini kwa kuzingatia ufinyu wa muda, ninaomba majina yao yaingizwe katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge; na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Mbunge Alexander Mnyeti, Mbunge, kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Prof. Riziki Shemdoe, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kuhakikisha sekta za mifugo na uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kuwashukuru sana Wapigakura wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha uwakilishi wangu. Aidha, ninawaahidi na kuwahakikishia kuwa nitaendelea kuwa mtumishi mwema kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaishukuru familia yangu kipekee kabisa ikiongozwa na mke wangu kipenzi Vaileth Medard Matogolo Chananja Kalumbete Kalemani, kwa upendo, ukarimu

na uvumilivu alionionesha kwa kipindi chote katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

#### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu Msingi wa Uchambuzi, Muundo wa taarifa na njia zilizotumika kutekeleza jukumu la kushughulikia bajeti hii;

(ii) Sehemu ya Pili inatoa maelezo kamili kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri kutokana na uchambuzi na kuhitimisha maudhui ya Taarifa hii.

**1.2 Msingi wa Uchambuzi na Uwasilishaji wa Taarifa Hii**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6(1)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka masharti yaliyoitaka Kamati kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, yaliitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka fedha 2024/2025 ili kulinganisha na Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Kamati za Kisekta kuchambua Taarifa za Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, shughuli ya Bunge kujadili hoja hii leo imestahili kutanguliwa na uchambuzi kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi na Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa inagusa maeneo yafuatayo: -

(i) Hali ya jumla ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
(ii) Tathmini ya jumla ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;
(iii) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;
(iv) Tathmini ya Ukusanyaji wa maduhuli; na
(v) Upatikanaji wa fedha kutoka hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) iliyotaka matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti yatumike kufanya ulinganisho na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2025/2026. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo uliiwezesha Kamati kupata masuala ya kuzingatia kuhusu hoja inayojadiliwa leo.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 27 na 28 Machi, 2025 Kamati ilikutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika maelezo hayo Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu

ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa majukumu, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

### *2.2.1 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, **Fungu 99** ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 69,105,000,000**. Hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 42,657,490,976.16** sawa na **asilimia 62** ya lengo la makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua maduhuli hayo ili kujiridhisha na juhudi za ukusanyaji wa maduhuli. Matokeo ya uchambuzi yanaonekana katika **Kielelezo Na. 1**.

Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli 2024/2025

| **Fungu** | **Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2024/2025** | **Makusanyo ya Maduhuli hadi Kufikia Februari, 2025** | **Asilimia ya Makusanyo** |
|---|---|---|---|
| **Fungu 99** - Sekta ya Mifugo na Uvuvi | 69,105,000,000.00 | 42,657,490,976.16 | 62 |

***Chanzo:*** *Randama Fungu 99*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(i) Jumla ya makusanyo ya maduhuli hadi kufikia Februari, 2024 yamefikia **asilimia 62** ya lengo la kukusanya shilingi **69,105,000,000.00;**

(ii) Sekta ya Mifugo imekusanya **shilingi 22,746,263,749.28** sawa na **asilimia 63** ya lengo la makusanyo; na

(iii) Sekta ya Uvuvi imekusanya **shilingi 19,911,227,226.88** sawa na asilimia **60.3** ya lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya ukusanyaji wa maduhuli inaonesha kuwa jitihada zaidi za ukusanyaji mapato zinahitajika ili kufikia lengo lililowekwa la ukusanyaji wa maduhuli.

**2.2.2 Mwenendo na Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilitengewa kiasi cha **Shilingi 363,118,170,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **Shilingi 242,078,803,000.00**; na Fedha za Nje ni **Shilingi 121,039,367,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025, Wizara ilipokea **asilimia 18.07** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. **(Kielelezo Na. 2).**

Kielelezo Na. 2: Mwenendo na mtririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2024/2025

| **MTIRIRIKO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO HADI FEBRUARI, 2025** | | | |
|---|---|---|---|
| **MIRADI** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2024/2025** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2025** | **Asilimia ya Fedha zilizopokelewa** |
| Fedha za Ndani | 242,078,803,000.00 | 65,641,025,571.57 | 27 |
| Fedha za Nje | 121,039,367,000.00 | 1,480,000,000.00 | 1.2 |
| **Jumla** | **363,118,170,000.00** | **65,641,025,571.57** | **18.07** |

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, ni wazi kuwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa na Serikali kupitia Wizara hii haiwezi kufikiwa. Hali hii inaweza kusababisha Sekta ya Mifugo na Uvuvi kutochangia ipasavyo katika Pato la Taifa, hivyo, kutoshiriki katika malengo ya Serikali ya kukuza ajira na kupunguza umasikini miongoni wa Watanzania kupitia Sekta hizi. Vile vile, ucheleweshaji wa miradi unasababisha ongezeko la gharama hivyo kuongeza mzigo kwa

Serikali ya kukamilisha miradi kwa gharama kubwa tofauti na ilivyokusudiwa.

**2.2.3 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa miwili (2) ya Geita na Dodoma na kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Miradi hiyo ni: -

(i) Mradi wa Ujenzi wa soko la Samaki - Mwalo wa Chato Beach (**Mradi Na. 4486**);

(ii) Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Malisho ya Mifugo Mpwapwa, Dodoma. (**Mradi Na. 4486**); na

(iii) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mtumba, Dodoma (**Mradi Na. 4486);**

**2.2.4 Mradi wa Ujenzi wa soko la Samaki - Mwalo wa Chato Beach (Mradi Na. 4486);**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa soko la Samaki - Mwalo wa Chato Beach ulioko Mkoani Geita (**Mradi Na. 4486**), una thamani ya **Shilingi 1,763,876,493.** Mradi huu unalenga Kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kutoka asilimia 50 hadi 10, kuongeza fursa za ajira, kuongeza kipato kwa wananchi wa Chato na Taifa kwa ujumla pamoja na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi. Aidha, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 91** na unategemewa kukamilika tarehe 30 Julai, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huu, Kamati inashauri kuwa, eneo lote la mradi lijengewe uzio ili kudhibiti wizi na uharibifu. Pia Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri wahakikishe mradi huu unalindwa na kutumika ipasavyo ili kuleta tija iliyokusudiwa.

**2.2.5 Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Malisho ya Mifugo Mpwapwa, Dodoma (Mradi Na. 4486).**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ambao umekamilika kwa asilimia 100 na umeanza kutumika ulitengewa jumla ya **Shilingi 219,717,404.20.**

**Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji huu ni muhimu kwa kuwa utaimarisha upatikanaji wa malisho kwa wafugaji hasa katika kipindi cha kiangazi. Pia utachangia katika kuleta tija ya uzalishaji wa mifugo na mazao yake pamoja na kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

**2.2.6 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mtumba, Dodoma (Mradi Na. 4486);**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huo una gharama ya jumla ya **shilingi 24,982,137,132.45** ambapo kati ya fedha hizo, **shilingi 23,239,197,332.51** ni gharama ya Mkandarasi na **shilingi 1,742,939,799.94** ni gharama ya Mshauri elekezi. Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 93**. Hadi sasa Mkandarasi amelipwa **shilingi 18,149,165,703.84** sawa na **asilimia 78.1** ya gharama kwa mujibu wa Mkataba wa ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huu, kwani ukikamilika utaboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wadau.

**Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo umebainisha mambo yafuatayo:-**

(a) **Mradi wa Ujenzi wa soko la Samaki - Mwalo wa Chato Beach (Mradi Na. 4486);**

(i) Eneo lote la mradi halina uzio hali inayoweza kupelekea uharibifu wa miundombinu pamoja na wizi wa bidhaa;

(ii) Mradi huu ni muhimu katika kuimarisha Sekta ya Uvuvi hasa kupunguza uharibifu wa mazao ya Uvuvi baada ya kuvuliwa kutoka asilimia 50 hadi 10 na kuhamasisha shughuli za uvuvi katika eneo la Wilaya ya Chato;

(iii) Mradi utaongeza fursa za ajira, kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla pia utasaidia kukuza biashara ya mazao ya uvuvi; na

(iv) Mradi utasaidia kutoa fursa kwa wafugaji samaki kuhifadhi na kuuza mazao yao katika viwango vya ubora na usalama na kuhakikisha uwepo wa soko la uhakika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa ni dhahiri lengo la Mradi ni kuimarisha Sekta ya Uvuvi na kukuza biashara ya Mazao ya Uvuvi nchini, hali itakayopelekea kuinua Maisha ya wavuvi na kukuza Pato la Taifa. Kamati ina maoni kwamba, fedha za ukamilishaji wa mradi huu zitolewe ili utekelezaji wake ukamilike kwa **asilimia 100**.

(b) **Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Malisho ya Mifugo Mpwapwa, Dodoma. (Mradi Na. 4486);**

(i) Shamba la Malisho ya Mifugo Mpwapwa linakabiliwa na ukosefu wa mitambo ya kuvunia majani, ikiwemo trekta na mashine ya kukatia na kufunga majani (*Moe*) hali inayokwamisha ufanisi wa uvunaji wa malisho;

(ii) Shamba linakabiliwa na hatari ya kuungua na moto kutokana na kutokuwa na uzio na vidhibiti moto;

(iii) Shamba halina miundombinu ya umwagiliaji hali inayopelekea kuzalisha chini ya kiwango kwa kutegemea mvua;

(iv) Ghala halina vichanja vya kusaidia majani yanayohifadhiwa yasilowane endapo maji yataingia ghalani; na

(v) Shamba halina Hati Miliki ya Ardhi, hali inayoweza kuibua mgogoro wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huo wa utekelezaji wa mradi huu, ni vigumu kufikia lengo la kuzalisha na kuhifadhi malisho ya mifugo ikiwa changamoto zilizojitokeza hazitatatuliwa mapema.

(c) **Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mtumba, Dodoma (Mradi Na. 4486);**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao utaleta tija kubwa kwa watumishi watakaofanya shughuli zao katika ofisi hizo. Kwa sasa Watumishi hao wametawanyika katika maeneo tofauti tofauti hali inayochelewesha na kukwamisha kufanya kazi kwa ufanisi. Aidha, mradi huu utanufaisha wadau watakaopata huduma mbalimbali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kupata huduma katika jengo moja;

**2.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Mifugo na Uvuvi **(Fungu 99)** ilitengewa jumla ya **Shilingi 97,215,432,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **363,118,170,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kama ilivyofafanuliwa kwenye **Kielelezo Na. 3**.

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2025**

| **UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO FUNGU (99) HADI FEBRUARI, 2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maelezo** | | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2024/2025** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2025** | **Asilimia ya Fedha zilizopokelewa** |
| **Matumizi ya Kawaida** | Mishahara | 44,847,492,000 | 25,511,132,878.93 | *56.88* |
| | (OC) | 52,367,940,000 | 14,815,033,447.57 | 28.29 |
| ***Jumla Ndogo*** | | 97,215,432,000 | 40,326,166,326.5 | 41.48 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maendeleo** | *Fedha za ndani* | 242,078,803,000 | 65,641,025,571.57 | 27 |
| | *Fedha za nje* | 121,039,367,000 | 1,480,000,000.00 | 1.2 |
| **Jumla Ndogo** | | **363,118,170,000** | **65,641,025,571.57** | **18.07** |
| **JUMLA KUU** | | **460,333,602,000** | **105,967,191,898.07** | **23.2** |

***Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Fungu 99***

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:-

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilipokea **asilimia 23.2** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha, kwa Wizara hii yenye Sekta mbili yaani Sekta ya Mifugo na Uvuvi haitarajiwi kukamilisha majukumu yake yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, pamoja na kuwa mwenendo wa jumla unaonesha hali ngumu ya upatikanaji wa fedha, Sekta ya **Mifugo** imekabiliwa na hali ngumu zaidi ikilinganishwa na Sekta ya **Uvuvi**.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo inadhoofisha mchango wa Sekta hizo katika Uchumi wa Taifa. Vile vile inaathiri ustawi wa watu ambao shughuli zao za uchumi zinategemea Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kamati ina maoni kuwa ni vema Serikali ihakikishe kuwa fedha zilizobaki kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Sekta hizo zinapatikana kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri, fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa.

### 2.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya Ushauri ambao utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inashauri SERIKALI kuendelea kutekeleza na kukamilisha ushauri unaotolewa na Kamati.

### 2.5 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Mifugo na Uvuvi - **Fungu 99** imekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 kama ifuatavyo: -

#### *2.5.1 Makadirio ya Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa Makadirio ya Maduhuli yaliyopangwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi - **Fungu 99.** Ili kujenga msingi wa maoni na ushauri kuhusu Maduhuli. Kamati ilichambua maduhuli hayo kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara hii yameongezeka kwa **asilimia 7.24** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025; na

(ii) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kufikia **asilimia 54.5** huku muda halisi wa utekelezaji wa bajeti ukiwa umefikia **asilimia 66**, ni vigumu kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kawaida makadirio ya jumla ya bajeti ya nchi, huzingatia makadirio ya makusanyo kwa Sekta moja moja. Uwekaji wa lengo la makusanyo usiozingatia uhalisia unaweza kuathiri uhalisia wa bajeti ya matumizi. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kuwa, ni vizuri kila Sekta inapokadiria ukusanyaji wa maduhuli izingatie uhalisia.

### *2.5.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida*

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha majukumu ya Wizara, makadirio ya Bajeti kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni jambo muhimu. Hivyo, Kamati ilichambua makadirio ya Matumizi ya **Fungu 99** – Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Matokeo ya uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio yameongezeka kwa **asilimia 3.26** ukilinganisha na mwaka unaoisha; na

(ii) Kutokana na uzoefu wa upatikanaji wa fedha wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaokwisha, kiasi cha fedha kinachokadiriwa kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 kinaweza kisipatikane kama inavyoombwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 aya ya 40 (uk 48 Mifugo) na aya ya 43 (uk54 Uvuvi) imeeleza kuwa bajeti ya Wizara hii inapaswa kuendelea kuongezwa kwa kuwa, Ilani ilitambua umuhimu wa kuongeza tija katika ufugaji wa kisasa na uvuvi kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha tofauti na matarajio hayo ya Ilani. Ni maoni ya Kamati kuwa, Sekta ya Mifugo na Uvuvi zinapaswa kupewa kipaumbele katika bajeti kwa kutoa fedha zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

### 2.5.3 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, uendelezaji wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa kiasi kikubwa unategemea bajeti inayopangwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo chini ya sekta hizo. Kwa madhumuni ya kupata

mwelekeo katika Sekta hizo, Kamati ilichambua makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo na kubaini mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yameongezeka kwa **asilimia 1.67** ikilinganishwa na mwaka 2024/2025;

(ii) Utegemezi wa vyanzo vya nje kwa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii umeongezeka kwa **asilimia 15.5** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha unaoisha **asilimia 33** ya bajeti ya maendeleo ilikuwa ni fedha za nje ikilinganishwa na **asilimia 38** kwa mwaka 2025/2026;

(iii) Pamoja na bajeti ya fedha za miradi kutoka nje kuongezeka kwa **asilimia 21.57** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ongezeko hilo haliendani na uhalisia uliojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha wa 2024/2025. Sekta ya Mifugo na Uvuvi ilipokea **asilimia 1.2** tu ya makadirio ya fedha za nje kwa mwaka huo; na

(iv) Uzoefu wa jumla wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kuwa, katika kipindi cha utekelezaji cha **asilimia 66,** Wizara ilipata fedha za maendeleo kwa **asilimia 18.48** tu ya makadirio. Hali hiyo inaashiria kuwa ongezeko la bajeti kwa **asilimia 3.26** linaweza lisiwe na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yana sura ya kuongeza ufanisi katika Sekta hizo. Hata hivyo, iwapo changamoto za upatikanaji wa fedha zilizojitokeza katika mwaka wa fedha ulioisha hazitapatiwa ufumbuzi, makadirio haya yanaweza yasiwe na tija. Kamati ina maoni kuwa, upo umuhimu wa Serikali kuongeza mkazo katika upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Sekta hizi.

**2.5.4 Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** ili kubaini matokeo ya bajeti inayojadiliwa Fungu 99, Kamati ilifanya mapitio ya maeneo ya vipaumbele katika bajeti ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na mapitio hayo Kamati ilibaini kuwa:-

(i) Maeneo yote ya vipaumbele yaliyobainishwa na Wizara yanaendana na mwelekeo wa nchi na mahitaji ya jamii;

(ii) Iwapo vipaumbele hivyo vitazingatiwa ipasavyo, Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi zitaongeza mchango katika Uchumi wa Taifa, kuchochea maendeleo ya nchi na kukuza ustawi wa watu nchini; na

(iii) Iwapo upatikanaji wa fedha zitakazoidhinishwa kutokana na makadirio hayo utakuwa wa kusuasua, vipaumbele hivyo vitabaki na mwonekano unaovutia lakini usiokuwa na tija.

**Mheshimiwa Spika**, kwa vipaumbele hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inastahili pongezi kwa nia yake njema ya kuboresha Sekta hizo. Aidha, Serikali kwa ujumla wake inahitaji kuzingatia umuhimu wa vipaumbele hivyo ili kuboresha zaidi Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa lengo la kuongeza mchango wake katika Uchumi wa nchi. Kwa msingi huo, Kamati inasisitiza kusimamia hali ya upatikanaji wa fedha zinazoombwa wakati wa utekelezaji wa miradi ili kuongeza mchango wa Sekta hizo katika pato la Taifa.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**3.1 Ufafanuzi wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kuliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa manufaa ya Taifa letu. Ili kufanikisha lengo hilo, Kamati imezingatia matokeo ya uchambuzi na tathmini na kutoa maoni na ushauri kwa namna mbili; ya

kwanza ni maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali na ya pili ni maoni na ushauri kwa kila Sekta.

**3.2 Maoni na Ushauri wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, maoni na ushauri katika sehemu hii, unatokana na kuzingatia vipaumbele vilivyobainishwa na Wizara kwa kulinganisha hali halisi ya Sekta. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kama ifuatavyo:-

(a) Ufinyu wa Bajeti na upatikanaji hafifu wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kunapelekea Sekta za Mifugo na Uvuvi kushindwa kutekeleza miradi kwa ufanisi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti kwa Sekta hizi, na fedha yote inayoidhinishwa na Bunge itolewe kwa wakati.

(b) Uhaba wa malighafi katika viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya mifugo na uvuvi kunasababisha viwanda vingi kufanyakazi kwa kusuasua na vingine kufungwa na hivyo kuathiri fursa za ajira na kutochangia katika Pato la Taifa. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa kisasa wa Samaki katika vizimba ili kupata malighafi za kutosha kulisha viwanda vya samaki.

(c) Changamoto ya utoroshwaji wa mifugo na mazao ya uvuvi kwenda nje ya mipaka ya Tanzania na uingizwaji wa zana haramu za uvuvi katika Maziwa Makuu na Bahari, unachangia nchi kutonufaika ipasavyo na rasilimali hizo. Kamati inaishauri Serikali:-

   (i) Kuimarisha doria za mara kwa mara katika vituo vyote vya mipakani ili kudhibiti utoroshwaji na uingizwaji wa mifugo, mazao ya mifugo na Uvuvi, bila kulipia tozo; na

   (ii) Kupunguza ushuru unaotozwa minadani na katika shughuli za uvuvi ambao ndio chanzo kikuu cha utoroshwaji wa rasilimali hizo.

(d) Wingi wa Tozo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi unakwamisha ukuaji wa maendeleo ya Sekta hizo nchini na kusababisha maisha ya wafugaji na wavuvi kuendelea kuwa duni. Kamati inaishauri Serikali ifanye mapitio ya tozo hizo ili kuziboresha na kupunguza usumbufu na kero kwa Wafugaji na Wavuvi.

(e) Kukosekana kwa Taasisi mahsusi za Usimamizi wa Utekelezaji wa Miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni jambo linalochangia kuzorota kwa ufanisi wa Sekta hizo. Aidha, hali hiyo inapunguza mchango wa Sekta za Mifugo na Uvuvi katika pato la Taifa, ustawi wa watu na maendeleo kwa ujumla. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali iharakishe kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Mamlaka ya Mifugo na Mamlaka ya Uvuvi.

(f) Uhaba wa Maafisa Ugani katika Sekta za Mifugo na Uvuvi unazorotesha jitihada za wafugaji na wavuvi kujikwamua katika umaskini na kulikosesha Taifa mapato. Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Kuendelea kuajiri wataalam wakutosha ili kukidhi mahitaji ya huduma za ugani;

(ii) Kuwapa mafunzo ya mara kwa mara Maafisa ugani wa Mifugo na Uvuvi ili kuwaongezea utaalamu wa kuhudumia Sekta hizi; na

(iii) Wataalamu waliopo wasambazwe kwenye maeneo husika ya uzalishaji.

### 3.3 Maoni na Ushauri Kisekta

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutimiza jukumu lake la kuishauri Serikali, Kamati imezingatia tathmini ya jumla ya kila Sekta chini ya Wizara hii na kuilinganisha na hali halisi. Aidha, matokeo ya tathmini hiyo yanaisukuma Kamati kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

### 3.3.1 Sekta ya Mifugo

**Mheshimiwa Spika**, Katika Sekta ya Mifugo Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Tatizo la utoroshwaji wa mifugo kwa njia za panya limekuwa likiongezeka jambo ambalo linachangia:-

(i) Serikali kukosa mapato yanayotokana na biashara ya mifugo;

(ii) Viwanda vya nyama hapa nchini kukosa malighafi ya kutosha ili viweze kuchakata nyama kulingana na uwezo wa kiwanda; na

(iii) Wananchi kukosa ajira zinazotokana na mnyororo mzima wa thamani.

Kamati inaishauri Serikali, kuweka mikakati ya kumaliza tatizo hili kwa kuweka ulinzi madhubuti kwenye maeneo yote ya mipakani nchini na wanaokamatwa kwa kutorosha mifugo wachukuliwe hatua kali za kisheria.

(b) Uhaba wa malisho hasa kipindi cha ukame unaathiri mifugo na kusababisha Wafugaji walazimike kutafuta malisho kwa kuhamahama. Hali hii inachangia kupoteza ubora wa mifugo, kuongeza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na kusababisha uharibifu wa mazingira. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kwamba:-

(i) Ihakikishe vituo vyote vya TALIRI vinakuwa na mashamba ya kuzalisha chakula cha mifugo na maghala ya kuhifadhia baada ya mavuno. Aidha uzalishaji uzingatie zaidi katika kuzalisha mbegu za kutosha za malisho;

(ii) Miundombinu ya mashamba ya mbegu na malisho iboreshwe ili kuongeza tija katika uzalishaji. Aidha, barabara zinazofika kwenye mashamba ya mbegu na malisho ziboreshwe ili ziweze kupitika wakati wote;

(iii) Serikali ijenge miundombinu ya umwagiliaji, ili kuhamasisha na kuongeza uzalishaji wa malisho hasa kipindi cha kiangazi; na

(iv) Serikali iisimamie TALIRI ili ianzishe mashamba ya malisho katika Wilaya za Kifugaji. Aidha mashamba ya malisho ambayo yametelekezwa yafufuliwe.

(c) Changamoto ya magonjwa ya mifugo yanayoathiri biashara ya mifugo na mazao yake na kukosekana kwa mfumo rasmi wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo kunadidimiza sekta hii, hivyo kupelekea kutochangia ipasavyo kwenye Pato la Taifa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya chanjo ili kuongeza ubora wa mifugo na mazao yake.

(d) Utitiri wa tozo, kodi na ushuru wa mamlaka na wakala mbalimbali za Serikali na gharama nyingine za ukaguzi unaotozwa kwenye maziwa yanayochakatwa nchini unasababisha wananchi wengi kushindwa kutumia bidhaa hiyo kutokana na kuuzwa kwa bei kubwa.

Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali ipunguze utitiri wa kodi, tozo na ushuru unaotozwa kwenye bidhaa za maziwa yaliyochakatwa nchini, aidha iondoe ushuru unaotozwa kwa bidhaa za maziwa zinazopelekwa Zanzibar kutoka Tanzania Bara; na

(ii) Ili kuweka ushindani wa soko katika maziwa na bidhaa zinazotokana na maziwa nchini, Serikali ihakikishe inafanya mapitio ya kodi pamoja na kuongeza ushuru katika maziwa na bidhaa za maziwa kutoka nje ya nchi ili kuwalinda wazalishaji wa ndani.

**3.3.2 Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Uvuvi Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Wingi wa Magugu maji ndani ya Maziwa mengi nchini likiwemo Ziwa Victoria licha ya kukwamisha shughuli za usafirishaji wa abiria pia huzuia shughuli za uvuvi, na hupunguza upatikanaji wa Samaki. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati wa haraka wa kumaliza tatizo hili ambalo linachangia uhaba wa Samaki.

(b) Sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu yanapotea kutokana na ukosefu wa nyenzo za uvuvi katika eneo hilo. Aidha, uwepo wa meli za kigeni zinazovua kunapelekea nchi kukosa mapato. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Kamati inashauri kwamba:-

 (i) Serikali ikamilishe mchakato wa kununua meli nne za uvuvi na mbili za doria ili zisaidie kufanya uvuvi na doria kwenye eneo la bahari kuu na kuongeza mapato ya nchi; na

 (ii) Ufanyike ukaguzi wa mara kwa mara kwa meli za kigeni zinazovua katika eneo la bahari kuu ili kujua kiasi na aina ya samaki wanaovuliwa.

(c) Uhaba wa Samaki katika Bahari, Maziwa, Mabwawa na mito unasababishwa kwa kiasi kikubwa na Uvuvi Haramu ambao unaathiri mazalia na biashara ya Samaki nchini. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri Serikali iwahamasishe wadau na Sekta binafsi kushiriki katika udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya samaki. Aidha, wanaojihusisha na uvuvi haramu wachukuliwe hatua kali za kisheria; na

(d) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa (*Post harvest losses*), unaokadiriwa kufikia asilimia 30 hadi 40 hususan katika maeneo ya vijijini umesababisha Sekta hii kutochangia ipasavyo katika Pato la Taifa tofauti na ukubwa wake. Kamati inaishauri Serikali kujenga masoko katika mialo yote nchini, ili kutoa fursa kwa wafugaji samaki kuhifadhi na kuuza mazao yao kwa viwango vya ubora, usalama na kuhakikisha uwepo wa soko la uhakika.

(e) Mazingira magumu, wingi wa tozo na ushuru katika viwanda vya usindikaji wa mazao ya uvuvi kunaathiri mchango wa sekta katika pato la Taifa,

Kamati inashauri Serikali:-

(i) Ifanye mapitio ya tozo na kuweka mazingira mazuri ya biashara katika viwanda vya usindikaji wa mazao hayo ili kuboresha mazingira ya biashara katika sekta ya uvuvi na kuongeza mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa; na

(ii) Ihamasishe Sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya usindikaji mazao ya uvuvi katika maeneo yenye uhitaji.

(f) Uhaba wa vifaranga bora na vyakula vya samaki vyenye ubora, vinachangia udumavu wa samaki wanaofugwa. Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Kuimarisha vituo vya kuzalisha vifaranga kwa kuboresha vitotoleshi na samaki wazazi ili kuzalisha vifaranga bora na vya kutosha;

(ii) Kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye uzalishaji wa vifaranga vyenye ubora; na

(iii) Kuwekeza kwenye viwanda vya kuzalisha vyakula bora vya Samaki kwenye maeneo mengi nchini ili kuhamasisha ufugaji wa samaki.

(g) Nyavu aina ya makila (*Gillnets*) maarufu kama Filimayaa ambazo zinatumiwa katika Ziwa Tanganyika husababisha Samaki na dagaa kuoza katika muda mfupi. Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Ifanye ukaguzi wa mara kwa mara katika viwanda vinavyozalisha nyavu nchini na kuchukua hatua dhidi ya viwanda vinavyozalisha nyavu

zisizozingatia viwango na sifa katika kulinda uvuvi endelevu na ubora wa Samaki na mazao yake;

(ii) Ihakikishe inafanya ukaguzi wa mara kwa mara wa nyavu zinazotoka nje ya nchi na kuchukua hatua stahiki kabla hazijfika sokoni au kwa wavuvi; na

(iii) Itoe elimu kwa wavuvi katika Ziwa Tanganyika na maeneo mengine nchini ili kupunguza madhara ya kutumia nyavu zisizokidhi ubora.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta za mifugo na uvuvi ni sekta za uzalishaji zikichangia katika pato la Taifa, Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kutoa kipaumbele katika sekta hizi kwa kuhakikisha inaipatia fedha zote kama zilizoidhinishwa na Bunge ili Wizara hii iweze kufikia malengo yake na kuongeza mchango wa Sekta hizi katika Uchumi wa Taifa letu.

**4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao, natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao, lakini kwa kuzingatia ufinyu wa muda, naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Deodatus Phillip Mwanyika, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb, - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb
5. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb
6. Mhe. Dkt. Christine Ishengoma, Mb
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb

8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb
10. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb
17. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
18. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb
19. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
20. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
21. Mhe. Toufiq Salim Turky, Mb
22. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb
23. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb
24. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) na Naibu Waziri - Mheshimiwa Alexander Mnyeti (Mb), kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha kutekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo yake wakiongozwa na Katibu Mkuu - Prof. Riziki Shemdoe, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kuhakikisha Sekta za Mifugo na Uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha

2025/2026, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Deodatus Phillip Mwanyika
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
23 MEI, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana *Doctor* kwa taarifa yako.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye uchangiaji na nina dharura ya Wabunge wawili na wote nina taarifa zao za kiafya. Tutaanza na Mheshimiwa Aida dakika tano, na Mheshimiwa Kaboyoka dakika tano. Atakuja Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Mtinga na Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kuwepo tena kwenye Bunge lako kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitaanza na Fungu 99. Nilikuwa ninajiuliza tatizo la Wizara hii ni nini? Nikagundua kwenye suala la usimamizi siyo changamoto, isipokuwa changamoto kubwa ni fedha ndiyo maana wanashindwa kukusanya vizuri, lakini kwenye suala la makusanyo wamefanya vizuri hasa kwenye hili Fungu 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, shida kubwa ni fedha, mpaka hapa tunazungumza ni 28% ya fedha ya maendeleo ndiyo wamepata. Hakuna muujiza unaoweza kufanyika tofauti na kupewa fedha wakasimamie fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ni muhimu sana na sijajua ni kwa nini kama Bunge tunatimiza wajibu wetu wa kutenga bajeti na fedha haziendi. Tunataka mapinduzi, hakuna mapinduzi

yanaweza yakafanyika bila kupeleka fedha. Tulitaka hapa tuwalaumu Wizara kwa kutosimamia, unawalaumu wapi kama fedha hawajapewa? Jambo hili halifurahishi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamefanya operesheni kulingana na changamoto iliyopo Ziwa Tanganyika ya Uvuvi Haramu. Mmefanya operesheni ambayo mimi mngeniambia niwape jina la operesheni ile ningewaambia ni Operesheni Kata Funua. Mmefanya operesheni kubwa yenye maumivu kwa watu wengi, lakini tunaomba operesheni hiyo isiwe zimamoto, na isiishie Wilaya ya Nkasi peke yake. Fanyeni maeneo yote, ili tuone matokeo chanya ya hizo operesheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima wawe na boti ya doria. Msiwe mnafanya hivi halafu mnaondoka, lazima ziwepo boti za doria za kila siku, lakini fuatilieni mnaowapa nafasi za kusimamia, wanasimamia kikamilifu? Kama kuna shida, fanyeni mabadiliko ili tuone matokeo chanya kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni utitiri wa tozo. Hili jambo nimelizungumza mara kadhaa. Ninajua kuna tozo ambazo zinaandaliwa na halmashauri kwa maana ya sheria ndogo, lakini ni lazima ninyi Wizara ndio mna wajibu wa kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna chombo kinaitwa *ring net,* kina wavuvi mle ndani zaidi ya 14. Sasa, mwenye chombo mwenyewe anatakiwa kupata leseni ya umiliki dola 50, lakini chombo chenyewe akilipie dola 55, halafu wale wavuvi kila mmoja aliyepo mle ndani kwenye hicho chombo kimoja naye anatakiwa kulipia leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kwa mfano rahisi, ni kwamba, wewe una shamba umelima, umeita vibarua. Wewe umepata hati ya eneo lile, halafu mtu anayekuja kupalilia na yeye anatakiwa kupata leseni. Hili jambo ni la wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kukusanya, tutengeneze mazingira rafiki ya hawa wavuvi ili waweze kufanya kazi. Lazima

leo ninyi mliopewa dhamana mje mseme ni wavuvi wangapi ambao walikuwa wanafikiri kuhusu kitoweo peke yake, mmewabadilisha fikra zao na mazingira yao kuwa wavuvi wanaofikiri kuhusu uchumi unaotokana na uvuvi, waache kufikiri kuhusu kwenda kutafuta mboga, na hili jambo linawezekana. Tunaomba hapa mje mtueleze, ni tozo zipi ambazo tunafikiri hazina sababu ziondolewe ili kutoa kero hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, huyu mvuvi mwenyewe anapokwenda wale wanavua siku 15 tu kwa mwezi. Kila siku mafuta *(petrol)* anayotumia ni lita 100 kwa siku 15. Hebu fikiria hawa wavuvi 14 wanatumia lita ngapi katika siku 15 na kule kwenye *petrol* kuna tozo wanalipa. Kwa hiyo, wanalipa kodi. Kwa nini wanalipa fedha zote hizo? Walipie nyavu, chombo na kibarua wake na yeye alipie. Tunaomba Wizara mje na jambo zuri kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tumesema hapa lazima tuwaambie wavuvi wetu waanze kuvua kisasa. Hivyo, vizimba mlivyotuambia toka mwaka 2024 vipo wapi? Mkija hapa mtueleze mmetupatia vizimba vingapi na mmezalisha samaki wangapi? Kwa sababu hamwezi kwenda kukusanya eneo ambalo hamjaenda kuwekeza, wote mnajua samaki wamepungua. Hakuna muujiza zaidi ya ninyi kuanza kufikiri upya kwenye uvuvi wa kisasa, ili tuweze kuwainua wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkija hapa mtuambie katika yale mliyoeleza mwaka 2024, mmetekeleza kwa kiasi gani kupeleka hivyo vizimba ili tuweze kujua leseni wanazolipa wananchi na wavuvi wetu hatuwaibii, ila tunataka walipe leseni za haki. Hawakati leseni kwa ajili ya kuuza mandazi, ni kwa ajili ya uvuvi. Sasa kama wanaenda kule hawavui, mnawakamata, sasa hawa watu wafanye nini jamani? Hakuna haki bila wajibu. Walipe leseni na nyie tengenezeni mazingira rafiki ya wao kuweza kuvua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwishoni tu, moja la mwisho. Jambo la mwisho ninyi mnajua kwamba Wizara ya Maji inachimba visima, Wizara ya Kilimo inachimba mabwawa, unganeni mwapatie wavuvi pale waweze kuweka samaki wazalishe. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ulivyoniambia unaumwa na ninajua unaumwa, sikutegemea ungekuwa na sauti kali kama hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika: -

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi; Ndugu Novitus Yanga, Mkurugenzi Mtendaji Programu ya Watu na Wanyamapori Tanzania; Ndugu Rashid Nassoro, Mkurugenzi Mkuu *Farmbase;* na Ndugu Jeremiah Temu, Kaimu Mkurugenzi Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo Tanzania, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni wengine wa Dkt. Kijaji, Waziri wa Mifugo: Mashirika ya Kimataifa *(International Organisations), welcome. (Makofi)*

Wadau kutoka Taasisi ya Kifedha *NMB, CRDB* na *TADB;* karibuni. Viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania *(CWT)* Wilaya ya Kondoa karibuni. Wafugaji kutoka Chama cha Wafugaji; Wazalishaji na Wasambazaji wa Chanjo za Mifugo, karibu. *(Makofi)*

Wasindikaji wa Mazao ya Mifugo ya Uvuvi; Wadau wa Uvuvi na Wakuzaji wa Viumbe Maji; Vijana wa Jenga Kesho Bora *(BBT)* wa Mifugo na Uvuvi; Wazalishaji wa Kuku; Vyama vya Wadau wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, karibuni. *(Makofi)*

Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Kondoa; Viongozi wa Chama cha Wanawake Wilaya ya Kondoa; Wanawake wa Kiislamu kutoka Taasisi ya *Ladies in Islam Tanzania* wakiongozwa na Ndugu Bibie Salum; Watumishi kutoka Ofisi ya

Mbunge; na Ndugu wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu kutoka Wilaya ya Kondoa. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Merdad Matogolo Kalemani, Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, kutoka Chato Mkoa wa Geita, karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kaboyoka dakika tano. Jiandae Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Mtinga na Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Ninaona mwenzangu, Mheshimiwa Aida amechangia sehemu kubwa, kwa hiyo, nitachangia sehemu chache. Kwanza nimpongeze Dkt. Ashatu Kijaji na Maafisa wake wote kwa taarifa ambayo imesheheni karibu sehemu zote muhimu ambazo tungependa tuzisikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninafikiri muhimu nimtaje Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba amekuwa Rais ambaye ana maono makubwa ambaye anataka nchi yetu ipate maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo niseme kwamba kitu kinachotakiwa sasa ni hao wote aliochagua ama aliowapatia nafasi hizi wafanye kazi zao kwa ubunifu mzuri, ili walete tija ile inayotakiwa. Ninaamini Mheshimiwa Dkt. Kijaji atafanya kazi hiyo pamoja na watumishi wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nizungumzie tu sehemu mbili ambazo ninaona kwamba, zinahitaji kuangaliwa kwa undani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora *(quality)* wa nyama yetu Tanzania bado ni hafifu sana. Unakuta unanunua nyama buchani ambapo ndipo watu wengi tunanunua huko, kwa kweli utachukua masaa kuichemsha ambayo ninaamini kwamba pia hata kwenye ulaji wake haina ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pia utunzaji wa ngozi sijaona hapa labda sijasoma vizuri. Utunzaji wa ngozi bado ni hafifu sana kiasi kwamba katika ngozi hii tungeweza kupata fedha za kigeni nyingi ambazo zingeweza kutusaidia kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba ninaamini tuna Maafisa ya Mifugo wengi, lakini ninafikiri elimu yao ile ya shule haijawapatia *exposure* nzuri ya kujua jinsi ya kutumikia wananchi na kuhakikisha kwamba tunakuwa na nyama na ngozi bora na *products* zote nzuri za wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri basi, kwa wenzetu kama Botswana ambao unakuta kwamba wana ng'ombe 2,500,000 tu au mpaka 2,800,000 lakini nyama yao inasifiwa kwa ubora na ladha nzuri, ndiyo maana wana-*export* kupeleka huko *Europe, EU* na *South Africa. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiangalia sisi kwa ng'ombe wetu tulionao, lakini utaona ng'ombe wengi wamechoka na wamekondeana sana kiasi kwamba tuki-*boast* kwamba tuna ng'ombe wengi kwa kweli tunajidanganya maana *quality* yake ni *very poor. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niseme kwamba, wanyama wengi wanaachwa wanazagaa mijini. Hata hapa ukipita Kisasa kwetu tunapoishi, ng'ombe wanapita kwenye *streets.* Sasa, unaona Wizara yetu yote hii kweli wao hawaoni kwamba hawa ng'ombe wanakuwa ni ghasia kwa wananchi? Halafu kama tuna-*boast* kwamba nchi yetu ina uchumi wa kati, ingawa ni wa chini, lakini hatuendani na hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inatakiwa tuone kwamba hivi hata miji yetu tunaiwekaje? Kwa nini uruhusu ng'ombe wawe wanazagaa kila mahali? Kwa nini hatu-*control* kwamba mfugaji yeyote aweze kutunza ng'ombe wake kwa kiasi anachoweza wasionekane wakikata mitaa? Tunapishana na ng'ombe utafikiri tuko huko vijijini. Ninaomba hili liangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema pia *exposure* za wafanyakazi wetu ni muhimu sana. Afadhali tuwe na wafanyakazi wachache, lakini wenye kujua *quality: quality* ni *more important* kuliko *quantity*. Yaani sisi kusifiwa kwetu kuwe kwa ubora wa vitu kuliko kwa wingi wa wanyama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niseme tu kwamba, hakika Wizara wanajitahidi sana: wanajitahidi sana. Ukiangalia wingi wa hii sekta ilivyo pana, basi kwa ajili hiyo nilifikiri bajeti yake isiwe mbali sana na bajeti ya Kilimo. Maana hasa tunataka lishe bora, na lishe bora inatoka kwenye mifugo. Kwa nini tuwe na *starch* nyingi, tule vitambi vitoke huko mbele ya matumbo yetu, halafu *quality* ya nyama ni ndogo? Hii kwa vile nyama haipatikani, tani kwa wingi, *quality* mbaya, halafu pia wananchi wengi hawawezi kuwa na *access* kwa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana, sekta hii ni muhimu na inaweza kutuletea uchumi mkubwa. Ukiangalia Sekta ya Kilimo, Ufugaji na Madini, ni sekta ambazo zingeweza kutupaisha sana. Kwa hiyo, isiwe mbali bajeti yake na Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mazungumzo)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage dakika 10, Mheshimiwa Francis Mtinga, Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Nina dakika 10 dakika tano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii, bajeti ya sekta ya kiuzalishaji. Nirudie kusema mimi ni muumini wa sekta hii na ni mdau, ni mdau. Kwa uzoefu wangu katika Kamati ambazo nimetumika, ninapenda nirudie

kusema kwamba tulipokuwa tumefika tukakubaliana bajeti inayotolewa au inayotengwa kwa Wizara hii ni ndogo sana. Taasisi ya *NARCO* tu tulikuwa tumependekeza kwa ushauri wa wataalam, tukakubaliana kwamba walipaswa kupata bilioni 400 ili *NARCO* iwe taasisi ya kufuga na iweze kusaidia watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu kuna msemo, wanasema uendelevu wa Ziwa Victoria. Uendelevu wa Ziwa Victoria unategemea Ziwa Ikimba; '*Ubhusinge Bhwa Rwelu ni Ikimba*', shangazi anaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuamua kwenda kupandikiza mbegu Ziwa Ikimba kusudi Ikimba iweze kuiambukiza Rwelu na kulifunga lile ziwa kusudi tupate samaki wa kweli. Hata hivyo, jambo la msingi, tukubali tuwe na mamlaka ya kusimamia rasilimali za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwaeleze, huwezi kutunza lile ziwa kwa *operation*, hakuna. Jifunze ninarudia kulisema ninasikitika kulisema hili, jifunze *Uganda*. Jifunze *Uganda*, ndiyo maana viwanda vya samaki viko *Uganda* haviko kwetu. Nyie mnavua mayai; mayai huwezi kuyachakata kwenye kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa samaki: ufugaji wa samaki tumezungumza katika vikao vilivyopita. Ninapongeza Serikali tumeanza, yaani hapa ndiyo tumeanza na ukiwauliza watu ambao wameshaanza wanasema *it is highly profitable*. Wanasema ukiwekeza milioni moja unapata milioni tano. Nami ni mtaalam wa biashara, Waziri wewe ni Mchumi. Hakuna *portfolio* zinaweza kulipa namna hiyo, lakini kwenye samaki *consult* wanakwambia *one to five* ndiyo *profitability*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vizimba nilivyoahidiwa, maeneo matano, maeneo tisa ya Wilaya ya Muleba hatujapata kizimba. Sina matatizo na wewe, wagawie wengine mimi utanigawia mwisho, silalamiki. Jambo ninalotaka kuwaeleza, wizara

mbadilishe, wananchi tunaowalenga kuwapa vizimba hawana uwezo wa kuandika michanganuo. Hawawezi kuandika *business plan*, hawa watu ndiyo mnawaita wavuvi haramu. Sasa huwezi kumwambia mvuvi haramu ufuge kwa vizimba, niandikie mchanganuo. Alikwenda lini shule? Ina maana unawaalika wasiohusika waje kwenye shughuli, halafu hao waliokuwepo watabaki watazamaji. Itakuwa ni mapigano ambayo hayatakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mauzo nje; sekta yoyote ya kizalishaji kwa Tanzania ni kuuza nje. Ninasikitika kuna kijana mmoja kwenye mtandao wa vijana alisema tuna ng'ombe wengi milioni 40, tunauza nje kiasi gani? Tunarudi pale pale kwamba *government* hatutoi pesa za kutosha kwa sekta hii. Hizi *opportunity* hatuja-*exploit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuwaeleza kwamba eneo la Gafu lina *potential* ya dola bilioni 10 ya nyama na Mheshimiwa Rais kupitia Diplomasia ya Uchumi amefungua masoko, ametuorodheshea lakini hamna nyama ya kupeleka. Pamoja na hiyo, hata uzalishaji wa nyama, nyama tunayozalisha haitutoshi, hatuwezi hata kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninaona mwanga unakuja kwenye ufugaji wa samaki. Mwanga unaokuja lakini bado; samaki tani unazofuga 130, bado hujafikia tani 1,500,000 za Misri. Hujafikia tani 600 za *Nigeria*. Kwa hiyo, tunataka sisi wenye *water body* kubwa tuweze kuwatangulia wale watu wanaojifunza kutoka kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba ufugaji wa samaki na ufugaji wa ng'ombe. Usimpe mtu kitalu ukamwambia akupe *business plan*, hapana. Wewe umwandikie *business plan* umpe. Hizo ndiyo *terms and condition* za kwenda kufuga au anafuga ng'ombe au anafuga wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *NARCO*; *NARCO* hasa kwetu nimshukuru Mheshimiwa Rais tulipewa eneo letu, lakini kwa *NARCO* nzima Tanzania nzima, hawa watu muwa-

*equip*. Wapeni mtaji wa kutosha, mkishawapa mtaji wa kutosha, wale waliopewa vizimba moja, waliopewa vitalu wapewe muda mrefu. Huwezi kunipa kitalu kwa miaka minne miaka mitano unaniambia nijenge Josho.

Mheshimiwa Naibu Spika, *lifespan* ya josho ni muda mrefu, huwezi kwenda benki kukopa, kung'oa visiki kwa ajili ya kulifuga pale. Hakuna! Mnachogawa *in fact* ngoja nikueleze Mheshimiwa Waziri, samahani na nyumbani isifike hii, yeye anawagawia watu misitu yenye visiki kama misitu ya Kongo unamwambia afuge, hawa ng'ombe wanakula nyasi, kwa hiyo, *we have to change*. Watu wote wanaopewa vile vitalu wafuge wasichunge, lakini kufuga kunatokana na wewe muda unaowapa waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine cha pili, Serikali lazima itusaidie kuleta mitamba. Mitamba inapatikana Namibia, inapatikana *South Africa*, inakwenda kwa bei nzuri. Serikali walete ngo'mbe watupe, hatukimbii nchi hii, kusudi sisi tuweze kufuga. Jimboni kwangu kuna mradi Wilaya ya Muleba, wa 'Kopa Ng'mbe Ulipe Maziwa', Wizara ya Kilimo na Ujasilia'. Ninaomba Mheshimiwa Waziri jasilia hiyo, ninapomwambia mimi ni mdau nimeingia gharama kwa kushirikiana na bwana Luvanda wa *SUA*, Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaleta malisho ninapanda kwa imani kwamba utaniona utaleta ng'ombe kusudi watu waweze kuzalisha maziwa tuweze kujenga *Dairy Industry* wa Mkoa wa Kagera. *Investment* inayoweza kulipa Kagera ni *Dairy Industry*, unaweza kutengeneza *Dairy Industry* Kagera. Moja, atusaide kwenye mbale aache malisho, malisho nitayashughulikia. Wale aliowapa vitalu kwenye mgogoro wetu wa Rutoro ambao alishaisha, awahimize wachunge kwenye maeneo waliyopewa, lakini siyo kuchunga tu, wafuge ili Watanzania tuweze kufaidi matunda ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za Wizara za *export* na ninampongeza kwa *BBT* ya *Kagoma Ranch*. *BBT* ya *Kagoma Ranch* nimefika nimeiona, nimeona picha zake, ndivyo

inavyopaswa kuwa. Jambo la kuchekesha au kusikitisha, ninapokuwa kwetu nimekaa Muhutwe ninaona malori yamepakia ng'ombe kutoka yatokako kule kwenye *Ranch* zetu yanapelekwa nchi jirani, siwezi kuitaja mjomba asije akanipa radhi. Tunafuga sisi tunanenepesha mjomba anakwenda kuuza kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nilizonazo, wanunuzi wanatoka kule Gafu wanaruka wanakuja pale, ng'ombe tulizofuga sisi wanakwenda kuchukua kirahisi. Ndiyo maana mauzo ya Waziri nje yanaonekana ni madogo. Yaani anachunga, yaani anazima mpira, anafunga mwingine, yeye anaambiwa *assist* yule ndiyo amefunga, anapewa *golden shoe*. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, ninaomba kuunga mkono hoja. Tuongeze bajeti katika Wizara hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga, Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Mama Kikwete wajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ya Mifugo na Uvuvi. Nitachangia tu mambo makubwa kama matatu hivi; lakini nianze tu kwa kumwomba sana Rais wangu katika suala zima la hii Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio changu ninamwomba Rais wangu atakaporejea kuja kutengeneza Wizara zake, ninaomba Wizara hii aigawanye. Aigawanye tupate Wizara mbili, Wizara ya Uvuvi na Usimamizi wa Bahari na Wizara ya Mifugo ibaki inajietegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina sababu nyingi ya kuomba haya. Hizi Sekta mbili kubwa za Uvuvi na Mifugo ni sekta zenye *potential* kubwa sana ya uchumi kwenye nchi yetu, kubwa sana, lakini hatuzitumii vizuri kwa sababu zimeungana na utekelezaji wake unakuwa mgumu kutokana na sekta zenyewe. Kwa hiyo, naamini kabisa Rais akigawanya hizi sekta mbili kuwa wizara kamili tutapata *potential* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirejea mfano wa Wizara iliyokuwa Nishati na Madini, wakati Wizara ile ilikuwa moja Nishati na Madini, madini yalikuwa yanachangia asilimia kama 3.4 kwenye pato la Taifa, lakini baada ya Wizara ya Madini kuwa wizara kamili, leo inachangia 10% kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wanaweza wakasema uendeshaji wa Wizara mbili utakuwa mkubwa. Naomba niwatoe hofu; kwa kutenganisha Wizara hizi, mapato ambayo yatapatikana yata-*compensate* kabisa zile gharama za uendeshaji kwa mbali kabisa na mapato yatakuwa ni makubwa sana, kwa sababu ufanisi utakuwa ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kumwomba Rais agawanye Uvuvi na Mifugo, mambo ya haraka kabisa ambayo yatapatikana, kwanza ni mapato. Pili, ufanisi; tatu, uwazi; na nne, uwajibikaji. Haya ni makubwa ya jumla ambayo yatapatikana kwa kugawanya Wizara hii. Kwa hiyo, ninaamini Mheshimiwa Rais huko anasikiliza Bunge na kilio hiki atakisikia kwa sababu kina faida kubwa sana kwenye pato la nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara mpya ambayo ninaiombea ya Uvuvi na Usimamizi wa Bahari, lazima niseme ili niweze kushawishi faida za wizara hii mpya. Wizara hii kwa uchache tu itaongeza usimamizi endelevu wa rasilimali za baharini na pwani na maziwa yetu. Sote tunafahamu jinsi tulivyo na ufukwe mrefu kutoka Tanga mpaka Mtwara. Sote tunafahamu jinsi tulivyo na Maziwa makubwa; Victoria, Tanganyika, Nyasa, Rukwa, lakini tuna maziwa madogo madogo lukuki yako katika nchi nzima hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa samaki vilevile unakuja kwa kasi. Kwa hivyo, kukiwa na Wizara maana yake usimamizi endelevu utakuwepo, lakini vilevile kuimarisha na kutekeleza Sera ya Uchumi wa Bluu utafanyika kwa ufanisi mkubwa. Tangu ninaingia hapa nasikia Uchumi wa Bluu, Uchumi wa Bluu, lakini sijaona ufanisi wake mkubwa. Nina hakika wizara hii ikianza haya mambo yatafanyika kwa ukubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Wizara ya Uvuvi na Usimamizi wa bahari itaongeza uwezo wa nchi kushiriki katika majadiliano ya kimataifa kuhusiana na mambo ya bahari. Ninakumbuka wakati ule marehemu Rais wetu alipokuwa Wizara ya Uvuvi, aliingia muda mfupi tu akakamata mameli kule na nini. Kwa hiyo, naamini hata majadiliano ya Kimataifa kuhusu kulinda rasilimali zetu, tukiwa na Wizara kamili haya mambo yatafanyika kwa ukubwa na kwa uwazi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuendeleza sera za utafiti. Utafiti utafanyika mkubwa sana kwenye bahari zetu na maziwa yetu na rasilimali hizi tutazitumia vizuri sana kama wizara itakuwepo ambayo itakuwa inasimamia mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora pia utapatikana na utekelezaji wa karibu. Haya mambo ya uvuvi haramu sijui nini, kuna watumishi wanahusika huko na manyavu. Sasa ikiwa wizara iko yenyewe huu utawala bora utapatikana kwa uhakika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa mifugo sasa, kwa kitendo cha kuondolewa uvuvi maana yake yenyewe pia itapanuka zaidi. Mifugo kuna sekta kubwa hapa kama tatu hivi. Kuna Sekta ya Nyama ni kubwa, kuna Sekta ya Maziwa ni kubwa, kuna Sekta ya Ngozi ni kubwa. Sekta hizi tatu peke yake zinafanya vibaya, hazichangii chochote kwenye nchi yetu, lakini zenyewe tu hizi zingesimamiwa zingeleta fedha nyingi sana za kigeni na ajira nyingi kwa nchi yetu. Hata hivyo, hazipati nafasi ya kutosha kwa sababu zimebebwa kwenye wizara kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Liuvuvi lenyewe likubwa, bado mifugo yenyewe ni mingi; nchi ya pili sijui Afrika. Ametoka kuongea hapa kaka yangu Mheshimiwa Mwijage kwamba inasemekana ni nchi ya pili, lakini hakuna kinachofanyika kwa sababu imebeba mzigo mkubwa. Kwa hiyo, kitendo cha kuondoa uvuvi ikabaki mifugo peke yake, hizi sekta kubwa hizi, mifugo yenyewe na hizi sekta nilizozitaja hapa zitafanyika kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa sana ambalo halijafanyika linalosababisha hata hizi sekta tatu zisifanye vizuri ni suala zima la chanjo ya mifugo. Chanjo ya mifugo kwa muda mrefu ilikuwa ikihusisha wafugaji wenyewe wahangaike na chanjo. Ningeomba sana Serikali yangu, chanjo ya mifugo ifanyike na Serikali tena bure. Kama ambavyo tunavyochanja watoto katika nchi yetu, mifugo ikichanjwa bure tena kwa usimamizi wa karibu wa Wizara ya Mifugo, tija kubwa itapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema mchangiaji aliyepita, hatuuzi nyama nje, lakini sababu kubwa ni chanjo. Ukitaka kupeleka nyama wanakwambia wewe umechanja vipi. Wakitaka ku-*track* jinsi ulivyochanja huwezi hata ku-*track* kwa sababu hakuna hata usimamizi unaoeleweka. Kwa hiyo, niiombe Serikali, nimwombe Rais wangu Mama wa Ruzuku, hebu aangalie hili suala la chanjo ya mifugo lifanyike bure kwa usimamizi wa Wizara ya Mifugo. Ili tuweze ku-*track* vizuri wafugaji wetu wamefugaje wamechanja vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kubwa ifanyike kwa sababu wafugaji wetu wanachanja mifugo iliyougua, matokeo yake akimwongezea dozi, maana yake anajua kuchanja ni kuweka vimelea vya ugonjwa unaohusika kwa mnyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mnyama mwenyewe tayari anaumwa, halafu ukimwongezea na vimelea wanakufa. Ni kwa sababu elimu ni ndogo, wizara imelemewa katika kutoa elimu, matokeo yake mtu anachanja kitu kinachoumwa. Kwa hiyo, niombe sana, wizara hii ikibaki yenyewe haya mambo yatafanyika kwa ukubwa na kwa usahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimshukuru Rais wangu pia katika suala zima la *BBT* ya Mifugo. Mheshimiwa Rais ametoa vizimba kupitia wizara hii, vizimba kwa vijana. Nitatolea mfano vijana wa Mwanza; walipewa vizimba wakakopeshwa. Wakasimamia kila kitu, kuanzia vizimba vyenyewe, vifaranga, chakula, uvunaji, mpaka kuuza. Wameuza wamepata faida kubwa na wamerejesha mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninataka niwaone kwa kufuata hii *pilot* niombe sasa wizara na hasa itakapoanzishwa hiyo ya mifugo ambayo nimeomba, maana yake kwa sababu tuna *water bodies* nyingi, maziwa makubwa mengi na bahari ni kubwa, hii *pilot* ambayo imefanikiwa sana sasa iende kwa nchi nzima kwa ukubwa wake. Vijana wengi watapata ajira na fedha ya mikopo itarejeshwa na nchi yetu itapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nchi inatusogelea sisi atika haya mambo. Kuanzia hiyo mifugo, samaki zenyewe na kila kitu, tunachokosa ni usimamizi tu. Kwa hiyo, ninaendelea kusisitiza kwamba kama Wizara hii itaanza na hii *Pilot Project* ambayo imefanyika Mwanza ikaenda kwenye maziwa yote na kwenye maeneo yote, nina hakika vijana wa nchi hii watapata ajira na fedha nyingi zitaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema mchangiaji yule wa kwanza pale muda ukamwishia. Wizara yetu ya kilimo inachimba mabwawa ya kutosha sana ya umwagiliaji, tena makubwa. Niko Kamati ya Kilimo, tumezunguka na tumeyaona. Ukienda bwawa ukiliangalia unaona kabisa hapa kuna uchumi, lakini bado hakujawa na *connection* nzuri kati ya mifugo, kwa maana ya uvuvi na kilimo. Kwa sababu watu wa kilimo shida yao ni kumwagilia, hawana habari ya shida nyingine. Lakini sasa wakiingia hapo Wizara ya Uvuvi, maana yake wao sasa shida yao ni kuyatumia yale maji kuweza kupata samaki, lakini kupata uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, halmashauri zetu zitasimamia vijana, zile 10% badala ya kuwapa fedha watawanunulia vizimba, watawawekea kwenye haya mabwawa, watawapatia chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana yake ni kwamba halmashauri zenyewe zitaingiza mapato, vijana watapata ajira, uchumi wa nchi utaongezeka na matumizi makubwa ya mamilioni ya pesa tuliyotumia kwenye Wizara ya Kilimo kuweka haya mabwawa yatakuwa yamefanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe sana Rais wangu hili alibebe. Anayo timu nzuri ya watu wa kushika hizi wizara, hakika akiyachukua haya uchumi wetu utakwenda vijana wetu watapata ajira.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mtinga umetoa ushauri Wizara hizi mbili zitenganishwe kutokana na umuhimu au kufanya kazi vizuri na kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Mawaziri hawa wawili nilitegemea ungesema basi mmoja aende huku mwingine aende kule, lakini hukusema. Basi tutaacha mamlaka itaamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Mama Kikwete ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri yeye na Naibu wake na timu yake nzima kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na wanaendelea kuifanya. Ninawapongeza kwa taarifa yao nzuri ambayo wameitoa. Nami nitajielekeza kwenye maeneo makubwa matatu ambayo yametajwa kwenye vipaumbele vya hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kuongeza uzalishaji, kuhamasisha uwekezaji na kuimarisha utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau niende kwenye mifugo nimeona kusudio la Wizara la kurejesha hereni. Tuliwahi kujadili jambo hili kwenye Bunge hili na tukaelekeza Wizara ikafanye utafiti wa kutosha ili kuona namna ambavyo linaweza likasimamiwa na hasa kwenye gharama za heleni zenyewe, kwa sababu ukitazama vizuri zoezi zima ni hitajio la Serikali kuliko hitajio

la mvuvi mwenyewe. Kwa hiyo, tulitaka kujua gharama hizi zinakuwaje na zinakuwa *controlled* namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunafahamu ufugaji ni maisha na zipo kila siku, kwa hiyo tunataka kuona namna ambavyo linaweza likasimamiwa bila ya kuleta kelele, lakini kwa ujumla wake tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, wafugaji kwa ujumla kelele zimepungua na nadhani kuna haja ya kutoa tu ushauri kwenye maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kwenye eneo hili naipongeza sana Serikali, pale Geita Mjini tumepata ujenzi wa mnada, kwenye eneo la mradi wamejenga mnada na iko karibu na josho, Geita Mjini tunayo machinjio ya kisasa ambayo imegharimu zaidi ya shilingi bilioni 12, sasa ninataka wataalam wako ofisini watusaidie ku-*connect* matumizi ya hiyo machinjio kama alivyosema Mheshimiwa Charles hapa, bado unaona mauzo ya samaki, mauzo ya nyama nje ya nchi pamoja na uwepo wa machinjio imegharimu pesa nyingi sana bado ni madogo, nadhani kunahitajika *connection* ya fursa hii kati ya Watanzania waliopo Tanzania na wateja waliopo nje pamoja na uwepo wa huo mnada ili kuongeza mauzo na kutumia hii fursa iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwenye mnada kinachopungua sasa ni bwawa lile la Kasamwa ambalo ndilo linalo *feed* josho, lile bwawa liliharibika na wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa mabwawa tuliomba lile bwawa liwe sehemu ya mpango wa kulikarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ninakwenda kwenye uvuvi. Ninaipongeza sana Serikali, *idea* ya vizimba wakati tunaizungumza humu ndani watu walikuwa hawaelewi tunazungumza nini na ulikuwa ukimaliza kuongea habari ya *fish cages* wanakuuliza hicho ni kitu gani, sasa hivi nadhani karibu kila mtu anona faida yake. Sasa mambo mawili makubwa kwenye eneo hilo Mheshimiwa Waziri, moja yale maeneo tuliyokusudia kuweka *cages* yanavamiwa sana na magugumaji na magugumaji yana uhusiano mkubwa sana na kupungua kwa

Samaki katika Ziwa Victoria. Nimeona kwenye hotuba yako umesema mahitaji ya samaki katika nchi yetu ni tani 1,200,000 lakini tunazalisha tani 500,000, maana yake tunao upungufu wa tani karibu 700,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, zinapungua kwa sababu gani, mazalia ya samaki kwa ujumla wake kama kuna mtu anafanya tathmini yanaendelea kupotea, yaani kadri siku zinavyokwenda magugumaji yanatengeneza *saltation*, yanatengeneza visiwa, Kwa hiyo zile *breeding area* zote zinasogea. Samaki hazaliwi kwenye maji marefu anazaliwa kwenye kandokando ya mito, kwenye maeneo ambapo hakuna magugu maji. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia namna ambavyo tunaweza tukafikiria kupambana na magugu maji. Kamati imesema vizuri sana, imezungumza kuhusu namna ambavyo Serikali iweke mkazo kwenye kupambana na magugu maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iko haja ya kuangalia namna ambavyo tunawekeza kwenye kufikiria namna ya kuongeza uzalishaji wa samaki kwa ujumla wake, kwa sababu kwa mfano Ziwa Victoria samaki *almost* wamepungua na wamepungua kwa sababu gani, mazalia yanazidi kuvamiwa na magugu maji. Kwa hiyo kadri tunavyowekeza kwenye vizimba tufikirie kuwekeza kwenye namna ya kupambana na magugu maji, kwa sababu mwisho wa siku tunahitaji vizimba lakini tutahitaji samaki wa asili wa ziwa Victoria au wa maeneo mengine waendelee kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu tunaotoka kandokando ya Ziwa yaani uvuvi ni maisha. Nimekusikia mara kadhaa unazungumzia mafanikio ya kufunga Ziwa, ni mafanikio mazuri sana kwa Serikali, lakini uvuvi ni maisha ya watu, yaani ni kama ambavyo unaamka unaoga unakwenda ofisini. Unapozungumzia kufunga ujue unafunga aina fulani ya maisha ya watu kwa miezi mitatu. Sasa ipo haja ya kupambana na changamoto kisayansi zaidi kuliko kufikiria kufunga kwa sababu tutaendelea kukusudia kufunga na upo muda utafika tutafunga hata miezi sita, lakini ninadhani *may be* tungelikuwa tunaweka hii *season,* lakini ukitaka ku-*control* vizuri ufunge kwa *export* usifunge kwa ajili ya watu wa

ndani, matumizi ya ndani, kwa sababu ukiacha mauzo ya nje ni chakula, lakini ni uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la tatu ni kwenye malisho ya mifugo. Mheshimiwa Waziri ninakupongeza kwa ujumla wake nimesema utulivu upo kwenye maeneo ya wafugaji, juzi tumefanya mabadiliko ya Pori la Kigosi. Pori la Kigosi lilikuwa *National Park*, tumebadilisha tukalishusha hadhi tukalipeleka kwenye *forest reserve*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *forest reserve* sasa hivi linaruhusu watu kutengeneza barabara, linaruhusu watu kuchimba madini *open pits*, linaruhusu watu kuanzisha mgodi mle ndani. Sasa ninajiuliza kama tunaweza kufanya vitu vyote hivyo, ng'ombe ana ugomvi gani na hifadhi, kwa nini wafugaji wasiruhusiwe kwa fomula ile ile wasiende kukata miti, waingie wafuge kwa sababu lile pori lina zaidi ya kilometa *square,* nadhani lina zaidi karibu 10,000, hekta karibu milioni kumi sijui na ngapi ambalo ni kubwa, kiasi kwamba mgogoro uliopo sasa hivi wa wafugaji kupambana na wakulima kama kutatokea utaratibu wa namna ya kuwapanga....

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Kuna nini?

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa namna ya kuwapanga wafugaji kwenye eneo lile upo uwezekano mkubwa kabisa, ugomvi kwa wafugaji ukaisha kwa sababu yanafanana.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, muda ni mdogo na kila mtu anataka kuchangia jambo lake.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa...

**NAIBU SPIKA:** Ahaaa! Sijakuruhusu, kaa chini. *(Kicheko)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaeleza kwamba kama utaratibu huu uliyotumika kwa wachimbaji wa madini, jambo jema kabisa na wamepewa maelekezo wanalipia *GN*. Wanapotaka kukata miti, lakini hawaruhusiwi kukata miti na ukiangalia namna ambavyo wafugaji wengi wamekuwa wakigombana na Maafisa wa Misitu, kumbe upo uwezekano wa kuwapanga kwenye eneo lile kwa sababu hawakati miti, tukaongeza wafugaji na uzalishaji wa ng'ombe kwenye ile misitu bila kugomba na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu mimi mgogoro uliopo sasa hivi maeneo yote ambayo tuliyatenga kuwa malisho ya mifugo, wakulima wakiingia mfugaji anasogea mbele. Maana yake ni kwamba kesho ukitenga tena sehemu nyingine kwa ajili ya malisho ya mifugo watajenga nyumba wale wafugaji, ataingia mkulima, wafugaji wanasogea mbele, kwa hiyo mwisho wa siku tutajikuta hakuna sehemu ya kufuga wala kulima. Kwa sababu kila sehemu unapotenga maeneo ya malisho kuna mtu anajenga nyumba anaanza kulima, lakini kumbe tunahitaji mpango mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachana na *NARCO* na mashamba mengine madogo madogo amesema hapa Mheshimiwa Mwijage ambayo kwa ujumla hayatoshi na mchakato wa kupata hayo mashamba ya *NARCO* umekuwa ni mkubwa kiasi kwamba wanaopata ni wachache, tunaweza tukakabiliana na upungufu huu kwa kutafuta *solution* nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwenye malisho ambayo Mheshimiwa Waziri, amezungumza. Tunazungumzia tani na uchumi mkubwa kwenye malisho haya, lakini Mheshimiwa Waziri awatazame wafugaji wako huko tunapotoka sisi, kwanza inaonekana kabisa siyo kipaumbele kwa sababu wanakimbizana

na nyasi kiangazi, wanahama kutoka *point* moja kwenda *point* nyingine wakati masika wana majani mengi ambayo ikikaribia kiangazi wanayachoma moto. Sasa pengine hapa kunahitajika aina fulani ya utaalam na ushauri ili hiki kinachochomwa moto badala ya kuchomwa moto hawa wafugaji badala ya kukimbizana na kufuata nyasi kila siku mwaka mzima, waweze kutumia vizuri maeneo haya kwa kutengeneza hizi nyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pale Ukiriguru, pale Mwabuki tuna eneo kubwa sana ambalo pengine kwa maoni yangu, lingeweza kutumika kama *pilot,* watu wakajifunza wakapata mbegu kama ambavyo tunafanya kwenye utafiti kwenye kupata mbegu. Shida kubwa nimeona kwenye utafiti Kurugenzi inayosimamia hizi taasisi karibu 12 nchi nzima inapata pesa nyingi kuliko taasisi nyingine zote, yaani ukichukua hii kurugenzi iliyopo hapa ofisini, ukachukua na pesa wanayowatengea waliopo kwenye hizi taasisi, ukigawa hawa waliopo huku wanapata karibu 1/10 ya pesa inayopatikana ofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo kazi ya utafiti haifanyiki huku ofisini, inafanyika kule kwenye taasisi zenyewe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, kengele ya pili.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, wewe umo kwenye kuchangia mtu wa 14, sasa unataka utoe taarifa, si jambo sahihi, subiri ikija nafasi yako uchangie,. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mungu, hatimaye nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ninampongeza Waziri wetu wa Mifugo, Mheshimiwa Ashatu Kijaji, pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara yake. Mheshimiwa Waziri kwa kweli anafanya kazi kubwa na nzuri sana katika Wizara hii na ndiyo maana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakukosea hata kidogo kumpa mwanamke shupavu, mwanamke hodari, mwanamke ambaye ana maono mazuri, kumpa Wizara hii ambayo ni Wizara nyeti sana katika ustawi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema ni Wizara nyeti? Wizara hii ni Wizara ambayo haiachani kwa mbali na Wizara ya Kilimo. Wizara ya Kilimo ni Wizara ambayo inazalisha chakula na Wizara hii nayo inazalisha chakula. Huku kwenye kilimo tunapata wanga na huku kwenye Wizara hii tunapata protini, wanga bila protini hakuna lishe, wanga bila protini lishe hakuna. Kwa hiyo, ni matarajio yangu na ni imani yangu kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni msikivu sana, Wizara hii ataiongezea bajeti kutoka hapa ilipo na kupata bajeti kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Rais huyu huyu ambaye aliiongezea bajeti kubwa kupita kiasi Wizara ya Kilimo baada ya kuona changamoto, leo hii kilimo kinajitosheleza kwa chakula. Kwa hiyo Mheshimiwa Ashatu asiwe na wasiwasi aendelee kupambana ni imani yetu ataongezewa bajeti na hata hao samaki watatoka hapo walipo watakuwa ni wengi na tutakula tutajitosheleza kwa chakula hapa nchini na kilichobaki tutauza nje ya mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie hali ya mifugo. Bara la Afrika ni miongoni na katika nchi yetu ya Tanzania, Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye mifugo mingi sana, ukiachana na Ethiopia. Sasa kutokana na muktadha huo na ndiyo maana nimesema usiwe na wasiwasi Rais atakuongezea tu, atatuongezea na sisi wenyewe tukiendelea kupambana

tutaongezewa hiyo bajeti hatimaye tutauza nje mifugo mingi na tutakuwa na ile mifugo ambayo itatutosheleza ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nataka nizungumzie suala hilo hilo la mifugo. Mifugo ndiyo kila kitu, mifugo ni rasilimali, wananchi wa Tanzania walio wengi ni wakulima na wafugaji na kwa kuwa wananchi hawa ni wakulima na wafugaji tunachohitaji sasa hivi ni yale maoni ambayo kama Kamati yameelezwa. Yale maoni yakitekelezwa mabadiliko makubwa yatatokea katika nchi yetu na Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala zima la vizimba, sisi tupo kwenye Ukanda wa Pwani, lakini hapa nilichokisikia sehemu kubwa nimesikia kwenye maziwa, hivi huku kwenye bahari kuna mpango gani kuhusiana na suala zima la vizimba, kwa sababu kuna maeneo mengine yanaweza kupelekewa vizimba na uzalishaji wa samaki ukawa ni mkubwa, ninaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. Ukanda wa Pwani huu ni ukanda mrefu sana, akiliangalia hili na akatuletea litatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwenye huu huu ukanda wa pwani tunaipongeza sana Serikali kwa kutuletea ile bandari kubwa ambayo ipo kwenye Mkoa wetu wa Lindi Wilaya ya Kilwa, mpaka sasa imeshakamilika kwa zaidi ya 90%, ongezeni nguvu tuweze kukamilisha ili wale samaki waje pale na wauzwe katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hilo hilo eneo la samaki, katika Jimbo langu waliniahidi watanijengea soko la samaki, mpaka leo hii lile soko la samaki bado halijajengwa, ninaomba wasaidie juu ya hili na ukanda ule na hasa Jimbo la Mchinga samaki ni wengi sana na bahati mbaya baada ya haya mafuriko yaliyotokea juzi lile soko lote limeharibiwa, limevunjika kabisa, ninaomba waangalie kwa jicho la pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusina na suala zima la majosho, ninawashukuru na ninaipongeza Serikali. Kwangu kule pamoja siyo eneo la wafugaji, lakini kuna wafugaji, kuna wafugaji wengi kutoka maeneo ya mifugo wamekuja kule na wamejengewa majosho tunashukuru na kuipongeza Serikali. Hata hivyo, kuna jambo moja pamoja na kukamilika kwa majosho yale kwa sababu eneo wanalofuga ni eneo la Kilangala, ni eneo la Mipingo Kata ya Mipingo na Kata ya Kitomanga, kuna wafugaji wengi utafikiri, yaani Wasukuma wale samahani kwa kuwataja wamejaa kule na wanafanya ufugaji mzuri wala sina mashaka nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja hakijafanyika, madawa hayajaletwa tunaomba watuletee hayo madawa. Baada ya kuyasema hayo, sikuwa na mambo mengi ya kuyasema, isipokuwa niipongeze Serikali kwa mchango ambao unapatikana kutokana na hayo mauzo ya samaki na mauzo ya nyama taratibu ndiyo mwendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anahitaji kila wizara aipatie pesa kwa 100% lakini kutokana na sababu moja au nyingine ndiyo maana unakuta Wizara hii anaipa kiasi hiki, Wizara hii anaipa kiasi hiki. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wala tusiwe na wasiwasi tuendelee kusema ni imani yetu kwa kuwa tunaenda kwenye uchaguzi, pengine tutakaporudi na imani yetu sisi sote tutarudi. Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa kwa nini tusirudi, tutarudi na tutakuja kuyasemea haya na tutayaona mabadiliko kama yaliyotokea kwenye Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ninawatakia Waheshimiwa Wabunge, kila la heri na mafanikio makubwa huko Majimboni. Tumwombe Mwenyezi Mungu wote tutarudi kwa kasi kubwa na nzuri ambayo tumeifanya. Nami ninawashukuru wapiga kura wangu wana imani sana na mimi sina mashaka nao, ninawatakia kila la heri na baraka, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ehee! Mwongozo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 76 ya Mwongozo wa Spika, kuhusiana na jambo lililotokea leo Bungeni, nikirejea kwenye Swali Namba 396 ambalo lilikuwa linahusu uandikishaji wa vitambulisho vya *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua umuhimu wa *NIDA* kwa sababu inatumika maeneo mbalimbali. Leo Mtanzania akitaka kuomba ajira lazima awe na *NIDA*, akitaka matibabu kwa maana ya bima lazima awe na *NIDA*, akiwa hata anasafiri nje hata kwenda upande wa pili wa Zanzibar lazima uoneshe *NIDA,* lakini hata hizi huduma za ruzuku, sijui gesi, mbolea na vinginevyo lazima uwe na *NIDA*, ukitaka hati, umeme na kila kitu. Kwa hiyo, *NIDA* imekuwa ni sehemu ya maisha yetu, ukitaka leseni ni *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu utaratibu ambao upo sasa hivi, ambao kwanza unachelewesha Watanzania kupata hizi *NIDA*. Ukitaka kujiandikisha kupigakura lazima uwe na *NIDA* pia, kwa hiyo na tunatambua kwamba mwanadamu kila mwezi anaongezeka umri kama alikuwa na miàka 17 mwezi jana labda mwezi huu kama amezaliwa Mei au Juni ataongezeka umri.

Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, twende kwenye mwongozo wako, kwenye hoja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu waliyokuwa wametoa Serikali inaonesha dhahiri kwamba ni Watanzania wengi bado tunawaacha nje bila kuwapa hivi vitambulisho vya *NIDA* ambavyo ni muhimu sana, kama nilivyoainisha kwenye uhitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu, nilikuwa ninataka kuonesha au ku-*suggest*, Serikali ione umuhimu kama ambavyo nimesema. Kwanza, kuwepo na vitambulisho vikitolewa visiwe kwanza hata na *expiration date*, kama hiki cha kwangu nimepewa kinaisha mwakani na kupatikana ni kazi sana, lakini pili tu-*introduce*, watoto wanapozaliwa waweze kuwa wanaandikishwa *NIDA* moja kwa moja ili kuondoa hii *process* ambayo inachukua muda mrefu pia. Jambo la tatu, hili zoezi liwe endelevu lisipewe *interval* yaani kila siku mtu akiona umri umeongezeka amefika miaka 18 ana *visit* sehemu ilipo, kwa hii *gap* iliyopo wakati tuki-*introduce* hiyo nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninakuomba mwongozo wako katika hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza Mheshimiwa Matiko, swali hilo limetokea leo Bungeni na swali hilo siyo lako na kwa mujibu wa Kanuni inabidi sasa, subiri basi, hivi kila mahali unapokuwepo upo hivi! *(Kicheko)*

Kwa hiyo ilikuwa kikanuni uli-*construct* mwenyewe ulilete upya ndani ya Bunge, lakini kwa vile Jumatatu Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo wana bajeti yao na wao ndiyo *instrument* yao na ndiyo *competent authority,* ninakushauri hoja yako uilete. Mwongozo wangu kwako ilete hoja yako Jumatatu ili Wizara iweze kukujibu kwa ukamilifu. Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, watafuata Profesa Ndakidemi, Mheshimiwa Raymond na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.01 Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

**23 MEI, 2025**

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Nimeshamtaja Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda; Mheshimiwa Profesa Ndakidemi na Mheshimiwa Shally wajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya Mifugo na Uvuvi. Pia, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uhai kuendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inafanya kazi kubwa sana na nianze kabisa kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii mahali popote pale walipo ikiwa ni pamoja na wale waliopo Mkoani kwangu Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni sawasawa na mtu aliyepewa watoto wawili kuwalea; mmoja anaitwa Mifugo, mwingine anaitwa Uvuvi. Katika watoto hawa wawili wanaolelewa, mmoja anaendelea kwa kasi, lakini mwingine hali yake inasuasua sana na hii inaonekana kwenye taarifa nzuri

aliyoitoa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya bajeti aliyoitoa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto anaitwa Mifugo anachangia pato la Taifa kwa asilimia 6.2 na anakua kwa asilimia tano, lakini mtoto anaitwa Uvuvi anachangia pato la Taifa kwa asilimia 1.7 na ukuaji wake ni asilimia 1.4. Mheshimiwa Waziri nimwombe wewe kama mlezi wa watoto hawa wawili utajua kabisa wapi unapotakiwa kuongeza kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi katika nchi yetu bado uko chini ukizingatia kwamba tuna Bahari ya Hindi, tuna Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Maziwa mengine mengi. Rasilimali hii ya maji aliyotusaidia Mwenyezi Mungu kutuwekea katika nchi yetu ni lazima ingetafsiri maendeleo makubwa katika Sekta ya Uvuvi. Kwa hiyo, nimwombe sana aongeze kasi kubwa katika uvuvi na uvuvi utasaidia kwa kiasi kikubwa sana kuinua pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Wizara nzuri zinazofanywa, lakini lazima sisi Wabunge tukubali kabisa kwamba bado Serikali haijaweka nguvu ya kutosha. Ninasema hivyo kwa sababu gani? Mwaka jana (bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025) tuliwatengea shilingi bilioni 460.3, lakini pesa tulizowapa ni shilingi bilioni 131.9 sawa na 28.7%.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukasema kwamba tupo *serious* na Wizara hii ili iweze kuchangia pato la Taifa kwa kuwapa 28% ya pesa tulizowatengea. Kwanza, pesa tulizowatengea ni ndogo, lakini hata hizo ndogo za shilingi bilioni 460.3 bado tumewapa shilingi bilioni 131 tu. Kwa kweli bado hatujaonesha umakini na kujali sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa hivi tunakwenda kupitisha bajeti ya shilingi bilioni 476. Haitakuwa na maana yoyote kama watakwenda tena kuwapa 28% ya pesa hizo. Nikifika wakati wa bajeti ya Wizara Fedha hapa, nitamtaka Waziri aji-*commit* kwamba Wizara hii ataipa fedha yote 100% ili tuone

namna ambavyo Wizara hii sasa inakwenda kusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuchangia kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo ambalo ninataka lipewe nguvu hasa katika uvuvi ni suala la ufugaji wa samaki. Ukichukua suala la uvuvi kwenye bahari zetu na kwenye maziwa tuliyonayo utaona kwamba kuvua katika bahari na katika maziwa ni sawasawa na kilimo cha kutegemea mvua, lakini kufuga samaki ambao mnawavua wale mliowafuga ni sawasawa na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji kina uhakika zaidi wa mavuno kuliko kilimo cha kutegemea mvua ndiyo ambavyo suala la ufugaji wa samaki lina uhakika zaidi wa kupata mazao kuliko watu wanaokwenda kuvua samaki katika ziwa au bahari wanaokwenda kuwatafuta ambao hawajui wapo wapi. Kwa hiyo, niseme Mheshimiwa Waziri katika kipindi hiki waweke nguvu kubwa sana katika ufugaji wa samaki na katika nafasi hii nimpe hongera kubwa sana, tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 21 ya mwezi huu wamekwenda kuanza kuvuna samaki katika vizimba kwenye Ziwa Tanganyika. Wafugaji wale wa samaki wanatoa pongezi kubwa na wameniambia nimpe pongezi yeye na Serikali yao chini ya kiongozi wao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu mpango huu wa kufuga samaki kwenye ziwa anakwenda kuwakomboa wavuvi wetu. Ahsanteni sana, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili la ufugaji, nikuombe Mheshimiwa Waziri boresha kanuni za uvuvi. Kanuni za uvuvi bado zinahitaji maboresho makubwa juu ya aina ya nyavu zinazotumika, vyombo vinavyotumika, suala la leseni za wavuvi, leseni za vyombo vya uvuvi kuna malalamiko mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu Mheshimiwa Aida hapa aliyazungumza sina sababu ya kuyarudia. Ninajua wewe ni mtu makini sana na tumekupa Naibu Waziri huyu askari mpiganaji

wa miguu ni mtu ambaye hashindwi na jambo watumie vizuri ili walete mabadiliko makubwa kwenye hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ninataka nilizungumzie ni zoezi walilolifanya la kufanya *stock assessment* kwenye Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika kwa takribani miaka zaidi ya 20 lilikuwa halijafanyiwa *stock assessment*. Mwaka juzi walifanya *stock assessment,* lakini mpaka sasa hawajatoa ripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti hii ndiyo inayoweza kutusaidia kuwa na uwekezaji mkubwa kwenye Ziwa Tanganyika. Wapo watu wanataka kuweka meli za uvuvi kwa sababu hili ni Ziwa lenye kina kikubwa. Hata hivyo, kwa sababu wao hawajatoa ripoti ya *stock assessment,* wanashindwa kujua kiwango cha samaki waliopo kwamba wanahitaji vyombo ya aina gani katika kuwavua. Niombe wakamilishe kazi hiyo ya kutoa ripoti ya *stock assessment* waliyoifanya ili tuweze kufanya uwekezaji mkubwa kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia kutoa pongezi nyingi kwa wachapakazi hawa na nina watia shime, kazi iendelee. Ahsanteni sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, wajiandae Mheshimiwa Raymond na Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kuwapongeza sana Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na Naibu wake Mheshimiwa Mnyeti, Katibu Mkuu Profesa Riziki Shemdoe, wasaidizi wake na Watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa wanayofanya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza kwa sababu kusema ukweli hawa watu pamoja na kupewa pesa ndogo kama alivyosema mchangiaji aliyepita, wamefanya kazi kubwa sana. Mimi ni Mwanakamati kwenye Kamati inayowasimamia. Tulitembelea miradi ambayo inatekelezwa na Wizara hii na tulijiridhisha kabisa kwamba kazi wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda kwenye ujenzi wa soko kule Chato, kazi zimekwenda vizuri. Tumetembelea ghala wanalojenga hapo *TARI* Mpwapwa limekaa vizuri kabisa na Makao Makuu ndiyo usiseme. Makao Makuu yamejengwa ya Kimataifa. Kwa hiyo, kazi kusema ukweli wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kama alivyosema Mheshimiwa Francis Mtinga na wewe ulikazia pale kidogo; inaonekana uvuvi na mifugo ni vitu viwili vikubwa ambavyo ni tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunataka tuone tija upande wa mifugo ambayo tunaweza tukawahukumu na tija upande wa uvuvi tu tuweze kuwahudumu, ninakubaliana kabisa na mchango na zile sababu alizotoa mwenzangu kwamba ni muda sasa tumwombe Mheshimiwa Rais ikimpendeza agawe hizi Wizara ili tuwe na Wizara ya Mifugo ambayo itaangalia mambo ya mifugo ambayo ni tofauti kabisa na uvuvi na Wizara ya Uvuvi na utunzaji au usimamizi wa rasilimali za maji. Tusiseme bahari tu kwa sababu tuna bahari, maziwa, mito na vitu vingine vyote. Kwa hiyo, nimeunga mkono alichosema Mheshimiwa Mtinga na Waziri amekazia pale; twende hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri kitu kimoja kabla sijaanza mchango wangu rasmi kuhusu kwenye Jimbo langu. Ombi langu, ninaomba wanisaidie kujenga majosho na birika za kunywa maji kwa wafugaji wa ukanda wa tambarare eneo la Mabogini na Arusha Chini. Pia, ninaomba miradi ya kizimba na mbegu bora za samaki kwa wavuvi wangu wa Nyumba ya Mungu. Asubuhi nimeuliza hili swali ni nyeti sana, Mheshimiwa Mnyeti alinijibu, lakini bado ninaomba hadharani kwamba wanisaidie tuweke vizimba kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia tuimarishe hivi vituo vya kuhimilisha mifugo kule kwani vimechakaa. Kwa mfano, kile Kituo pale Manushi kipo, lakini kimechakaa sana, tuvifanyie ukarabati. Ninaomba tukamilishe ujenzi wa mashamba darasa. Ninashukuru wameshapeleka zile hela nilizokuwa ninaomba; mashamba darasa ya kufuga kuku twende tukayakamilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia zile mbegu bora za ng'ombe wa maziwa na ng'ombe wa nyama. Wakulima wa milimani na wa tambarare wapatiwe ili tuweze kupata mbari ambazo ni nzuri zaidi. Pia, ikikupendeza hata hizi mbegu bora za malisho ambazo tayari amezieleza kwenye ripoti yako, ninaomba anisaidie nipelekee wakulima wangu kwenye Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mchango wangu nitatoa ushauri na nitaelekeza nguvu sana kwenye malisho kwa sababu kuna wakati nilienda Ethiopia na Wizara niliona vitu vizuri sana kule na inaniwia niseme kitu hapa. Mifugo kwa ujumla wake ni kitu muhimu, kinatusaidia kitoweo, usafiri hata mahari, wengine wanatambika kwa kutumia ng'ombe na mbuzi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa mifugo, bado kuna changamoto kubwa sana inayoikabili Sekta ya Mifugo na hii ni ya uhaba wa malisho kwenye maeneo karibu yote ya wafugaji Tanzania; kuna uhaba mkubwa wa malisho. Pia, kuna tatizo kubwa sana ambalo niwaambie bado hatujali-*address* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wengi wanakaa kwenye maeneo ambayo kama hamna mvua ya pili, nyasi zilizokuwepo ng'ombe wakishakula, kwa mfano maeneo ya Wamasai wakishakula zile nyasi zikiisha inakuwa ni kizaazaa. Hakuna kitu atakachokula ng'ombe, wanabaki aidha wafe ama hao wafugaji wanaamua kuwapeleka hawa ng'ombe maeneo mengine ili wakapate lishe kule na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tujiulize wenyewe tu hata ingekuwa ni wewe uone ng'ombe anakufa, ndiyo kitu unachokitegemea utafanya nini? Tujiulize tu hata ingekuwa ni wewe hata mimi, uone ng'ombe anakufa hana malisho utafanya nini? Ni lazima utatafuta namna mbadala ili ng'ombe wako wapate malisho na hapo ndiyo inatokea migogoro kati ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niiombe Serikali yangu Tukufu. Je, Serikali imefanya nini kuwasaidia hawa watu tangu tupate uhuru mpaka leo? Ninajua kusema ukweli umeeleza juhudi ambazo Serikali imeshachukua, wameshaanza kidogo kidogo lakini kwa unyeti wa sekta hii upande wa malisho hawa watu ni kama tumewaacha yatima na matatizo yanayotokea ni kwa sababu Serikali haijafanya kitu kikubwa kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe ushauri. Tulienda kule Ethiopia wako vizuri majani yanapatikana na ng'ombe hawafi na wao hawana hata maji mengi kama sisi, hawajabarikiwa kuwa na ardhi bora kama ya kwetu. Niombe sana Serikali yangu sikivu ihamasishe wafugaji wamiliki ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, Mmasai anapokwenda sasa anapeleka ng'ombe kwenye malisho maeneo mengine, akirudi anakuta wakulima wamejenga pale. Kwa hiyo, tunawa-*marginalize* tunawasogeza mpaka wanaishia kwenye mbuga za wanyama wanagombana Idara ya Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hebu tufanye haraka iwezekanavyo. Ninajua hapa wamesema wameshapima hekta 210,000 na vijiji 262 karibu hati zinatoka tangazo. Hii kitu iende *speed* ya *supersonic,* haya maeneo yasajiliwe tujue hapa ni kwa wafugaji, hapa ni kwa wakulima na kwenye urithi wa huko mbele ya safari tujue haya ni maeneo yao tusije tukayaingilia sana. Hebu tukubaliane kwamba wasipokuwa na maeneo siyo wote, tutakuwa tumeiua hii Sekta ya Mifugo na haitakuwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili ninaishauri Serikali na wadau mbalimbali waanzishe programu maalum ya kuzalisha malisho. Kwa mfano, kuna mbegu nyingi ambazo wamesha-*release*. Sasa hizi mbegu twende tuanzishe programu kwa kutumia sisi, Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa sababu ufugaji ni biashara na watu wakijua kuliko ng'ombe afe atahakikisha amenunua hivyo vitu ambavyo vitaanzishwa na programu hii hizi mbegu bora ambazo wameshatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupate hizo mbegu tujenge maghala ya kutosha kama lile la kule Mpwapwa. Hongereni sana lile ghala ni zuri. Tujenge maghala kama lile la pale Mpwapwa kwenye maeneo yote nchini ambako wafugaji wanafuga ili tufanye biashara tuwauzie wakati ambao hawana malisho waweze kupata kitu cha kulisha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji ni biashara. Wameanzisha programu za *BBT;* safi kabisa. Sasa malisho nayo ni fursa. Hebu tuwe na ka-*BBT* kakuelekeza hawa vijana wa kifugaji badala ya kufuga pia tuweke *component* ya kuzalisha malisho na vyakula vingine vya mifugo. Tuwe na ka-*BBT* ka malisho na chakula cha mifugo kwa ajili ya hawa vijana ili wasaidie hizo jamii zinazofuga waweze kuwapatia malisho kwa kutumia utaalam ambao tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua tumepeleka rafiki zangu wa Kimasai kule Msomera. Sasa kule kwa kuwa ni sehemu mpya, pale tuweke mashamba darasa ya kutosha ili Wamasai na wafugaji kutoka maeneo mengine waende wakajifunze vitu vizuri ambavyo tutakuwa tumevianzisha pale. Kujifunza ni kuona na mtu akiona, akiamini, akiona kwamba tunaweza tukatengeneza malisho itakuwa kitu kizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tunayosema ya malisho haitafanikiwa kabisa kama hakuna maji; kama hakuna maji tusahau kabisa. Tungekuwa tumeanzisha miradi ya umwagiliaji tuwe na maji kwenye hayo maeneo ambayo wakulima wanafuga tuwe na maji ya kutosha ambayo wanaweza wakaanzisha programu za kuzalisha nyasi mambo yangekwenda vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niishauri Wizara tuwe na programu za kuweka miradi ya umwagiliaji kwenye haya maeneo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa kengele ya pili hiyo.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, ninaishauri Serikali ikiwezekana tuanze bima ya mifugo kama ilivyo kwenye mazao kuna bima. Mfugaji akiweka bima kwa ajili ya mifugo yake atakuwa na uhakika kwamba atapata unafuu hata ng'ombe wakifa anajua atalipwa kitu kidogo na hii itawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Baada ya kusema hayo ninawapongeza sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Raymond, wajiandae Mheshimiwa Olelekaita na Mheshimiwa Mabula.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii mchana huu. Kipekee kabisa ninamshukuru Mungu kwa pumzi hii ya uhai. Pia, ninakuomba niwashukuru Wanawake wa Kilimanjaro kunituma huku Bungeni kuwasemea na siku zote nimekuwa mimi nikiitwa mama vifaranga na mama mitamba ya ng'ombe. Jambo hili nimekuwa nikilizungumza na ninajua sasa liko masikioni kwa Katibu Mkuu Shemdoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninaiona kazi kubwa anayoifanya kuboresha Wizara hii. Hakika ninafurahi na lilikuwa tamanio langu kuona mwanamke anakuwa Waziri kwenye hii Wizara; kama hujui uchungu wa mwana huwezi kumlea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii akinamama wengi tunaitegemea kwa mifugo kwa ajili ya lishe, mifugo kwa ajili ya biashara, mifugo kwa ajili pia ya kilimo katika maeneo yetu. Bila samadi huwezi kulima katika maeneo ambayo ni *zero grazing* na leo imekuwa, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kinyaji kwa kuwa Waziri wa Wizara hii na ninampongeza sana Naibu Waziri wako kwa sababu, ni mtu kazi. Ninamfahamu, ninajua akiamua hana la kumrudisha nyuma na timu waliyoikuta Wizarani ninajua mambo yanaenda kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nianze hivyo na niseme wazi kwamba, mambo mengi yanafanyika kwenye hii Wizara ya Mifugo na tunaoitegemea ni wengi. Hii ni Wizara pacha, Kilimo na Mifugo, lakini tunaona hii Wizara, niseme wazi mimi ninatokea kwenye Kamati ya Bajeti, bajeti yake ni finyu sana, ingeongezwa kidogo tungeweza kuona matokeo makubwa. Kwa nini ninasema hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, randama ilitoka jana, ukiiangalia ile randama na hela ambazo zimetoka mpaka kufikia sasa hivi unapata homa kidogo, sasa sijui kwa nini hela hazitoki au zinatoka hitaji ni kubwa mno. Serikalini wana njia yao ya kuleta bajeti na kusema ukomo, nani atakayevunja huo ukomo kama sio sisi Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi tuseme kweli, kama tuna nia ya kuisaidia Wizara hii, basi tuseme, tutoke nje ya hili *box,* huu ukomo usogee na mambo yatafanyika. Hii Wizara ya Mifugo inatakiwa iendeshwe kibiashara, ukifuga kibiashara utatoboa tu. Tumeona soko la malighafi au soko la mifugo yetu lipo ndani, ila ukienda kwenye ma-*grocery,* ma-*supermarket* makubwa, *shoppers,* wapi, bado tuna-*import* sana, hasa vitu kama nyama; nyama nzuri nzuri ile unaambiwa *imported*, mayai *imported*, maziwa *imported!* Sasa ninajiuliza, kwa nini tuna *import* wakati tuna soko? Hapo ninapata kizunguzungu kidogo!

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetamani kuona basi tunapata *products* ambazo zinakidhi hilo soko na sisi tu-*export* zaidi ya ku-*import*. Ukienda kwenye Maonesho ya Nanenane, ukiona ile mitambo ilivyo mikubwa, mbuzi wale wa mapacha, kuku wale chotara, unatamani igawiwe kwenye kata, vijiji mpaka kaya, isambae, angalau hata wafugaji 200/200, ili tulete mabadiliko, lakini tunaoneshwa tunashiba kwa macho. Madiwani wanalipiwa nauli wanaenda kuona, hawaoni kitu kinachoenda katika halmashauri zao wala nini! Sasa tutatoka vipi? Tunajua sera zipo vizuri, Maafisa Ugani wapo, nini kinachotukwamisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba basi waanze *pilot scheme* tu-*test* na ninawaomba sana waanzie Kilimanjaro. Nimeomba mitamba na Waziri Mkuu aliahidi, alipokuwa anamfanyia kampeni Prof. Ndakidemi, mitamba itakuja pale Kibosho Kati; mpaka leo haijaja mitamba! Nimeomba huku ndani, nimeongea miaka mitano sasa, hatujaona matokeo, lakini ninasikia imegaiwa kwenye maeneo fulani fulani, sasa na mimi ninangojea, huenda wamegawiwa kutokana na alfabeti za mikoa. Mkoa wangu Kamati haijafika, ninaamini kabisa kabla Bunge hili halijamalizika ninaondoka na mitamba kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe pia, hawa wazalishaji wakubwa, kwa nini wao kwenye *SCR* wanaenda kujenga madarasa? Wanafanya yale mambo Serikali inayayofanya badala ya kutupa vifaranga sisi akinamama tunaoomba hapa? Kwa nini wasitupe *SCR* kidogo? Nimepeleka majina yangu huko sioni jambo! Kwa kweli, jambo hili linaumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo niseme kwamba, hesabu za wafugaji wakubwa zimekaa vizuri; mfugaji mkubwa kauza ng'ombe kiasi gani, nyama kiasi gani, mayai kiasi gani. Mfugaji mdogo haijulikani, kwa vile ni kuku watatu, wanne, awaweke rekodi, wala haitambuliki. Nani atawasaidia wafugaji wadogo hawa kuweka rekodi, ili ijulikane wamefuga kiasi gani na wameuza kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo ningetamani, na ninashauri, yaboreshwe katika mifugo. Ni pamoja na mbegu bora za mifugo, hiyo mitamba, malisho bora, maji, huduma za ugani, elimu kwa wafugaji, mitaji na soko. Ninatamani kuona kila mwanamke anapata elimu nzuri ya ufugaji. Kama vile haitoshi, ninatamani hata wanafunzi shuleni wafundishwe kufuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona kwamba, aina za mifugo tunazopatiwa bado ni duni, tufanye *cross breading;* ilikuwepo na tulianza na nchi jirani, wao wakapata maziwa mengi na wanaendelea kupata. Tumefungua vituo vingi vya maziwa, lakini hatuna maziwa mengi yanayotoka; vyote hivyo, maziwa, mayai

yanatoka kwa wakulima, hata nyama ambayo inakwenda kuwa *processed,* lakini itapatikana vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo walipokuwa wanaonesha kamera hapa nimeona ng'ombe wanapigwa mpaka moyo wangu unauma. Hivi ni lini mtaleta Muswada hapa Bungeni tuzuie hao wanaoswaga ng'ombe kuwatandika na kuifanya ile nyama iwe haina ladha. Kwa nini mnawapiga ng'ombe nyie watu ambao mnafuga *in large scale?* Sisi wa *zero grazing*, kama kule mgombani Kilimanjaro, ng'ombe ni wa kubembelezwa, ni wa kuoshwa, ni wa kufurahi; kwa nini mnaswaga ng'ombe kwa kuwapiga?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba iwaingie akilini, huo ni unyanyasaji, ni utesaji wa wanyama, ninaumia. Mimi ni mtu ambaye ni *ambassador* wao, sitaki kuona mnyama anapigwa. Hilo ni jambo baya sana na ndiyo maana hata ngozi zetu huwa haziko vizuri. Ninaomba tutoe elimu kwa wale wafugaji wanaoswaga ng'ombe kwa kuwapiga iishe, sio dhana nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naona nina dakika chache. Ninaomba lishe iboreshwe, hatusikii tena majani ya luseni, hatusikii tena yale majani mazuri ya kulisha ng'ombe yanaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo ninaomba inapokuja kwenye samaki, Kilimanjaro tuna mabwawa mengi, tuna hilo la Nyumba ya Mungu, kuna Jipe, kuna Chala, tunaomba watuletee vifaranga watuwekee kwenye mabwawa hayo ili tuweze kuona kwamba na sisi tunapata samaki wazuri. Majirani zangu, ambao ni watani wangu, wao wakiona hata picha ya samaki wanafurahi tu. Ninaomba sana lile Ziwa Jipe wapewe samaki na wanenepeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, wajiandae Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula,

Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi na ninawapongeza Waheshimiwa hapa; kwanza Mheshimiwa Rais, kwa kazi na Programu aliyoanzisha ya Tutunzane, ilikuwa na maana kubwa sana. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, mtani na jirani yangu kwa kazi kubwa wanayofanya. Mheshimiwa Naibu Waziri na Mkuu wa Mkoa Mstaafu wa Mkoa wangu wa Manyara, kazi kubwa wanaifanya, hawa ni wachapakazi sana na Katibu Mkuu, Profesa Mdoe ni mtu ambaye anajulikana na kuheshimika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ambayo mwaajaribu kuifanya kwa wafugaji wa Tanzania ni njema sana na mtani wangu waliomwambia, kama ataweza, ameweza sana na ataweza sana. Tangu ameteuliwa tumemwona akienda huko kushiriki kwenye shughuli za ufugaji na kama alivyosema kwenye hotuba yake, wafugaji wamesema watampa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kura nyingi sana. Hiyo kazi sisi tumeshaimaliza, huwa sisi hatuna maneno mengi sana, tukishamaliza tumemaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoshauri tu ni mambo makubwa ya kuendelea kuboreshwa zaidi, ili wafugaji wa nchi hii waendelee kunufaika zaidi. Ninashukuru kwa kipindi hiki cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Kiteto majosho zaidi ya 16 yamejengwa na yanafanya kazi. Wafugaji wa Kiteto wanashukuru sana, lakini bado majosho yanahitajika sana, karibu 20, katika Kata za Leseri, Sunya, Bwawani, Njoro na Kiyungu pamoja na mabwawa. Kiteto ni kame, maeneo mengi ya wafugaji yanahitaji mabwawa, kukiwa na mabwawa itafanya wafugaji waendelee kufuga kwa raha kabisa. Miaka miwili, mitatu iliyopita tulipata ukame, mifugo mingi sana ilipotea kwa sababu ya ukame, Kiteto peke yake karibu ng'ombe 25,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, tunavyosema Wizara hii iongezewe bajeti kubwa tunamaanisha kwamba, kazi ni nyingi sana; wafugaji kuhitaji majosho, mabwawa maeneo ya malisho

yalindwe, tuwe na ardhi inayoitwa ni ya wafugaji na tunategemea yalindwe kama wanavyolinda maeneo ya wanyamapori, wale jamaa zetu wa maliasili. Wizara iwezeshwe, ipewe *resources* nyingi, maeneo haya yatambulike vizuri na yalindwe kisheria, hakuna mtu anayetaka tu kutembea kila mahali, lakini ni kwa sababu ya changamoto ya miundombinu ya maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, kama walivyosema wengine hapa, Watanzania nchi hii ni wakulima, wafugaji na wavuvi, kwa hivyo *attention* kubwa ya nchi inahitajika kwenye maeneo hayo kwa sababu, ndiyo Watanzania wamegawanyika kwenye makundi hayo. Hata waliosema kwamba Wizara hizi zingekuwa mbili zigawanywe, kwanza inatupa sisi fursa ya kuweka pesa nyingi kuonesha kwamba, *attention* kubwa inahitajika kwenye maeneo hayo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana kwenye kilimo na pesa imeongezeka, ni matumaini yetu kwamba, bajeti zijazo hizi sekta mbili za uvuvi na ufugaji zitapatiwa pesa nyingi kama walivyopatiwa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuongeza pesa zaidi. Tunamwombea aendelee kupata maono makubwa na apate pesa nyingi, kwa ajili ya kukwamua Watanzania hawa kwa miaka 60 ya uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanjo za mifugo; watu wamezungumza hapa, tunashukuru chanjo zinaendelea sasa. Ushauri wetu ni hizi chanjo kwa sababu, zinaendana na vipindi vya mvua vya mwaka tuwe *systematic* zaidi, ili hizi chanjo ziwe zinakuja kwa wakati, mvua zikianza kunyesha tu huwa magonjwa mengi yana-*erupt*. Sasa hizi chanjo tukiwa tunapanga, kama inavyokuja mbolea, kama zinavyokuja mbegu kwa wakati na wao wakijitahidi, tukifanya hivi ninadhani wafugaji hawa watakuwa wanafuga kwa raha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna lugha nyingi sana hapa zinatoka, kuna wengine wanatuambia tusichunge! Sasa unajua pamoja na kwamba, Kiswahili ni kigumu sana, lakini unajua

kuchunga ni kuangalia ng'ombe, kwa sisi tunaofuga. Sasa huyo anayetuambia tusiangalie ng'ombe anataka tufanye nini sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tutachunga na niwaambieni tu kwa sababu, unajua lazima watu waelewe sekta hizi; mifugo sio biashara, kama wnavyotamani wote iwe, ni sehemu ya biashara, lakini ni maisha ya watu na ni lazima watu wajenge *resilience* wafahamu haya mambo. Kwetu sisi wengine bila ng'ombe hupati mke, eeh! Hata ungekuwa na mabilioni kiasi gani, huna ng'ombe, huna mke. Kwa hiyo, sio mambo madogo madogo tu ya kufikiri kwamba, eti ni uchumi tu, lazima waelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengine wao maziwa siyo kinywaji ni chakula, *diet* kabisa na watu wengi sana wanategemea mifugo, wale wanaojifunza kufuga na kunenepesha. Kufanya *zero grazing* ni aina tu ya kufuga, lakini mifugo na kwa hali ya tabia ya nchi inavyokwenda, mashamba yangekuwa yanahamishika; wewe kijiji hiki mvua inyeshe, halafu ungeweza kuhamisha shamba la mtu na wewe ungehamisha kwenye shamba lile mvua inyeshe kwenye hicho kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo mfumo pekee ambao ile *mobility* inasaidia mifugo kwenye kupambana na *climate change*. Kwa hiyo, hata huko tunavyozidi kwenda mifugo ni *resilient* kwa sababu ya hiyo *mobility,* kinachotakiwa tu ni iwe *coordinated* na mifugo wana njia zao za kuhama, kama wanavyofanya wanyama. Kinachotakiwa ni kutokuleta migororo na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweka mfumo mzuri mbona kuhama ni kawaida tu; mbona Wabunge wanahama hama hapa kila wakati, anatoka huku anakuja anakaa huku! Kwa hiyo, wakati mwingine siyo lazima kuhama iwe ni kitu kibaya, siyo mbaya, si mnaenda kila miji, kuhama ni sehemu ya maisha. Kwa hiyo tunaweka tu utaratibu, hata watu wanaohama vyama hapa, mbona hatusemi, lakini tunawakaribisha, kuhama bila kuleta vurugu kuna shida gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunawapokea. Kwa hiyo, kuhama ikiwa *potential* wala hakuna tatizo lolote, lakini Mheshimiwa Waziri benki zetu wafugaji wengi sana wamejitokeza kuchukua mikopo, inahitajika elimu sana. Unajua bado hatujapata benki ambayo inatoa mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Unajua kumkopesha mfugaji, ambaye anataka kunenepesha ng'ombe kwa mwaka, unahitaji uweze kujua kabisa kwamba, siyo mikopo ya kulipa mwezi kwa mwezi, hapana! Kama ni kilimo, miezi sita, akishavuna ndiyo umwambie…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, *Advocate* ya pili hiyo.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninawatakia kila la kheri, tupitishe hii bajeti haraka sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane. Jiandae Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, jiandae Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kushiriki katika kuchangia Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa katika Wizara hii; kwa kweli, tulikuwa na miradi mikubwa na sisi Kilwa tumekuwa wanufaika wakubwa kupitia Mradi wenye thamani ya shilingi bilioni 266 wa Bandari ya Kisasa ya Uvuvi, lakini pia, tumepata maboti mengi, takribani 14, ambayo yamewezesha wavuvi takribani 236.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maboti yenye thamani ya shilingi milioni 752 yameweza kusambazwa katika Wilaya ya Kilwa. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, rafiki yangu Profesa Riziki Shemdoe, Naibu wake Katibu Mkuu na pia, Watumishi walio chini ya Wizara ya Mifugo na taasisi ambazo zipo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipompongeza dada yangu, Mheshimiwa Zainab Telaki, Mkuu wa Mkoa wa Lindi. Kwa kweli, amefanya kazi kubwa, hasa katika zoezi la kukomesha mapigano kati ya wakulima na wafugaji. Mapigano kati ya wakulima na wafugaji yamepungua sana kutokana na usimamizi mzuri wa Mkuu wetu wa Mkoa wa Lindi, ambaye kwa kweli, katika mambo ambayo amefanya vizuri sana mkoani kwetu ni pamoja na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupongeza hayo pia, nipongeze suala la chanjo. Kwa mara ya kwanza Wilaya ya Kilwa tumepata chanjo za kutosha, kwa ajili ya kuku 300,000, dozi 300,000, zimewasili Kilwa hadi wakati huu, bado hazijaanza kutolewa. Kwa hiyo, ninashauri katika eneo hili, msimu sasa wa magonjwa, ugonjwa ule wa mdondo unakaribia kuanza kwa sababu, kiangazi ndiyo kinaanza hivi karibuni. Ninafikiri kwamba, Wizara itoe tamko la kuruhusu zile chanjo zitolewe kabla kiangazi hakijakolea, ili kuku wetu kwa mara ya kwanza waweze kunusurika kwa sababu, miaka iliyopita zaidi ya 80% ya kuku wanaozaliwa wakati wa masika wamekuwa wakifa kwa ugonjwa wa mdondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kushauri pia, kwenye miradi ya *BBT* sisi Kilwa, kwa upande wa kilimo, mifugo na uvuvi, katika Awamu ya Kwanza ya Miradi ya *BBT* hakuna uwekezaji wowote ambao ulifanyika, lakini tuliombwa na Wizara, tulipata maelekezo na tukajipanga kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *BBT* upande wa kilimo na mifugo. Kwa upande wa Jimbo langu la Kilwa Kaskazini tuna Mradi wa Kunenepesha Mifugo pale kwenye mnada wa Njinjo, kwa hiyo, ninaomba Serikali iharakishe kuleta fedha, ili vijana wetu ambao wamekuwa *attached* kwenye mradi huu waweze kunufaika, kupata ajira, kupata kipato na kujineemesha kiuchumi kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka pia kuzungumzia suala la sasa, migogoro imepungua, lakini bado ipo. Kwa kiasi kikubwa migogoro hii imesababishwa na upungufu wa malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuzungumzia suala ambalo kwa sasa migogoro imepungua, lakini bado ipo. Kwa kiasi kikubwa migogoro hii imesababishwa na upungufu wa malisho pamoja na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nilikuwa ninaomba niishauri Serikali iwekeze vilivyo katika eneo, la moja, suala la kupata malambo; malambo ni machache katika Wilaya ya Kilwa katika maeneo ambayo wanaishi jamii ya wafugaji ambao wameingia kwa wingi baada ya kutoka katika Bonde la Ihefu katikati ya miaka ya 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yetu ya Kilwa pia ina mito mikubwa ambayo inatiririsha maji wakati wa masika, lakini maji yote yale yamekuwa yakiishia baharini. Tuna Mto Mbwemkuru, Mto Hanga na Mto Matandu, ambayo yote hiyo inatoka katika Milima ya Matumbi pamoja na Pori la Akiba la Selous ambako mvua nyingi huwa zinanyesha. Mpaka wakati huu ninapozungumza kule mvua inanyesha sana na hii mito inatiririsha maji kwenye baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba katika eneo hili, licha ya kujenga malambo kwa ajili ya kupata maji ya kunywa kwa wafugaji wetu, ninaomba tuwe sasa na mpango madhubiti kwenye vyanzo hivi mahsusi vya mito ambavyo kama mlisikia hivi karibuni na mwaka jana, viliharibu kabisa barabara zetu katika Ukanda huu wa Kusini. Tujenge mabwawa katika mito yote hiyo niliyoitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itatuwezesha, moja, kukabiliana na mafuriko ambayo kila baada ya miaka minne mitano yamekuwa yakijirudiarudia na kuharibu miundombinu pamoja na mipangilio mingine ya maisha ya watu wetu. Pia, tutaweza kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kuweza kupata maji ya kulisha mifugo, kuweza kumwagilia nyasi kwa ajili ya malisho ya wafugaji wa mifugo yetu, lakini pia tutaweza kupata ajira kwa vijana wetu wengi wanaotokea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia katika eneo la malisho basi tuone upatikanaji wa mbegu zipatikane za kutosha. Sisi katika Wilaya ya Kilwa tuna kaya zisizopungua 6,000 za wafugaji, lakini wafugaji lakini wafugaji ndiyo kama vile alivyozungumza Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Olelekaita kwamba, wengi wamekuwa wakichunga, siyo kufuga. Unakuta ng'ombe anachapwa viboko, lakini vilevile unakuta ng'ombe amechorwa chorwa; wengine wamechorwa namba za magari na kadhalika ili tu kuwa-*identify* huyu ng'ombe yuko hivi yuko vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya vile kwanza tunai-*frustrate* ile mifugo na hatimaye hatupati nyama ambayo ina *quality,* lakini hata ile ngozi inakosa viwango. Kwa hiyo, ninafikiri kuwa tunahitaji tuboreshe katika eneo hilo. Ikiwezekana basi kwa kuwa mwaka huu tumepata kama kilo 120, sasa ukilinganisha na kaya 6,000 zilizopo Kilwa kwa kweli ni kiwango kidogo sana. Kwa hiyo, ninaomba tuwekeze fedha nyingi, tuongeze idadi ya mbegu zinazopatikana, tuzipande katika kama viji-*ranch ranch* hivi ambavyo vitagawiwa kwa wale wakulima wetu wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninaomba vitendea kazi kama magari, pikipiki na vinginevyo kwa ajili ya wale maafisa mifugo wetu; kwa kweli vitawasaidia kuweza kusimamia hii sekta nzima ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masoko kama nilivyosema, ngozi nyingi zimekuwa hazina viwango kwa sababu zimechorwa chorwa, wale ng'ombe wana alama alama nyingi, na kwamba wamekwishateseka na viboko. Niliwahi kwenda kule Moshi kwenye kiwanda cha ngozi na kutengeneza viatu ambacho kinamilikiwa na *PSSSF* wakishirikiana na wabia wao wa magereza. Waliniambia kama ng'ombe wapo, kama unasema watu wa Kanda ya Ziwa wengi wamehamia huko Kilwa, waelimishe kuhusu suala la kutunza vizuri hizo ngozi, tutakuja kununua. Kwa hiyo, niiombe Serikali iwekeze katika kutoa elimu juu ya ufugaji bora na utunzaji bora wa hao ng'ombe ili waweze kutoa vizuri mazao yanayotokana na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uvuvi tunashukuru kwa bandari ya kisasa na tunashukuru kwa boti. Tunaomba bandari isimamiwe ili ikamilike kwa ubora, lakini pia *boat* ziongezwe katika awamu ya pili ya utoaji wa boti lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane, kengele ya pili.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** ...chanja na Soko la Samaki Kivinje na Somanga tunaomba ule mradi utekelezwe ambao uliahidiwa zaidi ya miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija Aboud, wajiandae Mheshimiwa Zacharia na Mheshimiwa Getere.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa jioni hii ya leo ili niweze utoa mchango wangu mchache kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzitambua na kuziona umuhimu wake sekta zetu hizi za uzalishaji ikiwemo Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi. Pongezi nyingine zimwendee Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu wetu na watendaji wote wa Wizara hii ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea, ninaomba Wizara iharakishe mchakato wa kumaliza mamlaka ya uvuvi na mamlaka ya mifugo ukamilike ili sekta zetu hizi ziweze kufanya kazi zao kwa weledi na bila kuwa na changamoto zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa Wizara yetu kuongezewa bajeti, kwa maana ya kuongezewa bajeti, lakini

tunataka jambo hili liende sambamba na utoaji wa zile fedha ambazo tunazipitisha. Wizara ina mambo mengi ya kufanya na mipango kazi mingi ya kufanya, lakini tunakwama au watendaji wetu wanakwama kwenye utekelezaji baada ya kuwa na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajielekeza kwenye uvuvi wa bahari kuu. Ninapenda kuipongeza sana Serikali kwamba, sasa Bandari yetu ya Uvuvi kule Kilwa inafikia tamati na karibu itazinduliwa rasmi. Sasa ninaomba tu na ule mchakato wa kununua meli za uvuvi uende sambamba ili kazi yetu hii ya uvuvi wa bahari kuu ifanyike kwa ustadi na kuweza kupata mapato kwa haraka zaidi kwa sababu vitu hivi vinaungana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kwenye maji yetu ya asili ya ndani ambayo Mwenyezi Mungu ametubariki maji mengi kwenye maziwa, mito na kwenye bahari. Ninashauri kwamba tuendelee kuwekeza zaidi kwenye maji yetu ya asili ili tuachane na kununua samaki kutoka nje ya nchi kwa kuwa sisi wenyewe wa kujitosheleza ndani ya nchi na tuna uwezo pia wa kuuza nje ya nchi na tukapata mapato zaidi kupitia sekta hii ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji wa viumbe kwenye maji. Tunaipongeza sana Wizara inajitahidi pamoja na kuwapambania hawa wafugaji wa viumbe kwenye maji, kuwaondolea kodi za pembejeo na vifaa ambavyo vinasaidia kwenye uzalishaji wa viumbe kwenye maji. Hapo ninapongeza sana, ninaomba juhudi hizi ziendelee ikiwa ni pamoja na kuangalia na changamoto zingine za kodi mbalimbali ambazo zinakabili kwenye sekta zetu hizi za uvuvi na mifugo ili wavuvi wetu na wafugaji wetu waweze kufanya kazi, kupata faida na kupata tija na hapo hapo na Serikali nayo ipate tija na faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta hii ya uvuvi tuna Chuo chetu kile cha Bagamoyo, Mbegani. Chuo hiki kinatoa mafunzo mbalimbali ya uvuvi ikimo hiyo ya viumbe kwenye maji (ufugaji). Hata hivyo, chuo chetu sasa hivi kinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo majengo ya walimu na pia kina changamoto ya miundombinu mbalimbali ya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaojifunza uvuvi au masomo ya uvuvi pale chuoni Bagamoyo, wanakabiliwa na changamoto ya malipo; kwa maana wanyonge; wanashindwa kujiunga na kile chuo kutokana na kukosa rasilimali, au wazazi wao hawana rasilimali za kuwalipia. Ninashauri Serikali ishirikiane na sekta inayotoa mikopo ili chuo hiki nacho kiingizwe kwenye vyuo vya kati ambavyo vitatoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wetu kwenda kusoma kwa sababu chuo hiki kinafunza ajira za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wakipata ajira za moja kwa moja ndiyo tunapunguza lile tatizo letu la ukosefu wa ajira kwa vijana, kwa sababu tayari wakitoka pale wana ujuzi wa kufuga, kuvua na vitu vingine. Mpaka ubaharia pale unasomeshwa sasa hivi. Kwa hiyo, vijana wetu watapata vyeti vya kwenda kujiunga kwenye meli kubwa za duniani huko ambako sasa hivi kuna changamoto hiyo, kwamba wanashindwa vile vigezo. Kwa hiyo, tukiwawekea na hawa mitaji wakapata mikopo nao wanafunzi watakuwa wengi kwenye chuo kile sambamba na Serikali kuwekeza kwenye miundombinu ili kiwe chuo cha kisasa kinachofundisha teknolojia za kisasa katika uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tuendelee kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wetu wa ndani kwenye Sekta zetu hizi za Mifugo na Uvuvi. Kwa mfano, kwenye sekta ya mifugo kwenye sehemu ya usindikaji wa maziwa na uchataji wa maziwa wananchi wamehamasika, wawekezaji wetu wa ndani. Kwa mfano, sasa hivi kituo chetu kile Kiwanda cha *ASAS* wanatengeneza maziwa ya unga na ndicho kiwanda pekee Tanzania kinachotengeneza maziwa ya unga. Hata hivyo, changamoto iliyopo kwenye maziwa ya unga ni kwamba bado tunaona kama maziwa ya unga ni anasa na kwamba bidhaa zinazotokana na maziwa ni anasa, kama jibini na vitu vingine. Hivi ni vyakula kama vyakula vingine ambavyo vinatupa lishe, protini na viini kwenye afya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa zile kodi na tozo ambazo ziko kwenye hizi bidhaa za maziwa zinazozalishwa za

usindikaji iondolewe ili wananchi tuweze kumudu kuvila hivi vyakula vinavyotokana na maziwa na sisi tupate afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna wananchi hawanywi maziwa ya kawaida, lakini wanatumia maziwa ya unga, lakini maziwa ya unga bei yake kubwa. Pia, kuna wengine wako mbali vijijini na hawana majokofu ya kuhifadhi. Maziwa ya unga yakiwa kwenye kopo anaweza kutumia mpaka miezi miwili, miezi mitatu. Haya maziwa ya kawaida yanakuwa hayawezi kuhimili. Kwa hivyo, vitu hivi navyo ni muhimu vikafikiriwa kodi ili na sisi wananchi tuweze kumudu kununua nasi tule hizo jibini, siagi, tule na vitu vingine. Hivi vinalinda afya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuendelea kuajiri Maafisa Ugani. Ninaendelea kuwapongeza Serikali, Wizara kuendelea kuajiri Madaktari wa Wanyama. Tulikuwa tuna uhaba mkubwa sana wa Madaktari wa Wanyama na hawa Maafisa Ugani; wanahitajika sana. Kwa hivyo, Serikali iendelee kuwaajiri kila inapopata nafasi ili wafugaji na wavuvi wetu wapete mafunzo mazuri yanayoendana na hali ya sasa na changamoto za sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Serikali kulifufua Shirika la *TAFICO*. Ninachokishauri hapa ni kwamba ukamilishwaji wa shirika hilo uende haraka kwa sababu hili shirika ndilo linalokwenda sambamba na ile Bandari yetu ya Uvuvi kule Kilwa. Kwa sababu shirika hili litatengemewa sana na kule bandari ya uvuvi ili tufanye kazi kwa pamoja, vifaa hivi vifanye kazi kwa pamoja ili tuingie kwenye uvuvi wa bahari kuu tukiwa tumekamilika kimiundombinu, kivifaa na kila kitu. Tuweze na sisi kuchuma fedha kutoka kwenye hizo rasilimali za uvuvi zilizoko kwenye bahari kuu ambavyo kwa muda mrefu sisi hatujavipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ushauri wangu, shirika hili lianze kazi, limalizie mambo yao miundombinu ikamilike ianze kazi. Kwa sababu ni muda mrefu, sasa tunaanza kufufua kidogo kidogo, ifike mahali tumalize tuachane na *TAFICO* tuguse kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana Wizara yetu inafanya ushirikishwaji mkubwa wa wadau mbalimbali kwenye Sekta za Mifugo na Uvuvi, zikiwemo za Taasisi Zisizo za Kiserikali *NGOs*. Ninawapongeza sana Wizara, wanazishirikisha na zinashiriki moja kwa moja katika kutoa mafunzo mbalimbali ya ugani, zinawasaidia wanapata masoko na mambo mengine yanayohusu uvuvi na ufugaji. Taasisi hizi zinashiriki kikamilifu kushirikiana na Serikali... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, wajiandae Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Maganga.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa heri aliyotujalia wakati huu na nafasi hii, lakini pia na baraka zake kwa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Serikali kuanzia kwa Mheshimiwa Rais, watendaji wake Serikalini na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa iliyofanyika katika nchi yetu kwa wakati mwingi na kwa sekta mbalimbali. Ninadhani kila mmoja ametambua michango mikubwa ya Serikali na kazi kubwa iliyofanyika Serikalini kupitia wananchi wetu na wananchi wananufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri dada yetu Kijaji na Mheshimiwa Naibu Waziri Mnyeti na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa anayofanya katika Wizara hii kwa ujumla. Tunawapongeza

sana. Ahsanteni sana kwa kazi kubwa wanayoifanya. Niipongeze pia Kamati yetu kwa ufupi kwa kazi kubwa wanayofanya. Nikupongeze na wewe unavyotuongoza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nizungumze mambo machache. Mchango wangu ni mdogo sana leo. La kwanza, nizungumzie sura halisi ya miji nchini, kwa maana ya Mji wa Mbulu. Mheshimiwa Mnyeti, Naibu Waziri aliwahi kuwa *RC* kule Manyara kabla ya kuwa Mbunge. Kwa kweli, anaufahamu Mkoa wa Manyara ulivyo. Jimbo la Mbulu Mjini kata 10 ni vijijini ama 11 na wana ng'ombe na wana mashamba, lakini kwa miaka miwili nzima hatujafanikiwa kupata mradi ule wa majosho kwa ajili ya bajeti kuwa ndogo na hatujaifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kama inawezekana, maeneo haya ya miji kwa mfano kama Mbulu na maeneo mengine, miradi hii hata tuanze kwa awamu kwa kidogo kidogo ili tuweze kufanikisha yale tuliyokusudia. Kwa sababu majosho kule tuna kata 10, tuna vijiji 34 lakini maeneo yetu kwa ujumla ni milima na mabonde kama wanavyofahamu na maeneo mengi ni ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili linahitaji zaidi majosho, lakini pia wafugaji hawataacha kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iangalie upya maeneo hayo yenye miji ya sura ya vijiji ikiwemo Mbulu na miji mingine; kwa sababu eneo la mji ni ile sehemu ya pale katikati tu, lakini ukienda nje zaidi kama kilometa tano, kilometa tatu pengine unakuta ni vijiji na miji na watu wanachunga na wana mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nizungumzie, ni kwamba, tuna programu ya kuzungumzia ufugaji wa mifugo, lakini ufugaji huo wa mifugo hauna tija kwa baadhi ya maeneo. Kwa mfano, unaweza kukuta mfugaji mmoja ana ng'ombe 100 lakini anaweza kupitwa kwa mapato na mfugaji mwenye ng'ombe mmoja wa maziwa ama watano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini tafsiri ya eneo hili? Ni lazima tuwekeze kwenye utaratibu wa kubadilisha koo za mifugo, wa

kutafuta fedha zaidi ili kuleta mifugo bora zaidi, hasa ng'ombe wa kisasa; na ule Mradi wa Kukopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe ambao kule Mbulu ulikuwepo. Kwa muda huu Serikali haijapata fedha kwa miaka karibu sita, saba ya kupeleka kwa ajili ya kuendeleza ule Mradi wa Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe. Ambapo ni ng'ombe anatoka kwa mfugaji wa kwanza mtamba wa jike anaenda kwa mfugaji wa pili ili kuleta tija na kuleta picha nzuri ya ufugaji ulio bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo maana yake ni kwamba tunazungumzia uhalisia wa hali halisi ya wale wananchi ambao tayari walikuwa wana ng'ombe wengi. Katika Eneo langu la Mbulu Mjini pamoja na vijiji hivyo 34 na kata 17, nusu nzima wameshahama, wamehama na mifugo. Sababu za kuhama ni maeneo ya malisho hayapo. Hebu tujiulize, wanakohama huko ardhi inaongezeka na wananchi hao wanapata maeneo ya kufuga? Ardhi haiongezeki, mifugo wanaongezeka na wanadamu tunaongezeka. Kwa hiyo, tuna haja kubwa ya kutazama namna ya kulizuia jambo hili ama kuiletea kwenye sura nzuri ya kuondoa uhamaji wa mifugo na namna ambavyo maeneo yale machache tunaweka ufugaji wenye tija na ili wananchi wetu wanufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninatataka kulizungumzia ni kuhusu upungufu wa maafisa. Ingawa siyo Wizara yao lakini wao ni Wizara inayohitaji wataalam. Maafisa Mifugo hatuna; kama Mbulu Mjini tuna sita tu. Kwa hiyo, kata zile zote 10 na vijiji 34 huduma yao inakuwa ngumu sana. Hapa ninashauri kama inawezekana yale maeneo yote tuliyoainisha kama vijiji kwa mujibu wa sheria na ugawaji wa mipaka, walau Serikali ijitahidi kutupatia hao Maafisa Ugani ambao wao watakuwa walimu, watakuwa wahamasishaji, lakini pia watakuwa wanatoa huduma kwa sekta hii ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda pia nizungumzie utaratibu wa programu ya mauzo ya mifugo minadani. Ninadhani tuangalie minada mikubwa nchini, tuweke utaratibu wa kuwa na mizani katika uuzwaji wa mifugo kwenye minada ili muuzaji apate

tija katika kile anachouza, lakini pia na mnunuzi anunue kile kitu kinachopata uhalisia katika mizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa wazi uko kwenye Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Mwaka 80 na kitu tuliletewa mizani kwenye mnada. Wananchi walikuwa kwa ajili ya uelewa walikuwa wanashindwa kuuza mifugo na wanakataa. Ninadhani wakati huo kutoka 80 na kitu mpaka sasa hivi ni miaka 40. Tuna haja ya kuangalia eneo hilo tunafanyaje ili tupate mauzo ili wananchi wauze mifugo yao kwa bei nzuri, lakini pia kwa manufaa yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, tumejitahidi sana kuchimba visima kila Kijiji, lakini hatujaweka sinia za mifugo kunywa maji. Ninadhani kama ni Wizara ya Maji ama Wizara hii ya Mifugo, tuangalie, kwa kuwa tunachimba kisima kwenye kijiji na lengo ni kupata maji, mifugo iwe sehemu ya wale wananchi, wapate pia sehemu ya mifereji kama *cattle track* ya kubwa maji. Mabeseni yale yatasaidia kwa ajili ya mifeleji ile ili mifugo kuweza kupata maja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninataka kulichangia kwenye eneo hili ni kwamba, ninaishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayofanya lakini hebu tutazame namna ya kuongeza Bajeti ya Wizara hii. Hii bajeti ni ndogo sana katika taarifa waliyowasilisha. Kwa kuwa bajeti ni ndogo na bajeti ni mwendelezo, kadri tunavyoona mahitaji ni makubwa tutazame utaratibu wa walau bajeti yao iwe inafanikiwa kwa 100% hii waliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafute pia namna ya kuongeza bajeti ya Wizara hii kwa sababu, wanapohama kule wanapata kadhia kubwa sana, mifugo inapotea, mingine inakufa, mingine inakamatwa, tunajenga taswira ya kuona ng'ombe ni wanyama wabaya sana, wafugaji na wakulima wanagombana. Namna pekee ni kuandaa mazingira ya namna gani uhamiaji huu utapungua kwa kuleta ufugaji wenye tija, lakini koo za mifugo ambapo tutatafuta programu kwa nchi nzima kila kijiji walau tuwe na mashamba darasa madogo ambayo yataanzishwa kwa

utaratibu ambao Serikali itaona ruzuku hii iliyopatikana inaleta tija katika kila kijiji na kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninajua hili hatutalipenda sisi wachaguliwa, lakini niseme tu kwamba, hatuna namna nyingine zaidi ya kuhamasisha upunguzaji wa mifugo. Mifugo imekuwa mingi zaidi ya uwezo wa uhudumiaji na jinsi wanavyokuwa wengi wanakuwa kero kwa Taifa letu na wamejenga matabaka mawili ya wafugaji na wale wakulima wanakuwa na vita na wasielewane kwa namna moja ama nyingine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla ninaishukuru Serikali kwa kazi kubwa na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Maganga na Mheshimiwa Felix, wajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Wizara muhimu sana. Ninamshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi, dada yetu Mheshimiwa Dkt. Ashatu ni mchapakazi sana; Naibu wake Mnyeti; na Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kazi za Serikali ni kubwa sana za kufanya na hii Wizara ina kazi kubwa sana. Wote kwa ujumla wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kweli kipekee tulikuwa na migogoro mikubwa sana kati ya wafugaji na hifadhi na migogoro mikubwa sana kati ya wafugaji na wakulima. Kwa sasa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi imefanya kazi nzuri sana ya kupunguza hii migogoro, ninawashukuru sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwateua na kuwapa kazi maalum ya kupunguza hii migogoro ambayo kwa kweli bado inaendelea. Wote kwa ujumla wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wamezungumza hapa kwenye bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Hivi kwa mfano bajeti iliyokuwepo tumesema wengi shilingi bilioni 460 na *point*, lakini hela iliyotoka shilingi bilioni 131 na *point*, yaani hiyo ni 28%. Sasa ninajiuliza, sisi Wabunge tunataka majosho yote yajengwe, tunataka mabwawa yajengwe, tunataka vizimba vijengwe, tunataka chanjo zije, hivi kweli kwa bajeti hii tutafika kweli au kuna nini? Au bajeti hii sasa tufanyaje au tuwaambie wakulima wetu sasa na wafugaji wajiandae sasa kuhudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha kiukweli haijaitendea haki hii Wizara, kiukweli. Tuliomba Wizara ya Fedha itoe fedha za kutosha bado tuna mwezi, mwezi Julai bado haujafika, kwa hiyo waendelee kuongeza Wizara hii ipate fedha. Ukiangalia bajeti mpya ni shilingi bilioni 476 ni ongezeko la shilingi bilioni 16 sawasawa na asilimia tatu, bado hali siyo shwari sana kwenye hii hoja. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara hii ya Fedha iendelee kuongeza, lakini Serikali isaidie hii Wizara ifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara ni moja ya mikoa yenye wafugaji wengi sana, wengi sana. Huko nyuma enzi zetu tulikuwa na viwanda vingi sana vya maziwa, vyote vimekufa havipo. Mheshimiwa Waziri ninamfahamu, ninamjua tulikuwa naye kwenye Viwanda na Biashara, ninajua alivyotembea mpaka China kushughulikia Mgogoro wa Liganga na Mchuchuma, ninamjua sana, alifanya kazi nzito sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe atembelee Mkoa wa Mara, ninajua juzi tumekuja kwenye jimbo lake tunajua wale watu wametuahidi atarudi. Sasa kama atarudi atabaki kwenye hii Wizara tumwombe aende Mkoa wa Mara ahamasishe viwanda. Hali yetu hata kama tungekuwa na mifugo, lakini hatuna viwanda tutaishije? Mapato ya watu wetu yanakuwa kidogo. Kwa hiyo, tunakuomba, kwa wafugaji wa Mara ufike pale tuanzishe viwanda, vitusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nimezungumza, nimeuliza swali hapa. Tulichimba Lambo la Kihumbu, tumetumia milioni mia saba sijui na kitu, imebaki 15% limalizike, sasa linaendelea

kuharibika, linaendelea kuharibika, linaendelea kuharibika. Sasa ninajiuliza tutakuja tena kutafuta hela shilingi shilingi milioni 800 itatoka wapi ya kumaliza lile bwawa? Ni eneo dogo. Mheshimiwa Mnyeti wewe ni Waziri ulikuja pale, unajua wakati fulani Wabunge humu huwa hatuelewi mambo mengine. Huyu Mnyeti huyu akiwa na Waziri kama Dkt. Ashatu, akipanga mipango akasema shambulia, hiyo kazi itaisha mara moja, yaani kazi ya kushambulia Mnyeti anaijua na wote tunamjua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba lile Bwawa la Kihumbu tafadhali ninaomba tulimalizie, kwa sababu litaharibika hatutapata namna ya kufanya. Watafute namna mabwawa ya mifugo: Bwawa la Mikomariro, Bwawa la Kyandege na mabwawa mengine madogo madogo yapo mpaka Nyang'aranga yameharibiwa na mvua na yalikuwa yanasaidia wakulima. Tutafute vibajeti vya kusaidia kuboresha yale mabwawa ili mifugo iendelee kuwepo kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la hereni. Hii hereni tulipiga vita sana, lakini baadaye wameileta kwa mtindo fulani hivi siyo mbaya, wafugaji wetu wamegawanyika kwenye makundi mbalimbali, wako wafugaji wana ng'ombe mmoja mpaka ng'ombe 10; wako wafugaji wana ng'ombe 10 mpaka ng'ombe 20; wako wafugaji wana ng'ombe 100 mpaka ng'ombe 500; wako wafugaji wana ng'ombe 500 mpaka 1,000, kama Mnyeti alivyo hapa, huyu ana ng'ombe 1,000. Ng'ombe wa Mnyeti anatoka kwa 3,000,000; wako wafugaji wana ng'ombe 1,000 mpaka ng'ombe 10,000, kwa hiyo ninaomba hii hereni ianze na wafugaji wakubwa. Hawa wafugaji wadogo wadogo twende nao polepole, tutoe elimu kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli tunaanzisha sheria, eti mimi nikienda kuoa nipate vibali kutoka wilayani, nikipeleka ng'ombe mnadani nipate sijui vibali vya nani, nikifanya hivi sijui nipate, hapana! Hii mali ni ya kwetu sisi wenyewe wafugaji watupeleke polepole, watuletee sheria watuelimishe. Wale wafugaji wakubwa ambao tuko huku ndani tuendelee kupata hereni, hereni ni nzuri sana lakini wananchi wetu hawajawa na elimu ya hili suala la hereni. Kwa hiyo, twende nao polepole

polepole. Mheshimiwa Dkt. Ashatu, anajua haya mambo na yeye ni mfugaji na ana wafugaji wengi, tuendelee polepole kuwaelimisha wananchi, tusiende haraka tutaua, tutaleta kesi nyingine ambayo ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru mama pia kwa kuleta chanjo, ametoa chanjo bure. Mama Samia huyu jamani, kwa kweli chanjo bure nchi nzima hivi tunafanyaje sasa? Hivi mtu afanyaje? Niliwahi kusema humu ndani, huyu mama siku akitoka kwenye Urais akaja Rais mwingine, atapewa makofi miaka miwili mpaka miaka mitatu, atakuwa amefanya kazi kubwa ya demokrasia lakini na ya kuhudumia wananchi. Kwenye suala la chanjo, lilikuwa linasumbua sana wananchi, linaenda kutoka bure. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara hii, ninawaamini, ninaunga mkono hoja, ninawaamini sana, waende wakatengeneze Bwawa la Kihumbu; waende wakatengeneze Josho la Kiroreli; waende wakatengeneze Josho la Sarakwa; na wakajenge majosho kwenye maeneo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Wizara ya Kilimo wanaenda wanatengeneza josho halafu hawatengenezi maji. Wanajenga josho, lakini hawaweki kisima cha maji, wanaoshaje? Kwa hiyo, ninaomba kama wakipata nafasi ya kutengeneza majosho, watengeneze na kisima cha maji, watengeneze hesabu ikae vizuri, milioni 22 kwa milioni 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo ninawaamini sana na ninawaunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, Mheshimiwa Felix jiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi na fursa hii niweze kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu, tukiwa tunapitisha bajeti hii muhimu sana ya wafugaji pamoja na wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, hakika ameleta mapinduzi makubwa na amepunguza kero kubwa upande huu wa wafugaji. Na-*declare interest*, ninatokea familia ya kifugaji, lakini pia hata mimi asili yangu ni mfugaji na ninataka niwape shule tu wale ambao hawajawahi kupitia biashara hii, biashara hii ni nzuri kuliko biashara za *M-Pesa* pamoja na biashara nyingine za kitaalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na mifugo yako sisi Kisukuma tunaita *"Ndogosa"* yaani kwa maana ya majike yale ya wastani "mtamba" sijui wanasema Kiswahili chake fasaha, ukiwa nayo 100 yaani mwenye *M-Pesa* akasome pamoja na mwenye mtaji wa shilingi milioni 200 na kuendelea. Kwa sababu una uhakika kila siku ndama wanazaliwa na mambo yanaenda vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wasukuma pia benki yetu ni ng'ombe na niishauri Serikali pamoja na dada yangu Waziri na kaka yangu Mnyeti kuna kila sababu Wizara yenu kuionea wivu. Tumeona kweli wanajitahidi kadri ya uwezo, lakini ninaomba wajitahidi na wakipangilia vizuri mipango yao hapa kuna mapato mengi zaidi, kwa sababu wafugaji hasa sisi Wasukuma tumesambaa kote sasa. Ukienda Mbeya utakuta maporini humo Wasukuma tumo; lakini pia ukiwa Longido huko kwa Wamasai, Wasukuma tupo, sema changamoto moja tu ambayo tulitaka kujiharibia ni ile ya ukataji wa miti. Serikali inapaswa kulichukua hili kama ajenda kuwapa semina tu Wasukuma kwamba, miti haitakiwi kukatwa, lakini ng'ombe wachungwe kwenye mapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Rais na mchana nilimupa taarifa nilikuwa nina maana nzuri tu ya kumpa kampani mzungumzaji mwenzangu Kanyasu, alizungumzia suala la Pori la Kigosi, tunamshukuru Rais ametupatia fursa kuweza kuchimba mle, lakini hilo eneo ni kuwa sana, wafugaji wa maeneo hayo kwa maana ya Mkoa wa Shinyanga, Geita na Tabora kwa ujumla wanaomba waruhusiwe ng'ombe wao waingie wachunge kwa sababu wenyewe hawakati miti wala hawaharibu mazingira. Kilichopo kupitia Wizara hii wafugaji

wapewe semina kwamba ng'ombe wachungwe, lakini miti isikatwe. Hakika tutaongeza pato kubwa sana na hata pato la Taifa tutaliongezea mapato mengi, kwa sababu ng'ombe watazaliwa wengi, lakini vilevile ng'ombe wakiwa wanakula wanashiba ndiyo wanavyozidi kuzaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine ambalo limeleta shida sana kwa wafugaji wangu Mbogwe, hii mihuri ya Vitongoji pamoja na Wenyeviti. Kama nilivyosema kwamba, sisi *M-Pesa* yetu ni ng'ombe, kwa hiyo tuna utaratibu ukitaka kupeleka ng'ombe mnadani ni lazima upite kwenye Kitongoji uandikiwe kibali. Hivi Vitongoji ndivyo vinavyojua wafugaji kwamba fulani ana ng'ombe na fulani ana ng'ombe. Sasa hivi utaratibu huu kupitia waraka wa mwaka 2016 unaozuia vitongoji pamoja na Wenyeviti kukaa na mihuri, hii shida imekuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii shida inasababisha sasa hivi wafugaji wengine wasipeleke hata ng'ombe mnadani. Kwa sababu, huwezi ukapeleka mfugo wako mnadani usipokuwa na kibali unachotambuliwa kwamba wewe unatoka wapi, wewe Serikali inakutambua kivipi, huwezi ukaswaga ng'ombe wako. Kwa hiyo, niiombe Serikali, ninajua kwamba yapo maeneo mengine hawa Wenyeviti kweli wamefanya vibaya, lakini mimi kwenye wilaya yangu hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo atengeneze semina kwa hawa Wenyeviti warudishiwe mihuri ili kusudi wafugaji hawa waendelee kufanya biashara zao kupitia mifugo yao. Kwa maana kule kwetu yaani ukitaka kupeleka, kwa mfano mnada wa Masabi ama Bukombe ni lazima upite kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji akupe kibali ili uende ukauze ng'ombe wako. Mpaka sasa hivi ina maana watu hawapati hiyo fursa. Nikizungumza hayo, Naibu Waziri anafahamu kwa sababu mazingira yako na yangu yanafanana sisi sote tunatoka maeneo yaleyale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mhangu ili umpeleke ng'ombe ni lazima uwe na kibali. Sasa hivi mamlaka ikirudishwa kwa Watendaji tu, Watendaji hawa wanatoka maeneo mbalimbali hawawajui wafugaji na kunaweza kukatokea wimbi la

wezi wengi sana. Kwa sababu Mtendaji huyu yeye anaenda kwenye kijiji ni mgeni, hawajui waliomzunguka kwamba ni nani na nani ambaye ana mifugo hapa. Kupitia Wenyeviti na Vitongoji wa maeneo ndio wanaowafahamu kwamba, huyu kweli ana ng'ombe na huyu ana mbuzi na huyu ana kuku. Kwa hiyo, hii ajenda ninaomba ichukuliwe kwa maamuzi makubwa sana haraka iwezekanavyo ili usumbufu huu na mwaka huu kama tunavyojua ni wa uchaguz,i ili kusudi wenzetu waendelee kufanya biashara ya Mifugo yao, Vitongoji waruhusiwe kukaa na mihuri ili kusudi kuendelea kutoa vibali pale wafugaji wanapopeleka ng'ombe kwenye minada waweze kufanya biashara bila usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine hapa, ninapenda niishukuru Serikali jinsi inavyotuhudumia na pamoja tunavyoleta kero na shida zetu hapa inatusikiliza. Hata hivyo, lipo suala la majosho, Waziri wa Mifugo hawa wafugaji wanahitaji majosho kila kata na nilishawahi kuzungumza na Mheshimiwa Mnyeti akasema kwamba kwenye bajeti hii lazima iingie. Sasa nitaisikiliza hotuba yako pale mwishoni kwamba, je, tunaenda sasa kuwawekea majosho haya wafugaji wa Mbogwe? Kwa sababu, aliyekuwa Waziri mwaka 2021/2022 alienda kuwaahidi kwamba tutaleta majosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ilichukue hili haraka sana iwezekavyo ili kusudi hawa ng'ombe wawe wanaoshwa kwenye majosho kwa maana kupe pamoja na wadudu wengine na wao wanaleta changamoto kwenye ng'ombe na kuweza kuwa na afya mbaya ambazo hazistahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uzio. Tuna minada ambayo inajaza mifugo mingi, utakuta utoroshaji, utoroshaji haupo kwenye madini tu, hata kwenye mifugo utoroshaji upo. Unakuta ng'ombe zaidi ya 2,000 au 3,000 wameenda kwenye mnada, lakini unakuta wanaolipa kodi ni ng'ombe 200 au 300 tu. Ukiangalia Mhangu hakuna uzio, lakini pia pale Mbogwe mimi nina minada miwili nina mnada wa Masumbwe pale. Ninaiomba Serikali itoe pesa kupitia bajeti hii tunayoenda kuipitisha ili tukazungushe uzio, ili wafugaji wanapoleta mnadani ng'ombe

hawa Serikali ipate pato la uhakika ili asipatikane mtu wa kutorosha. Kwa sababu kukiwa na uzio, wataona hata uingizaji wao wa mapato utakuwa mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niiombe Serikali isiwe na masharti na milolongo mingi mara sijui mwisho ng'ombe wa ngapi, iwe tu biashara huria kama biashara nyingine. Mwenye uwezo wa kufuga ng'ombe 10 afuge; na mwenye uwezo wa kufuga ng'ombe wa kisasa, afuge; mwenye uwezo wa kufuga ng'ombe wa kienyeji afuge. Ukiniambia kufuga ng'ombe wa kisasa sijui, mimi ninajua ng'ombe wa kienyeji kwa sababu hawana longolongo nyingi. Ukinunua ng'ombe wako ni *kupamila* tu yaani peleka mbugani watazaa wenyewe utakuwa unachukua faida tu. Kwa hiyo tusiwekewe ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwekewe masharti. Ninaiomba sana Serikali iondoe usumbufu kwa wafugaji ili tufuge vizuri na tuweze kuendesha nchi yetu kwa raha na starehe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix, Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Kaijage na Mheshimiwa Kunti wajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo. Nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wake Dkt. Phillip Isdor Mpango, kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa Wizara hiyo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kubwa sana kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, hongera kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya. Pongezi za pekee kwa ndugu yangu Alexander

Pastory Mnyeti, hakika Wizara hii anaitendea haki hongera sana. Pongezi nyingine ziende kwa Katibu Mkuu Profesa Riziki Shemdoe kwa kazi kubwa anayoifanya na Manaibu wake wote wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa sababu ya muda utaenda kujikita kwenye Uvuvi. Tanzania tumejaaliwa, Mwenyezi Mungu ametupatia maziwa makubwa katika Bara la Afrika, sisi ndiyo matajiri. Tuna ziwa Victoria, tuna Ziwa Tanganyika, tuna Nyasa, tuna Rukwa, lakini tuna maziwa mengine madogo madogo ambayo ndani yake Mwenyezi Mungu aliweka viumbe ambapo kimoja wapo ni samaki ambacho kinatupatia lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi yetu Watanzania inaongezeka kila siku. Mahitaji ya mboga ya *protein* inayotokana na samaki kutoka kwenye maziwa yetu ni makubwa sana. Nianze kwa mfano na Ziwa Tanganyika, *fish catch* (uvuvi), mapato yatokanayo na uvuvi kati ya miaka ya 1990 hadi 2012 tulikuwa tunapata tani 220,000. Leo tunapozungumza mapato ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa mwaka yameshuka hadi kufikia tani 58,000. Hali kadhalika, ukienda katika Ziwa Victoria mapato ya uvuvi yameshuka. Hata viwanda vilivyokuwa vimeanza kuongezeka na kushamiri hadi kufika 2022 katika Ziwa Victoria vilitegemea malighafi ya mazao ya uvuvi, sasa viwanda hivyo vinajiendesha kwa kusuasua na vingine vimesimama kwa sababu ya kukosa malighafi ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza ni nini, mahitaji yetu yameongezeka. Sasa hivi ukienda katika haya Maziwa Makuu, katika Ziwa Tanganyika tunategemea dagaa, ambao dagaa hao wanapatikana katika Ziwa Tanganyika katika dunia yote. Aina ya dagaa wanaopatikana katika Ziwa Tanganyika, hawapatikani sehemu yoyote duniani, hali kadhalika migebuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Ziwa Victoria tunao samaki kama vile sato lakini sangara, miaka ya nyuma tulikuwa tunaona ndege kubwa zikija kupakia samaki na kwenda nje. Sasa

hivi hali ya uvuvi imeshuka, sababu ipi imesababisha kushuka kwa hali ya uvuvi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio changu naomba Serikali iweze kuongeza fedha kuwasaidia idara ya uvuvi ili waweze kulinda hazina hii ya uvuvi. Pato la uvuvi ni dogo, lakini ukiangalia ukipima ile *potentiality* ya hazina hii ni nini ni kubwa. Kitu gani ambacho kimesababisha mapato haya ya uvuvi yapungue? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza sisi wenyewe tumeongezeka, tunahitaji lishe, tunahitaji protini. Kwa hiyo, mahitaji ya samaki ni makubwa, imesukuma wavuvi wengi kuingiza mpaka zana haramu ambazo sasa zimeshamiri kila kona katika maziwa yetu, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua juhudi kubwa ambayo Serikali inafanya na hongera Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mnyeti kwa kazi kubwa na kwa kikosi kazi ambacho sasa kinaendesha *operation* ya kupambana na wavuvi haramu katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatutaweza kuiangalia na kusaidia idara ya uvuvi kupata fedha ili waweze kulinda mali hii haya maziwa yetu yanaweza yakabakia kuwa *swimming pool* katika miaka ijayo. Kwa hiyo, ninashauri sana Serikali iwapatie fedha idara ya uvuvi ili waweze kuendesha *operation* za kulinda hazina hii ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika na katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna nyavu ambazo hazikidhi viwango vilivyotolewa na wizara, kuna kushamiri kwa nyavu zinazoitwa makila ambayo ni *Gillnet* ambazo sasa haziendani kisheria, kwa kule Ziwa Tanganyika zinaitwa *frimayaa* zimetapakaa. Mpaka sasa hivi upo uvuvi haramu wa kutumia vyandarua, uvuvi wa kila aina ambao sasa umeenda kumaliza samaki zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kwa dhati kabisa kama inawezekana kama Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi haiwezi ikazaa Wizara mbili tukapata Wizara ya Mifugo au tukapata Wizara ya

Uvuvi basi huu ni wakati muafaka ambapo sasa idara ya uvuvi inatakiwa iwe mamlaka ili iweze kupambana na changamoto ambazo sasa hivi zinakabili shughuli ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninatoa ushauri wa idara ya uvuvi iwezeshwe, izunguke katika maziwa makuu yote ikitoa elimu kwa jamii ya wavuvi wote juu ya umuhimu wa kutumia nyavu zinazoruhusiwa kisheria kwa ajili ya kulinda hazina hii ya Samaki, ili sisi tunaofaidika na watoto watakaokuja na watakaozaliwa na watoto wetu nao waweze kufaidika na hazina hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo. Kumekuwepo na malalamiko ya tozo zinazohusiana na shughuli hizi za uvuvi, sasa ni wakati ambapo Serikali ikae chini iangalie ni tozo gani ambazo zinaonekana zimekuwa kero kwa wananchi, wazipunguze ili kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kuendeleza uhifadhi na wa maliasili hii ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ninaomba, idara hii ya uvuvi kila sehemu ambapo kuna bandari wawe tayari kukagua aina ya nyavu zinazoingia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix haya ahsante.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, wajiandae Mheshimiwa Kaijage, Mheshimiwa Kunti na Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa ambayo ameyafanya kwenye Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi. Halikadhalika nampongeza sana Mheshimiwa Waziri,

Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mnyeti, Katibu Mkuu Profesa Shemdoe na viongozi wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, ninampongeza sana wifi yetu Mheshimiwa Waziri Dkt. Ashatu Kijaji kwa kuteuliwa kama mwanamke wa kwanza wa kushika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi na ni imani yetu kubwa kwamba kwa uwepo wake kwenye Wizara hii basi wanawake wanaojihusisha na sekta ya mifugo na uvuvi watakwenda kuneemeka na naamini hiyo ni moja ya malengo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuelekeza mchango wangu katika maeneo mawili; eneo la kwanza ni namna ambavyo sekta hii ya uvuvi imewezesha wanawake wanaojishughulisha na uchakataji wa mzao ya uvuvi halafu nitahitimisha na eneo la lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishukuru sana Serikali kwa mambo makubwa ambayo imefanya kwa ajili ya wanawake wavuvi lakini na hususani wanawake wanaojihusisha na uchakataji wa mazao ya sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa mafunzo ya ujasirimali kwa wanawake takribani vikundi 41 na hii ni hatua kubwa sana, lakini hali kadhalika vizimba vya kufugia samaki 222 ambavyo Serikali imetoa wanufaika 1,213 wamenufaika. Kati ya hawa wanufaika 615 ni wanawake. Kwa hiyo tunasema ahsante kubwa sana kwa kuendelea kuwainua wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye boti pia wanawake hatujaachwa nyuma, kati ya boti 219 ambazo zimetolewa zenye thamani ya bilioni 19.7 na 34% ya wanufaika wa boti hizi ni wanawake na wanawake hawa wanajumuisha wanawake wa vikundi kutoka Mtwara, Ruvuma, Kisiwa cha Ukerewe, Mwanza – Kirumba, Rukwa pamoja na Kigoma. Kwa hiyo, tunaendelea kusema ahsante sana kwa kuendelea kuangalia wanawake kwa jicho la kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika baadhi ya vikundi vya wanawake wanaochakata dagaa wamepata chanja za kisasa. Jambo hili ni kubwa na ambalo linaendelea kuboresha ubora wa dagaa, dagaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile vikundi 125 vya wanawake katika sekta ya uvuvi wamepata mikopo, mikopo yenye riba nafuu na mikopo isiyokuwa na riba. Hapa niseme jitihada ziongezeke kwa sababu Tanzania ina zaidi ya vikundi 300 vya wanawake kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana viongozi wanawake wa Chama cha Wanawake Wanaochakata Mazao ya Uvuvi, kwa upande wa Kanda ya ziwa, Ziwa Victoria Mama Julita, Felista, Jovita pamoja na Mkurugenzi wa Shirika la *EMEDO* kwa kazi kubwa wanayofanya kwa kushirikiana na Serikali kuendelea kulinda maslahi ya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na shukrani hizi, nitumie fursa hii kuiomba Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, nilishawasilisha hapa Bungeni ombi ambalo lilikubaliwa na Serikali, kwamba katika ule Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi basi sehemu ya fedha zile zielekezwe kwenye kuwezesha wanawake, kuwapa elimu wanawake katika eneo la kupambana na ukatili wa kijinsia, kuwapa wanawake uwezeshaji wa namna ambavyo wanaweza wakapata vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ombi hili lilikubaliwa nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri anavyohitimisha atuambie namna gani ambavyo wizara imejipanga kutumia Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi kuendeleza wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili ni kwamba kwa kuwa sekta hii ya uvuvi inaleta fursa nyingi sana hususani kwa wanawake. Ningependa kuishauri Serikali ione namna ya kuwekeza kwa kujenga kituo cha kuchakata mazao ya sekta ya uvuvi katika kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapokuwa na kituo cha kuchakata mazao ya uvuvi itakuwa ni kama shamba darasa, lakini pia itawezesha wanawake ambao hawana vifaa kutumia sehemu hiyo jambo ambalo litapunguza gharama, lakini jambo ambalo litatuhakikishia kwamba tunalinda usalama wa chakula kwa maana ya *food safety,* tunaongeza ubora wa bidhaa zetu, hali kadhalika kuinua uchumi wa wanawake. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ione namna ya kuwekeza katika kituo cha kuchakata mazao haya ya uvuvi katika kila mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu la tatu, ni kwamba tunatambua kipindi cha mvua ndipo ambapo kunakuwa na dagaa wengi, lakini akinamama wanateseka kuona wapi ambako wataweza kukausha dagaa zao ili hali kuna mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Serikali chini ya wizara ya wifi yetu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji Daktari bingwa kabisa aone namna ambavyo watawekeza katika *solar tents,* ili *solar tents* hizi ziweze kuwawezesha akinamama waweze kuendelea kukausha dagaa zao, jambo hilo litaendelea kulinda usalama wa chakula kwa maana *food safety,* lakini pia litaendelea kulinda ubora wa dagaa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nihitimishe kwa kusema kwamba ni muhimu sana sekta hii ya uvuvi iendelee kuwaangalia wanawake wavuvi na wachakataji ili na wenyewe waendelee kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe na eneo langu la pili; inatambulika kwamba sekta ya mifugo na uvuvi inachangia kwa kiwango kikubwa kwenye upatikanaji wa protini na virutubisho vingine, jambo ambalo linachangia moja kwa moja katika lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hata mipango ya Wizara hii, inaonekana Wizara hii

inajielekeza zaidi katika uzalishaji na biashara, lakini lazima tuweke jitihada pia katika kuhamasisha ulaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu tukiangalia takwimu za ulaji bado, ulaji wetu upo chini tukiangalia tu mathalani kwenye eneo la unywaji maziwa tunaambiwa takribani sisi unywaji wa maziwa upo kwenye wastani wa lita 68 kwa kila mtu kwa mwaka, wakati vigezo vya dunia vinaelekeza tuwe kwenye wastani wa lita 200 kwa mtu mmoja kwa mwaka. Kwa hiyo, utaona namna gani ambavyo bado tuko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo pia hata katika ulaji wa nyama tupo kwenye watani wa kilo 17 kwa mtu mmoja kwa mwaka, wakati viwango vya dunia vinaelekeza kwamba tuwe kwenye wastani wa kilo 50 kwa kila mtu kwa mwaka. Kwa hiyo, hii inaonyesha kwamba Wizara hii iweke jitihada kubwa pia katika kuhamasisha ulaji na siyo tu uzalishaji na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikielekea kuhitimisha, upande wa mifugo yupo Mkurugenzi Msaidizi wa Masuala ya Usalama wa Chakula na Lishe, Dkt. Nyamizi, anayefanya kazi kubwa sana, lakini kwa upande wa uvuvi hakuna kitengo hicho na hakuna mtu huyo. Kwa hiyo, niombe sana wizara hii waone namna ambavyo watahakikisha kwamba suala la usalama wa chakula na lishe liangaliwe pia kwa upande wa uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninawapongeza sana kwa kazi kubwa wanayofanya na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kaijage dakika tano, Mheshimiwa Kunti dakika tano.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta neema kubwa sana katika sekta ya uchumi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi na Mifugo ni muhimu sana katika uchumi wa jimbo langu lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi haijaendelezwa ipasavyo. Kwa mfano, ukiangalia jimbo langu karibu robo tatu limezungukwa na maji na kazi kubwa pale ni uvuvi, lakini ukiangalia mapato yatokanayo na uvuvi bado ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kuu ni mbili; kwanza kuna *over fishing;* na pili ni uvuvi haramu kwa sababu sasa samaki hawapatikani unakuta watu wanatumia sana sumu na nyavu ambazo hazikubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni matumizi ya vifaa vya kizamani, kwa mfano tangu nizaliwe naona wavuvi katika sehemu yangu wanatumia vifaa vile vile zana zile zile. Kwa hiyo, sasa imekuwa ni vigumu sana kuweza kupata samaki kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona *trendy* nyingine samaki nao wanaanza kuwa wajanja, sasa hivi siyo rahisi samaki wa sasa hivi kumvua kwa kutumia zana za zamani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizi ninashauri Serikali ifanye mambo yafuatayo hasa katika jimbo langu; kwa sababu sehemu kubwa ya vijana wanajishughulisha sana na uvuvi. Ninaomba Serikali itujengee vizimba na nikisema vizimba nimewahi kuleta maombi katika Wizara na Wizara ikaniahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sasa hivi hapa wakati wa kufunga mjadala, nina imani Mheshimiwa Waziri atazungumzia kuhusu vizimba ambavyo nilimwomba. Vizimba angalau 24 na boti za kisasa 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine naona ni Maafisa Samaki sijui wanaitwa Maafisa Uvuvi sijui maafisa nani, lakini naona kwamba na wao ni tatizo. Kwa sababu badala ya kwenda kuendeleza uvuvi wao sasa kazi yao ni kukamata wavuvi. Kwa hiyo, ninaomba wizara ifikirie kama ikiwezekana, niiombe Serikali kwamba ikiwezekana katika Jimbo langu la Mwibara,

watuondolee hawa Maafisa Uvuvi watuletee Maafisa Uvuvi ambao wanakuja kuendeleza uvuvi siyo kukamata wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mifugo na sisi tuna mifugo mingi sana katika jimbo langu, lakini ukiangalia *facilities* zingine za kusaidia mifugo inakuwa hamna kwa mfano tuna josho moja tu wakati tuna kata 12. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ifikirie kuongeza majosho katika maeneo ya Namuhula, Kitengule na Igundu. Nina imani kwamba tukishapata hayo majosho tutakuwa tutaanza kupata mazao mazuri na bora ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umenipa nafasi ya upendeleo kwa hiyo nisingependa sana nichukue muda wako mwingi. Ninaomba nitumie muda huu sasa kuiunga mkono hoja. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti dakika tano, Mheshimiwa Naibu Waziri jiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa muda wako na mimi ili niweze kupata fursa ya kuchangia Wizara hii na kwa kuwa muda ni dakika tano, ninaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri hongera, wakati anateuliwa Mheshimiwa Rais alisema Mheshimiwa Dkt. Ashatu nakupa nafasi hii na Wizara hii nataka ukaondoe changamoto za wafugaji na wewe bila kusita ulivua moka ukavaa buti ukaingia *site* kuwatafuta wafugaji walipo, hongera sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo wafugaji wetu bado wana changamoto zao hususani kwenye migogoro imetulia, lakini tumwombe Waziri na mimi namwombea *Insha Allah* atarudi na naomba abaki hapo hapo ili aendeleze yale aliyokwishayaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii bado ni changamoto kwa hiyo, tumwombe sana tunajua Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine mpo wakati sisi tunaenda kwenye michakato. Waendelee kutengeneza mfumo ambao utaendelea kuwasaidia wafugaji wetu waondokane na hizo changamoto za migogoro ya ardhi, wapewe haki kama Watanzania wengine ndani ya Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utashi wake wa kisiasa. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema hapa mimi ni Mjumbe wa Kamati wamezungumzia suala la hereni, suala la hereni Mheshimiwa Rais ameamua kutoa hereni bure kwa Watanzania wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ameweza kupunguza chanjo huko nyuma Watanzania wafugaji walikuwa wana adha kubwa sana ya chanjo, lakini chanjo hizo pia zilikuwa ni chanjo feki ambazo wafugaji wetu wengi walikuwa wanaumia wanaenda kuchanja mifugo, mifugo yao inakufa na bajeti zote tulikuwa tukipiga kelele nikiwemo hata mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sasa kwa jitihada na utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wako wote, niwaombeni cha kwanza tusaidieni elimu kwa Watanzania, lakini watoe maelekezo kwa Maafisa Mifugo wetu wafikishe hizi taarifa kule chini ili kusiwe na upotoshaji wa watu wengine wenye dhamira mbaya ya kwenda kuwarubuni, lakini pia na kuwalaghai wafugaji wetu, hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo hilo kwenye chanjo, chanjo ya kuku ni bure Mheshimiwa Rais ametoa bure. Kwa hiyo, wafugaji wetu akinamama, vijana na wetu wengine ambao ni wafugaji wa kuku wanaenda kupata chanjo hii bure, lakini mbuzi, kondoo ni shilingi 300 na ng'ombe, punda ni shilingi 500. Kwa hiyo, kusiwe na bei nyingine yoyote kwa wafugaji wajue hizo ndiyo bei ambazo watazitumia wakati watakapofika ule wa kuletewa chanjo na chanjo hizi zianze basi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametuonyesha hereni hizo hapo ni nzuri tunazitamani wafugaji wanahitaji, twende wapelekeeni hizo hereni waende tukatambue mifugo yetu tujue tuna nini ili Serikali pia ipate fursa ya kuweka mipango yake vizuri ya kuwahudumia wafugaji kwa mujibu wa idadi ya mifugo iliyopo ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni kituo cha uzalishaji wa chanjo tulichonacho pale Kibaha. Mheshimiwa Waziri kituo kile tulikitembelea, kina changamoto ya watumishi kwa maana ya nguvu kazi, lakini pili kina changamoto ya fedha. Tunaomba kupitia wewe na Wizara ya Fedha wakisaidie kile kituo kimalize lile jengo na wawaongezee fedha ili waweze kuzalisha chanjo nyingi zaidi tuachane na biashara ya kuagiza chanjo nje, tuanze kuzalisha chanjo sisi wenyewe ndani ya Taifa letu zenye uhakika, zinazoendana na mazingira ya kwetu hapa Tanzania ili tuepuke pia kuwa na chanjo ambazo tuna mashaka nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninatamani kulisemea, Mheshimiwa Waziri kumekuwa na usafirishaji wa ng'ombe, tunamtoa ng'ombe Shinyanga anahangaika barabarani mpaka Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri tunawaombeni hebu tengenezeni kuna viwanda viko pale Mwanza baadhi vimekufa, vipo vingine ambavyo vimebaki, tufufue viwanda vya nyama, tuache kumtesa ng'ombe, kumsafirisha kutoka Shinyanga, Kagera mpaka Dar es Salaam ndiyo akachinjwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ng'ombe huyo akifika Dar es Salaam hata muda wa kupumzika ili atengeneze mazingira na mwili wake auandae kwamba sasa nime-*relax* na aanze kutengeneza mazingira nitakuwepo au sitakuwepo ili tuweze kupata hiyo nyama bora anapofika usiku wa manane saa tisa, saa kumi, kumi na moja kaingizwa kwenye machinjio kachinjwa. Tunakula ng'ombe utafikiri mipira.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ng'ombe ana *stress*, ng'ombe hana ladha, kwa sababu gani?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ng'ombe ameteseka kwa kusafirishwa umbali mrefu. Kwa hiyo, tuone namna gani ya kujenga viwanda vya nyama ambavyo vitakuwa kwenye maeno yetu ya wafugani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu lingine. Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Chemba ni Mji unaokua, tuna mnada wetu mkubwa sana wa Soya, tunaomba kwenye bajeti hii tuwepo kwenye ujenzi wa mnada wa Soya, lakini tunaomba machinjio ya kisasa kwenye mnada ule ili tuweze kuukuza mnada ule na huo mnada sisi ndiyo unaotupatia mapato ndani ya Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa muda wako Mungu akubariki sana na ushinde kwa kishindo Jimbo la Ilala. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na takwimu za mifugo na uvuvi ya mwaka wa kilimo ulioishia Juni, 2023 inaonesha kuwa idadi ya ng'ombe ilikuwa milioni 36.6. Kati ya hao, wakulima wadogo walikuwa na ng'ombe milioni 36.4 na mashamba makubwa yalikuwa na ng'ombe milioni 0.2. Aidha, wakulima wadogo walikuwa na mbuzi milioni 26.3 na mashamba makubwa mbuzi milioni 0.34. Kwa upande wa kondoo, wakulima wadogo walikuwa na kondoo milioni 8.9 na mashamba makubwa kondoo milioni 0.24. Vilevile, nguruwe waliofugwa na wakulima wadogo walikuwa milioni 3.7 na mashamba makubwa yalikuwa na nguruwe 5,123 na kulikuwa na jumla ya kuku milioni 98 ambapo wakulima wadogo walikuwa na kuku milioni 85.5 na mashamba makubwa yalikuwa na kuku milioni 12.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na idadi hiyo kubwa ya mifugo, mchango wa sekta ya mifugo na uvuvi bado ipo chini sana na tija ikiboreshwa kuna fursa kubwa ya sekta hii kuchangia sehemu kubwa ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Tanzania kuwa nafasi ya tatu kwa nchi za Bara la Afrika na kuchangia katika uchumi wa Taifa, sekta hii ya mifugo na uvuvi inazalishwa kwa tija ndogo. Katika hali hii, sekta ya mifugo haijamsaidia mfugaji na mvuvi kwa kiasi kikubwa kujinasua kwenye umaskini na kimeendelea kutoa mchango mdogo kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue hatua zaidi ili kuboresha sekta ya mifugo na uvuvi ikiwemo ujenzi wa mabwawa, kuwezesha mashamba ya kuzalisha lishe/chakula cha mifugo, kuwezesha sekta binafsi kuzalisha mitamba ya kisasa na vifaranga wa samaki. Ninapendekeza Serikali ianzishe vitalu vya mifugo katika Kata ya Mjele na Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ikiwemo kuchimba mabwawa na visima. Pia ninapendekeza kuwezesha kuanzisha mashamba makubwa ya kuzalisha lishe ya mifugo ikiwemo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Serikali imalizie kujenga Kiwanda cha Nyama cha Utengule (Mji Mdogo wa Mbalizi) ambacho kwa muda mrefu ujenzi umesimama pamoja na

kuwepo vifaa vyote muhimu vilivyotolewa na wafadhili. Kutokana na kuwepo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe ambao ni wa kimkakati kusafirisha mazao ya kilimo na mifugo kwa masoko ya nje, ninapendekeza umaliziaji wa kiwanda hiki cha nyama na pia uwezeshaji wa vitalu vya kunenepesha mifugo katika Kata za Mjele na Mshewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze Maafisa Ugani waliopo kwenye Halmashauri ya Mbeya ni wachache na wale waliopo hawaonekani kutoa huduma za ugani kwa wananchi. Wizara iweke msukumo wa kuhamasisha, kuanzisha na kutoa elimu kuhusu kilimo cha malisho ili kuwezesha malisho kutosheleza mifugo mwaka mzima. Serikali iongeze kasi ya uzalishaji wa mitamba kutokana na idadi ndogo ya ng'ombe wazazi kwenye mashamba ya Serikali na matumizi madogo ya teknolojia ya uhimilishaji kwa kutumia mbegu bora za mifugo. Pia kuwepo na mkakati wa kuongeza mazao ya uvuvi ili kuwezesha samaki wapatikane kwa tija kuwezesha ushindani kwa soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wenye nia thabiti na wanaopenda kujishughulisha na ujasiriamali wa ufugaji samaki kwenye mabwawa watambuliwe na uwekwe utaratibu maalumu wa uwezeshaji kupitia halmashauri zao kupata mitaji na utaalamu wa kufuga samaki kwenye vizimba na mabwawa na hivyo kuweza kujiajiri wenyewe na kujipatia kipato. Serikali ishughulikie changamoto ya chakula cha samaki na uhaba wa vifaranga hapa nchini. Vijengwe vitotoleshi vingi katika vituo vya ukuzaji viumbe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ombi; ujenzi wa machinjio ya kisasa Ngelewala, Kata ya Mwangata Jimbo la Iringa Mjini. Machinjio hii ni moja kati ya machinjio za kimkakati nchini Tanzania ambazo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliahidi kuimalizia na kuwa siyo tu machinjio ya kisasa bali kuwa kiwanda cha nyama. Kutokana na umuhimu, uhitaji na tija yake kijamii na kiuchumi, tunaomba mchinjio hii ikamilishwe ili kuleta tija iliyokusudiwa. Bahati nzuri miundombinu

ya majengo katika machinjio hii zimekalika kwa kiasi kikubwa, kilichobaki kukamilika ni mitambo au mashine za kuchinjia na kufanyia *packaging*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili, tunomba vizimba hata vitano tu, vya kufundishia ufugaji wa samaki katika chuo chetu cha *CDTI* (Chuo cha Maendeleo ya Jamii) na wafugaji wadogo wadogo wanaofuga pembezoni mwa Mto Ruaha Mdogo. Pia tunaomba majosho yetu yakarabatiwe yawe ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la tatu, tunaomba mitamba kwa ajili ya vikundi au wafugaji ndani ya Manispaa ya Iringa. Aliyekuwa Waziri wa Mifugo Mheshimiwa Ulega, aliahidi kutoa mitamba hiyo baada ya maombi kutoka kwa wananchi alipokuwa kwenye ziara. Pia tunaomba mbegu bora ya mbuzi na kondoo ili tuweze kufuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu tunaomba pia Wizara hii, iwe na mkakati wa kufanya utafiti na kutunza mbegu zetu za asili, pia kutoa mafunzo ya kufuga na wanyama wengine wanaohitaji kuhama toka kuwa wanyama pori na kuwa wa kufugwa. Pia wafugaji wafundishwe kulima chakula cha wanyama kwa kutumia hao hao wanyama kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaye kwa kweli tangu amefika Wizarani ameleta chachu ya mafanikio makubwa ambayo leo tunayasema hapa mbele yako. Mama huyu ni Mama wa tofauti, upendo wake na

maelekezo yake vyote vinaambatana kwa pamoja nasi wasaidizi wake kwa kweli tumekuwa katika wakati mzuri wa kufanya kazi kwa ushirikiano kwa kujiamini lakini pia tunatumia nafasi hii kumshauri vizuri ili mambo yote yaende vizuri hapo Wizarani na lisiharibike jambo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunaendelea kufundishwa. Mheshimiwa Waziri, amekuwa ni mwalimu mzuri hata ukimpelekea taarifa yenye *page* mia tano ataisoma yote nukta kwa mkato na hata kama umeficha vitu ndani vyote vitagundulika na Mheshimiwa Waziri atatoa maelekezo. *PhD* ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli tunaiona ikifanya kazi kwa faida ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana walioko chini yangu, Katibu Mkuu, Prof. Shemdoe, Naibu Makatibu Wakuu wote wawili Dkt. Mhede na Mhinte, lakini pia Wakurugenzi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa na ushirikiano mzuri ambao wametupa kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja ambacho tumetekeleza bajeti hii iliyokwisha. Tuna imani kwamba kazi hii ambayo Waheshimiwa Wabunge leo mnakwenda kutupitishia tunakwenda kuifanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa kwa kushirikiana na wataalam hawa ili malengo ya Watanzania yaweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa moyo mkunjufu kabisa tuna watendaji, tuna timu nzuri sana Wizarani na Wizara zingine kama zinapata nafasi ya kuja kujifunza Wizara ya Mifugo karibuni sana. Sisi ni shamba darasa tuna Maprofesa wa kutosha, tuna Madaktari wa kutosha na watu ni weledi, wana weledi wa kiwango cha juu na wana uadilifu wa kiwango cha juu na Taifa hili lina hazina kubwa sana kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, mengi yamesemwa, pale walipotuelekeza tumepokea, pale walipotuonya tutajirekebisha, pale waliporekebisha tutahakikisha kwamba tunakwenda kufanya vizuri zaidi na hata pale walipotusifu tumepokea lakini

hatuendi kulitilia maji. Tutakwenda kuliboresha zaidi na kuhakikisha kwamba pote ambapo Waheshimiwa Wabunge wamechangia na kutuelekeza tunafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa sababu *Boss* wangu atasimama hapa kuhitimisha, kwa kifupi sana nizungumzie mambo machache sana yanayohusu mifugo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamejaribu kuyagusia. Jambo la kwanza limesemwa kwa nguvu kubwa hapa ni kuhusiana na ubora wa nyama yetu iliyoko ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kwa sababu tunaongea sisi humu ndani ni lazima tuambizane ukweli, ukweli ni kwamba nyama yetu kuna muda haina sifa labda nikiongea kauli hii kidogo isije ikaleta utata, sisi tunapenda kusema tu ukweli kwamba nyama yetu haina ubora wa kwenda nje ya nchi na hii ni kwa sababu huko nyuma hatukutaka kuchanja mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuseme ukweli, bila kuchanja mifugo yetu, kule nje ili tufanye hii biashara kule nje wanataka wajue historia ya huu mfugo, ulizaliwa lini, uliumwa nini hapa katikati, ulifariki lini, uliuchanja lini na uliuchanja nini, wakishajua hayo ndipo unapata kibali cha kuingiza nyama katika nchi zao zilizoendelea. Sasa sisi hatukuwa na huu utamaduni, utamaduni huu Mheshimiwa Rais ameelekeza mwaka huu, tunakwenda kuzindua chanjo ya kitaifa tarehe 16 mwezi Juni, mifugo yote nchi hii lazima ichanjwe kwa lazima na baada ya kuchanja mifugo yetu ndiyo tutakuwa na uwezo wa kuanza kuuza nyama yetu nje ya nchi kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tusiulizane kwa nini hatuuzi nje ng'ombe, hatuuzi nje mbuzi wala kondoo, kwa uchache sana tunauza kondoo na mbuzi, lakini ng'ombe kwa kweli hatuna soko kwa sababu hatukuwa na utamaduni wa kutibu mifugo yetu. Ng'ombe anavyozaliwa ndivyo atakavyofariki. Hii haiwezekani lazima wafugaji wa nchi hii waamke na wajue kwamba mambo haya yanakwenda kwa afya, ubora wa chakula lazima uzingatiwe na wafugaji wetu wameshaelewa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hii ya kusema wengine bado hawajaelewa, mimi ninataka kuwahakikishia wafugaji wameshaelewa kwamba lazima ng'ombe atibiwe, lazima ng'ombe achanjwe ili tuweze kuwa na masoko nje ya nchi. Nami ninawapongeza sana nimemwona Mwenyekiti wa Wafugaji Tanzania yuko hapa, tunamshukuru sana kwa kuwa mwalimu. Chama hiki kimekuwa ni chama cha kufundisha kuwafugaji na siyo chama cha uharakati maana huko nyuma tulizoea chama cha wafugaji na chenyewe kinakuwa ni chama cha siasa ndani ya wafugaji, leo tunaona chama kizuri kimesimama, kinasaidia wafugaji kuwaelimisha juu ya umuhimu wa namna ya kuboresha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili kwa kweli lazima tuambizane ukweli kuanzia mwezi Juni na kuendelea mifugo yetu lazima ichanjwe ili iweze kukidhi soko la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, limezungumzwa hapa ni kuhusu mashamba ya *NARCO*. Mashamba haya ya *NARCO* tumegawia wawekezaji na ninasema hapa bila kuficha, wawekezaji hawa tulipowapa mashamba tumekuja kuwakagua wawekezaji hao wala siyo wawekezaji, nao ni wachungaji kama ambavyo wachungaji wengine tu. Mtu ana hekari 10,000, lakini ana ng'ombe 50 wakati jirani yake pale pembeni ana ng'ombe 5,000, halafu hana pa kuwapeleka, mwisho wa siku mwenye ng'ombe 5,000 anaamua kuwapeleka kwenye mashamba ya watu ili ng'ombe waweze kula. Yule mwenye ng'ombe 50 halafu ana hekta 10,000 amekaa hapo analima lile shamba bila kufuga. Tumeshatoa maelekezo mashamba haya yote lazima yarejeshwe *NARCO* ili tutafute wafugaji wa uhakika katika Taifa hili waweze kupewa mashamba hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wawekezaji ambao tumewapa mashamba hasa maeneo ya Kagera na hili tusije tukalaumiana, mashamba ya kule Kagera wamekwenda kukodisha watu kutoka nje ya nchi, ng'ombe kutoka nje ya nchi wanaingia, wanachunga, wanamaliza wanaondoka na mwisho wa siku hatupati faida! Mbaya zaidi hatujui hata hawa ng'ombe kama ni wa kwetu ama siyo wa kwetu kwa sababu hata

utambulisho hawana. Ndiyo maana tukasema twende kwenye zoezi la hereni, hereni itatufahamisha kwamba huyu ng'ombe aliyeingia hapa ni wa nchi gani ili tumkamate vizuri tumtaifishe vizuri tuweze kupata faida katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliopewa mashamba haya wameyaendeleza na mikataba yao ni mwaka mmoja na wengine miaka mitano, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri ameelekeza wale wote walioendeleza yale mashamba wapewe miaka 25, 33 ili wawekeze zaidi kama ambavyo Mheshimiwa Mwijage alivyochangia katika mchango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa harakaharaka sana nizungumzie habari ya ujenzi wa majosho. Sisi wakitupa pesa hata kila kitongoji tutajenga josho, kila kitongoji. Shida ni ufinyu wa bajeti, tukipata fedha hata kila kaya tunaweza kujenga josho, fedha tu, watupe fedha tu. Wakitupa fedha hata kila baada ya nyumba mbili tunajenga josho, tunajenga na lambo na tunamshukuru sana Mheshimiwa Bashe malambo yake haya yanatusaidia sasa tunakwenda kupandikiza samaki kwenye yale malambo yake ili wafugaji wetu wa samaki pia waweze kupata faida, lakini pia hata mifugo inapata maji kwenye malambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa malisho Wizara imejitahidi kwa kiasi kikubwa sana tumetangaza sana habari ya mbegu ya majani, sasa hivi karibu kila Kanda kuna *centre* ambayo tumeweka kwa ajili ya mbegu za malisho. Ukienda kule Mbeya Mbarali tunayo *centre* pale, tuna *JUNCAO* nzuri ambayo inazalishwa pale, wafugaji wote wa kanda hiyo wanaweza kwenda pale kuchukua mbegu kwa bei ya chini sana ili tuweze kuzalisha. Ukienda Pwani pale Kibaha tuna shamba letu zuri sana tunazalisha, ukienda Kagera tuna shamba zuri sana tunazalisha na kwa kweli tunahamasisha na mbegu hizi za nyasi zimekuwa na mafanikio makubwa na wafugaji wameona mafanikio makubwa sana kupitia nyasi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shally Raymond amesema kuhusu Mtamba ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu

aliahidi. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Shally kwamba kabla ya Bunge hili kuahirishwa atakuwa ameshapata mitamba yake miwili ataondoka nayo, akishakamilisha upatikanaji wa usafiri hata kesho tuko tayari kumletea mitamba yake ili aweze kuwapelekea wafugaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Getere. Mheshimiwa Getere tumeshazungumza katika korido huko tumemhakikishia kwamba fedha ziko tayari Bwawa lake litakamilika, yeye na Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Simbachawene wote kilio chao ni hichohicho, basi tutakwenda kuyakamilisha mabwawa yao katika maeneo yenu yote ambapo wameweza kuyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa mambo mengi atakuja kuyahitimisha Mheshimiwa Waziri na kwa sababu siruhusiwi kumkaribisha ninaomba nihitimishe hapo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuketi siku ya leo na tukaweza kujadili masuala muhimu sana kwa ajili ya Taifa letu kupitia Fungu 99 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshukuru na yeye kwa jinsi ambavyo ameongoza mjadala huu tangu alipokalia Kiti hicho asubuhi. Ametuongoza vyema kabisa kwa weledi mkubwa tunamshukuru sana, hata Ndugu yangu Mheshimiwa Kunti alikuwa hayupo kwenye orodha, lakini amejikuta akichangia, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliyochangia kwa umahiri mkubwa juu ya mjadala huu wa leo, wameweza kuudadavua vizuri na ninaomba kipekee kabisa nipokee pongezi zao, lakini tuzielekeze kwa mfugaji namba moja na mvuvi namba moja nchi

hii Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa utayari wake, kwa uzalendo wake na ujasiri wa hali ya juu wa kusema sasa anazipa kipaumbele sekta hizi za uzalishaji ili ziende kubadilisha maisha ya wananchi wetu. Kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza sana kama ambavyo ninyi mmeweza kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamechangia Waheshimiwa Wabunge wenzangu 19 kwa kuongea kwa siku hii ya leo juu ya mjadala wetu wa leo na Waheshimiwa Wabunge wawili wamechangia kwa maandishi, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu pia nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Viwanda, Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa waliyoifanya yeye pamoja na Wajumbe wenzetu wote wa Kamati yetu. Walifanya kazi kubwa tukiwa kwenye Kamati, lakini hata leo asilimia kubwa ya waliyochangia wamekuwa Wajumbe wa Kamati, hakika ninawashukuru sana sana kwa miongozo yao mema na hadi kufikia siku ya leo tunapohitimisha mjadala wetu huu, ahsanteni sana. Sisi tutabaki kuwa watiifu kwao, tutasikiliza na kutekeleza yale yote wanayotuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani kwa uwasilishaji mzuri alivyowasilisha siku ya leo kwa niaba ya Mwenyekiti, hakika ninamshukuru sana, amewasilisha kwa ufupi, lakini ameeleweka vyema na sisi tunasema tumepokea maelekezo yote na tunakwenda kuyataekeleza. Ushauri tumeuchukua tangu tulipoanzia kwenye miradi na hadi leo, ahsanteni sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba auniruhusu nimpongeze sana Kamanda wa Nchi kavu Ndugu yangu Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, ninaamini wameiona kazi yake, amesema na wamemwona, huyu ndiye Mnyeti bwana! Kule Misungwi ninaomba niwaambie huyu ni mtu sahihi sana bado tunamhitaji ndani ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Yeye ni mfugaji na akisimama kuongea na wafugaji wote huwa wanakaa kimya. Mwenyekiti wetu wa Chama cha Wafugaji yuko pale, siku moja

niliwaambia nimwachie Naibu Waziri Kikao wakasema Mheshimiwa usimwachie huyu hatamaliza dakika kumi kikao kitakuwa kimekwisha, lakini kimeisha kwa ufanisi mkubwa. Ninamshukuru na kumpongeza sana sana kwa ujasiri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nilisema, wakati nimeteuliwa, niliulizwa utawaweza wafugaji? Swali la pili lilikuwa utaweza kufanya kazi na Mnyeti? Nikawaambia kwani kuna shida gani? Hakika ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais aliyenileta Wizara hii nikamkuta Mheshimiwa Mnyeti. Lugha yake huwa ni moja tu Mheshimiwa nitume mimi niende kwanza nikavuruge halafu wewe utatengeneza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimtuma kwenda kwenye ranchi zetu za Taifa, aliyoyakuta kwa kweli inasikitisha. Wanaojiita wawekezaji na bahati mbaya wengine tumo humu, lazima tuseme ukweli ili tuwasaidie Watanzania. Leo hii nimemsikiliza Mheshimiwa mtani wangu Mbunge wa Kiteto, anasema wao wanachunga na wanatakiwa kuswaga na kwenda lakini ndiyo ile ile tunarudi hatuwezi kusafirisha nyama za mifugo hii inayozunguka nchi nzima kutafuta malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maeneo yetu kwenye ranchi zetu 15 ni kwa ajili ya wafugaji. Tunasikia kelele nikamwambia Mheshimiwa Alexander Mnyeti nenda, akaenda, akakuta kama alivyosema anayejiita mwekezaji amepewa hekta 10,000 ana ng'ombe 50, halafu kati ya hekta 10,000, kwa 90% amelima mpunga na mahindi, hii si sawa, si sawa hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri alitoa maelekezo huko alikokuwa *site,* lakini ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu alitoa maelekezo mwaka 2022 alipokuwa anahitimisha Nane Nane pale Mbeya, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Rais, Shirika letu la Ranchi za Taifa linakwenda kufanya kazi iliyokusudiwa wakati linaundwa Awamu ya Kwanza ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufikia wenzetu kama mlivyosema wa Botswana, Ethiopia waliamua na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua na mimi nimeamua kumwezesha Mheshimiwa Rais kufikisha maono yake na kuyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna sababu ya wawekezaji kulisha kwenye Hifadhi za Taifa, kama tutasimamia maeneo haya ya ranchi 15 za Taifa, ninaomba niwaambie wafugaji, Mwenyekiti wetu yuko pale, kuweni na amani, kazi inayo mwenyewe, mwenyewe ni Alexander Mnyeti ameianzisha na mimi nahitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wa kule Misungwi turejesheeni Mnyeti ili aendelee kuchapa kazi na tuwahudumie wafugaji wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu kwa sababu tutakuwa tunafuata sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tayari tumeshampelekea, ninaomba atuwezeshe kuifuta ile mikataba yote ili tuanze upya na wafugaji watumie maeneo yao. Hili ndilo nililotumwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na tutalifanya kwa ajili ya wananchi wetu tunaowawakilisha Waheshimiwa Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niwashukuru sana watendaji wetu wakiongozwa na kaka yangu Profesa Riziki Shemdoe; nilisema asubuhi ni Katibu Mkuu wa aina yake. Amefanya kazi na Mawaziri nane na mimi nimefanya kazi na Makatibu Wakuu, yeye ni wa nane; huyu ni wa aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anawaelekeza wataalam wake lakini ni mvumilivu na anaweza kushaurika kutoka kwa wataalam wake. Pia, atakuletea na wewe Mheshimiwa Waziri, mnakaa mnaongea. Kwa kweli ninampongeza sana kaka yangu Profesa, aendelee kuchapa kazi yake. Anao wasaidizi makini sana, ndugu yangu Abdul Mhinte na Dkt. Edwin Mhede; waendelee kumsaidia kaka yetu huyu ili tuweze kuyafikia maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu ninaomba niseme hatuwezi kuyajibu yote ambayo wameyasema na waliyoyashauri na kutuelekeza. Ninaahidi tutaleta kwa maandishi ili sote tuweze kuona wapi tupo na kipi tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema machache sana na la kwanza ambalo ninatamani niseme pia ni ulinzi wa rasilimali za uvuvi. Kwenye ulinzi wa rasilimali za uvuvi ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Wamesema vema kuhusu uvuvi haramu kwenye maziwa yetu yote na Bahari yetu ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; kwa mara ya kwanza mwaka mzima huu hatujapata uvuvi wa vilipuzi kwenye Bahari yetu ya Hindi. Kazi kubwa inafanyika na wala hatujasikia kelele. Wenyewe wanasimama wanasema sasa tunarudi ili tuvue kupitia nyenzo halali na tufanye uvuvi halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliweza kuwarasimisha tulipokuwa kule Tanga waliokuwa wanavua haramu lakini kwa kazi kubwa iliyofanywa na vijana wetu wakasema tunarejesha zana zote na sasa tunaomba watukabidhi boti ili na sisi twende tukavue. Mheshimiwa Rais akasema wapeni na sasa wamekuwa ni watu wema wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikia Mheshimiwa Aida asubuhi alisema kule Tanganyika tumepeleka kazi akaiita katafunua na ni katafunua kweli. Kwa muda wa wiki mbili tumekusanya nyavu ambazo ni haramu 17,500 ambazo zilikuwa zinavua vifaranga vya samaki na nyavu hizi tulizokusanya wataalam wanasema haijawahi kukusanywa kwenye historia ya nchi hii ndani ya kipindi cha wiki mbili, wakasema waliwahi kukusanya kwa miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kusema nini? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kulinda rasilimali za uvuvi. Huwa ninauliza swali na mimi Waziri sitaki uvuvi haramu; ukiongea na wataalam hawataki uvuvi haramu, ukiongea na

wavuvi hawataki uvuvi haramu; huyu mvuvi haramu ni nani? Tumeamua kumsaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana wananchi wa Kigoma, Rukwa, Katavi; nimepokea jumbe zao nyingi za kunipongeza kwa kazi kubwa iliyofanywa na kikosi kazi na pongezi zao ninazielekeza kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni kwa maelekezo yake lakini nimepokea jumbe chache hazizidi tano, kati ya jumbe hizi jumbe tano, zenyewe zinanitisha kwamba huu ni mwaka wa uchaguzi. Sasa kama nimepokea jumbe zaidi ya 100 zikinipongeza halafu jumbe tano zinanitishia mwaka wa uchaguzi, mimi ninasikiliza jumbe 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale juu kwenye *gallery* yako yupo aliyekuwa mvuvi haramu. Lazima tuseme ukweli; yupo nilimwambia njoo, alitorokea Dubai nikamwambia rudi na utaingia Bungeni na nitakupa kazi. Ndugu yangu Paschal Francis Mwakatenya, tumekubaliana na yeye lazima tuiseme wazi na Watanzania wajue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ni kijana mdogo, amejenga kiwanda lakini alikuwa na boti zaidi ya 20 ambazo zote zimefunga zana haramu za kuvua vifaranga vyetu ndani ya Ziwa Tanganyika. Kikosi kazi kikamwibua, nikamtafuta tukasema kwa pamoja amekiri kweli nilikuwa ninafanya. Alikuwa anafanya na sababu zake anazo, lakini yuko nje ya sheria na tumekaa naye tumekubaliana tukishafifilisha kosa lake, yeye sasa atakuwa Balozi wetu namba moja ndani ya Taifa letu ili aweze kuhakikisha hatuna uvuvi haramu siyo Ziwa Tanganyika peke yake ni kwenye maziwa yetu yote tuliyonayo ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika tukifika hata kule Ziwa Victoria wapo atapata Mabalozi wenzake na ninaamini tutayafikia maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kulinda rasilimali za uvuvi ili zitunufaishe sisi na zinufaishe kizazi chetu na *generation* yetu yote kama sisi tulivyorithishwa na wazee wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vizimba ndugu zangu tumeianza kazi. Kazi ni nzuri na hili nalo tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mpaka leo tumeshatoa vizimba 507 na sasa awamu ya pili tuna vizimba 394 ambavyo tutavitoa mwezi huu wa sita. Kwa hiyo hata kule Mwibara tutapeleka kwenye maeneo yote na kwa shemeji yangu Mwijage yeye alisema awe wa mwisho. Bado ndoa ninaitaka nitaleta hatakuwa wa mwisho. Kwa hiyo tutawafikia wote, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na leo hii wakitupitishia bajeti hii, nina uhakika tunakwenda kuleta vizimba vingine vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema kuhusu vizimba, wamesema vema kwamba hii ndiyo biashara ya kufanya. Baada ya kusikilizwa ninyi hapa na taasisi za kifedha tumetoka hapo nje wameniambia Mheshimiwa Waziri njoo tukae ili sasa tutoe pesa kwa ajili ya wavuvi wote nchi hii wanaotaka kufuga kwa mfumo wa vizimba. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wenzangu hii ni fursa kubwa sana kwetu. Ninatamani nitoe mchanganuo mmoja ili hata sisi tuione hii fursa na tukafanye hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatolea mfano wa ghrama za kizimba cha kipenyo cha mita sita. Gharama ya kutengeneza kizimba hiki ni shilingi 6,990,000 na kwenye kizimba hiki unaweka vifaranga 10,080 ambavyo gharama yake ni 1,814,400. Gharama za chakula mwanzo mpaka utakapovua ni kilo 3,024 za chakula ambayo gharama yake ni shilingi 8,972,752.32. Kwa hiyo, jumla kuanzia unatengeneza kizimba mpaka unakuja kuvuna ni shilingi 17,777,152.32.

Mheshimiwa Naibu Spika, mavuno tunayokadiria uvune ni kilo 3,528; piga kwa shilingi 7,500 kwa kila kilo utapata shilingi 26,460,000 toa hapo ndani ya miezi sita una faida ya 8,682,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo niliposema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kutekeleza maono ya Baba wa Taifa. Tutumie rasilimali zetu kwa manufaa ya Watanzania hasa vijana wetu na akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi kile cha pale Ilemela walipovuna mvuno mmoja wakasema wanarudisha mkopo wote wala hawataki tena mkopo wetu kwa sababu huu ni mvuno mmoja na bado utavuna zaidi. Wale vijana walirejesha mkopo na mwisho wa siku wakaendelea kuvuna wakapata faida zaidi ya mara 10; huyu ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ametupongeza. Kazi imeanza pale Kigoma wamevuna vijana wanashangilia, twendeni tuwawezeshe vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana. Yeye aliamua 10% za mapato ya Halmashauri yake yaelekezwe kwenye vizimba vya samaki; hakuna mradi unaolipa kama mradi wa vizimba vya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mikopo ya 10%, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu huku ndiko pesa ilipo. Utajiri upo kwenye uvuvi, upo kwenye mifugo. Kule kwenye mahindi upo lakini siyo sana na Mheshimiwa Bashe, Baba watoto kule tupo na tumesema hatutaki *starch* sana tunataka kuchanganya na *protein.* Kwa hiyo twendeni tu-*balance* hizi hesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kizimba cha kipenyo cha mita sita. Vipo vipenyo mpaka mita 20, mavuno yake ni makubwa twendeni tuwawezeshe vijana wetu. Taasisi za kifedha zimekubali twendeni tuchape kazi tuwawezeshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara kama ambavyo wametushauri tulichoamua kukifanya ni kufanya utafiti kwenye maji yote tuliyonayo ndani ya ya nchi hii ili tujue Ziwa Victoria lina uwezo wa kubeba vizimba vingapi, Ziwa Tanganyika vizimba vingapi, Ziwa Rukwa vizimba vingapi ili twende kazi tuwawezeshe vijana wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishalimaliza hilo, ni wazi hata kesi iliyosemwa hapa ya magugu maji na kaka yangu Mheshimiwa Kanyasu tunakwenda kwenye utafiti kujiridhisha magugu maji tunashughulika na hili gugu maji vamizi kwa sababu mengine ni mazalia ya samaki. Kwa hiyo tunashughulika na hili gugu maji vamizi kama ambavyo tumeweza kuliondoa lote pale Kigongo - Busisi na sasa vyombo vya usafiri vinapita, lakini na vizimba vyetu vinaendelea kupendeza ili vijana wetu waendelee na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa hili la malisho. Waheshimiwa wafugaji wenzangu si faraja kuzunguka nchi nzima; hapana. Tumekubaliana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI maeneo yote yaliyoainishwa ya malisho tuweze kuyatengea mbegu na twende yakapandwe malisho kwa ajili ya wafugaji wetu. Wabunge watupitishie bajeti tukaifanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; tunaendelea na kuwashajihisha wafugaji wetu waweze kumiliki ardhi, sisi tuwapatie mbegu kwa bei ya ruzuku ili walime nao wapande malisho na tuweze kuishi vizuri ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alisema Mheshimiwa Mbunge hapa Mheshimiwa Mnyeti ana ng'ombe 1,000 wala hawazunguki. Alipanda malisho na wala ng'ombe wake hawazunguki na alikuwa ananichekesha hapa kuwa ana ng'ombe mmoja hamuuzi chini ya shilingi milioni 20. Kwa hiyo Mheshimiwa mtani wangu Olelekaita tubadilike kidogo sisi wa upande huu tutafika tu na tutaweza na kuoa tutaoa. Hakuna mashaka kabisa tunataka kuvuka huku kwenye ufugaji wa asili twende kwenye ufugaji wa kibiashara ili tuifikie dunia. Soko la China wanataka tani 54,000 kwa mwaka; hazipo mtani wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana wafugaji wenzangu baada ya zoezi la chanjo na hereni, tunaingia Soko la China ambalo liko tayari linatusubiri tu tupeleke mazao yetu na mifugo yetu. Kwa hiyo, niwaombe sana tushirikiane na tuweze kuwashajihisha wafugaji wenzetu ili tulifikie soko hilo. Ufugaji ni

maisha yetu na maisha yetu ni ufugaji na utajiri uko kwenye mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme nimepokea hoja ile ya ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Maji ili kila kwenye mabwawa ya Wizara ya Kilimo tuweze kuweka samaki kwa ajili ya vijana wetu na akinamama. Pia, kwenye visima tuangalie ni jinsi gani ya kuweka miundombinu ya mifugo yetu kunyweshea. Hii tunakwenda kushirikiana, tumelipokea na tulishaanza kulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, ninaomba nishukuru tena kwa mjadala mzuri wa siku hii ya leo na sisi tunasema tuko tayari kufanya kazi na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi, Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99- Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management Division*…..Sh. 6,091,782,262
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 2,051,683,171
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*.............Sh. 2,171,534,750
Kifungu 1004 – *Veterinary Council of Tanzania*….......Sh. 561,421,000
Kifungu 1005 – *Information, Education & Communication Unit*……………………………....Sh. 0
Kifungu 1006 – *Fisheries Laboratory Unit*...................Sh. 2,343,236,000
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*…...............................Sh.605,375,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*........Sh. 835,313,000
Kifungu 1009 – *Legal Services Unit*……........................Sh. 595,600,000
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*………….………………Sh. 871,383,000
Kifungu 1011 – *Environmental Management Unit*…Sh. 1,296,252,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*….....Sh.1,057,662,000
Kifungu 1013 – *Government Comm. Unit*.................Sh.1,116,712,000
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*…………………...Sh.12,249,447,515
Kifungu 7003 – *Infrastructure Dev. Division*…………Sh. 6,673,928,000
Kifungu 7005 – *Research, Training & Extension Services Division*…………………….…..Sh. 30,504,491,176
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing Development Division*.…Sh. 9,673,772,854
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Dev. Division*…………….Sh. 2,211,772,000
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*.…...Sh.12,066,717,696
Kifungu 9002 – *Aquaculture Dev. Division*…………...Sh.8,538,586,576

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1003 – *Policy andPlanning Division*………………………..Sh. 0
Kifungu 1004 – *Veterinary Council of Tanzania*............................Sh. 0
Kifungu 1006 – *Fisheries Laboratory Unit*…...................Sh. 500,000,000
Kifungu 1011 - *Environmental Management Unit*.......Sh. 500,000,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 700,000,000
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*………………….Sh. 21,283,599,008
Kifungu 7003 – *Infrastructure Dev. Division*……….Sh. 192,227,520,000
Kifungu 7005 – *Research, Training & Extension Services Division*…………Sh. 38,524,430,287
Kifungu 8001 – *Livestock Production & Marketing Development Division*………………Sh. 37,315,176,226
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Dev. Division*….….Sh. 8,034,988,354
Kifungu 9001– *Fisheries Development Division*…....Sh. 61,119,117,603
Kifungu 9002 – *Aquaculture Dev. Division*………….Sh.14,933,570,522

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa Hoja.

**T A AR I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, kanuni ya 123(3)(a) na (b), ninaomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji; kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa bajeti yako kupita. Mmefanya kazi nzuri sana wewe na Naibu Waziri na timu yenu ya wataalam ambao kwa kweli mmeshirikiana pamoja na matokeo yake ni haya. Kama nilivyosema jana, maelekezo ya Mheshimiwa Rais mmeyatekeleza na mkifuata maelekezo ya kiongozi wa nchi, mambo yenu yatakwenda vizuri.

Niwapongeze sana Wabunge kwa michango mizuri, pokeeni ushauri wa kitaalam, jana tuliambiwa kwenye kilimo. Kilimo na sayansi vilevile tunaambiwa na watalaam hapa. Mheshimiwa Mnyeti yeye ni mtaalam mzuri sana wa masuala ya ng'ombe; twendeni na sayansi kwenye mifugo. Bila sayansi

tutakuwa na ng'ombe wengi kama aliokuwa nao Mheshimiwa Maganga lakini hawana afya. *(Makofi)*

Kwa hiyo nendeni, fuateni ushauri mzuri huu na hasa kwenye chanjo. Utakuta dawa nyingine tunauziwa mjini na baadhi ya watu dawa hizi za mitishamba, lakini badala ya kushughulikia ng'ombe, wanashughulikia binadamu. Kwa hiyo niwaombe tu muanze kubadilika.

Hili la vizimba pia nimefurahi sana wale watu ambao wako kwenye mito. Mheshimiwa Kaijage huna hata haja ya kuomba vizimba Serikalini, unaweza mwenyewe ukatafuta vijana wako ukawapa vizimba 10 na ukajipatia heshima kubwa sana kwenye eneo lako. Milioni 50 tu na wewe ni tajiri siyo kama watu ambao hawana uwezo. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya machache, Jumapili tuna jambo letu zito la kitaifa. Haya makofi yawe dhati maana wengine msitu... Kwa hiyo jamani tuliombee Taifa letu Jumapili. Heshima hii ni heshima ya Rais wetu na ni heshima ya Taifa letu. Kwa mara ya kwanza nchi yetu itang'aa kwenye Bara la Afrika. *(Makofi/ Kicheko)*

Baada ya maneo haya ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.26 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 26 Mei, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*